

**MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA
MWAKA 2020/21**

YALIYOMO

SURA YA KWANZA-----	1
UTANGULIZI-----	1
1.1 Rejea-----	1
1.2 Miradi ya Kipaumbele-----	2
1.3 Mawanda yaliyoongoza Mpango-----	2
1.4 Ushirikishwaji wa Wadau-----	2
1.5 Matokeo ya Utekelezaji wa Mpango 2020/21-----	3
1.6 Mpangilio wa Kitabu-----	3
SURA YA PILI-----	4
HALI YA UCHUMI-----	4
2.1. Utangulizi-----	4
2.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi-----	4
2.2.1. Uchumi wa Dunia-----	4
2.2.1.1. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea-----	4
2.2.1.2. Uchumi wa Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea-----	4
2.2.2. Uchumi wa Afrika na Kanda-----	5
2.2.2.1. Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki-----	5
2.2.3. Uchumi wa Taifa-----	6
2.2.3.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi-----	6
2.2.3.2 Wastani wa Pato la kila Mtu-----	6
2.2.3.3 Mwenendo wa Bei Nchini-----	6
2.2.3.4 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki---	7
2.2.3.5 Sekta ya Nje-----	8
2.2.3.6 Sekta ya Fedha-----	9
2.2.3.7 Deni la Serikali-----	12
2.3 Idadi ya Watu na Mwenendo wa Umaskini-----	14
2.3.1 Ongezeko la Idadi ya Watu-----	14
2.3.2 Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini-----	14
2.3.2.1 Umiliki wa Mali za Kudumu-----	15
2.3.2.2 Umiliki wa Akaunti za Benki-----	16
2.3.2.3 Hali ya Makazi-----	16
2.3.2.4 Matumizi ya Nishati-----	17
2.3.3 Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi-----	18
SURA YA TATU-----	19
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO-----	19
3.1 Utangulizi-----	19

3.2	Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka 2019/20-----	19
3.3	Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo -----	20
3.3.1	Miradi ya Kielelezo -----	20
3.3.2	Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda -----	24
3.3.3	Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu -----	40
3.3.4	Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji-----	61
3.3.5	Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango -----	78
SURA YA NNE -----		85
MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2020/21 -----		85
4.1	Utangulizi-----	85
4.2	Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi-----	85
4.2.1	Misingi ya Mpango wa Mwaka 2020/21-----	85
4.2.2	Shabaha za Ukuaji wa Uchumi-----	85
4.3	Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2020/21 -----	86
4.3.1	Miradi ya Kielelezo-----	86
4.3.2	Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda -----	88
	4.3.2.1 Viwanda-----	88
	4.3.2.2 Utafiti wa Teknolojia na Bidhaa za Viwandani -----	89
	4.3.2.3 Kilimo-----	90
	4.3.2.4 Mifugo-----	94
	4.3.2.5 Uvuvi-----	96
	4.3.2.6 Maliasili na Misitu-----	97
	4.3.2.7 Utalii-----	98
	4.3.2.8 Madini -----	98
4.3.3	Kufungamanisha Uchumi na Maendeleo ya Watu-----	99
	4.3.3.1 Elimu, Sayansi na Teknolojia -----	99
	4.3.3.2 Afya na Ustawi wa Jamii-----	106
	4.3.3.3 Maji na Usafi wa Mazingira-----	109
	4.3.3.4 Ujuzi na Uwezesaji-----	112
	4.3.3.5 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo -----	112
	4.3.3.6 Utawala Bora na Huduma Bora kwa Wananchi -----	113
	4.3.3.7 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi-----	117
4.3.4	Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji-----	119
	4.3.4.1 Miundombinu -----	119
	4.3.4.2 Ardhi na Maeneo ya Uwekezaji na Biashara -----	134
	4.3.4.3 Huduma za Fedha, Biashara na Masoko-----	136
	4.3.4.4 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa -----	139

4.3.4.5 Ushiriki wa Sekta Binafsi, Mashirika na Taasisi za Umma-----	139
SURA YA TANO-----	141
UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2020/21 -----	141
5.0 Utangulizi-----	141
5.1 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2020/21 -----	141
5.1.1 Vyanzo vya Ndani-----	141
5.1.2 Vyanzo vya Nje-----	141
5.1.3 Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje ya Nchi (FDI)-----	142
5.1.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi -----	142
5.1.5 Mifuko ya Kimataifa ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira-----	142
5.2 Gharama za Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2020/21-----	143
SURA YA SITA -----	144
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA -----	144
6.1 Utangulizi-----	144
6.2 Malengo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango -----	144
6.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa 2020/21-----	145
6.4 Mikakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango -----	145
6.5 Utoaji Taarifa-----	146
6.6 Mgawanyo wa Majukumu-----	146
SURA YA SABA -----	149
VIHATARISHI KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO-----	149
7.1 Utangulizi-----	149
7.2 Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo-----	149
7.3 Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana navyo -----	153
Kiambatisho I:Utekezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 -----	158

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Rejea

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21 ni wa tano na wa mwisho katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka ya kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 wenye dhima ya *Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu*. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 umejikita katika kutekeleza maeneo manne ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Miaka Mitano, ambayo ni: (i) Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda. Lengo ni kujenga viwanda vinavyotumia kwa wingi malighafi zinazopatikana nchini, hususan za kilimo na madini ili kukuza mnyororo wa thamani; (ii) Kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Eneo hili linalenga kuendeleza jitihada za kuboresha ustawi wa maisha ya Watanzania. Msisitizo utakuwa ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, elimu na ujuzi, huduma za ustawi wa jamii, uhakika wa chakula na lishe bora, kuendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali maji ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma za maji safi na salama mijini na vijijini, na kuimarisha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; (iii) Uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji. Eneo hili linalenga kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu, ikijumuisha miundombinu ya nishati, usafirishaji (reli, barabara, madaraja, viwanja vya ndege na bandari) na ununuzi na ukarabati wa mabehewa, meli na vivuko; na (iv) Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango. Eneo hili linalenga kuboresha ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango, ikiwa ni pamoja na: kuimarisha mifumo na taasisi za utekelezaji wa Mpango; kuweka mfumo utakaowezesha upatikanaji wa uhakika wa rasilimali fedha kwa maandalizi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi; na kuweka vigezo vya upimaji wa mafanikio ya utekelezaji. Vile vile, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa utawala bora.

Katika mwaka 2020/21 Serikali inatarajia kuandaa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) ambao kwa mujibu wa Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 – 2025/26) unatarajiwa kuwa na dhima ya *“Kujenga Uchumi Shindani Unaoongozwa na Mauzo Nje”* na utajumuisha miradi ambayo haitakamilika katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Miaka Mitano. Andiko dhana litakalowezesha kuanza rasmi kwa uandishi wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) linaandaliwa. Mpango huo utakuwa ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, ambayo ina dhamira ya kugeuza Tanzania kuwa Taifa lenye kipato na uchumi wa

kati wa viwanda ifikapo 2025.

1.2 Miradi ya Kipaumbele

Miradi itakayotekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2020/21 inatokana na maeneo manne ya kipaumbele ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambayo yameainishwa katika sura ya nne. Kipaumbele cha kipekee kimewekwa katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo ikiwemo: Ujenzi wa Reli ya Kati ya *Standard Gauge*; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere - MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Kusomesha kwa Wingi katika Fani na Ujuzi Adimu na Maalum; na Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi.

1.3 Mawanda yaliyoongoza Mpango

Uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21 umezingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 yenye lengo la kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya hadhi ya uchumi wa kipato cha kati inayoongozwa na viwanda ifikapo 2025; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21); Sera na mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda (EAC na SADC), Umoja wa Afrika (Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika) na kimataifa (Agenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu); na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Vile vile, Mpango umezingatia hali halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/20 na changamoto zilizojitokeza, hali ya uchumi kitaifa, kikanda na kidunia kwa mwaka 2019 na maoteo ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2020.

Katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2020/21 maandalizi yamezingatia Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21. Mkakati huo unaainisha hatua za utekelezaji na vigezo vya kupima ufanisi wa utekelezaji wa miradi kwa mwaka husika; hatua za kuchukuliwa kuwezesha upatikanaji wa fedha; mfumo wa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini; na mfumo wa mawasiliano kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Aidha, Mkakati huo unatumika kama rejea kwa taasisi katika kubainisha vipaumbele na hatua za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka husika.

1.4 Ushirikishwaji wa Wadau

Wadau mbalimbali wakiwemo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi wameshirikishwa katika uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2020/21. Aidha, mchakato huu wa uandishi wa Mpango

uliwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wakati wa maandalizi yake yaliyowasilishwa Bungeni na Serikali mnamo Novemba 2019. Vile vile, Washirika wa Maendeleo walishirikishwa kupitia majadiliano ya kufikia maeneo ya ushirikiano, ufadhili wa miradi mahsusi na misaada ya kisekta.

1.5 Matokeo ya Utekelezaji wa Mpango 2020/21

Utekelezaji wa Mpango huu utakuwa ni wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na hivyo kuchochea azma ya Serikali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu. Mafanikio yatakayotokana na utekelezaji wa Mpango huu ni pamoja na: kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla; kuimarisha utoaji wa huduma za jamii zikijumuisha huduma za maji, elimu, afya na umeme vijijini; kuimarika kwa biashara na uwekezaji; na kuongezeka kwa ajira na kipato cha wananchi na hatimaye kupungua kwa kiwango cha umaskini nchini.

1.6 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2020/21 kimegawanywa katika sura saba (7): Sura ya kwanza ni utangulizi; Sura ya pili inaelezea kwa kina mapitio ya hali ya uchumi; Sura ya tatu inahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2019/20; Sura ya nne inaainisha maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2020/21; Sura ya tano inaelezea ugharamiaji wa Mpango; Sura ya sita inaainisha mfumo na utaratibu wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango; na Sura ya saba inabainisha vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na hatua za kukabiliana navyo.

SURA YA PILI

HALI YA UCHUMI

2.1. Utangulizi

Sura hii inaelezea hali ya uchumi kwa kuzingatia viashiria mbalimbali vya kiuchumi na kijamii. Kuimarika kwa viashiria hivyo ndiyo msingi wa kuboreshwa utekelezaji wa Mpango na hatimaye maisha ya watu. Baadhi ya viashiria vilivyotolewa ufafanuzi ni pamoja na: Pato la Taifa; Pato la wastani la kila mtu; Mfumuko wa bei; Mwenendo wa sekta ya nje; Sekta ya fedha; Deni la Serikali; Idadi ya watu; na Hali ya umasikini nchini.

2.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi

2.2.1. Uchumi wa Dunia

Kwa kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili 2020, uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 2.9 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 3.6 mwaka 2018. Aidha, uchumi wa dunia unakadiriwa kupungua na kufikia ukuaji wa asilimia hasi 3.0 mwaka 2020. Matarajio ya kupungua kwa ukuaji wa uchumi wa dunia yanatokana na mlipuko wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya CORONA ulioathiri shughuli za kiuchumi. Aidha, katika mwaka 2021 uchumi wa dunia unakadiriwa kuimarika na kufikia ukuaji wa asilimia 5.8. Hii inatokana na matarajio ya kutoweka kwa virusi hivyo katika nusu ya pili ya mwaka 2020 na hivyo, kuimarika kwa shughuli za kiuchumi duniani ikijumuisha biashara na uzalishaji viwandani; na utekelezaji wa sera za kuongeza ukwasi katika nchi mbalimbali.

2.2.1.1. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Uchumi wa nchi zilizoendelea ulikua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2019 na unakadiriwa kupungua kufikia ukuaji wa asilimia hasi 6.1 mwaka 2020 kutokana na atahri za ugonjwa wa COVID-19. Aidha, matarajio ni kuimarika kwa uchumi kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2021 kutokana na juhudi mbalimbali za kuinua uchumi zikijumuisha sera za bajati na zile za fedha za kuongeza ukwasi na kuchochea uzalishaji katika uchumi.

2.2.1.2. Uchumi wa Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea

Uchumi wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2019 na unatarajiwa kupungua kufikia ukuaji wa asilimia hasi 1.0 mwaka 2020 kutokana na madhara ya ugonjwa wa COVID-19. Hali

hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na matarajio ya kupungua kwa uchumi wa nchi za China na India zinazotajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 1.2 na 1.9 mwaka 2020 kwa mtiririko huo. Vile vile, nchi zinazoibukia za Mashariki ya mbali (ASIAN5 ambazo ni Indonesia, Malaysia, Philippines, Thailand, Vietnam), nchi zinazoibukia za Ulaya na zile za Atlantiki na Karibeani zinatarajiwa kuwa kupungua na kuwa na ukuaji hasi kwa mwaka 2020. Matarajio ni kuimarika tena kwa uchumi wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 6.6 mwaka 2021 kutokana na hatua za kufufua uchumi. **Jedwali Na. 2.1** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Dunia kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 na matarajio kwa mwaka 2020 na 2021.

Jedwali 2.1: Ukuaji wa Pato halisi la Dunia 2015 - 2018, na Matarajio 2019 - 2020

Kundi/Mwaka	Ukuaji Halisi (asilimia)				Matarajio (asilimia)	
	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Dunia	3.2	3.8	3.6	2.9	-3.0	5.8
Nchi Zilizoendelea	1.7	2.4	2.2	1.7	-6.1	4.5
Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea	4.3	4.8	4.5	3.7	-1.0	6.6
Nchi Zinazoibukia Barani Asia	6.4	6.6	6.4	5.5	1.0	8.5
Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara	1.3	2.9	3.2	3.1	-1.6	4.1

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa, Aprili 2020

2.2.2. Uchumi wa Afrika na Kanda

Kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia hasi 1.6 mwaka 2020 kutoka ukuaji wa asilimia 3.3 mwaka 2019. Kushuka kwa ukuaji wa uchumi kunatokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ambao unatarajiwa kusababisha kupungua ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Aidha, ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, unatarajiwa kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2021. Ongezeko hilo litatokana na jitihada za kupambana na ugonjwa wa COVID-19, matarajio ya kuongezeka kwa misaada kutoka nchi zilizoendelea kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo na matarajio ya utulivu wa bei ya nishati ya mafuta katika soko la Dunia.

2.2.2.1. Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Katika mwaka 2019, nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulianda kuimarika ambapo Tanzania ilikuwa na ukuaji wa asilimia 7.0, Rwanda (asilimia 9.4), Uganda (asilimia 4.9) na Kenya (asilimia 5.4). Matarajio ni kuendelea kuimarika kwa ukuaji wa uchumi katika ukanda wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutokana na juhudi zinazofanyika katika nchi wanachama zikiwemo utekelezaji wa

miradi mikubwa ya maendeleo ambayo ni pamoja na miradi ya reli, barabara, maji, nishati, elimu, afya, usafiri na usafirishaji.

2.2.3. Uchumi wa Taifa

2.2.3.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Katika mwaka 2019, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 7.0 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji kwa kipindi hicho ni pamoja na uchimbaji madini na mawe (asilimia 17.7), ujenzi (asilimia 14.1), sanaa na burudani (asilimia 11.2) usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.7). Shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu zinazoajiri sehemu kubwa ya watanzania zilikuwa kwa wastani wa asilimia 4.4. Ukuaji huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa mavuno kutokana na msimu wa kilimo 2018/19, kuongezeka kwa idadi na mazao ya wanyama waliovunwa, usimamizina uvunaji endelevu wa mazao ya misitu na kuongezeka kwa samaki na mazao ya samaki yaliyovunwa katika kipindi husika.

Kwa upande wa mchango wa shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa, kilimo kilikuwa na mchango mkubwa zaidi wa asilimia 26.6 ikifuatiwa na shughuli za Ujenzi (asilimia 14.3), Biashara ya jumla na rejareja (asilimia 8.8) na Uzalishaji viwandani (asilimia 8.5).

2.2.3.2 Wastani wa Pato la kila Mtu


Mwaka 2019, Pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilikuwa shilingi milioni 139,893,804 ikilinganishwa na shilingi milioni 129,043,901 mwaka 2018. Aidha, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 54,265,158 mwaka 2019 ikilinganishwa na watu 52,619,314 mwaka 2018. Pato la wastani la kila mtu kwa mwaka 2019 lilikuwa shilingi 2,577,967 ikilinganishwa na shilingi 2,452,406 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Vile vile, Pato la wastani kwa kila mtu katika Dola za Marekani liliongezeka hadi kufikia Dola 1,121 mwaka 2019 kutoka Dola 1,078 mwaka 2018.

2.2.3.3 Mwenendo wa Bei Nchini

Katika mwaka 2019, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2018. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2019, mwenendo wa mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu kati ya wastani wa asilimia 3.0 Januari 2019 na asilimia 3.8 Desemba 2019. Wastani wa bei za vyakula ulikuwa asilimia 4.3 mwaka 2019 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2018. Katika kipindi husika, mfumuko wa bei za vyakula uliongezeka kutoka

asilimia 2.3 Januari 2019 hadi kufikia asilimia 6.9 Desemba 2019. Aidha, mfumuko wa bei za nishati ulipungua kutoka asilimia 15.7 Januari 2019 hadi kufikia asilima 2.8 Desemba 2019 kutokana na kupungua kwa bei za nishati ya mafuta katika soko la Dunia. Katika kipindi cha Januari – Mei 2020, mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa tulivu ambapo umeendelea kupungua kufikia asilimia 3.2 Mei 2020.

Kielelezo Na. 2.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Januari 2017 – Mei, 2020)



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

2.2.3.4 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2019, mfumuko wa bei katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja. Katika kipindi hicho wastani wa mfumuko wa bei kwa Tanzania ulikuwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2018. Aidha, mwaka 2019 wastani wa mfumuko wa bei kwa nchi za Uganda ulikuwa asilimia 2.9, Kenya asilimia 5.2 na Rwanda asilimia 1.7. Hali ya utulivu katika mfumuko wa bei ilitokana na hali nzuri ya hewa iliyopelekea kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nje ya ukanda huo pamoja na utulivu katika bei za nishati ya mafuta katika soko la dunia.

Jedwali Na. 2.2: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Afrika Mashariki, Mwaka 2019

Nchi/Mwezi	Mfumuko wa bei mwaka 2019												Wastani Jan-Des.19	Wastani Jan-Des.18
	Jan	Feb	Machi	Apr	Mei	Juni	Julai	Agosti	Sep	Okt	Nov	Des		
Tanzania	3.0	3.0	3.1	3.2	3.5	3.7	3.7	3.6	3.4	3.6	3.8	3.8	3.4	3.5
Kenya	4.7	4.1	4.4	6.6	5.5	5.7	6.3	5.0	3.8	4.9	5.6	5.8	5.2	4.7
Uganda	2.7	3.0	3.0	3.5	3.3	3.4	2.6	2.1	1.9	2.5	3.0	3.6	2.9	2.5
Rwanda	1.3	1.3	1.4	1.2	1.0	0.8	0.8	0.8	1.0	1.4	2.0	2.4	1.7	1.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Taarifa za Nchi Husika.

2.2.3.5 Sekta ya Nje

(a) Urari wa Malipo Yote

Hadi Aprili 2020, urari wa jumla wa malipo ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 897.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani bilioni 1.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Hii ilichangiwa na kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje kulikotokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi.

(b) Urari wa Malipo ya Kawaida

Nakisi kwenye urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ulipungua hadi kufikia dola za Marekani milioni 333.3 mwezi Aprili 2020, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani bilioni 1.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kupungua huku kulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi, hususa katika bidhaa asilia na zisizo asilia kama vile dhahabu.

Hadi Aprili 2020, mauzo ya bidhaa na huduma nje yaliongezeka kufikia dola za Marekani bilioni 8.6 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 7.3 Aprili 2019. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka na kufikia dola za Marekani bilioni 3.7 Aprili 2020, ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 3.0 Aprili 2019. Hii ilichangiwa na kuanzishwa kwa masoko ya madini nchini kulikopelekea kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu sanjari na ongezeko la bei katika soko la dunia. Vile vile, mauzo ya bidhaa asilia yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 988.1 mwezi Aprili 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 473.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa zote asilia isipokuwa kahawa, chai na tumbaku.

Hadi Aprili 2020, thamani ya uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani bilioni 8.6, ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 8.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Sehemu kubwa ilitumika katika uagizaji mafuta na bidhaa za mitaji ikiwemo mitambo na mashine inayotumika katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu ya reli, barabara, madaraja na uzalishaji umeme.

(c) Akiba ya Fedha za Kigeni

Akiba ya fedha za kigeni imebakia katika viwango vya juu vyenye kukidhi mahitaji ya nchi ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje. Hadi Aprili 2020, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5.3, kiasi kinachotosheleza kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 6.1. Kiwango hiki kilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan mazao ya biashara na madini. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la

nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni ya kutosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.0. Aidha, kiwango hiki kipo pia juu ya lengo lililokubalika katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki la miezi isiyopungua 4.5 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika la miezi isiyopungua 6.0.

2.2.3.6 Sekta ya Fedha

(a) Ujazi wa Fedha na Karadha

Ujazi wa fedha uliendelea kukua kwa kasi inayoendana na mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa asilimia 9.9 na kufikia shilingi trilioni 28.8 mwezi Aprili 2020 kutoka shilingi trilioni 25.6 mwezi Aprili 2019. Vile vile, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) uliongezeka kwa wastani wa asilimia 11.4 na kufikia shilingi trilioni 22.0 Aprili 2020 ikilinganishwa na shilingi trilioni 19.3 Aprili 2019. Ongezeko hili la ujazi wa fedha ni matokeo ya utekelezaji thabiti wa sera ya fedha, ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi pamoja na rasilimali fedha za kigeni katika sekta ya benki.

(b) Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi

Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, wastani wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa asilimia 8.7 ikilinganishwaa na wastani wa ukuaji wa asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Aidha, jumla ya mikopo kwa sekta binafsi ilifikia shilingi trilioni 19.7 ikilinganishwa na shilingi trilioni 18.6 Aprili 2019. Ongezeko hilo lilitokana na usimamizi thabiti wa sera ya fedha iliyoongeza ukwasi kwenye uchumi, utekelezaji wa mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara na kuongezeka kwa uwekezaji. Aidha, sehemu kubwa ya mikopo imeendelea kuwekezwa kwenye shughuli binafsi ambazo zinashikilia kiasi cha asilimia 31.1 ya mikopo yote, ikifuatiwa na shughuli za biashara asilimia 17.6, uzalishaji viwandani asilimia 11.0 na kilimo asilimia 7.7.

(c) Mwenendo wa Sekta ya Benki

Katika kipindi cha mwaka 2019, sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha juu ya ukomo kwa kiwango kinachohitajika kisheria. Katika kipindi kinachoishia Desemba 2019, uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki ulikuwa asilimia 16.8 ikilinganishwa na kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 10.0. Aidha, uwiano wa rasilimali kwa amana zinazoweza kubadilishwa kwa muda mfupi kuwa fedha taslimu ulifikia asilimia 32.4, ikilinganishwa na uwiano wa chini unaohitajika

kisheria wa asilimia 20.0. Vile vile, rasilimali za sekta ya benki ziliimarika zaidi kutokana na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu kutoka asilimia 10.7 Desemba 2018 hadi kufikia asilimia 9.8 ya mikopo yote Desemba 2019. Pamoja na maendeleo haya, Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha sekta ya kibenki hasa katika kupunguza uwiano wa mikopo chechefu ili kufikia lengo la asilimia 5. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na, kuzitaka benki na taasisi za fedha: kuboresha usimamizi katika utoaji mikopo; utekelezaji wa mpango kazi wa jinsi ya kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kwa benki zilizokuwa na uwiano mkubwa; na kutumia kwa lazima taarifa ya historia za wakopaji zilizo kwenye kanzidata ya wakopaji kabla ya utoaji wa mikopo. Aidha, Benki Kuu imezitaka benki za biashara kupeleka taarifa za mikopo kwenye kanzidata hizo, na kutekeleza kanuni za maadili kwa watumishi wa sekta ya kibenki.

(d) Mwenendo wa Viwango vya Riba


Serikali kupitia Benki Kuu imeendelea kutekeleza sera ya fedha ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi ambayo imesaidia kupunguza viwango vya riba katika masoko ya fedha hususan riba za mikopo. Wastani wa riba za mikopo ya benki kwa ujumla katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020 ulipungua hadi asilimia 16.85 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.16 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19, na riba za mikopo ya kipindi cha mwaka mmoja zimepungua na kufikia wastani wa asilimia 16.24 kutoka asilimia 17.79. Vile vile, wastani wa riba za amana kwa ujumla ulikuwa asilimia 7.02 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.62 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Aidha, riba za amana za kipindi cha mwaka mmoja ziliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 8.77 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020 kutoka wastani wa asilimia 8.21 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19.

(e) Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine kubwa duniani imeendelea kuwa tulivu kwa kipindi chote cha mwaka 2019/20. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa kati ya shilingi 2,299.3 na shilingi 2,302.7 kwa dola moja ya Marekani katika soko la fedha la jumla ikilinganishwa na wastani wa kati ya shilingi 2,276.4 na shilingi 2,300.9 kwa dola moja ya Marekani katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Hali hii ilitokana na: utekelezaji mzuri wa sera za fedha na bajeti; kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje; hatua zilizotekelezwa na Benki Kuu katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri wa ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni nchini kupitia maduka ya kubadilisha fedha; na utulivu wa mfumuko wa bei katika viwango vya chini vilivyopelekea kuwa na

tofauti ndogo ya mfumuko wa bei kati ya Tanzania na washirika wake wa biashara.

**Kielelezo Na. 2.2: Mwenendo wa Thamani ya Shilingi Dhidi ya Dola ya Marekani
(Wastani wa mwezi husika)**



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

(f) Sekta Ndogo ya Fedha

Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 2018. Pamoja na masuala mengine, Sheria hiyo inaipa Benki Kuu nguvu na wajibu wa kusimamia watoa huduma ndogo za fedha (Microfinance Service Providers) waliogawanywa katika madaraja manne yaani benki za huduma ndogo za fedha (micro finance banks); watoa huduma ndogo za fedha wasiopokea amana (non-deposit taking micro finance service providers); vyama vya akiba na mikopo (*Savings and Credit Cooperative Societies*); na vikundi vya kijamii (*Community Microfinance Groups*).

Baada ya kuchapishwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wengine iliandaa kanuni za usimamizi wa watoa huduma ndogo za fedha walio katika madaraja ya 2-4. Kanuni hizi zilichapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 13 Septemba 2019 na kuwekwa katika tovuti ya Benki Kuu ya www.bot.go.tz. Sanjari na hilo, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau husika iliandaa Hati ya Ukasimishaji (Instruments of Delegation) wa mamlaka na majukumu ya Benki Kuu ya usimamizi wa watoa huduma ndogo za fedha wa madaraja ya 3 na 4 kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (*Tanzania Cooperative Development Commission*) na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (*Local Government*

Authorities), mtawalia, kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018. Hati hizi zilichapishwa katika Gazeti la Serikali tarehe 22 Novemba 2019.

Katika juhudi za kuelimisha umma, Benki Kuu ilitoa matangazo kadhaa katika vyombo vya habari ikiwemo luninga, redio na kwenye tovuti kuhusu kuanza kutumika kwa Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha. Hivi sasa, Benki Kuu inafanya tathmini ya mahitaji ya Mamlaka Kasimishwa (*Delegated Authorities*) ili kuwawezesha kufanya majukumu yao ya usimamizi kwa ufanisi zaidi. Aidha, Mamlaka Kasimishwa zimepelekwa mwongozo unaozitaka kupeleka taarifa katika Serikali za Mitaa na Halmashauri ili waanze kupokea maombi ya leseni ya watoa huduma ndogo za fedha wa madaraja ya 3 na 4. Kwa upande wa usimamizi wa watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la 2, Benki Kuu imefanya maandalizi yote muhimu na imeanza kupokea maombi ya leseni.

Vile vile, Benki Kuu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imeendelea kutekeleza mpango wa elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (*Public Awareness Programme on Microfinance Policy, Law and Regulations*).

(g) Mwenendo wa Soko la Hisa

Masoko ya mitaji ni sehemu ya mfumo wa sekta ya fedha inayowezesha upatikanaji wa fedha za muda mrefu, kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili 2020, mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani uliongezeka kwa asilimia 0.2 na kufikia Shilingi trilioni 9.18 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 9.16 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa bei ya hisa ya baadhi ya kampuni zilizo rodheshwa katika Soko la Hisa. Aidha, Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa ulikuwa Shilingi trilioni 14.8 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 19.4 mwaka 2019. Kupungua kwa Mtaji wa Jumla kumetokana na kuondolewa (*delisting*) kwa Kampuni ya Madini ya Acacia kwenye Soko la Hisa (DSE) baada ya kampuni hiyo kuondolewa katika Soko la Hisa la London kufuatia utekelezaji wa makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Barrick Gold Corporation ambapo Serikali imepata umiliki wa asilimia 16 na mgawanyo wa maslahi ya kiuchumi ya 50/50 kwenye Kampuni ya Barrick Gold Corporation nchini Tanzania.

2.2.3.7 Deni la Serikali

Hadi Aprili 2020, deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 55.43. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa shilingi trilioni 40.57 na deni la ndani shilingi trilioni 14.85. Deni

la Serikali lilichangiwa na kupokelewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2019, imeonesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

Serikali imekuwa ikifanya tathmini ya Uhimilivu wa Deni (Debt Sustainability Analysis) kila mwaka ili kupima hali ya deni na uhimilivu wake. Tathmini hii hufanywa kwa kutumia vigezo vya kimataifa vilivyowekwa na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na hutumiwa na nchi zote zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Desemba 2019 inaonesha kuwa deni ni himilivu kwa muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa: Thamani ya Sasa ya Jumla ya Deni la Serikali (Present Value of Total Public Debt) kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; Thamani ya Sasa ya Deni la Nje (Present Value of External Debt) kwa Pato la Taifa ni asilimia 16.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; Thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 103.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240; Ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 11.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 21.

Uhimilivu wa deni umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa uchumi pamoja na usimamizi thabiti wa Deni la Serikali ambapo kwa mujibu wa tathmini ya Benki ya Dunia, Tanzania imewekwa kwenye kundi la daraja la kwanza (Strong performer) kwenye usimamizi wa deni. Ili kuendelea kulinda uhimilivu huu, Serikali imeendelea kuwekeza mikopo inayokopwa kwenye miradi ya maendeleo inayochochea ukuaji wa uchumi na kuongeza mapato. Aidha, Serikali imeanzisha utaratibu wa kuandaa mikakati ya kusimamia madeni wa miaka mitatu unaohuishwa kila mwaka ambapo mkakati uliopo sasa uliandaliwa Machi 2019.

Jedwali Na. 2.3: Matokeo ya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

	Ukomo	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23	2023/24	2029/30	2039/40
Thamani ya sasa ya jumla ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa	70	27.1	27.5	28.1	29.2	29.6	33.2	28.2
Thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa	55	16.3	16.8	17.6	18.2	18	13.7	9.1
Thamani ya sasa ya deni la nje kwa thamani ya mauzo ya nje	240	103.9	105.5	110.9	116.7	115.4	83.9	53.5
Uwiano wa malipo ya deni la nje kwa thamani ya mauzo ya nje	21	11.9	11.1	9.5	10.3	11.2	11.7	8.1
Uwiano wa malipo ya deni la nje kwa mapato ya ndani.	23	11.9	11.9	10.1	10.7	11.6	11.8	7.9
Uwiano wa malipo ya deni la nje na ndani kwa mapato ya ndani	N/A	33.4	29.7	27.5	29.3	29.9	46.8	44.8

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

2.3 Idadi ya Watu na Mwenendo wa Umaskini

2.3.1 Ongezeko la Idadi ya Watu


Kwa kuzingatia maoteo ya idadi ya watu kwa mwaka 2019, idadi ya watu Tanzania Bara imefikia 54,265,158 ikilinganishwa na watu 52,619,314 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Kati ya hao, wanaume walikadiriwa kuwa asilimia 49.0 na wanawake asilimia 51.0. Aidha, akiba kubwa ya mtaji-watu inayojumuisha watoto wenye umri kati ya miaka 0 - 14, imeongezeka na kufikia watu 23,667,991 mwaka 2019 ikilinganishwa na watu 22,998,096 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Akiba hii ya mtaji-watu ni rasilimali muhimu katika ukuzaji wa sekta mbalimbali za uchumi hasa sekta ya viwanda. Serikali inaendelea kuwekeza zaidi katika elimu, lishe na afya ili kuongeza ubora wa rasilimali hii.

Vile vile, watu wenye umri wa miaka kati ya 15 hadi 64 ambao ndio nguvu kazi ya Taifa, wameongezeka na kufikia 28,907,674 mwaka 2019 kutoka watu 27,957,929 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi wameongezeka kwa asilimia 1.5. Kwa upande mwingine, umri wa kuishi kwa Tanzania Bara umeongezeka kutoka wastani wa miaka 65.0 mwaka 2018 na kufikia wastani wa miaka 65.5 mwaka 2019. Umri wa kuishi ni kigezo muhimu katika kupima maendeleo ya watu; hivyo, ongezeko hilo linaashiria kuimarika kwa viwango vya ubora wa maendeleo ya watu. Serikali inaendelea kutekeleza mipango na mikakati madhubuti itakayohakikisha kwamba upatikanaji wa huduma za msingi kwa jamii unaendana na kasi ya ongezeko la watu.

2.3.2 Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini

Serikali imeendelea kutekeleza sera, mipango na mikakati mbalimbali ya kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya watanzania. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18, unaonesha kuwa asilimia 8.0 ya watu wa Tanzania Bara wanaishi katika umaskini wa chakula ikilinganishwa na asilimia 9.7 mwaka 2011/12. Kwa mujibu wa Utafiti huo, umaskini wa mahitaji ya msingi kwa mwaka 2017/18 ulikuwa asilimia 26.4 ikilinganishwa na asilimia 28.2 mwaka 2011/12. Vile vile, ni muhimu kutambua kuwa asilimia 81 ya watu wenye umaskini wa mahitaji ya msingi wanaishi maeneo ya vijijini, wakati asilimia 16.1 wanaishi maeneo ya mijini na asilimia 3 katika jiji la Dar es Salaam. Hivyo, Serikali inaendelea kutekeleza sera na mikakati ya kupunguza umaskini katika kuboresha maisha na ustawi wa jamii hususan katika maeneo ya vijijini.

Kielelezo Na. 2.3: Mgawanyo wa Watu Maskini




Chanzo: Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18

2.3.2.1 Umiliki wa Mali za Kudumu

Umiliki wa mali za kudumu ni moja ya kiashiria muhimu cha umaskini usio wa kipato. Umiliki wa mali husaidia kuongeza kipato cha watu maskini na kuboresha hali yao ya maisha. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18, umiliki wa mali hasa simu za mkononi, pikipiki na runinga umeongezeka. Kiwango cha kaya zinazomiliki simu za mkononi kilikuwa asilimia 78 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 57 mwaka 2011/12. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya simu hususan katika shughuli za kuzalisha kipato pamoja na kuwepo kwa huduma za fedha kwa simu za mkononi. Aidha, kaya zinazomiliki pikipiki zimeongezeka na kufikia asilimia 11 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 4.0 mwaka 2011/12. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya pikipiki katika shughuli za biashara hasusan usafirishaji wa abiria. Vile vile, umiliki wa runinga ulikuwa asilimia 24 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 16 mwaka 2011/12. Hata hivyo, matumizi ya teknolojia bora zaidi yamesababisha umiliki wa redio na simu za mezani kupungua kutoka asilimia 55 na asilimia moja (1) mwaka 2011/12 hadi asilimia 43 na asilimia 0.2 mwaka 2017/18 kwa mtiririko huo. Kwa mujibu wa takwimu hizi, kuongezeka kwa umiliki wa mali za kudumu kunategemea mchango wa mali husika katika kuongeza mapato na kuboresha maisha ya watu. Kwa kuzingatia mchango wa mali za kudumu katika kupunguza umaskini, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa watazania hususan maskini kumiliki mali hizo.

Kielelezo Na. 2.4: Kiwango cha Umiliki wa Mali za Kudumu (%)



Chanzo: Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18

2.3.2.2 Umiliki wa Akaunti za Benki

Umiliki wa akaunti za benki pamoja na kuweka akiba benki ni muhimu katika kuboresha maisha ya watu na kukuza shughuli za uchumi na biashara. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18, unaonesha kuwa kiwango cha watu wanaomiliki akaunti za benki kimeongezeka ambapo kaya zenye angalau mtu mmoja mwenye akaunti benki zimefikia asilimia 12.3 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 10 mwaka 2007. Kasi ndogo ya ongezeko la umiliki wa akaunti inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kipato kidogo cha wananchi hasa maskini na kuongezeka kwa wigo wa kuweka akiba kupitia sekta rasmi isiyo ya kibenki inayojumuisha huduma za fedha kwa simu za mkononi. Kaya za mijini zina kiwango kikubwa cha watu wenye akaunti benki ambapo asilimia 23.8 ya kaya zina angalau mtu mmoja mwenye akaunti benki. Kiwango hiki ni takribani mara nne ya kaya za vijijini ambapo asilimia 6.1 ya kaya zina angalau mtu mmoja mwenye akaunti benki. Hivyo, asilimia kubwa ya watu wanaoishi vijijini wanapata huduma za fedha kupitia mfumo wa fedha usio rasmi kama ushirika wa kuweka akiba na kukopa kwa zamu (ROSCAs). Kwa upande mwingine, kiwango cha kaya zenye angalau mtu mmoja mwenye akaunti benki zinatofautiana kimkoa ambapo mkoa wa Kigoma una kiwango kidogo cha asilimia 2.3 ikilinganishwa na mikoa yote Tanzania Bara wakati mkoa wa Dar es Salaam una kiwango kikubwa cha asilimia 31.4.

2.3.2.3 Hali ya Makazi

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18 unaonesha kuwa kuna ongezeko la kaya zinazoishi katika makazi yaliyojengwa kwa kutumia paa, kuta na sakafu za kisasa. Kaya zinazoishi kwenye makazi yaliyojengwa kwa paa za kisasa

zimeongezeka kutoka asilimia 68 mwaka 2011/12 hadi asilimia 84.1 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la nukta za asilimia 16.1. Vile vile, utafiti unaonesha kuwa kaya zinazoishi kwenye makazi yaliyojengwa kwa kuta imara zimeongezeka hadi asilimia 78.8 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 46 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la nukta za asilimia 32.8. Kaya zinazoishi kwenye makazi yaliyojengwa kwa sakafu za kisasa zimeongezeka hadi asilimia 50.1 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 40 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la nukta za asilimia 10.1.

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18 unaonesha kuwa kaya za maeneo ya vijijini zina asilimia ndogo ya makazi yaliyojengwa kwa kutumia paa, kuta na sakafu za kisasa. Makazi ya vijijini yaliyojengwa kwa kutumia paa, kuta na sakafu za kisasa ni asilimia 76.6, asilimia 70.5 na asilimia 32.1 ikilinganishwa na asilimia 97.6, asilimia 94.0 na asilimia 85.6 katika maeneo ya mjini kwa mtiririko huo.

2.3.2.4 Matumizi ya Nishati

Matumizi ya nishati ni moja ya kiashiria muhimu katika kupima umaskini wa kaya; matumizi madogo huashiria kiwango kikubwa cha umaskini na matumizi makubwa huashiria kiwango kidogo cha umaskini. Kulingana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18, asilimia 29.0 ya kaya za Tanzania bara zinatumia umeme wa TANESCO kama chanzo kikuu cha kuangazia ikifuatiwa na taa ya kurunzi/taa ya kuchaji (asilimia 27.5), umeme wa mionzi ya jua (asilimia 26.5) na vyanzo vingine (asilimia 17). Aidha, kiwango cha kaya zinazotumia umeme kwa kuangazia ni kikubwa katika maeneo ya mijini (asilimia 63.8) ikilinganishwa na maeneo ya vijijini (asilimia 10.0).

Kwa upande wa nishati ya kupikia, asilimia 60.9 ya kaya za Tanzania Bara zinatumia kuni kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia ikilinganishwa na asilimia 66.3 za kaya mwaka 2011/12. Kaya zinazotumia mkaa zimeongezeka kutoka asilimia 28.2 hadi asilimia 28.8 mwaka 2017/18. Aidha, gesi ya viwandani inatumiwa na asilimia 3.2 ya kaya, umeme asilimia 2.1, mafuta ya taa asilimia 1.3, umeme wa mionzi ya jua asilimia 1.1 na vyanzo vingine vinatumiwa na asilimia 2.5 ya kaya. Matumizi ya kuni ni makubwa zaidi maeneo ya vijijini (asilimia 84.8) ikilinganishwa na maeneo ya mjini (asilimia 17.4). Kujumla, takwimu hizi zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 89 ya kaya Tanzania Bara zinategemea kuni na mkaa kama chanzo kikuu cha nishati. Matumizi ya nishati hizi ni makubwa kutokana na kuwa zinapatikana kwa urahisi na gharama zake ni ndogo ikilinganishwa na nishati mbadala kama umeme na gesi ya viwandani. Hata hivyo, ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa unaharibu ikolojia ya misitu na kusababisha uharibifu wa

mazingira. Hivyo, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuchochea na kuibua vyanzo mbadala vya nishati vyenye gharama nafuu. Hii itachangia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 yanayohusiana na mazingira.

2.3.3 Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi

Mwaka 2019/20, Serikali ilifanya utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi mkoani Dar es Salaam kwa lengo la kubaini mchango wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa kwa kutumia makadirio ya mapato na ongezeko la thamani ya uzalishaji wa bidhaa na huduma kutoka shughuli za kilimo na zisizo za kilimo; tija katika uwekezaji; kiwango cha ukuzaji mtaji; kutambua mahali biashara zilipo; thamani ya uzalishaji kwa kila mtu; ajira na mgawanyo wake; na mahusiano kati ya Sekta Isiyo Rasmi na sekta nyingine za kiuchumi.

Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa: Mkoa wa Dar es Salaam una wamiliki wa shughuli za Sekta Isiyo Rasmi wapatao 1,023,520 ambapo asilimia 47.6 wanajihusisha na biashara ya jumla na rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki; uwekezaji wa mitaji katika sekta isiyo rasmi ni shilingi bilioni 901.5 kwa mwaka 2019; jumla ya ongezeko la thamani kwa mwaka katika bidhaa na huduma zinazozalishwa katika sekta isiyo rasmi ni shilingi trilioni 6.2; na ajira katika sekta isiyo rasmi kwa watu wenye umri wa miaka 15 au zaidi imepungua kutoka watu 1,208,250 (asilimia 61.5) mwaka 2014 hadi 1,154,336 (asilimia 55.2) mwaka 2019. Hii inatokana na juhudi kubwa za Serikali ya Awamu ya Tano katika kupanua wigo wa kujenga uchumi wa viwanda ambao matokeo yake ni kukuza upatikanaji wa kazi zenye staha (*decent work*) na kuongezeka kwa ajira katika sekta rasmi.

SURA YA TATU

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20, kwa kuelezea bajeti iliyo pangwa na kiasi cha fedha kilichotumika kwa kipindi husika. Vile vile, inaelezea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na changamoto zilizojitokeza.

3.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka 2019/20

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 ulitengewa jumla ya shilingi trilioni 12.25 sawa na asilimia 37.0 ya bajeti ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 9.74 sawa na asilimia 79.5 ya fedha za maendeleo zilikuwa fedha za ndani na shilingi trilioni 2.51 sawa na asilimia 20.5 ya fedha za maendeleo ni fedha za nje. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, jumla ya shilingi trilioni 7.63 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Fedha hizo zinajumuisha shilingi trilioni 6.65 fedha za ndani na shilingi bilioni 976.9 fedha za nje. Aidha, kiasi cha shilingi trilioni 1.28 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilielekezwa moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo bila kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Miradi ya maendeleo iliyopokea fedha katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020 ni pamoja na ifuatayo:

- (a) Shilingi trilioni 2.44 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya barabara, reli na viwanja vya ndege;
- (b) Shilingi bilioni 467.89 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, uimarishaji wa vyuo vya VETA na kukuza ujuzi kwa vijana;
- (c) Shilingi bilioni 346.01 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini;
- (d) Ununuzi wa ndege na uimarishaji wa Shirika la Ndege Tanzania shilingi bilioni 315.20;
- (e) Shilingi bilioni 356.72 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji;
- (f) Shilingi bilioni 280.95 kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu na huduma za umeme mijini na vijijini; na
- (g) Shilingi bilioni 211.28 kwa ajili ya elimumsingi bila ada.

3.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

3.3.1 Miradi ya Kielelezo

Utekelezaji wa baadhi ya miradi mikubwa ya kielelezo hadi Januari 2020 ulikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Reli ya Kati ya *Standard Gauge*

Ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 76.63 na kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 28. Aidha, jitihada za utafutaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora (km 294), Tabora – Isaka (km 133), Isaka – Mwanza (km 249), Isaka – Rusumo (km 371), Tabora – Kigoma (km 411), Keza - Ruvubu (km 36), Kaliua – Mpanda hadi Karema (km 321) zinaendelea.

Aidha, faida za mradi zilizopatikana ni pamoja na: ajira kwa Watanzania takribani 13,117; ushiriki wa wakandarasi na wazabuni wa ndani 640 ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 664.70 zimetolewa kwa wazabuni wa ndani na kuongeza ushiriki wa viwanda na wajasiriamali wa ndani. Vile vile, ujenzi wa reli ya *standard gauge* unakadiriwa kutumia mifuko ya saruji milioni 9 na nondo za madaraja kilogramu milioni 115 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Makutupora na hivyo kuzalisha ajira zisizo za moja kwa moja kwa wananchi.

(b) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania

Hatua iliyofikiwa ni: kupokelewa kwa ndege mbili (2) ambazo ni Boeing 787-8 Dreamliner na Bombardier Dash 8 Q400; kufanyika kwa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege mpya tatu (3) ambapo mbili (2) ni aina ya Airbus A220-300 na moja (1) ni aina ya De Havilland Dash 8-400. Aidha, Serikali imegharamia mafunzo ya marubani (110), wahandisi (127) na wahudumu (125), kulipa bima za ndege na gharama za awali za kuendesha ndege tatu zilizopokelewa, ukarabati wa karakana ya ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) hususan katika mfumo wa umeme, mfumo wa kupambana na majanga ya moto na ufungaji wa jenereta na kukamilika kwa ukarabati wa jengo la karakana ya matengenezo ya ndege. Vile vile, Shirika limeongeza idadi ya vituo vya safari za ndani kufikia 13 na nje kufikia vituo sita (6) ambavyo ni Hahaya (Comoro), Entebbe (Uganda), Bujumbura (Burundi), Mumbai (India), Lusaka (Zambia) na Harare (Zimbabwe). Ufufuaji wa Shirika la Ndege Tanzania umezalisha ajira 436 za moja kwa moja.

(c) Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115

Hatua iliyofikiwa ni: kuanza ujenzi wa bwawa (main dam); kuendelea na ujenzi wa handaki la kuchepusha maji (diversion tunnel); kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu wezeshi ikijumuisha: njia ya kusafirisha umeme; barabara kwa kiwango cha changarawe; mifumo ya maji; mawasiliano ya simu; na nyumba za kuishi wakandarasi. Kazi zingine zinazoendelea ni maandalizi ya mgodi wa kufua umeme, njia za maji kwenda kwenye mitambo na ununuzi ya vifaa mbalimbali vya mradi. Utekelezaji wa mradi umeajiri jumla ya wafanyakazi wapatao 3,897 ambapo kati ya wafanyakazi hao watanzania ni 3,422 sawa na asilimia 87.81 na wafanyakazi kutoka nje ya nchi ni 475 sawa na asilimia 12.19 ya wafanyakazi wote wa mradi. Aidha, inakadiriwa kuwa hadi kukamilika kwa Mradi Watanzania 6,000 wataajiriwa katika shughuli za Mradi.

(d) Kanda Maalum za Kiuchumi

(i) Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo

Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa uwekezaji wa viwanda 11 (*Seif Tobacco Trade Limited, Fujian Hexingwang Industry Company Limited, Siparcoci International Limited, Hua Teng Metalurgical Company Limited, Wegmar Paking Limited, Jambo Food Products Limited, Phiss Tannery Limited, Tube Limited, Ramky Tanzania Limited, Tanfroz Limited, na Africa Dragon Enterprises Limited*). Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) ambavyo ni *Africa Dragon Enterprises Limited na Phiss Tannery Limited* vimeanza uzalishaji na kuzalisha ajira za moja kwa moja 120 na ujenzi wa viwanda tisa (9) unaendelea. Vile vile, andiko la uendelezaji na makisio ya gharama za kuweka miundombinu wezeshi katika eneo lililolipiwa fidia limekamilika.

(ii) Eneo Maalum la Uwekezaji Kigoma

Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu na Mpango Kabambe (Master Plan) wa uendelezaji wa eneo na ugawaji wa viwanja kwa ajili ya kupewa wawekezaji; kujenga barabara katika eneo la mradi zenye jumla ya km 28.46 na kuweka alama za mipaka 106; kupatikana kwa wawekezaji watatu watakojenga mitambo ya kuzalisha umeme wa jua (Next Gen Solowazi Limited), kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki (Third Man Limited) na kiwanda cha kuchakata zao la michikichi na ghala (SGC Investment Limited).

(iii) Eneo Maalum la Uwekezaji la Ukanda Huru wa Bandari ya Mtwara

Kazi zilizotekelezwa ni kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara za ndani ya eneo la mradi yenye urefu wa kilomita tatu.

- (e) **Kuongeza Rasilimali Watu Wenye Ujuzi Adimu na Maalumu kwa Maendeleo ya Viwanda na Watu:**
- (i) **Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:** hadi Machi 2020, hatua iliyofikiwa ni kutolewa kwa mafunzo katika nyanja mbalimbali za ubingwa na ubobezi, ambapo jumla ya watumishi 550 wameendelea kulipiwa gharama za masomo ya uzamili (postgraduate studies) katika vyuo vikuu vya ndani (531) na nje ya nchi (19). Vile vile, jumla ya wataalam bingwa 137 walihitimu mafunzo ya shahada ya uzamili kwa ufadhili wa Serikali ikilinganishwa na wataalam bingwa 82 ambao walihitimu mafunzo hayo mwaka 2018.
 - (ii) **Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea kugharamia mafunzo kwa wanafunzi 72 wa Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Mionzi (Bachelor of Science in Radiation Therapy Technology) na wanafunzi 32 wa Shahada ya Uzamili ya Onkolojia (Masters of Medicine in Clinical Oncology) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili. Mafunzo haya yameongeza uwepo wa wataalam wa huduma za saratani hapa nchini ambapo Taasisi ina madaktari bingwa wa Onkolojia 30, ikilinganishwa na madaktari bingwa 13 waliokuwepo mwaka 2015.
 - (iii) **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea kudhamini mafunzo kwa wanafunzi madaktari 158 ndani na nje ya nchi katika fani za ubobezi kwa magonjwa ya damu na utoaji damu (1), Magonjwa ya utumbo na ini (2), upasuaji wa utumbo na ini (3), Magonjwa ya figo (1), magonjwa ya kifua (1), udaktari bingwa (102), ufamasia (6), uuguzi (14), afya ya jamii na mazingira, menejimenti na taarifa za afya (28);
 - (iv) **Hospitali ya Taifa ya Muhimbili:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea kudhamini mafunzo ya shahada za uzamili katika tiba kwa wataalam ambapo jumla ya wataalam 81 wapo masomoni kati ya hao madaktari 27 wapo nje ya nchi kwa ajili ya kupata mafunzo katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma za ICU, magonjwa ya kinamama, huduma za masikio, pua na koo. Aidha, Hospitali imepeleka timu ya wataalamu 11 katika mafunzo ya mwezi mmoja nchini India kwa ajili ya kupata utaalamu wa huduma za kupandikiza uloto (bone marrow transplant) ambayo ilianza kutolewa Mei, 2020;
 - (v) **Hospitali ya Mloganzila:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na udhamini wa mafunzo ya shahada ya uzamili katika tiba kwa wataalam 45 ambao wapo masomoni. Vile vile, hospitali kwa kushirikiana na Korea

Foundation for International Healthcare (KOFIH) na Vyuo Vikuu vya Afya vya nchini Korea imeweza kufadhili watumishi 7 kwenda nchini Korea kwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Aidha, Hospitali imeendelea kushirikiana na wataalamu kutoka Korea katika kuwajengea uwezo wataalamu wa hapa nchini na hasa katika Hospitali ya Mloganzila, katika maeneo ya magonjwa ya kina mama pamoja na Upasuaji wa Ubongo (NeuroSurgery);

- (vi) **Wizara ya Nishati:** hatua iliyofikiwa kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Aprili, 2020 ni kugharamiwa kwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 55 katika fani za mafuta na gesi; na
- (vii) **Wizara ya Madini:** hatua iliyofikiwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, ni kupatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi 16 wa Wizara ndani na nje ya nchi.

(f) Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi

- (i) **Shamba la Mkulazi I:** Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa utafiti wa udongo na tathmini ya athari ya kimazingira (Environmental Impact Assessment); kuendelea kwa matayarisho ya kitalu nyumba na kukamilika kwa usanifu wa mfumo wa umwagiliaji katika hekta 150.
- (ii) **Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mbigiri - Mkulazi II:** Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa mfumo wa umwagiliaji katika hekta 300; kukamilika ufungaji wa mabomba makubwa yenye urefu wa mita 700 na madogo yenye urefu wa mita 92,400 katika hekta 150; kuanza kwa vitalu nyumba vya mbegu aina 11 katika hekta 38; kukamilika kwa maandalizi ya eneo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda na barabara yenye kilometa 1.36 ya kuelekea kiwandani na kulimwa kwa hekta 1,400 ambapo hekta 1,108 zimepandwa miwa.

(g) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia - LNG

Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kuendelea kwa tafiti za namna ya kuzalisha na kusafirisha gesi kutoka bahari kuu hadi eneo la mradi; kuendelea na majadiliano ya Mikataba Hodhi baina ya Serikali na Kampuni za utafutaji na uendelezaji zitakazotekeleza mradi na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi katika mkoa wa Lindi.

(h) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa Tathmini ya Athari za Mazingira; na

kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa maeneo ya pembezoni mwa eneo la mradi.

(i) Makaa ya Mawe Mchuchuma na Vanadium, Titanium na Chuma Liganga

Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa uhakiki wa mali za wananchi watakaopisha ujenzi wa miradi hiyo ambapo kiasi cha shilingi bilioni 11.04 kinatarajiwa kulipwa kama fidia kwa wananchi 1,145 kwa maeneo yote ya miradi. Aidha, upitiaji mikataba kati ya NDC na mwekezaji unaendelea; na kulipwa kwa ada za leseni za kuchimba madini (*Primary Mining Licence - PML*) katika maeneo yaliyo chini ya NDC katika eneo la mradi.

3.3.2 Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

3.3.2.1 Viwanda

(a) Shirika la Viwanda Vidogo - SIDO

Kazi zilizotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa ofisi nne (4) za Simiyu, Katavi, Geita na Chato; na ujenzi wa majengo ya viwanda (*Industrial Shades*) kumi na mbili (12) katika mitaa ya viwanda ya SIDO iliyopo mikoa ya Dodoma (3), Manyara (3), Kagera (1), Mtwara (1) na Geita (4) ambapo mitambo 29 ya viwanda imefungwa katika majengo hayo na kutoa ajira 648. Aidha, SIDO ilitoa mikopo 16,954 yenye thamani ya shilingi bilioni 25.29 kwa wajasiriamali, ambapo asilimia 52 ya mikopo ilitolewa kwa wanawake na asilimia 48 kwa wanaume. Aidha, asilimia 38 ya mikopo hiyo ilitolewa kwa maeneo ya vijijini na asilimia 62 maeneo ya mijini. Vile vile, miradi iliyoanzishwa kupitia mikopo hiyo imechangia kutoa jumla ya ajira 40,998, kati ya ajira hizo asilimia 54 ni kwa wanawake na asilimia 46 kwa wanaume.

(b) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)

Kazi zilizotekelezwa ni: kubuniwa, kutengenezwa na kufanyiwa majaribio ya awali mashine za kubangua korosho zinazoendeshwa kwa kutumia miguu ambapo jumla ya mashine 36 zimetengenezwa; kubuni na kutengeneza mashine ya kubangua na kutenganisha mbegu za chikichi; kufanya utafiti wa awali uliosaidia kutengeneza mashine ya kuvunja na kutenganisha maganda ya chikichi inayoendeshwa kwa mkono; na kubuni njia rahisi ya kuzifanya mbegu za pamba zenye manyoya kutumika kwa urahisi katika kipandio cha ng'ombe bila kukwama.

(c) Kuendeleza Kongane ya Viwanda TAMCO - Kibaha

Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa asilimia 98 ya ujenzi wa barabara ya urefu wa mita 580 kwa kiwango cha lami; kupatikana kwa Mtaalamu Mwelekezi kwa ajili

ya usanifu wa ujenzi wa kituo cha umeme; na kuendelea na maandalizi ya Mpango Kabambe wa kuendeleza eneo la ekari 201.6 ili kuvutia uwekezaji.

(d) Mradi wa Magadi Soda - Bonde la Engaruka, Arusha

Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa uthaminishaji na uhakiki wa ardhi na mali za wananchi; kuendelea kufanya *Techno-Economic Study* inayojumuisha upembuzi yakinifu katika eneo la Magadi Soda, Tathmini ya Athari za Kimazingira (EIA) na Utafiti wa masoko ya Magadi Soda na kuendelea kutangaza mradi ili kuvutia wawekezaji.

(e) Mradi wa Kuunganisha Matrika TAMCO - Kibaha

Kazi zilizofanyika ni: kuendelea na ujenzi wa kiwanda kipya cha kuunganisha Matrika ambapo ujenzi wa jengo la kiwanda umekamilika. Aidha, matrika 822 kati ya 2,400 aina ya URSUS yameingizwa nchini kutoka Poland yakiwa katika vipande (semi *knocked down*) ambapo matrika 736 yameuzwa, kati ya hayo, 681 yameuzwa kwa mkopo na 55 kwa fedha taslimu.

(f) Kongane ya Viwanda vya Ngozi (Zuzu - Dodoma)

Hatua iliyofikiwa katika kuendeleza ekari 107 ni kusafisha eneo na kuandaa usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na majengo ya viwanda na kuendelea na uvutaji wa umeme na maji umekamilika, Ujenzi wa msingi wa jengo unaendelea.

(g) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuendelea na kazi za utafiti wa teknolojia za ubanguaji korosho na usindikaji wa michikichi; na kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya tafiti mbalimbali.

(h) Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO)

Kazi zilizofanyika ni: kubuni na kutengeneza chasili cha mtambo wa kukausha mazao, kubuni na kutengeneza chasili cha kutengeneza brikwiti kutokana na vumbi la makaa ya mawe kwa ajili ya kupata teknolojia bora ya nishati na yenye gharama nafuu katika kukausha korosho; na kuimarisha maabara za utafiti kwa kununua mitambo na vifaa vya kisasa. Aidha, TEMDO imeweza kupata mtambo mdogo wa kuchakata mafuta ya mawese tani 1.25 kwa siku ili kutumika kudurufu mitambo mingine kama huo.

(i) Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools (KMTC)

Kazi zilizotekelezwa ni kuzalishwa kwa matrela arobaini (40) kwa ajili ya matrika ya URSUS, mashine za kuchakata mbao, kukoboa na kusaga nafaka, pampu za maji,

pamoja na vipuri vyake.

(j) Kuendeleza Shirika la Nyumbu - Kibaha

Shughuli zilizotekelezwa ni: kufanyika kwa utafiti na uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali; kuunganisha magari mawili ya zimamoto; kutengeneza vipuri vya mitambo mbalimbali kwa ajili ya matumizi katika sekta za kilimo, usafirishaji, madini na maji; kutengeneza terminal traillers tano kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA); na Brake blocks kwa ajili ya matumizi ya Shirika la Reli Tanzania.

3.3.2.2 Kilimo

(a) Kilimo cha Kahawa

Hatua iliyofikiwa ni: uzalishaji wa kahawa tani 55,979 ambapo kahawa aina ya robusta ni tani 22,320, arabica laini tani 32,057 na arabica ngumu tani 1,602; kuzalishwa kwa miche 3,692,780; kutolewa mafunzo kwa wakulima 62,523, Maafisa Ugani 58, na Wakulima Viongozi; kuuzwa kwa tani 21,929 zenye thamani ya dola za Marekani 47,666,919 katika minada 17 ya Kanda; kuuzwa kwa tani 25,574 zenye thamani ya dola za Marekani 39,860,860 kupitia soko la moja kwa moja; kutolewa kwa mikopo ya mbolea kupitia viwanda vya kukoboa kahawa na taasisi za fedha ambapo wakulima wadogo 286,297 na wakubwa 101 walisajiliwa sawa na asilimia 89.5 kwa wadogo na asilimia 100 kwa wakubwa; uhamasishaji wa matumizi ya *Central Pulpuly Unit - CPU* katika kuchakata kahawa aina ya arabica; uboreshwaji wa maabara za kahawa kwa kununua vifaa vya kisasa; utolewaji wa mafunzo kwa wanafunzi 50 wa cheti cha ubora wa kahawa na biashara (CQT) katika Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU). Aidha, Bodi imesajili wakulima 305,260 wakiwemo wakulima wadogo 305,159 na Wakulima wakubwa 101. Usajili huo ni sawa na asilimia 67.82 kwa wakulima wadogo na asilimia 100 kwa wakubwa.

Kazi nyingine zilizotekelezwa ni: kuandaliwa kwa maonesho ya uhamasishaji wa unywaji wa kahawa katika nchi za Afrika, na kushiriki Maonesho ya Kimataifa ya Kahawa Tokyo - Japani (SCAJ 2019) yaliyowezesha kuongezeka kwa wanunuzi wawili (2) wakubwa wa kahawa ya Tanzania; na kukamilika kwa mapitio ya vigezo vya utoaji wa vibali vya ufungashaji kahawa ili kuongeza thamani ya bidhaa za kahawa kwa ajili ya soko la ndani.

(b) Kilimo cha Chai

Hatua iliyofikiwa ni: kuongezeka kwa uzalishaji wa chai kavu kufikia tani 11,185 kati ya hizo, wakulima wadogo wa chai wamezalisha tani 4,811, ambapo tija kwa wakulima wadogo ilikuwa kilo 415 za chai kavu kwa hekta na wakulima wakubwa

kilo 522 kwa hekta; kuongezeka kwa wastani wa ubora wa majani mabichi kutoka 50 hadi kufikia asilimia 60 kutokana na ukaguzi na uhamasishaji; kuandaliwa kwa mikakati ya kuanzisha kituo cha pamoja cha wadau wa sekta ndogo ya chai kwa lengo la kupunguza gharama na muda; Vilevile, uhamasishaji wa unywaji wa chai umeendelea, ambapo hadi Machi 2020, chai iliyochanganywa na kufungwa kwenye vikasha ilikuwa tani 2,700 sawa na unywaji wa gramu 65 kwa mtu kwa mwaka. Mauzo ya chai kavu nje ya nchi; tani 11,270 yenye thamani ya Dola za Marekani 15,877,037 na usajili wa wakulima 31,092 sawa na asilimia 69 ya lengo.

Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA) kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Njombe, Rungwe na vikundi vya wakulima wamefanya yafuatayo; imezalisha miche bora ya chai 3,998,000 na kusambaza kwa wakulima; na kutunzwa vitalu vyenye miche 9,910,000.

(c) Kilimo cha Tumbaku

Hatua iliyofikiwa ni: kuuzwa kwa tani 70,824.21 za tumbaku zenye thamani ya shilingi 231,694,899,410; kufanyika majaribio kwa aina nne (4) za mbegu za tumbaku ya mvuke kutoka nchini China; kusajiliwa kwa wakulima 53,758 wa tumbaku sawa asilimia 116.87; kupatikana kwa wanunuzi wapya wanne (4) wa tumbaku ambao ni kampuni za Grand Tobacco Co Ltd, Magefa Growers Ltd, Petrobena East Africa Ltd, na Pachetc Co Ltd; kukaguliwa na kusajiliwa kwa vituo 1,578 vya kuchambua na kufungasha tumbaku na vituo 632 vya kuuzia tumbaku; kutolewa mafunzo ya kilimo bora cha tumbaku kwa wakulima 50,000; kufanyika maandalizi ya awali ya ujenzi wa kiwanda kipya katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ambacho kitajengwa kwa ushirikiano kati ya wakulima na Serikali. Hatua hizi zimepelekea kuimarika kwa ubora wa tumbaku ambapo tumbaku isiyo na dosari ni asilimia 93 na yenye dosari ni asilimia.

(d) Kilimo cha Miwa

Shughuli zilizofanyika ni: hadi Aprili, 2020 uzalishaji wa Sukari ni tani 298,948.61 sawa na asilimia 86 ya lengo; mafunzo ya kilimo bora cha miwa kwa maafisa ugani 17 kutoka Mbigiri (Mkulazi) na Dabalo (Chamwino); TEMDO imetengeneza “hot water treatment plant” itakayoweza wakulima wadogo kupata mbegu bora; imesajili wakulima wa miwa 6,745 sawa na asilimia 92.92 ya lengo; imetoa vitambulisho 5,488 kwa wakulima. Vilevile, kuongeza eneo la kuzalisha miwa; Bagamoyo Sugar Co. Ltd (hekta 2,280), Kagera Sugar Co. Ltd (hekta 2,300), TPC (hekta 400) na Mkulazi II (hekta 1,500).

(e) Kilimo cha Mpunga

Shughuli zilizofanyika ni; uzalishaji wa zao la mpunga tani 3,174,766; upatikanaji wa mbegu bora za mpunga ulikuwa tani 614.66; ukarabati kinu cha kukoboa mpunga chenye uwezo wa tani 3.5 katika kijiji cha Madibira - Mbarali; na imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza zao la Mpunga Awamu ya Pili - NRDS II (2019/20 - 2029/30). Vile vile, mafunzo kwa wakulima 1,463 (wanawake 835 na wanaume 628) kuhusu matumizi ya pembejeo na kilimo shadidi; kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya Wakala wa Mbegu za Kilimo; na utoaji mafunzo kwa maafisa ugani 66 kuhusu uzalishaji wa mbegu na kulinda ubora na teknolojia ya uzalishaji mpunga.

(f) Kilimo cha Korosho

Hatua iliyofikiwa ni: uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2019/20 ni tani 232,527.55 ikilinganishwa na tani 224,552 za msimu wa 2018/2019; TARI Naliendele kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya zinazolima zao la korosho pamoja na wazalishaji binafsi imezalisha tani 111.2 na imesambaza tani 81.97 za mbegu bora za korosho; TARI Naliendele imezalisha miche bora ya korosho 51,438 na kusambaza miche 38,338; tani 19,631 za Salfa ya Unga na lita 280,201 za viuatilifu vya maji zimesambaza; mafunzo kwa wakulima 364 na Maafisa ugani 352 juu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu vya zao la korosho; mafunzo ya kudhibiti ubora wa korosho ghafi kwa wataalam 62 wa udhibiti ubora katika maghala ya mnada na watendaji wa AMCOS 1,102. Vilevile, Bodi ya Korosho imesajili wakulima 309,006 sawa na asilimia 97.05 ya lengo.

(g) Kilimo cha Pamba

Hatua zilizofikiwa ni: upatikanaji wa mbegu bora za pamba UKM 08 umefikia tani 35,000 kwa mbegu zenye manyoya; imesambaza tani 17,942 sawa na asilimia 90 ya lengo; imesambaza viudadudu lita 6,070,000 sawa na asilimia 86.7; na imesambaza lita 7,000,000. Pia vinyunyizi 23,000,000 vilisambazwa sawa na asilimia 115 ya lengo.

Hatua zilizofikiwa; uzalishaji ni tani 352,405.29 sawa na asilimia 78 ya lengo; tani 352,405.29 zenye thamani ya Shilingi 422,900,000,000 zimekusanywa; kati ya hizo tani 348,726.62 zenye thamani ya Shilingi 418,700,000,000 zimenunuliwa kwa bei ya Shilingi 1,200 kwa kilo; tija kwa mkulima kutoka wastani wa tani 250 hadi 316 kwa hekta; kuongezeka kwa daraja la Gany ya juu kutoka asilimia 43 hadi asilimia 45; imesajili wakulima 556,306 sawa na asilimia 98.81 ya lengo; na leseni za ununuzi wa pamba katika msimu wa mwaka 2019/20 kwa Kampuni 25 zimetolewa.

(h) Kilimo cha Mkonge

Hatua zilizofikiwa; uzalishaji wa mkonge ulifikia tani 35,551.86; uzalishaji wa bidhaa za mkonge ulifikia tani 5,701; mauzo ya mkonge ndani ya nchi ni tani 12,673.96 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 37 na mauzo nje ya nchi ni tani 21,043.95 yenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 34.75. Pia, bidhaa za mkonge zilizouzwa ndani ya nchi ni tani 2,214.77 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 8.78 na bidhaa zilizouzwa nje ya nchi ni tani 3,146 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 6.56. Vilevile, hekta 5,529.50 zimepandwa mkonge mpya; wakulima wadogo wa mkonge 2,365 na wakulima wakubwa 22 sawa na asilimia 30.9 kwa wakulima wadogo na asilimia 100 kwa wakubwa wamesajiliwa; na ajira 129,022 kupitia mashamba na viwanda vya mkonge.

(i) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji

Hatua iliyofikiwa ni: ukarabati na uboreshaji wa miundombinu katika skimu 21 za umwagiliaji. Skimu tisa (9) zimekamilika ambazo ni Soko (hekta 285) - Moshi DC; Kituani Mwenzae (hekta 180) na Kwemugiriti (Hekta 250) - Lushoto DC; Katela Ntaba (hekta 250), - Busokelo DC; Ngongowe (hekta-250) na Nanganga (hekta 300) - Ruangwa DC; Mwalunili (Hekta 630) - Igunga DC na Ngage (Hekta 402) - Simajiro DC. Skimu saba za umwagiliaji (7) zimefikia wastani wa asilimia 78 na ukarabati wa skimu 5 umefikia asilimia 51.

Eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 461,326 mwaka 2015/2016 hadi hekta 694,715 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 33.6; tija ya uzalishaji imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 - 2.0 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi kufikia wastani wa tani 4.0 - 5.0 kwa hekta 2019/20 kwa zao la mpunga; tani 1.5 kwa hekta mwaka 2015/16 hadi tani 3.7- 5.0 kwa hekta mwaka 2019/20 kwa zao la mahindi; tani 13 kwa hekta mwaka 2015/16 hadi 26 kwa hekta mwaka 2019/20 kwa hekta kwa zao la vitunguu na tani 5 kwa hekta mwaka 2015/16 hadi tani 18 kwa hekta mwaka 2019/20 kwa zao la nyanya.

(j) Ujenzi wa Maghala na Kuboresha Hifadhi ya Taifa ya Chakula

Kupitia Mradi wa ERPP, Wizara inakamilisha ujenzi wa ghala tano (5) za kuhifadhi mpunga na hatua iliyofikiwa ni: Msolwa Ujamaa (1,700 MT) asilimia 82, Njage (1,700 MT) asilimia 87, Mvumi (1,300 MT) asilimia 99, Kigugu (1,000 MT) asilimia 80 na Mbogo Komtonga (1,000 MT) asilimia 70. Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi mazao hatua iliyofikiwa ni: asilimia 60.5 ya utekelezaji, ambapo katika maeneo ya Songea, Makambako, Mbozi, Dodoma na Shinyanga umefikia asilimia 79 na ujenzi katika maeneo ya Mpanda, Sumbawanga na Babati umefikia asilimia 59. Awamu ya kwanza ya mradi huu inatarajiwa kukamilika Agosti, 2020 ambapo Wakala

utaongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 251,000 za sasa hadi kufikia tani 501,000.

(k) Upatikanaji Pembejeo za Kilimo

Hatua iliyofikiwa ni: tani 633,197 za mbolea zimepatikana; viwanda vinavyotengeneza mbolea na visaidizi vya mbolea (fertilizer supplement) vifikia 13 kati ya viwanda hivyo, viwili (2) ni vya visaidizi na 11 ni vya mbolea; tani 16,869.10 za viuatilifu. Vile vile, imesambaza lita 22,628 za kiuatilifu aina ya Duduba katika mikoa 7 na lita 146.5 za Methyl Euganol katika Mikoa nane (8) kwa ajili ya kudhibiti Viwavijeshi Vamizi na Nzi wa matunda. Vile vile, Wizara imesambaza tani 3,011.21 za viuadudu (insecticides), tani 3,232.38 za vizuiakuvu (fungicides), tani 2,314.654 za viuagugu (herbicides) na tani 161.287 za viuatilifu vingine kwa ajili ya kudhibiti panya na minyoo.

(l) Utafiti wa Kilimo

Hatua iliyofikiwa ni: kugunduliwa kwa aina 22 za mbegu bora za mazao (muhogo (9), alizeti (2), mahindi (2), mpunga (2), ulezi (1) na viazi vitamu (6)). Mbegu zilizogunduliwa zinatarajiwa kuongeza uzalishaji ambapo: mbegu za muhogo zina sifa za kustahilimili ugonjwa wa michirizi kahawia na batobato na zinatoa mavuno kati ya tani 25 hadi 30 kwa hekta; mbegu za alizeti zina kiwango kikubwa cha mafuta ukilinganisha na mbegu zilizopo sokoni hivi sasa; mbegu za viazi vitamu zina virutubishi vya vitamin A; mbegu za mpunga zinatoa mavuno kati ya tani 7.3 hadi 7.9 kwa hekta; na mbegu za mahindi zinatoa mavuno kati ya tani 7 hadi 10 kwa hekta na zina ukinzani dhidi ya ugonjwa wa Maize Streak na Turcium Blight virus. Shughuli nyingine ni kuzalishwa kwa tani 940.94 za mbegu bora za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta (mbegu mama tani 228.2, mbegu za awali tani 521.75, mbegu za msingi tani 59.656 na mbegu zilizothibitishwa tani 131.332). Vile vile, jumla ya watumishi 84 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali chini ya ufadhili wa wadau mbalimbali wa maendeleo. Kati yao, 34 ni wa shahada ya uzamivu, 23 shaada ya uzamili, 26 shahada ya kwanza na mmoja (1) stashahada.

(m) Miundombinu ya Utafiti wa Kilimo

Hatua iliyofikiwa ni: imekarabati maabara mbili (2) za kusindika mvinyo katika kituo cha utafiti Makutupora na maabara ya tissue culture ya kituo cha Tengeru; Wizara imeingia mkataba na Wakala wa Majengo (Tanzania Building Agency) kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu na Ofisi za Kituo cha Utafiti wa Michikichi TARI Kihinga. usanifu wa majengo na makadirio ya ujenzi (Bill of Quantities-BOQ) wa ofisi hizo umeandaliwa; makubaliano na Wakala wa Majengo Dodoma, kwa ajili

ya ukarabati wa ofisi ya kituo cha TARI Bwanga na nyumba tatu (3; makadirio ya gharama ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika vituo vya Ilonga, Naliendele, Ukiriguru na miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika vituo vya Uyole, Ilonga na Selian yameandaliwa; na mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 84.

(n) Uzalishaji wa Mbegu Bora za Mazao

Hatua iliyofikiwa ni: upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani tani 76,725.52; ambapo uzalishaji wa ndani wa mbegu bora umefikia tani 69,173.17; Vile vile, uzalishaji wa miche umefikia miche 25,285,859 mwaka 2019/20; na eneo linalolimwa mbegu limeongezeka kufikia hekta 94,368; TARI kwa kushirikiana na FELISA, Ndugu Development Foundation na Yangu Macho imezalisha jumla ya mbegu 1,791,768 za michikichi na kuzisambaza kwa ASA, Magereza ya Kwitanga na Ilagala, JKT-Bulombola na Halmashauri sita (6); kuzalishwa kwa vikonyo 1,649,379 ya viazi vitamu na pingili 4,064,620 za muhogo; kuongeza uzalishaji kupitia makampuni binafsi kwenye ardhi ya ASA kutoka tani 2584.8 kufikia tani 3037.47; kuoteshwa kwa mbegu 61,384 za michikichi; kuzalisha vipando bora vya muhogo pingili 7,000,000; na ununuzi wa zana mpya zikiwemo trekta 3 (trekta 2 za HP 95 na moja la HP 125), mashine 2 za kupanda, majembe mawili, mashine 3 za kunyunyiza dawa na mashine ya kulainisha udongo.

(o) Huduma za Upimaji wa Matabaka na Ubora wa Udongo

Hatua iliyofikiwa ni: Wizara imeandaa rasimu ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo wa miaka 15 (2020/21 - 2035/36; imehakiki mashamba 43 ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta 124,924.13 katika Mkoa wa Tanga na kubaini kuwa hekta 27,007 hazijaendelezwa; TARI kwa kushirikiana na Kampuni ya Yara na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeendelea kudhibiti tindikali kwenye udongo ulioathirika kwa kutumia teknolojia ya chokaa katika vijiji 36 vya Wilaya ya Mbozi-Songwe; kiwango cha tindikali kimepungua kutoka 4.2 kufikia kiwango cha 5.4 hadi 6.4 na tija imeongezeka katika zao la mahindi kutoka wastani wa magunia nane (8) hadi magunia 18 kwa ekari. Vilevile, TARI imepima udongo na kutoa mapendekezo ya viwango vya matumizi bora ya mbolea katika uzalishaji wa viazi mviringo katika wilaya za Makete, Rungwe, Mbeya, Mbozi, Wanging'ombe, Halmashauri ya Mji Njombe, Halmashauri ya wilaya ya Njombe, Mufindi, Kilolo na Busokelo. Wizara imepima maeneo ya Vituo vidogo vya Mbimba na Milundikwa na kutoa ekari 50 (Mbimba) na ekari 1,000 (Mlindukwa) kwa ajili ya kupewa wananchi kwa matumizi ya kijamii.

(p) Huduma za Ushauri Kuhusu Utafiti, Mafunzo na Usambazaji Taarifa za Kilimo na Sayansi Shirikishi

Hatua iliyofikiwa ni: Wizara imesambaza teknolojia za kilimo kupitia maonesho ya kilimo Nanenane yaliyofanyika kitaifa mkoani Simiyu katika Uwanja wa Nyakabindi pamoja na Kanda saba (7) za maonesho; elimu kuhusu upatikanaji wa mtaji, kanuni bora za uzalishaji, matumizi sahihi ya pembejeo, zana bora za kilimo, kuongeza thamani mazao ya kilimo na upatikanaji wa masoko ilitolewa kwa wadau wa kilimo 1,283; kupitia maonesho hayo, wakulima 1,950 walipatiwa elimu ya matumizi bora ya ardhi, maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani; washiriki 593 (me 403 na ke 190) walifanyiwa tathmini ya hali ya lishe kwa kutumia Uwiano wa Uzito na Urefu (BMI) ambapo watu 305 (51.4%) walibainika kuwa na uzito uliopitiliza.

(q) Mkakati wa Uzalishaji wa zao la Michikichi

Hatua iliyofikiwa ni: Wizara kupitia TARI, ASA, Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza, Sekretarieti za Mikoa na Sekta Binafsi imezalisha mbegu bora 1,775,200 za michikichi; ASA imezalisha miche 9,000 ya michikichi na kuisambaza kwa wakulima; imehamasisha kilimo cha zao la michikichi katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Mbeya na Morogoro.

(r) Soko la Bidhaa (Tanzania Mercantile Exchange –TMX)

Katika kuhakikisha ufanisi wa mfumo wa mauzo wa mazao ya kilimo kupitia Soko la Bidhaa, kuanzia Julai hadi Agosti 2019, Soko la Bidhaa Tanzania lilifanikiwa kufanya mauzo ya zao la ufuta kwa majaribio katika mikoa ya Dodoma (Kondoa) na Manyara (Babati) kwa njia ya kidigitali ambapo wakulima walilipwa takriban shilingi 3,500 kwa kilo ikilinganishwa na shilingi 1,500 kwa kilo iliyokuwa ikilipwa kabla ya mfumo wa mauzo kwa njia ya mtandao – OTS. Kupitia mfumo huo, wakulima wa Kondoa na Babati walilipwa shilingi milioni 1,405.26 na Halmashauri za Kondoa na Babati zilikusanya mapato ya shilingi 27,645,968.00 kutokana na mauzo ya zao la ufuta ikilinganishwa na shilingi 4,936,780.00 kabla ya mfumo huo.

Katika mwaka 2019/20, TMX ilifanya uhamasishaji kwa viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika na Wakulima 3,200 katika Halmashauri za Wilaya za Bukoba Vijijini, Bukoba Manispaa, Missenyi, Karagwe, Kyerwa, Ngara, Biharamulo na Muleba. Aidha, TMX imeanza maandalizi ya kuuza korosho kupitia mfumo wa OTS katika msimu wa mwaka 2019/20 ambapo imetoa mafunzo kwa wadau wa zao la korosho katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Ruvuma na Tanga. Vile vile, maandalizi ya majaribio ya kuuza pamba iliyochakatwa kwa maana ya nyuzi na mbegu yameanza kufanyika ambapo AMCOS 106 zilipewa mafunzo wakiwemo

viongozi na wakulima 730 kutoka Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) na Chama cha Msingi Ordoy Babati, Manyara.

3.3.2.3 Mifugo

(i) Kuimarisha Vituo vya Uhimilishaji Kitaifa na Kanda:

Kazi zilizotekelezwa ni: kununua mitungi 20 ya kuhifadhi kimiminika cha hewa baridi ya naitrojeni yenye ujazo wa lita 35 kila mmoja na kusambaza lita 7,441.25 za kimiminika baridi cha Naitrojeni; kununuliwa kwa chupa 10,000 za homoni na kusambazwa katika vituo vya kanda vya uhimilishaji; kuanzisha kambi 8 za kuendesha uhimilishaji katika Mikoa ya Simiyu (2), Katavi (1), Dodoma (1), Kagera (2) na Geita (2); kutolewa kwa mafunzo ya uhimilishaji kwa wahimilishaji 48 wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Njombe, Mtwara, Dodoma, Songwe, Mbeya na Tanga; wahimilishaji 37 wamepatiwa mafunzo kwa vitendo kuhusu uhimilishaji katika Halmashauri 8; na mbegu bora za madume dozi 45,617 zimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji kwa ajili ya kuboresha mifugo.

(ii) Kutenga Maeneo ya Malisho na Upatikanaji wa Maji: kazi zilizotekelezwa ni kutenga na kupima na kuweka alama katika mashamba 8 yenye ukubwa wa hekta 23,066.94 ya Hangangadinga (4,200), Mahukuru Lilahi (3,100), Chibe (2,054), Shishiyu (3,170), Mkwese (5,036), Kinyangiri (3,419.94), Nachingwea (1,497) na Kelema (590). Aidha, Halmashauri za Wilaya zimetenga jumla ya hekta 2,818,687.17 kwa ajili ya malisho ambapo hekta 108,427.49 zimepimwa. Pia, jumla ya tani 127.3 za mbegu bora za malisho na vipandikizi zimezalishwa katika mashamba ya Serikali. Vile vile, mashamba darasa 20 ya malisho yameanzishwa, kati ya hayo, matano (5) yapo Wilaya ya Monduli na 15 yapo katika halmashauri za mkoa wa Singida.

(iii) Kuimarisha Tiba na Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo: Kazi zilizotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa jengo la kuzalisha chanjo za bakteria katika Kituo cha Kuzalisha Chanjo cha Kibaha (TVI) ambapo kwa sasa umefikia asilimia 75, ujenzi wa jengo hilo utakapokamilika utawezesha kiwanda kuzalisha chanjo za Magonjwa 13 ya kipaumbele zinazohitajika hapa nchini ikiwemo chanjo mpya tatu (3) za Magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na Kichaa cha Mbwa; kuzalishwa na kusambazwa kwa dozi 49,008,325 (dozi 47,347,700 dhidi ya ugonjwa wa mdondo, 626,000 dhidi ya ugonjwa wa kimeta, 113,000 dhidi ya ugonjwa wa chambavu, 756,600 dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP), 19,275 dhidi ya ugonjwa wa kutupa mimba na dozi 145,750 ya chanjo mchanganyiko wa kimeta na chambavu (TECOBLAX)) za chanjo za mifugo nchini ambapo halmashauri 40 dozi 1,287,000 na wasambazaji wa pembejeo za mifugo na wachanjaji binafsi dozi 47,721,325.

(iv) Kuimarisha huduma za Utafiti, Ugani na Mafunzo kwa Maafisa Ugani wa Mifugo: kazi zilizotekelezwa ni kutoa elimu ya mafunzo rejea na maarifa mapya kuhusu uzalishaji wa kibiashara kwa wadau 8,158 katika halmashauri 25 wakiwemo wafugaji 6,030 maafisa ugani 471, wanafunzi wa shule za sekondari na msingi 1,433, wakuu wa shule za sekondari na msingi 87 na watendaji wa kata na vijiji 137. Aidha, ukarabati mkubwa umefanyika katika Hosteli 10 katika Kampasi za LITA, madarasa matatu (3), kumbi mbili (2) za mihadhara, maabara mbili (2), maktaba mbili (2) na kujenga vyoo vipya vitatu (3) vya wanafunzi. Pia, wachunaji ngozi 735 na wataalam wa mifugo 94 wamejengewa uwezo kuhusu uchunaji bora wa ngozi unaozingatia mahitaji ya soko kutoka katika Mikoja nane 8. Vile vile, wafugaji na wadau 115,979 wamepatiwa elimu ya ufugaji bora wa kibiashara kupitia maonesho ya Saba Saba (25,200), Nane Nane (75,089) na Siku ya Chakula Duniani (15,670).

(v) Kuongeza Thamani Bidhaa za Mifugo na Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli na Udhubiti wa Biashara ya Magendo ya Mifugo.

Kazi zilizotekelezwa ni: kununua ng'ombe 2,283 kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kutoka kwa wafugaji wa asili kwa ajili ya kunenepesha ili kuzalisha nyama bora; jumla ya ekari 6,771 za ranchi za NARCO zimefyekwa vichaka kwa ajili ya kuruhusu ukuaji wa malisho; jumla ya ndama 4,781 wamezalishwa na kukuzwa katika ranchi za NARCO; na mipaka ya kuonekana imewekwa katika Ranchi za Missenyi, Ruvu na Uvinza. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza operesheni Nzagamba ili kudhibiti utoroshaji wa mifugo na mazao ndani na nje ya nchi na upotevu wa mapato katika maeneo matano ya kimkakati ya Nzega (Tabora), Lamadi (Simiyu), Babati (Manyara), Longido (Arusha) na Handeni (Tanga). Kupitia operesheni hiyo, jumla ya ng'ombe 392,661, mbuzi na kondoo 676,715 walikaguliwa ambapo jumla ya mifugo 3,363 (ng'ombe, mbuzi na kondoo) iliyokuwa inatoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulipiwa vibali na ushuru ilikamatwa na kutozwa faini.

3.3.2.4 Uvuvi

Katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20 Sekta ya Uvuvi imetekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha Shughuli za Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Uvuvi
Hatua iliyofikiwa ni: kufanya utafiti wa kuangalia wingi wa samaki katika Ziwa Victoria ambapo matokeo yanaonyesha kuongezeka kwa samaki aina ya Sangara kutoka tani 553,770 mwaka 2018/19 hadi tani 816,694 mwaka 2019/20. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za kupiga vita uvuvi haramu. Aidha, utafiti wa kuzalisha mbegu bora za samaki inayofaa kufugwa umefanyika ambao ulihusisha mbegu

mbili za sato (*Oreochromis niloticus*) ambazo ni “TAFIRI 1 strain” ambayo ni sato waliotoka Ziwa Victoria upande wa Tanzania na “TAFIRI 2 strain” ni sato waliotoka Ziwa Victoria upande wa Uganda; kuandaliwa na kuzinduliwa kwa Agenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji (The Fisheries and Aquaculture Research Agenda 2020 - 2025) ambayo imeanisha maeneo matano ya vipaumbele ambayo ni mfumo wa ikolojia ya viumbe maji; uvuvi endelevu katika maji ya asili; ukuaji wa tasnia ya ukuzaji viumbe maji; masoko na biashara ya samaki na mazao yake; na masuala mtambuka. Pia, kuendelea na utoaji wa huduma za ugani juu ya uvuvi endelevu, uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi, ufugaji bora wa samaki na umuhimu wa uanzishwaji wa vyama vya ushirika kwa wadau 3,266.

(b) Kuongeza Upatikanaji wa Vifaranga vya Samaki

Hatua iliyofikiwa ni: kuzalishwa kwa vifaranga 15,041,401 ambapo vifaranga 950,401 ni kutoka vituo vya Serikali na vifaranga 14,088,000 kutoka vituo binafsi; kutoa mafunzo ya ufugaji wa samaki kwa wananchi 3,595 sawa na asilimia 89.88 ya lengo lililokusudiwa; kununuliwa kwa matanki 27 yenye uwezo wa kuhifadhi vifaranga 324,000 kwa wakati mmoja na kupelekwa katika vituo vya Ruhila, Kingolwira na Mwamapuli; kufungwa kwa happa nets 50 katika vituo vya Ruhila (30), Mwamapuli (20) kwa ajili ya kukuzia wazazi na kukusanya mayai; kupandikiza samaki wazazi wapatao 27,640 katika vituo vya Ruhila (2,100), Mwamapuli (5,900), Kingolwira (11,640) na Mtama/Nyengedi (8,000) na kuunganisha umeme katika vituo vya Mwamapuli na Ruhila; kukarabati mabwawa 11 katika vituo vya Mtama/Nyengedi (8) na Kingolwira (8); kukarabati mabwawa matatu (3) na nyumba moja (1) ya mtumishi katika kituo cha Kingolwira; na kununuliwa kwa mashine mbili (2) za kusukuma maji kwa ajili ya vituo vya Ruhila na Mwamapuli.

(c) Kuimarisha na Kuendeleza Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira

Shughuli zilizotekelezwa ni: kufanyika kwa operesheni na doria zenye jumla ya siku kazi 7,472 katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu, na katika Bahari ya Hindi na kuvuka lengo la mwaka lililokuwa na Siku kazi 6,500 ambapo zana haramu mbalimbali zilikamatwa zikiwemo; nyavu za makila 166,177, makokoro 808, nyavu za timba 31,671, nyavu za dagaa 547, kamba za kokoro zenye urefu wa mita 149,071, ndoano 12,000, mitumbwi 736, boti 56, nyavu za ring net 204, vyandarua 22, katuli 10, injini za boti 275 na kasia 8; kuanzishwa kwa vituo vinne (4) vya usimamizi wa rasilimali za Uvuvi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali ambavyo ni Rorya, Bwawa la Nyumba ya Mungu, Bwawa la Mtera na Ziwa Rukwa; na kutolewa kwa vitendea kazi katika vituo 27 vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi.

(d) Kusimamia na Kuhamasisha Uwekezaji katika Uvuvi na Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Uvuvi

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuanzishwa vituo vya ubora na uthibiti wa mazao ya uvuvi vya Singida, Kisesya na Murusagamba; kufanyika kwa kaguzi 2,904 za samaki na mazao ya uvuvi katika viwanda vya uchakataji wa Samaki, maghala ya kuhifadhia samaki na magari ya kusafirisha samaki pamoja na kaguzi 191 za kina katika viwanda vinavyochakata samaki na masoko; kuimarishwa kwa Maabara za samaki za Nyegezi (Mwanza) na ya viuatilifu Dar es Salaam kwa kupatiwa vitendea kazi ikiwemo madawa na vifaa vya kufanyia uchunguzi wa sampuli ambapo sampuli 2,848 za minofu ya samaki, dagaa, maji na udongo zimechunguzwa ili kubaini uwepo wa vimelea, kemikali na madini tembo; kuweka mazingira wezeshi katika uvuvi wa bahari kuu kwa kuweka vivutio kwa wawekezaji wa ndani ya nchi na nje, kufuatia kutungwa kwa Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2020; kuhamasisha sekta binafsi kwa kuiunganisha na taasisi za kifedha ili iwekeze katika ujenzi wa viwanda vya uchakataji wa mazao ya uvuvi.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya Wavuvi na Wakuzaji Viumbe Maji katika mikoa ya Mwanza, Tanga, Kagera, Geita, Mbeya, Ruvuma, Songwe na Mara. Aidha, Dawati la Sekta Binafsi limetambua Vyama vya Ushirika vya Wavuvi 102, kuwezesha kuanzishwa kwa vyama vipya 14 na kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa Vyama vya Ushirika viwili (2), kampuni saba (7) za ukuzaji viumbe maji ambapo shilingi milioni 944.2 zimepitishwa na shilingi milioni 323.8 tayari zimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Vilevile, vyama vitano (5) vimepatiwa Injini za Boti 5 na vyama 14 viko katika hatua za mwisho za kupatiwa mikopo.

(e) Kuimarisha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu

Shughuli iliyotekelezwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ambao umependekeza maeneo matatu yanayofaa kwa ujenzi wa bandari hiyo: Mbegani-Bagamoyo, Kilwa Masoko na eneo la Bandari ya Lindi; kuhuishwa kwa mfumo wa kufuatilia mienendo ya meli kwa kununua mtambo wa Automatic Identification System-AIS; kutungwa kwa Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2020 ambayo imezingatia mahitaji ya sasa; kuwajengea uwezo waangalizi 11 wa shughuli za uvuvi melini kutoka katika Mamlaka na Idara za Uvuvi (SMT na SMZ).

(f) Kuimarisha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari

Shughuli iliyotekelezwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ambao umependekeza maeneo matatu yanayofaa kwa ujenzi wa bandari hiyo: Mbegani-Bagamoyo, Kilwa Masoko na Lindi; kuhuishwa kwa mfumo wa kufuatilia mienendo ya meli kwa kununua mtambo wa Automatic Identification System-AIS; kutungwa kwa Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2020 ambayo imezingatia mahitaji ya sasa; kuwajengea uwezo waangalizi 11 wa shughuli za uvuvi melini kutoka katika Mamlaka na Idara za Uvuvi (SMT na SMZ).

(g) Kuimarisha Miundombinu na Kukuza Biashara ya Mazao ya Uvuvi

Shughuli zilizotekelezwa ni: kufanya tathmini katika masoko manne (4) na mialo 26 ikiwemo ya Sota, Marehe, Kigangama, Kahunda, Ikumbaitale, Bwai, Nyamisati, Igombe, Ihale, Mafia, Kilwa ili kupata hali halisi na changamoto za uendeshaji; na Soko la Samaki la Feri – Dar es Salaam limeboreshwa kwa kujengwa ofisi mbili (2), stoo mbili (2) na choo cha kisasa chenye matundu 12 na mabafu nane (8).

3.3.2.5 Maliasili na Utalii

(a) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili

Hatua iliyofikiwa ni: kujengwa kwa maboma ya kujilinda na wanyama wakali wakati wa usiku katika vijiji 10 vya Wilaya ya Serengeti; kutoa mafunzo kwa maafisa mazingira na uhifadhi katika ngazi ya Kata na Vijiji katika wilaya ya Ngorongoro; kuandaliwa kwa mwongozo wa uwindaji wa Simba na Chui kwa kuzingatia mahitaji ya Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya viumbe vilivyo katika hatari ya kutoweka; kuandaa mpango wa usimamizi wa Pori la Akiba la Kijereshi na kubainisha maeneo ya uwekezaji na uendelezaji utalii; kuendelea na maandalizi ya Mpango wa Usimamizi wa Pori la Akiba la Mkungunero; kuandaliwa kwa mpango shirikishi ya usimamizi wa misitu na sheria ndogo katika vijiji sita (6) katika Wilaya ya Serengeti na Ngorongoro; na kufanya ufuatiliaji na mafunzo rejea kwa vikundi 6 vya kuweka na kukopa vya ufugaji wa nyuki kibiashara.

(b) Mradi wa Uhifadhi wa Misitu Asilia

Shughuli zilizotekelezwa ni: kujengwa kwa barabara za msituni (km 85.53) katika Hifadhi zote za Misitu ya Asili; kujengwa kwa njia za msituni (km 37.3) katika hifadhi za misitu asilia ya Udzungwa *Scarp*, Kilombero, Mlima Hanang na Minziro; kuanzishwa kwa manzuki, vitalu vya miche, ufugaji samaki kwa jamii zinazopakana na hifadhi za misitu asilia ya Chome, Mkingu, Minziro, Kilombero, Mlima Rungwe, Mlima Hanang na Magamba; ushirikishwaji wa jamii

zinazozunguka hifadhi katika Hifadhi za Misitu Asilia ya Minziro, Chome, Magamba, Mlima Rungwe na Mkingu; na kutangaza shughuli za utalii ikolojia kwa nia ya kuongeza idadi ya watalii na kuongeza mapato.

(c) Mradi wa Usimamizi wa Maliasili kwa ajili ya Kuendeleza Uchumi Mkoa wa Kigoma

Hatua iliyofikiwa ni: kutolewa kwa hati za kimila 3,500 za umiliki wa ardhi; kukamilika kwa Mipango 29 ya Matumizi Bora ya Ardhi; kutolewa mafunzo kwa timu za Mradi za Wilaya na Vijiji na Kamati za Mialo kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Maliasili na Sheria ndogo; kuandaliwa kwa mipango ya usimamizi na uvunaji wa misitu kwa vijiji nane (8) katika wilaya za Kibondo na Kasulu; kuanzisha hifadhi za misitu ya vijiji katika vijiji 28 vyenye jumla ya misitu 39 na ukubwa wa hekta 39,449; kuanzisha Kamati za fukwe tatu (3) za Mtanga, Kagalye na Kalalangabo; kuanzisha vikundi vitano (5) vya wavuvi katika vijiji vya Kasisi, Mtego wa noti, Malagarasi, Itebula na Chagu; kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuongeza thamani katika asali na samaki kwa wajumbe 86 wa timu za uendeshaji mradi za wilaya na vikundi 73 vya uzalishaji mali; kuwezesha vikundi vidogo vya uzalishaji mali 25 kutekeleza miradi ya kuhifadhi maliasili; na kuwezesha upatikanaji wa mitumbwi ya kisasa 23 kwa ajili ya doria, ufuatiliaji na uvuvi wa samaki katika Ziwa Nyamagoma na Ziwa Sagara.

(d) Programu ya Misitu na Uendelezaji wa Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu - FORVAC

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuandaliwa kwa Mipango 25 ya Matumizi Bora ya Ardhi; kusambaza miche 230,000 ya mitiki katika vinne (4) vya Wilaya ya Nyasa kwa ajili ya kupanda kwenye mashamba yao; kuchapishwa kwa nakala 3,500 za Kitabu cha Usimamizi wa Misitu ya Jamii; kupatiwa mafunzo kwa waandishi wa habari 27 kuhusu mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na uandishi wa habari za kiuchunguzi; kufungwa kwa mfumo wa utoaji na upashanaji wa taarifa; kuanzisha Misitu ya Vijiji 32 yenye ukubwa wa hekta 32,245; kuandaa mtaala wa kuongeza thamani mazao ya misitu, mifumo ya masoko na kuendeleza biashara; kuanzisha mfumo wa Taarifa wa Programu ya FORVAC ikiwa ni pamoja na kuanzisha Tovuti ya Programu; kuandaa mwongozo wa kuandaa Mpango wa Usimamizi wa misitu ya Asili Tanzania; kuunda na kujenga uwezo wa Kamati za Hifadhi ya Mazingira za vijiji 12; kuunda na kutoa mafunzo kwa vikundi 10 vya ujasiriamali vyenye jumla ya wanachama 520; na kuandaa mtaala wa ongezeko la thamani ya mazao ya misitu, mifumo ya masoko na maendeleo ya biashara.

(e) Mradi wa kuendeleza Utalii Ukanda wa Kusini - REGROW

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuandaliwa kwa maandiko kwa ajili ya kuwajengea uwezo wananchi wanaopakana na Hifadhi ya Taifa Ruaha kwenye skimu ya umwagiliaji ya Madibira katika wilaya ya Mbarali ili kulinda hifadhi dhidi ya uharibifu wa mazingira; kukamilika kwa tathmini ya kuandaa mpango mkakati wa masoko ya utalii katika maeneo ya kusini; ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kufanya doria katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Mikumi, na Udzungwa; kutangazwa na kutolewa kwa elimu kuhusu vivutio vya utalii kupitia maonesho ya Karibu Kusini yaliyofanyika mkoani Iringa; kufanyika kwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo ili kujua mapungufu yaliyopo kwa wakulima wa vyama vya umwagiliaji; kufanyika kwa mapitio ya katiba na ada za huduma ya umwagiliaji kulingana na Sheria ya Umwagiliaji; na kusajiliwa na kuzinduliwa kwa chama kimoja (1) cha watumiaji wa maji wa Mto Mbarali wa Chini.

3.3.2.6 Madini

(a) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini - SMMRP

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya mfano vya uchenjuaji madini vya Katente (Bukombe) na Lwamgasa (Geita); kukamilika kwa utafiti wa kina wa jiosayansi kwa lengo la kubaini uwepo na kiasi cha madini kinachopatikana katika maeneo sita (6) ya wachimbaji wadogo ya Kapanda (Mpanda), Buhemba (Musoma), Katente (Bukombe), Itumbi (Chunya), Kyerwa (Kagera) na Kange (Tanga); kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne (4) vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni; kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Mpango wa Utunzaji wa Mazingira; kukamilika kwa ufungaji wa miundombinu ya umeme na taa katika jengo la Kituo cha Pamoja (one stop centre) Mirerani na kuendelea na ufungaji wa kamera za ulinzi (CCTV) kuzunguka eneo la ukuta; kuendelea na ujenzi wa vituo vya umahiri vya Songea, Mpanda na Chunya; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha uchenjuaji madini cha Itumbi (Chunya).

(b) Mradi wa Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia - TEITI

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ukamilishaji wa taarifa ya TEITI ya mwaka 2016/17 na 2017/18; kuelimisha umma kupitia redio na runinga kuhusu matumizi ya takwimu za taarifa za TEITI katika kuhoji ufanisi wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia ambapo zaidi ya wananchi 500 wameelimishwa; na kuanzishwa kwa Rejesta ya Taarifa na majina ya watu wanaomiliki hisa katika kampuni 37 za madini, mafuta na gesi asilia.

3.3.3 Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu

3.3.3.1 Elimu, Sayansi na Teknolojia

A. Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari

(a) Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu - EP4R)

Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa kwa magari 39 na kusambazwa katika vyuo vyote vya ualimu vya Serikali ambapo magari 35 yamegawiwa katika vyuo vyote vya ualimu vya Serikali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika vyuo hivyo na magari 4 ni kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini Wizarani; kukarabatiwa kwa vyuo vya ualimu 26 na kujenga upya chuo kimoja (1) kati ya vyuo 35 vya Serikali; kukamilisha ujenzi wa ofisi mpya 100 za uthibiti ubora wa shule za wilaya; kuendelea kwa taratibu za ununuzi wa magari 65 kwa ajili ya kuimarisha uthibiti ubora wa shule pamoja na magari matano (5) na Malori mawili (2) kwa ajili ya Baraza la Mitihani la Taifa; na kuendelea na taratibu za ujenzi wa ofisi 55 za wilaya za uthibiti wa ubora wa shule ili kuimarisha mazingira ya utendaji kazi. Vile vile, kuendelea na taratibu za ujenzi wa shule ya sekondari ya mfano katika jiji la Dodoma.

(b) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi (MEMEM) - Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK)

Hatua iliyofikiwa ni: kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano na wadau wa Maendeleo - GPE Januari, 2020 kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi; kubainishwa kwa shule zenye upungufu wa vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa ajili ya kufanya manunuzi kulingana na mahitaji; na kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa LANES awamu ya pili baina ya Serikali na Sweden.

(c) Elimumsingi bila Ada

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi bila ada ambapo katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019, jumla ya shilingi bilioni 128 zimetolewa kugharamia elimumsingi bila ada ikijumuisha posho ya madaraka kwa walimu wakuu na maafisa elimu kata.

(d) Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni - SWASH

Hatua iliyofikiwa ni: kuwezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 9,712 (wasichana matundu 5,539, wavulana matundu 3,645 na walimu matundu 528), miundombinu

ya maji na matanki 911 kwa ajili ya kunawa mikono katika shule za msingi 602. Miundombinu hii inatarajiwa kuwanufaisha wanafunzi 446,155 waliopo katika shule hizo.

B. Mamlaka ya Elimu Tanzania - TEA

Ujenzi na Ukarabati wa Shule za Sekondari: kuendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 (madarasa matatu (3) kwa kila shule) katika shule za msingi 23 na shule za sekondari nne (4) zenye uhitaji mkubwa; ujenzi wa mabweni 16 ya wasichana katika shule 16 za sekondari (kidato cha 5 na 6) zilizo katika mazingira hatarishi; kuendelea na ujenzi wa nyumba 40 za walimu kwa shule 10 za sekondari ikiwa ni nyumba vinne (4) kwa kila shule; kuendelea na ujenzi wa mabweni matatu (3) katika shule tatu (3) za msingi, ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa na chumba maalum (Audiology room); na ujenzi wa matundu 528 ya vyoo (matundu 24 kwa kila shule) katika shule za msingi 18 na shule za sekondari nne (4) zenye uhitaji mkubwa.

C. Elimu ya Ufundi na Ualimu

(a) Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma katika mikoa ya Kagera, Geita, Rukwa, Njombe na Simiyu; ujenzi wa vyuo 33 vya wilaya za Buhigwe, Butiama, Chemba, Chunya, Ikungi, Igunga, Kishapu, Kwimba, Monduli, Mbarali, Mafia, Pangani, Ulanga, Uvinza, Kilindi, Korogwe, Longido, Masasi, Mkinga, Ukerewe, Uyui, Bahi, Iringa, Lushoto, Rufiji, Kongwa, Ruangwa, Nyasa, Chato, Karagwe, Ileje, Newala na Simanjiro.

Vile vile, ujenzi wa karakana za uungaji vyuma katika vyuo vya ufundi stadi na huduma Pwani na Manyara pamoja na ujenzi wa karakana za viyoyozi, majokofu na ubunifu na ushonaji wa mavazi katika Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Lindi unaendelea; kufikiwa kwa asilimia 90 kwa kazi ya utengenezaji wa samani kwa ajili ya Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Kihonda, Morogoro; kukamilika kwa uunganishaji wa Mkongo wa Taifa kwa vyuo 27 vya mafunzo ya ufundi stadi; kukamilika kwa ujenzi wa vyuo nane (8) vya mafunzo ya ufundi stadi katika Wilaya za Kilindi (Mabalanga), Babati (Gorowa), Ngorongoro (Samunge), Urambo (Chekereni), Nkasi (Paramawe), Kasulu (Nyamidaho) Muleba (Ndolage), Itilima (Kanadi); kuendelea kugharamia upimaji na upatikanaji wa hati miliki ya maeneo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kote nchini; na kuratibu ujenzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi 25 vya Wilaya.

(b) Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma vya Mkoa ya Geita, Simiyu na Rukwa; kuendelea na taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha Ufundi Stadi kwa Mkoa wa Njombe; kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro; kuendelea na ujenzi katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa kwa kujenga bweni, nyumba za watumishi, bwalo na Jengo la TEHAMA; na kuendelea na upanuzi wa miundombinu katika vyuo vya ualimu vitano (5) ambavyo ni Mpwapwa, Kleruu, Marangu, Tabora na Dakawa.

(c) Chuo cha Ufundi Arusha

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kufundishia matumizi ya nishati jadidifu ya umeme wa jua lenye uwezo wa kuchukua washiriki 20, ujenzi na ukarabati wa kituo cha mafunzo ya kufua umeme kwa kutumia nguvu ya maji cha Kikuletwa; kuendelea na ukarabati wa nyumba chakavu 68 za watumishi na mabweni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa nishati jadidifu (kW 70) ambao umefikia asilimia 40; kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu; na kutoa ushauri wa kitaalamu katika usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi, upimaji wa udongo, upimaji lami na usanifu na ufungaji wa taa za kuongozea magari barabarani katika Jiji la Arusha.

(d) Kuendeleza Elimu ya Ualimu

Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa kwa kompyuta 480, vifaa vya kudurufu 35, kompyuta mpakato 43 katika vyuo vya ualimu vya Serikali; kuendelea na kazi ya usanifu kwa ajili uunganishaji wa vyuo 35 vya ualimu katika Mkongo wa Taifa kwa lengo la kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA; kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga; kukamilika kwa mtaala wa elimu ya ualimu; kutoa mafunzo kazini kwa walimu 269 kutoka shule 23 za sekondari nchini kuhusu matumizi ya lugha ya alama na mbinu za kufundishia, mafunzo ya TEHAMA na Teknolojia saidizi kwa walimu 125 na wakufunzi tisa (9) wenye ulemavu; kununuliwa kwa vifaa vya maabara za sayansi kwa vyuo 11 vya ualimu; kununuliwa na kusambazwa kwa vifaa vya wanafunzi na wakufunzi wenye mahitaji maalum katika vyuo vya Patandi, Mpwapwa na Mtwara Kawaida; kununuliwa na kusambazwa kwa nakala 25,709 za aina 449 za vitabu kwa ajili ya masomo yote katika vyuo vya Ualimu vya Serikali; kutoa mafunzo kazini ya TEHAMA kwa wakufunzi 530 kutoka katika vyuo 17 vya ualimu; kuandaliwa kwa miongozo ya mafunzo ya TEHAMA na teknolojia saidizi kwa wakufunzi na walimu

wenye mahitaji maalumu na mafunzo kazini kuhusu Mtaala wa Umahiri (Competence Based Curriculum) kwa wawezeshaji wa kitaifa wakiwemo walimu wa shule za msingi, sekondari na wakufunzi wa vyuo vya ualimu; na kutolewa kwa mafunzo kazini kwa walimu 771 (Msingi 451 na Sekondari 320) katika halmashauri 20 zenye ufaulu wa chini katika somo la Hisabati kwenye mitihani ya kitaifa.

(e) Kuimarisha Taasisi ya Elimu Tanzania

Hatua iliyofikiwa ni: kuchapishwa na kusambazwa kwa kitabu cha kiongozi cha mwalimu (nakala 41,642) kwa darasa la I na II na vitabu vya kiada vya elimu ya awali (nakala 719,905) na moduli za mafunzo kazini katika halmashauri zote nchini; kukamilika kwa uandishi wa vitabu 15 vya masomo ya sayansi (Fizikia, Kemia na Baiolojia), Kiswahili na *Basic Applied Mathematics* kwa kidato cha tano (5) na sita (6); kuandaa Mwongozo wa kufundishia Elimu ya Awali na miongozo mitano ya kufundishia kwa kutumia mbinu za michezo (Play and Learn); kuchapishwa na kusambazwa kwa vitabu vya kiada kwa ngazi ya elimu ya awali na msingi darasa la I - III kwa ajili ya shule zinazotumia lugha ya Kiingereza; kuchapishwa na kusambazwa kwa nakala 8,750 za vitabu vya kiada vya maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu; kuandaliwa na kusambazwa kwa nakala 272,000 za kiongozi cha mwalimu kwa masomo nane (8) na mihtasari ya kufundishia lugha ya kichina kwa kidato cha kwanza (1) hadi cha nne (4); kuchapishwa na kusambazwa kwa nakala 1,359,350 za vitabu vya masomo yote kwa ngazi ya elimu awali na msingi darasa la I-V kwa matumizi ya shule zinazotumia Kiingereza; kuandika vitabu vya kiada vya masomo matano (5) kwa darasa la VI kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia; kuandikwa, kuchapishwa na kusambazwa kwa nakala 11,402 za vitabu vya kiada vya nukta nundu (Braille) aina 18 kwa Darasa la I, II, na V kwa ajili ya wanafunzi wasioona; kuchapishwa katika maandishi ya nukta nundu na kusambazwa kwa Mtaala wa Darasa la I - VII ulioboreshwa mwaka 2019; kuendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu kupitia huduma ya maktaba mtandao (TIE - online library); na kukamilisha uandishi, uchapishaji na usambazaji wa nakala 2,962,155 katika halmashauri za mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa uwiano wa 1:3 za aina nane (8) za vitabu vya kiada vya darasa la VI kwa masomo ya Kiswahili, Hisabati, Kiingereza, Uraia na Maadili, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi, Sayansi na Teknolojia na Kifaransa kwa kuzingatia mtaala wa mwaka 2015.

D. Elimu ya Juu

(a) Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Hatua iliyofikiwa ni kutolewa kwa mikopo kwa wanafunzi 49,799 yenye thamani ya

shilingi bilioni 173.2 ili kuwezesha wanafunzi wengi kupata elimu ya juu. Aidha, wametambulika wadaiwa wapya 14,731 wenye mikopo iliyoiva yenye thamani ya shilingi bilioni 100.7.

(b) Ukarabati na Ujenzi wa Chuo Kikuu Mzumbe

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa hosteli mbili (2) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 256 katika Kampasi ya Mbeya; kukamilika kwa hosteli tatu (3), nyumba 10 za watumishi na kuendelea na ujenzi wa madarasa Kampasi Kuu; na kuendelea na uwekaji wa samani katika majengo ya Kampasi ya Tegeta - Dar es Salaam.

(c) Ujenzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Ardhi

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la Ardhi (Lands Building) pamoja na miundombinu ya TEHAMA na kuweka samani; na kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 592 kwa wakati mmoja.

(d) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu; na kufanya maboresho katika shule ya meno hususan chumba kwa ajili ya kutolea huduma binafsi.

(e) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kafeteria moja kwa ajili ya kuongeza maeneo ya utoaji wa huduma ya chakula kwa wanafunzi na wafanyakazi katika Kampasi ya Moshi; ukarabati na upanuzi wa mabweni tisa (9), mabweni sita (6) katika Kampasi Kuu ya Moshi na matatu (3) katika kituo cha kufundishia Kizumbi - Shinyanga na kukamilika kwa ujenzi wa ukuta wenye urefu wa mita 200.

(f) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na kufunga viti 326 katika jengo jipya la mihadhara.

(g) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala; na kuanza ujenzi wa maabara za sayansi na vyumba vya madarasa katika shule ya

sekondari ya mazoezi.

(h) **Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwl. Julius Nyerere**
Hatua iliyofikiwa ni kupatikana kwa hatimiliki ya ekari 231 zikiwemo ekari 95 katika Kampasi ya Kinesi Halmashauri ya Rorya na ekari 136 kampasi ya Kisangura Wilaya ya Serengeti.

(i) **Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha**
Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea kuboresha miradi ya utafiti katika kilimo, maji, TEHAMA na usalama wa chakula kama vile uzalishaji wa miche bora ya ndizi inayohimili magonjwa ya kitropiki; na kuondoa sumu kuvu katika nafaka na kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa kimeta kwa mifugo na wanyamapori.

(j) **Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - DIT**
Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa jengo la maabara ya kompyuta, darasa na bwalo la chakula katika Kampasi ya Myunga iliyopo mkoani Songwe; kukarabati miundombinu ya Kampasi ya Mwanza ikiwemo maabara na ununuzi wa mashine ya kuchakata na kutengeneza bidhaa za ngozi; ujenzi wa jengo la maabara ya kompyuta, darasa na bwalo la chakula katika Kampasi ya Myunga iliyopo mkoani Songwe; upanuzi wa jengo la maktaba (Vertical Extension of DIT Library) pamoja na kuweka samani na miundombinu ya TEHAMA katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam na hivyo kuongeza uwezo wa matumizi ya Maktaba kutoka wanafunzi 150 hadi 450 kwa wakati mmoja; ujenzi wa mabweni manne (4) ya wanafunzi na majengo mawili (2) ya vituo vya umahiri katika kampasi za Mwanza na Dar es Salaam; na kupima ubora wa vifaa vya ujenzi katika miradi miwili mikubwa ya kimkakati ambayo ni mradi wa kufua umeme wa maji (Julius Nyerere Hydropower project) na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway).

(k) **Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**
Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ambao umefikia asilimia 97; ukarabati wa ofisi za wafanyakazi wa Chuo; kukamilika kwa ujenzi wa madarasa mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja; na kukarabati ofisi 80 za wafanyakazi 320; na kufungwa kwa viti katika madarasa matano (5).

(l) **Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine - SUA**
Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la maabara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja ambao

umefikia asilimia 90; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la utafiti wa wanyama na wadudu; kuendelea na ukarabati wa madarasa ambao umefikia asilimia 92; kuendelea na ukarabati wa jengo la Hay Building; kuendelea na ukarabati wa karakana za uhandisi kilimo; kuboresha shamba la Chuo kwa kupanda mazao ya Taifa ya kimkakati; na kuanzishwa kwa kampasi mpya ya Mizengo Kayanza Peter Pinda katika kijiji cha Kibaoni, Katavi.

(m) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa kituo cha huduma za kijamii lenye ghorofa tano (5) kwa wanafunzi ambapo ujenzi umefikia asilimia 70; kukamilika kwa ukarabati mkubwa wa nyumba tano za watumishi; kukarabati bweni Na. I Kitalu G linalotumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalum lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 63; kuendelea na ujenzi wa mfumo mpya wa maji katika Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere; kuendelea na ujenzi wa Jengo la huduma katika Hosteli za Dkt. J. P. Magufuli na kuendelea na ukarabati wa majengo ya Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia ambao umefikia asilimia 50.

E. Ujuzi na Utafiti

(a) Kukuza Stadi za Kazi kwa ajili ya Shughuli za Kuzalisha na Kukuza Uchumi

Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi (FDC); kuendelea na awamu ya pili ya ukarabati wa Vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi; kuanza ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika halmashauri za Ruangwa, Kongwa, Kasulu Mji na Nyasa; kuwezesha vijana 2,534 kupata mafunzo ya uanagenzi katika Taasisi mbalimbali; na kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa watumishi 318 wanaosimamia stadi za ujuzi katika taasisi za TEA, TCU, NACTE, HESLB na VETA.

(b) Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH

Hatua iliyofikiwa ni: kubaini mahitaji ya bunifu na kutoa mafunzo katika nyanja za ulinzi miliki wa bunifu, ujasiriamali, ubiasharishaji na usimamizi wa mikataba kwa wabunifu 60 ambao ni washindi wa Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU); na kuendelea kugharamia uanzishaji wa kituo kimoja cha mfano kwa ajili ya uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje.

(c) Maabara ya Mionzi ya Nguvu za Atomiki

Hatua iliyofikiwa ni: kukaguliwa kwa migodi miwili ya Buzwagi ambayo iko kwenye hatua za mwisho za ufungwaji; kufanya ukaguzi kwa vituo 209 vyenye vyanzo vya mionzi ambapo vituo 11 vilizuiliwa kutoa huduma za kutumia vyanzo

vya mionzi, vituo 4 viliruhusiwa kutoa huduma baada ya kufanya maboresho na vituo 194 viliendelea kutoa huduma baada ya kukutwa vipo salama; kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maabara ya kupima mionzi; na kufunguliwa kwa ofisi moja (1) ya mipakani katika Wilaya ya Bagamoyo.

3.3.3.2 Afya

(a) Mradi wa Kupunguza Vifo vya akina Mama Vitokanavyo na Uzazi

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya Afya na kununuliwa kwa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji katika mikoa ya Mara (7), Mwanza (6), Simiyu (6) na Geita (6); na kuendelea na ujenzi wa kituo cha damu salama katika mkoa wa Njombe ambapo ujenzi umefikia hatua ya kupaua.

(b) Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa

Hatua iliyofikiwa ni: kuboreshwa kwa miundombinu ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na mtandao kiambo katika hospitali sita (6) za rufaa za mikoa (Temeke, Geita, Njombe, Dodoma, Bombo na Mbeya); na kuendelea na ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma katika hospitali za mikoa ya Mara (Kwangwa), Mwanza (Sekou Toure), Mbeya, Ruvuma (Songea), Lindi (Sokoine), Mtwara (Ligula), Kilimanjaro (Mawenzi), Arusha (Mount Meru), Manyara, Tabora (Kitete), Pwani (Tumbi), Singida, Shinyanga na Dar es Salaam (Mwananyamala). Aidha, katika mikoa mipya ya Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Katavi ujenzi wa hospitali za rufaa unaendelea ambapo kwa mikoa ya Njombe, Geita na Simiyu huduma zimeanza kutolewa na kuendelea na ujenzi wa majengo ya huduma za dharura katika hospitali za rufaa za mikoa za Songwe, Mawenzi, Njombe, Tabora, Sumbawanga, Songea na Mbeya.

(c) Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa tiba na Vitendanishi

Hatua iliyofikiwa ni: upatikanaji na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi umefikia asilimia 91.4 ya vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya; na kununuliwa na kusambazwa kwa mashine nne (4) za X-ray za kidigitali katika hospitali za rufaa za Manyara, Mt. Meru (Arusha), Songwe na Mwananyamala (Dar es Salaam).

(d) Taasisi ya Saratani Ocean Road

Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa kwa majokofu manne (4) kwa ajili ya maabara; kufunga mashine mpya yenye uwezo wa kupima vipimo vya kemia; kununuliwa kwa mashine tisa (9) za *oxygen concentrators* kwa ajili ya wagonjwa wanaolazwa na wenye uhitaji wa hewa ya oksijeni; kutoa vipimo vya radiolojia 9,897 ikiwa ni sawa

na asilimia 141.4 zaidi ya lengo kwa mwaka; kufanyika kwa uchunguzi na tiba za dawa ya nyuklia kwa kutumia mashine za *Gamma Camera*; kununuliwa kwa mashine za kuchunguza matokeo ya tiba ya saratani kwa njia ya damu (*tumor markers*); kutibu wagonjwa 22,462 kwa kutumia tiba za mionzi na kemia, wagonjwa 14,384 tiba kemia na wagonjwa 21,362 walipata tiba ya kemia na mionzi; kutoa mafunzo kwa Watumishi 52 kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Mionzi; na kuendelea na ukarabati wa miundombinu ikiwemo mfumo wa majitaka.

(e) Taasisi ya Tiba ya Moyo ya Jakaya Kikwete

Hatua iliyofikiwa ni: kufanyiwa upasuaji kwa wagonjwa 1,410 wa moyo kupitia tundu dogo kwa kutumia mtambo maalum “Catheterization Laboratory”; kufanyiwa upasuaji kwa wagonjwa 101 wenye matatizo ya mishipa ya damu kwa njia ya kisasa (Vascular surgery); kukamilika kwa malipo ya ununuzi na ufungaji wa mtambo maalum “Catheterization Laboratory” (wa pili) kwa ajili ya kupasua moyo kupitia tundu dogo; kufanya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa 384; na kuendelea na upembuzi yakinifu wa mradi wa kupanua eneo la Mlongazila awamu ya pili kwa ajili ya wagonjwa wa moyo.

(f) Hospitali ya Rufaa Kibong’oto

Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa na kusambazwa kwa mashine 27 aina ya *HbA1c Analyser* katika vituo vya afya 27 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa wenye magonjwa ambata ya kifua kikuu na kisukari; kutolewa mafunzo ya kudhibiti magonjwa ambata ya kifua kikuu na kisukari kwa wataalam 89 katika mikoa mitatu (3) ya Iringa, Dar es Salaam na Kilimanjaro; kununuliwa kwa mashine nne (4) za uchunguzi wa madhara yatokanayo na dawa na mashine moja (1) ya *ultrasound* kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa; kupanua wigo na uelewa katika Tiba ya Kifua Kikuu Sugu bila utumiaji wa sindano kwa watumishi 361 wa afya kutoka Mikoa ya Mwanza, Iringa, Rukwa, Mtwara, Singida, Morogoro na Kilimanjaro; na kukamilika kwa michoro ya eneo itakapowekwa mashine ya CT – Scan.

(g) Hospitali ya Rufaa Bugando

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa Maabara ya kisasa ya uchunguzi wa magonjwa kupitia Vinasaba (DNA); kuzalishwa kwa maji tiba ambapo chupa 6,000 hadi 7,000 kwa mwezi za maji tiba ya aina tisa (9) tofauti; na kuzalishwa kwa mitungi 1,768 ya oksijeni kila mwezi kupitia mitambo miwili (2) iliyosimikwa hospitalini; na kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa wodi ya kulaza wagonjwa wa saratani.

(h) Hospitali ya Taifa Muhimbili

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa jengo la watoto wanaohitaji uangalizi maalum; kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Chuo cha Tiba Shirikishi - Muhimbili pamoja na hosteli za wauguzi; kukamilika kwa mchoro wa jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa binafsi; kumilika kwa asilimia 95 ya ujenzi wa jengo la kuwahudumia wagonjwa wenye magonjwa ya kuambukiza; kukamilika kwa upanuzi wa jengo la Huduma za Dharura (EMD); kugharamia mafunzo ya shahada za uzamili katika tiba kwa wataalam 81; kununuliwa kwa mashine na vitendea kazi vya huduma za kupandikiza uloto; kununuliwa kwa vifaa tiba mbalimbali ikiwa ni pamoja na *Endoscopy machine* na *full blood picture machine*; kutolewa kwa huduma ya kupandikizwa Figo kwa wagonjwa 13; kupandikizwa vifaa vya usikivu kwa wagonjwa tisa (9); na kupatiwa huduma ya matibabu kwa wagonjwa 288 ya *“interventional radiology”*.

(i) Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vyenye uwezo wa kulaza wagonjwa sita (6) kwa wakati mmoja kwa ajili ya huduma za kupandikiza uloto (Bone marrow transplant); kuanzishwa kwa chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (High Dependency Unit - HDU); kugharamia mafunzo ya shahada za uzamili kwa watumishi 45; kuendelea na ukarabati wa jengo la huduma za magonjwa ya akili; na kukamilika kwa ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa lita 960,000.

(j) Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa chumba cha wagonjwa wenye uangalizi maalum na kuwekewa vifaa, chumba maalum cha kisasa kwa ajili ya matibabu ya ubongo kupitia mishipa ya damu na kufungwa kwa mitambo ya kisasa ya upasuaji; kukamilika kwa chumba cha Tiba Mtandao (Telemedicine) na kufunga mitambo inayounganisha Hospitali za Rufaa za Mikoa na Wilaya; na kutolewa mafunzo kwa madaktari watatu (3) na wauguzi wawili (2) ya kutumia mitambo na teknolojia ya matibabu ya ubongo kupitia mishipa ya damu nchini China.

(k) Kujenga Hospitali ya Kanda ya Ziwa- Burigi

Hatua iliyofikiwa ni uwekaji wa mifumo ya TEHAMA, miundombinu ya umeme, marumaru, mifumo ya majitaka na kupaka rangi katika majengo yote ya hospitali ambapo utekelezaji umefikia asilimia 93.

(l) Udhibiti Magonjwa ya Kuambukiza

Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kununuliwa na kusambazwa kwa chanjo na vifaa

vya kutolea huduma za chanjo kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa ya kuambukiza kama vile surua, dondakoo na ugonjwa wa kupooza ambapo huduma za chanjo kwa watoto wenye umri wa chini ya mwaka mmoja zimetolewa kwa kiwango cha asilimia 99.

(m) Hospitali ya Benjamin Mkapa

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha Damu Salama, jengo la kusubiri ndugu wa wagonjwa, uzio wa hospitali, jengo la kuhifadhi maiti na ufungwaji wa vifaa vya kuhifadhi maiti; kutolewa kwa huduma ya upandikizaji wa figo kwa wagonjwa watano (5); na kutolewa kwa huduma ya uchunguzi na matibabu ya moyo kwa kutumia maabara maalumu (cathlab).

(n) Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi na kuanza kutumika kwa jengo la ghorofa mbili (2) la huduma za uchunguzi wa mionzi (Radiolojia); kuendelea na ukarabati na upanuzi wa jengo la kutolea huduma za dharura; na ujenzi wa jengo la wazazi umefikia asilimia 50.

(o) Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini - Mtwara

Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa awamu ya pili ya jengo la wagonjwa wa nje (OPD) umefikia asilimia 45.

(p) Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC)

Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa na kufungwa kwa mitambo mipya ya MRI, CT scan, Digital X-ray; kununuliwa kwa kinu cha kufua hewa ya Oksijeni chenye uwezo wa kuzalisha mitungi 400 kwa siku; ujenzi wa wodi maalumu ya wagonjwa wa saratani umefikia asilimia 70; na ujenzi wa vyumba vinne vya upasuaji umefikia asilimia 50.

(q) Ujenzi wa Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa Hospitali mpya za Wilaya 71 zikijumuisha hospitali tatu (3) za Uhuru (Dodoma), Mji wa Tunduma (Songwe) na Manispaa ya Ubungo (Dar es Salaam) ambapo utekelezaji katika baadhi ya hospitali umefikia asilimia kati ya 80 hadi 99, baadhi ya halmashauri ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji ikijumuisha kupaka rangi, kuunganisha umeme, maji na kuweka milango na madirisha; na ujenzi wa vituo vya afya 133 umekamilika.

3.3.3.3 Maendeleo ya Jamii

(a) Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa hosteli ya Sigimbi; kukarabatiwa kwa vyoo na mabafu, miundombinu ya umeme na bwalo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi; ukarabati wa nyumba nne (4) za watumishi, bwani la wasichana na maktaba katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli; kukamilika kwa ujenzi wa Maktaba katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole; na kukamilika kwa ujenzi wa Vituo nane (8) vya Kidigitali vya Ubunifu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Misungwi, Monduli, Rungemba, Buhare, Ruaha, Uyole na Mlale na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.

(b) Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake

Shughuli zilizotekelezwa ni: jumla ya Shilingi Bilioni 12.92 zimetolewa kwa wanawake wajasiriamali 14,295 kutoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri; na mikopo yenye masharti nafuu yenye thamani ya Shilingi 3,586,400,000.00 imetolewa kwa wanawake wajasiriamali 14,271 kupitia Dirisha la Wanawake lililoanzishwa katika Benki ya Posta Tanzania (TPB).

(c) Uhai na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuanzishwa kwa vikundi vya malezi 2,777 kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii katika kuzuia ukatili dhidi ya watoto; kuanzishwa kwa madawati ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto katika shule 17 za msingi na shule 8 za sekondari katika Mkoa wa Rukwa; kuanzishwa kwa vituo 125 vya kijamii vya malezi na makuzi ya awali ya watoto wadogo; kuanzishwa kwa Madawati ya Jinsia na Watoto 10 katika vituo vya Polisi vya Mbwani, Kimara, Mburahati, Kakonko, Kibondo, Kigoma Central, Mugumu Serengeti, Kiabakari na Butiama; na kuandaa Taarifa ya Sita ya Nchi ya Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto.

(d) Huduma za Ustawi wa Jamii

Hatua iliyofikiwa ni: kutambuliwa kwa watu wa kuaminika 295 ambao wanalea na kutoa huduma za msingi za chakula, malazi, matibabu na elimu kwa watoto 527 walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto yatima katika Halmashauri 19 za Wilaya za Magu, Kasulu, Musoma, Iringa, Mufindi, Njombe, Makete, Mbeya, Mbarali, Hai, Temeke, Arusha, Kakonko, Kibondo, Misenyi na Chunya; Halmashauri ya Mji wa Kasulu; Manispaa ya Iringa; na Jiji la Mbeya; kuanza ujenzi wa Makao ya Taifa ya Watoto katika eneo la Kikombo katika Jiji la Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa (Information Resource Center) katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

(e) Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuzinduliwa kwa mradi wa kutokomeza vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto katika maeneo ya masoko ambapo madawati ya mfano ya kutolea taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yameanzishwa katika maeneo ya masoko ya Jiji la Dodoma na Manispaa ya Shinyanga; Madawati ya Jinsia 153 yameanzishwa katika Jeshi la Magereza ili kuwezesha uwepo wa fursa sawa za kijinsia na kupambana na vitendo vya ukatili katika taasisi hiyo na kuzuia ukatili kwa wafungwa wakiwemo watoto walio kwenye magereza; kuanzishwa kwa Dawati la Jinsia katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili kushughulikia masuala ya rushwa ya ngono; na Madawati ya Jinsia matano yameanzishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu Mzumbe, Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ili kuzuia ukatili wa kijinsia hususan rushwa ya ngono.

3.3.3.4 Maji na Usafi wa Mazingira

(a) Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini

Hatua iliyofikiwa ni: kutambuliwa kwa vyanzo 35 vya maji; kuweka mipaka katika vyanzo 22 vya maji; kutangazwa kwa vidakio sita (6) vya maji katika Gazeti la Serikali; kupandwa kwa miche 16,400 ya miti rafiki ya maji; kuundwa kwa jumuiya 13 za Watumia Maji; kuanza maandalizi ya ujenzi wa bwawa la Farkwa ambapo wananchi 2,612 kati ya 2,868 wanaostahili fidia wamelipwa; na kukarabatiwa kwa vituo 53 vya kukusanyia takwimu za rasilimali za maji.

(b) Kuimarisha Huduma za Ubora wa Maji

Kazi zilizotekelezwa ni: kuendelea na ukarabati, ujenzi na uimarishaji wa ofisi za maji za mabonde na maabara za maji ambapo katika Bonde la Kati ujenzi umefikia (asilimia 99), Ruvuma na Pwani ya Kusini (asilimia 95), Ziwa Rukwa (asilimia 70), Ziwa Nyasa (asilimia 65), Rufiji Makao Makuu (asilimia 30), Rufiji Kimani na Mkoji (asilimia 85) na Wami-Ruvu (asilimia 60); kukusanywa na kuhakikiwa usalama kwa sampuli za maji 2,667 ambapo asilimia 95.8 zilikidhi viwango vinavyokubalika; kusambazwa kwa mitambo 200 ya kuondoa madini ya *Fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa kutumia chengachenga za mkaa wa mifupa ya Ng'ombe katika Mkoa wa Manyara maeneo ya Minjingu na Olasiti itakayonufaisha wananchi wapatao 1,600.

(c) Kuboresha Huduma za Maji Vijijini

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na utekelezaji wa miradi 802 ya huduma za maji

ambapo miradi 75 imekamilika na kuwezesha upatikanaji wa huduma za maji vijijini kufikia asilimia 70.1.

(d) Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Usambazaji wa Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa

Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa mradi wa usambazaji wa maji katika mji wa Serikali; kukamilishwa kwa rasimu ya usanifu wa kina wa miundombinu ya kuboresha huduma za maji jijini Dodoma; na kuendelea kwa ujenzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa ambapo Geita umekamilika, Njombe (asilimia 95); Songwe (asilimia 95); Kigoma (asilimia 93).

(e) Mradi wa Maji Masasi - Nachingwea

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa mradi ambapo wananchi 24,077 wanapata huduma ya maji na taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kutibu na kusafisha maji.

(f) Mradi wa Maji Same - Mwanga - Korogwe

Hatua iliyofikiwa ni: kufikiwa kwa asilimia 81 ya ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika miji ya Same utekelezaji umefikia asilimia 73 na Mwanga asilimia 38 mtawalia.

(g) Mradi wa Maji Kahama - Nzega - Tabora

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ulazaji wa mabomba makubwa ya kusafirisha maji kutoka Kijiji cha Solwa - Nzega, Nzega - Tabora na Nzega - Igunga kwa umbali wa kilomita 290.7; kukamilika kwa ujenzi wa matanki 17; ulazaji wa mabomba ya matawi umefikia asilimia 86; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji mijini na vijijini umefikia asilimia 98.6.

(h) Maji kutoka Ziwa Victoria - Shinyanga na Kahama

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ulazaji wa bomba la kusambazia maji katika miji ya Isaka, Tinde na Kagongwa na kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji katika vijiji vya Mwasekagi na Mwakatola.

(i) Kuboresha Huduma za Maji Dar es Salaam

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na usambazaji wa maji kutoka mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini katika jiji la Dar es salaam na maeneo ya Bagamoyo, Kibaha na Mlandizi; kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa dira za maji pamoja na vifaa vya uboreshaji wa huduma za maji; kuendelea na ujenzi wa bomba la maji kutoka Kibamba kwenda Kisarawe ambapo utekelezaji umefikia

wastani wa asilimia 74; kukamilika kwa ufungaji wa mita mpya 8,022 na matengenezo ya mita 5,231; ubadilishaji wa mabomba ya zamani kilomita 62 na kuongeza mtandao wa usambazaji kwa umbali wa kilomita 4.5; kuunganishiwa huduma ya maji kwa wateja wapya 27,000; na kupatikana kwa Mtaalam Mshauri atakayesimamia mradi wa Majitaka katika eneo la Jangwani.

(j) Mradi wa Maji wa Kimbiji na Mpera

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa visima 19 kati ya 20 vilivyopangwa kuchimbwa katika eneo la Kimbiji na Mpera; na kuanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza huduma ya maji kutoka katika visima vitano (5) vya awali vya Kimbiji kwenda kwa wananchi wa maeneo ya Kigamboni, Temeke, Mbagala na Mkuranga.

3.3.3.5 Ujuzi na Uwezeshaji

(a) Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi

Hatua iliyofikiwa ni: kutolewa kwa mafunzo ya miezi sita (6) ya uanagenzi kwa vijana 5,875 katika vyuo 17 nchini; kupatiwa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wa elimu ya juu 2,297 mahali pa kazi katika fani mbalimbali ikiwemo katika Mamlaka ya Mapato Tanzania; kutolewa kwa mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa vijana 8,900 kupitia teknolojia ya kitalu nyumba ambapo Vitalu Nyumba vya Mafunzo 87 vimejengwa katika halmashauri 84 za mikoa 12 nchini pamoja na kugharamia mafunzo ya kilimo cha kisasa nchini Israeli kwa vijana 100; vijana 1,390 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali katika mikoa nane (8); vijana 5,395 wamepewa mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo kupitia watathmini kutoka vyuo vya ufundi visivyomilikiwa na VETA (asilimia 65), watathmini kutoka vyuo vya VETA (asilimia 31) na watathmini kutoka maeneo ya kazi hususan Viwandani (asilimia 3); na kuendelea na maandalizi ya kutoa mafunzo ya ujuzi utokanao na maendeleo ya teknolojia na mbinu mpya za uzalishaji na utendaji kazi kwa wafanyakazi 450 waliopo sekta rasmi kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania - TPSF.

(b) Mfuko wa Maendeleo ya Vijana

Hatua iliyofikiwa ni: kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.2 kwa miradi 586 ya vikundi vya vijana 586 yenye jumla ya vijana 4,222 katika halmashauri za wilaya 155 Tanzania Bara; na kukamilika kwa mapitio ya Mwongozo Sanifu wa Stadi za Maisha kwa vijana walio nje ya mfumo wa elimu.

(c) Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III): Hatua iliyofikiwa ni: kutambuliwa na

kuandikishwa kwa jumla ya kaya 1,067,041 zenye wanakaya 5,130,001 katika vijiji na mitaa 9,627 kwenye halmashauri 159 za Tanzania Bara na kaya 32,248 zenye wanakaya 169,999 katika shehia 204 za Zanzibar; ruzuku ya fedha shilingi bilioni 968.73 imehawilishwa katika kaya hizo ambapo shilingi bilioni 935.94 ni kwa Tanzania Bara na shilingi bilioni 32.79 ni kwa Zanzibar.

Kazi nyingine zilizofanyika ni: kutekelezwa kwa miradi 8,384 ambayo imezalisha ajira za muda kwa kaya zipatazo 230,738 katika halmashauri 42 za Tanzania Bara na kaya 14,555 katika miradi 251 kwa Zanzibar; kuundwa kwa vikundi 16,366 vya kuweka akiba vyenye wanachama 226,050 kwenye halmashauri 44 za Tanzania Bara ambavyo vimeweka akiba ya shilingi bilioni 2.5 na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.13. Aidha, vikundi 1,957 vyenye wanachama 27,398 kutoka Zanzibar vimeweka akiba ya shilingi bilioni 1.1 na shilingi milioni 628.0 zimekopeshwa. Vile vile, miradi 47 ya kuendeleza miundombinu katika sekta za elimu, afya na maji Tanzania Bara na miradi 8 katika sekta za elimu na afya kwa Zanzibar imekamilika.

3.3.3.6 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

(a) Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

Shughuli zilizotekelezwa ni: kununuliwa kwa vifaa kwa ajili ya Chaneli ya Utalii zikiwemo kamera (12), *Drones* (2), Kompyuta mpakato maalum mbili (2), na vifaa viwili (2) vya kurushia matangazo mubashara (*Transmitters*); kununuliwa kwa magari mawili (2) na kuyafanyia marekebisho maalum ili yaendane na matakwa ya uandaaji wa vipindi vya utalii maeneo ya hifadhi; kupokelewa na kufungwa kwa vifaa kwa ajili ya mfumo wa TEHAMA; kukamilika kwa ukarabati wa jengo la studio; na kuingizwa katika kisimbuzi cha DSTV Chaneli ya Tanzania Safari.

(b) Habari kwa Umma

Shughuli iliyotekelezwa ni kuhabarisha umma kupitia vyombo vya habari mbalimbali vikiwemo redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii kwa kuelekezea mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kununuliwa kwa vifaa mbalimbali vya kukusanya, kuchakata na kutoa habari kwa wananchi.

3.3.3.7 Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

(a) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Ikolojia ili Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa tathmini ya athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwenye maeneo yote ya utekelezaji wa mradi; kupatiwa mafunzo wadau 54 ambao ni viongozi na wataalam mbalimbali wa Serikali, Taasisi za Elimu ya Juu, Asasi za

Kiraia na sekta binafsi kuhusu namna ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya Ikolojia; kufanyika kwa utafiti kwenye wilaya zinazotekeleza mradi (Mvomero, Kishapu, Simanjiro, Mpwapwa na Kaskazini A) kuhusu kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi; na kuanza kwa maandalizi ya mfumo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia nyenzo rahisi zinazopatikana.

(b) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi Kusimamia na Kupunguza Athari za Mazingira kwa Jamii za Vijijini Katika Sehemu Zenye Ukame

Hatua uliyofikiwa ni: kuendelea na taratibu za kupata wakandarasi wa kujenga skimu mbili za usambazaji wa maji katika Wilaya ya Mwanga na Kukarabati mita 1800 za njia za umwagiliaji katika Wilaya ya Same; kupatiwa mafunzo vikundi vya wakulima vyenye jumla ya watu 50 kuhusu uendeshaji endelevu wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika vijiji vya Mabilioni, Jipe, Makuyuni na Kambi ya Simba katika Wilaya ya Same; kuendelea na taratibu za kumpata Mtaalam Elekezi wa kufanya utafiti wa awali kuhusu uwezekano wa kupata athari za mabadiliko ya tabianchi; na kukamilika kwa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa mradi.

(c) Mradi wa Kusimamia Uhifadhi na Matumizi Endelevu ya Bonde la Ziwa Nyasa

Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa warsha ya kukuza uelewa wa usimamizi endelevu wa ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa; vikundi vya wakulima vimepatiwa mafunzo ya uandaaji wa bustani za miche ya miti, utengenezaji wa mizinga ya nyuki, uhifadhi wa misitu; vikundi vya wakulima katika kijiji cha Utengule vimepatiwa mafunzo ya njia bora za kilimo cha ngano katika chuo cha Utafiti Uyole; na wakulima wa kijiji cha Kipangala wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa mashamba ya korosho.

(d) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Upunguzaji wa Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa andiko la awamu ya pili ya Mpango wa Kuondosha Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni ifikapo 2030; na kufanyiwa mapitio kwa Kanuni za Mwaka 2007 za Udhhibiti wa Kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni ili kujumuisha marekebisho ya Kigali; na Kutolewa mafunzo kwa Maafisa forodha na Wasimamizi wa Sheria nchini kuhusu Kanuni za Usimamizi wa Mazingira na Utekelezaji wa Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal.

(e) Mradi wa Kutekeleza Mkataba wa Stockholm unaohusu Udhhibiti wa

Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira kwa Muda Mrefu

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa Mkakati wa Usimamizi wa Kemikali na Taka Hatarishi nchini; Kuandaliwa kwa Mfumo wa kimtandao wa upatikanaji wa taarifa za kemikali na taka nchini; na Kuandaliwa kwa taarifa ya tathmini ya uwezo wa kitaasisi katika udhibiti na usimamizi wa kemikali na taka nchini; Kukamilika kwa Mpango Kazi wa uelimishaji jamii kuhusu kemikali aina ya *Polychlorinated Biphenyl - PCB*, 2019; Kuandaliwa vipeperushi, mabango, vipindi vya redio na runinga kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu madhara ya PCB kwa afya ya binadamu na mazingira; Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa TANESCO; kuelimisha jamii juu ya madhara yatokanayo na kemikali za PCB katika mikoa tisa (9) nchini; na Kuandaliwa kwa Kanuni za Usimamizi wa Zebaki nchini.

3.3.3.8 Utawala Bora na Huduma kwa Wananchi

(a) Kuharakisha Azma ya Serikali Kuu Kuhamia Dodoma

Hatua iliyofikiwa ni: kuhamishwa kwa watumishi 15,361 wa Wizara, Ofisi ya Rais - Ikulu na taasisi zake, muhimili wa Bunge, vyombo vya ulinzi na usalama na baadhi ya taasisi za Serikali; kukamilika kwa ujenzi wa awali wa Ofisi za Serikali katika mji wa Serikali - Mtumba na kuendelea na maandalizi ya ujenzi awamu ya pili; kutolewa hati 67 za umiliki wa viwanja kwa mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa nchini na mashirika ya kimataifa zitakazowezesha kuanza ujenzi; kutolewa kwa hati 190,000 ili kuhakikisha uendelezaji wa maeneo unazingatia Sheria ya mipango miji; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara za lami na changarawe, umeme, masoko, usafiri na usafirishaji katika maeneo ya Dodoma ikiwemo Mji wa Serikali; na kukamilika kwa Mpango Kabambe wa jiji la Dodoma ambao utakidhi na kuendana na uendelezaji wa Makao Makuu ya nchi.

(b) Mfuko wa Bunge

- (i) **Ukarabati wa Majengo ya Bunge:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa ghorofa ya tano katika jengo la Utawala; kukamilika kwa ukarabati wa ofisi na kumbi za vikao vya Kamati za Bunge; kununuliwa na kufungwa kwa vifaa vya kituo cha matangazo ya redio na runinga; na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA (*Tablets 460 na Servers 2*) kwa ajili ya Bunge Mtandao (e-Parliament).
- (ii) **Mradi wa kulijengea uwezo Bunge:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Wabunge na Watumishi kwenye maeneo ya uandaaji wa Miswada, Sheria, na Bajeti; kutolewa kwa mafunzo ya utafiti wa Kibunge na ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge; kukamilika kwa mfumo wa

kieletroniki wa kutunza kumbukumbu za ofisi na mfumo wa kieletroniki wa Maktaba; na kuandaliwa kwa Mipango Mikakati ya Vyama vya hiari vya Kibunge (APNAC, TAPAFE, TYPF).

- (iii) **Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge:** shughuli zilizotekelezwa ni ununuzi na ufungaji wa mitambo ya usalama na ujenzi wa nyumba za makazi ya Viongozi wa Bunge ambapo nyumba ya Katibu wa Bunge imekamilika kwa asilimia 80 na ya Naibu Spika ipo katika hatua za awali za ujenzi.

(c) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi Wastaafu wa Kitaifa

Shughuli zilizotekelezwa ni kuendelea na ukarabati wa nyumba za marais wastaafu wa awamu ya pili na ya nne.

(d) Ujenzi wa Majengo ya Utawala kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa majengo 57 ya halmashauri kati ya 70 yaliyokuwa kwenye Mpango na kuendelea na ujenzi wa ofisi na makazi ya viongozi katika mikoa na wilaya mbalimbali nchini.

(e) Mifumo ya Kuhifadhi Taarifa za Watumishi wa Umma

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) – Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa vituo vya Kuhifadhi Mifumo ya Serikali Mtandao na Taarifa ambapo taasisi 23 zimewezesha kuhifadhi mifumo kwenye vituo hivyo na kufanya jumla ya taasisi zote kufikia 72.

(f) Utoaji Haki na Huduma za Kisheria

- (i) **Mfuko wa Mahakama:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Kigoma na Mara; kuendelea na ukarabati wa Mahakama Kuu ya Sumbawanga; kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi Manyara, Simiyu, Njombe na Geita; kukamilika kwa Mahakama za Wilaya za Longido, Chato, Geita, Bukombe, Bariadi, Njombe, Ruangwa, Kilwa, Chunya, Kondoa, Kasulu na mahakama za mwanzo za Mkunya (Newala), Magoma (Korogwe), Msanzina Mtowisa (Sumbawanga), Uyole (Mbeya) na Mlowo (Mbozi); kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Kasulu, Wanging'ombe, Bunda, Makete, Sikonge, Kilindi na Rungwe; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba tatu (3) za kufikia Majaji mkoani Mtwara; kukamilika kwa

ujenzi wa nyumba mbili (2) za Majaji Kigoma na nyumba mbili (2) za Majaji Musoma; kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba mbili (2) za Mahakimu Loliondo; kuanza kwa ujenzi wa vituo sita (6) vya Haki Jumuishi (Integrated Justice Centre) katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Dar es Salaam, Arusha na Dodoma; kuendelea na ujenzi wa mabweni katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama na kukamilika kwa Mfumo Mpya wa Usajili wa Mashauri (Judiciary Statistics Dashboard System).

- (ii) **Usalama wa Raia:** hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa majengo sita ya ghorofa (yenye floor 3 kila moja) kwa ajili ya kuishi familia 24 za Askari Musoma – Mara katika kitalu namba mbili ambapo askari wameanza kutumia majengo hayo; kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi ya askari Mabatini Mwanza ambao umefikia hatua za umaliziaji wa kupaka rangi, kuweka makabati, madirisha, na kuweka mabomba kwa ajili ya mfumo wa maji; kukamilika kwa ujenzi wa bweni la kuishi wanafunzi 180, madarasa ya wanafunzi 140 na ofisi za walimu na stoo katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam na tayari vimekabidhiwa; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 400 za makazi ya askari polisi nchi nzima; kuendelea na ukamilishaji wa kituo cha Zimamoto na Uokoaji Wilayani Chato (Geita); ununuzi wa magari matano (5) na boti mbili (2) pamoja na vifaa vya kuzimia moto; na kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Uhamiaji Jijini Dodoma ambao umefikia asilimia 35.
- (iii) **Usajili wa Vizazi na Vifo:** hatua iliyofikiwa ni kusajiliwa kwa vizazi 4,257,705 vya watoto wenye umri chini ya miaka 5 katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Shinyanga, Geita, Lindi, Mtwara, Mara, Simiyu, Dodoma, Singida, Morogoro, na Pwani ambapo kiwango cha usajili kimeongezeka kutoka asilimia 38 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 45 mwaka 2019; kusajiliwa kwa vizazi 325,583 vya watoto walio shuleni katika wilaya 19 za Kigamboni, Temeke, Kinondoni, Ilala, Iringa, Kilindi, Ludewa, Makete, Wang'ing'ombe, Njombe, Songea, Singida, Musoma, Tarime, Bunda, Bariadi, Maswa, Kahama na Manyoni; kusajili na kutoa vyeti vya vifo 52,753; na kuboreshwa kwa usajili wa vizazi na vifo kwa kutumia Mfumo wa TEHAMA kwa kufunga mfumo wa kielektroniki wa Usajili wa vizazi na vifo katika vituo 166.
- (iv) **Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Haki na kulinda Haki za Binadamu.** hatua zilizofikiwa ni kuimarika kwa Mifumo ya Utoaji Haki na kulinda Haki za Binadamu; kupungua kwa mianya ya rushwa

kwenye Mifumo ya Haki-Jinai ambayo ni kikwazo katika kupiga vita umaskini; kuanza kwa huduma ya mahakama inayotembea kwa mikoa ya Dar es salaam na Mwanza; kutolewa kwa mafunzo ya kujenga uwezo wa Kamati za Ulinzi wa wanawake na watoto katika wilaya za Kasulu na Sengerema; kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya msaada wa kisheria ili kutoa fursa na mazingira mazuri ya kupata haki; na kutolewa kwa mafunzo kuhusu sheria ya huduma ya msaada wa sheria kwa watendaji wa Serikali zaidi ya 1,080 ili kuwajengea uwezo watendaji wa vijiji, vitongoji na mitaa.

- (v) **Mradi wa Haki Mtandao (e-Justice):** shughuli zilizotekelezwa ni kukamilika kwa Mfumo wa Kielekroniki wa Ukusanyaji Taarifa za Usajili wa Mashauri Mahakamani na kuhifadhi takwimu za Mahakama; kuimarishwa kwa matumizi ya TEHAMA katika mifumo ya utoaji haki; na kuanzishwa kwa kanzidata ya Wanasheria walio katika utumishi wa umma ili kuharakisha upatikanaji wa huduma za utoaji haki nchini.

(g) Vitambulisho vya Taifa

Shughuli zilizotekelezwa ni: kutoa namba za utambulisho na Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wenye umri wa miaka 18 na kuendelea ambapo jumla ya watu 21,823,026 wametambuliwa na kusajiliwa, namba za utambulisho 18,137,246 zimetolewa na vitambulisho 6,144,549 vimezalishwa; kuendelea na usajili na utambuzi wa wakimbizi katika kambi (Nyarugusu, Mtendeli, Nduta) na makazi (Mishamo, Ulyankulu, Katumba) na wakimbizi wenye vibali vya kuishi Dar es Salaam ambapo jumla ya wakimbizi 207,644 wamesajiliwa; kuanza usajili wa majaribio kwa wafungwa, ambapo wafungwa 380 walisajiliwa katika Magereza ya Bagamoyo (Pwani) na Isanga (Dodoma); kuunganishwa kwa ofisi 15 za usajili na utambuzi za Wilaya na Makao Makuu kupitia Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa; kununuliwa kwa vifaa mbalimbali kwa ajili ya usajili ikijumuisha vifaa vya TEHAMA, gari moja (1) na mashine mbili mpya za uchapaji wa Vitambulisho vya Taifa zenye uwezo wa kuzalisha vitambulisho 9,000 kwa saa; kuendelea na uunganishaji wa mifumo ya mawasiliano kati ya taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi ili kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali ambapo jumla ya Taasisi 69 zimeunganishwa; na kwa kutumia mfumo wa usajili na utambuzi, Kampuni za Simu nchini zimefanikiwa kusajili laini za simu 37,297,930 kwa kutumia alama za vidole.

(h) Uhamiaji

Shughuli zilizotekelezwa ni ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji Jijini Dodoma

umefikia asilimia 35, ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi umefikia asilimia 53, ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Geita umefikia asilimia 60, ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara umefikia asilimia 21, ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara umefikia asilimia 65, ujenzi wa nyumba ya makazi ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza umefikia asilimia 98, ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Masaki – Dar es Salaam umefikia asilimia 75, na ukarabati wa Nyumba za Makazi ya Watumishi zilizopo Ibinzamata Shinyanga umefikia asilimia 85.

3.3.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

3.3.4.1 Miundombinu

A. Reli

(a) Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ukarabati wa njia, madaraja na ujenzi wa makalavati kati ya Dar es Salaam – Isaka (km 970) ambapo kwa upande wa vipande vya Dar es Salaam - Ngerengere (km 145), Ngerengere - Kilosa (km 138), Kilosa - Itigi (km 343) na Itigi - Isaka (km 344) utekelezaji kwa ujumla umefikia asilimia 86.

(b) Ufufuaji wa Njia ya Reli ya Tanga – Arusha (km 439)

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa kipande cha Tanga – Moshi (km 359) ambacho kimeanza kufanya kazi ya kusafirisha abiria na mizigo; kukamilika kwa ukarabati wa kipande cha Moshi – Arusha (km 86) kwa kubadili reli na mataruma, kurejesha madaraja na makalavati, stesheni na kufungua mifereji ya maji ya mvua.

(c) Ukarabati wa Mabehewa

Hatua iliyofikiwa ni kukarabatiwa kwa mabehewa 133 kati ya mabehewa 240 yatakayotumika kwenye njia kuu ya reli ya kati ambapo mabehewa 200 yamekarabatiwa kwa fedha za mfuko wa reli na mabehewa 40 kwa makubaliano ya kibiashara na *World Food Programme*.

(d) Kuboresha Miundombinu ya Reli ya TAZARA

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ununuzi wa mitambo (*Excavator, Dumper Track na Drill Rig*) ambayo imeanza kufanya kazi; na kununuziwa *traction motors* 42 kwa ajili ya injini saba (7) ambapo *traction motors* zote 42 zimepokelewa na kazi ya ukarabati wa injini inaendelea; ununuzi wa vichwa vipya vinne (4) vya Treni ya njia kuu, vichwa vinne (4) vya sogeza, mabehewa mapya 18 ya abiria, ukarabati wa mabehewa 400 ya mizigo, uboreshaji wa Kituo cha Reli cha Fuga na nyumba nane

(8) za watumishi kwa ajili ya kuhudumia Mradi mkubwa wa Umeme wa Mto Rufiji.

B. Barabara na Madaraja

Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi

- (i) **Barabara ya Kidatu - Ifakara - Lupilo - Mahenge/Malinyi - Londo - Lumecha/Songea (km 499):** ujenzi umefikia asilimia 12 kwa sehemu ya Kidatu - Ifakara (km 66.9).
- (ii) **Barabara ya Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 370):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa sehemu ya Tabora - Sikonge (km 30); na kuendelea na utekelezaji katika sehemu za Usesula - Komanga (km 108) ambapo ujenzi umefikia asilimia 40, Komanga - Kasinde (km 108) asilimia 56, na Kasinde - Mpanda (km 108) asilimia 44.5.
- (iii) **Barabara ya Makutano - Natta - Mugumu (km 125)/Loliondo - Mto wa Mbu (km 213):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi sehemu ya Makutano - Sanzate (km 50) ambapo umefikia asilimia 82.5, Mto wa Mbu - Loliondo sehemu ya Wasso - Sale Junction (km 49) umefikia asilimia 46. Aidha, ujenzi wa barabara kwa sehemu ya Sanzate - Natta - Mugumu (km 85) upo katika hatua ya kumpata Mkandarasi.
- (iv) **Barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora (km 259.7):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi sehemu za Tabora - Nyahua (km 85) na Manyoni - Itigi - Chaya (km 89.35). Aidha, ujenzi kwa sehemu ya Nyahua - Chaya (km 85.4) umefikia asilimia 65.
- (v) **Barabara ya Itoni - Ludewa - Manda (km 211):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa kiwango cha lami na zege katika sehemu ya Lusitu - Mawengi (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 42.4.
- (vi) **Barabara ya Dodoma - Mtera - Iringa (km 260):** mradi umekamilika na kazi za ujenzi zimeanza katika barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3).
- (vii) **Barabara ya Mbeya - Makongolosi - Rungwa - Itigi - Mkiwa (km 577.90):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa sehemu za Chunya - Makongolosi (km 43) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 61.
- (viii) **Barabara ya Kigoma - Kidahwe - Uvinza - Kaliua - Tabora (km 389.7):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Urambo - Kaliua (km 28) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80. Vile vile, mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Chagu - Kazilambwa (km 36) umesainiwa na mkandarasi yuko katika maandalizi ya kuanza kazi.
- (ix) **Barabara ya Mtwara - Masasi - Songea - Mbamba Bay (km 1,211.70):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Mbinga - Mbamba Bay (km 66) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52 na sehemu ya Mtwara - Mnivata

- (km 50) asilimia 76; na kukamilika kwa kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 107).
- (x) **Barabara ya Msimba - Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Igawa - Mbarali - Ubaruku (km 16) sehemu ya Mbarali - Ubaruku (km 8.9). Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe - Moronga (km 53.9) umefikia asilimia 64 na Moronga - Makete (km 53.5) umefikia asilimia 47.
- (xi) **Dumila - Kilosa - Mikumi(km 141):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi sehemu ya Rudewa - Kilosa (km 24) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20.

Barabara zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani

- (i) **Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 112):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 112) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95.
- (ii) **Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai - Kamwanga /Bomang'ombe - Sanya Juu (km 330.31):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu - Elerai (km 32.2); Kiboroloni - Kiharara - Tsuduni - Kidia (km 10.8); Kwa Sadala - Masama - Machame Junction (km 16) . Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa 3 zilizobaki kati ya kilometa 14 za barabara ya Kijenge - Usa River unaendelea na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Mianzini - Ngaramtoni (km 18) yanaendelea.
- (iii) **Barabara ya Isaka - Lusahunga (km 474):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa sehemu ya Ushirombo - Lusahunga (km 110) na kuendelea na matengenezo ya dharura katika maeneo korofi sehemu ya Lusahunga - Rusumo (km 92).
- (iv) **Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 517.4):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mpanda - Mishamo (km 100) sehemu ya Mpanda - Ifukutwa - Vikonge (km 30) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87.
- (v) **Barabara ya Nyanguge - Musoma, na Michepuo ya Usagara - Kisesa na Bulamba - Kisorya (km 483.9):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nansio - Kisorya - Bunda - Nyamuswa sehemu ya Kisorya - Bulamba (km 51) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 84.
- (vi) **Barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 265.8):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Maswa - Bariadi (km 49.7) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 77.6.
- (vii) **Barabara ya Kidahwe - Kasulu - Kibondo - Nyakanazi (km 434.25):** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara sehemu za Kidahwe - Kasulu (km 63) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.5 na Nyakanazi - Kibondo

(km 50) asilimia 78; na kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kabingo – Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 260) na barabara sehemu ya njia panda ya Nduta - Kibondo Mjini (km 25.6).

- (viii) **Barabara ya Usagara - Geita - Buzirayombo - Kyamyorwa (km 388.00):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Geita – Bulyanhulu *Junction* (km 58.3), Bulyanhulu *Junction* – Kahama (km 61.7) na Nyamirembe *Port* – Katoke (km 50).

Barabara za Mikoa

Hatua iliyofikiwa ni kujengwa kwa km 24.23 za barabara kwa kiwango cha lami, kukarabatiwa kwa km 255.21 kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Barabara za Vijijini na Mijini

Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 169.66)

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66) sehemu ya Kibamba – Mloganzila (km 4.0) na barabara ya Ardhi – Makongo – Goba (km 9.0) sehemu ya Goba – Makongo (km 4.0); ujenzi wa barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7) sehemu ya Kitunda– Kivule (km 3.2) umefikia asilimia 40. Aidha, kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni umekamilika kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Mjimwema – Kimbiji (km 27.0) na Kongowe – Mjimwema – Kivukoni (km 25.1).

Vile vile, mradi wa upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) ujenzi umefikia asilimia 80 ya upanuzi wa sehemu ya Kimara – Kiluvya (km 19.2) kuwa njia nane na upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji.

Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Kasi (Awamu ya Pili):

Hatua ya ujenzi wa awamu ya pili Lot 1 unaohusisha barabara zenye urefu wa km 20.3 umefikia asilimia 3.3; na kwa Lot 2 inayohusisha ujenzi wa majengo (vituo 2, yadi 1 na vituo mlisho 4) umefikia asilimia 22.

Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyover) Jijini Dar es Salaam

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi kwa mradi wa *Interchange* katika makutano ya Ubungo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 77.

Ujenzi wa Madaraja

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa madaraja ya Mara (Mara), na Magara (Manyara); na kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Ruhuhu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 86, Mitomoni (asilimia 75), Kitengule (asilimia 50), Msingi (asilimia 40), Selander (asilimia 38.2) na *New Wami* (asilimia 39).

C. Ujenzi wa Nyumba za Serikali

Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa nyumba moja ya Jaji Jijini Dar es Salaam umekamilika; ujenzi wa nyumba 5 za Majaji zipo katika hatua mbalimbali; ujenzi wa nyumba za Makazi ya Magomeni "*Quarters*" umefikia asilimia 70; awamu ya kwanza ya ukarabati wa karakana ya TBA Dodoma imekamilika kwa asilimia 90; na usanifu wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika Mji wa Serikali - Mtumba Jijini Dodoma upo kwenye hatua ya mapitio ya michoro na gharama.

D. Usafiri Majini

- (i) **Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika kivuko cha Lindi - Kitunda; na kuanza kwa awamu ya pili ya upanuzi wa jengo la abiria na maegesho ya kivuko cha Kigamboni - Magogoni na ujenzi wa maegesho ya Bukondo.
- (ii) **Ujenzi na Ununuzi wa Vivuko Vipya:** hatua iliyofikiwa ni kuanza ujenzi wa vivuko vipya vya Nyamisati-Mafia (asilimia 40), Bugolora-Ukara (asilimia 70); ununuzi wa boti mpya za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana), Magogoni - Kigamboni pamoja na boti moja ya uokozi kwa kivuko cha Lindi - Kitunda unaendelea.
- (iii) **Ukarabati wa Vivuko:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa kivuko cha MV Kigamboni na kuendelea na ukarabati wa vivuko vya MV Sengerema (asilimia 60) na MV Misungwi (asilimia 35); na kuendelea na taratibu za kupata mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa MV Tegemeo, MV Ujenzi, MV Musoma, MV KIU na MV Mara.
- (iv) **Ununuzi na Ukarakabati wa Meli katika Maziwa Makuu:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 60; ujenzi wa chelezo umefikia asilimia 98; ukarakabati wa meli ya MV Victoria umefikia asilimia 98 na MV Butiama asilimia 98; na kukamilika kwa ujenzi wa Meli moja mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 katika Ziwa Nyasa.

Aidha, makandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV Umoja na MV Serengeti katika Ziwa Victoria wamepatikana na maandalizi ya mikataba kwa ajili ya ukarabati wa meli hizo yamekamilika; na mikataba kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 pamoja na ukarabati wa meli ya MV Liemba katika Ziwa Tanganyika imekamilika.

E. Bandari

- (i) **Bandari ya Dar es Salaam:** hatua zilizofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa gati Na. 1, 2, 3 na 4; kukamilika kwa ujenzi wa gati ya kupakia na kupakua magari(Ro-Ro); kuendelea na ujenzi wa gati Na. 5, 6 na 7 ikijumuisha ununuzi wa vifaa mbalimbali vinavyotumika katika kuhudumia mizigo bandarini.
- (ii) **Bandari ya Tanga:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa asilimia 40 ya kazi ya uboreshaji wa bandari awamu ya kwanza unaojumuisha uchimbaji wa lango la kuingilia meli, utafiti wa athari za kimazingira na ununuzi wa mitambo. Vile vile, maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya gati la mafuta ghafi kutoka Uganda yanaendelea.
- (iii) **Bandari ya Mtwara:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa gati lenye urefu wa mita 300 la kuhudumia shehena mchanganyiko ambapo utekelezaji umefikia asilimia 61.
- (iv) **Bandari Kavu katika eneo la Ruvu:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa yadi, njia ya reli na ofisi za muda kwenye eneo la hekta tano (5). Maandalizi kwa ajili ya Bandari Kavu kuanza kutumika Julai, 2020 yapo kwenye hatua za mwisho. Aidha, usanifu wa matumizi bora ya eneo lote la bandari kavu umefikia asilimia 58.
- (v) **Bandari za Maziwa Makuu**
Ziwa Victoria: hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Lushamba, Ntama, Nyamirembe, Magarine na gati la majahazi Mwigobero; kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo na meli, ukarabati wa majengo na ofisi za bandari, na ujenzi wa mitaro katika bandari ya Mwanza South; kuendelea na taratibu za utwaaji ardhi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na jengo la abiria katika bandari ya Kyamkwikwi; kuendelea na uboreshaji wa sehemu ya kushukia abiria bandari ya Mwanza North; na kuendelea na ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya Mwanza South.

Ziwa Tanganyika: hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa uboreshaji wa gati la Kagunga; kufikia asilimia 98 kwa ujenzi wa gati la Sibwesa; kufikia asilimia 56 kwa ujenzi wa miundombinu na gati la Bandari ya Kabwe; kufikia asilimia 53 ya ujenzi wa miundombinu na gati la Bandari ya Lagosa; kuendelea kwa ujenzi wa gati za Kibirizi, Ujiji na Ofisi ya Meneja wa Bandari-Kigoma; kuendelea na ujenzi wa barabara za bandari ya Kagunga; na uboreshaji na upanuzi wa Bandari ya Kasanga umefikia asilimia 10. Vile vile, upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati la Karema ili kuunganishwa na Bandari ya Kalemie nchini Kongo (DRC) umekamilika.

Ziwa Nyasa: hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu kwa ajili ya maegesho katika bandari ya Kiwira; kuendelea na ujenzi wa gati la Ndumbi; na kufikia hatua za mwisho za upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati za Mbamba Bay, Manda na Matema.

F. Usafiri wa Anga

- (i) **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro:** hatua iliyofikiwa ni kufungwa kwa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa maegesho ya magari; na kuendelea na taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa tabaka la juu la barabara ya kuruka na kutua ndege.
- (ii) **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo, uzio wa kiwanja, jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani na kufunga taa za kuongozea ndege.
- (iii) **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, ujenzi wa barabara ya kuingilia kiwanjani na maegesho ya magari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 33.
- (iv) **Kiwanja cha Ndege cha Kigoma:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege pamoja na miundombinu yake ikiwemo mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa kituo kidogo cha umeme, ujenzi wa kituo cha uangalizi wa hali ya hewa pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingilia uwanjani na maegesho ya magari.
- (v) **Viwanja vya Ndege vya Sumbawanga na Shinyanga:** hatua iliyofikiwa ni kusainiwa kwa mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali

- ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.
- (vi) **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Songwe:** hatua iliyofikiwa ni kusainiwa kwa mikataba kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na ufungaji wa taa za kuongozea ndege. Vile vile, kuendelea na taratibu za ununuzi ili kumpata Mkandarasi atakayemalizia ujenzi wa jengo la abiria.
 - (vii) **Viwanja vya Ndege vya Mikoa:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka Ndege kwa kiwango cha changarawe kwa kiwanja cha Nachingwea; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Geita (asilimia 78) na Songea (asilimia 34).
 - (viii) **Kuboresha huduma za Ulinzi na Usalama katika Viwanja vya Ndege:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ufungaji wa Mifumo ya Kamera za Kiusalama (CCTV) katika kiwanja cha ndege cha Dodoma; ununuzi wa mitambo miwili (2) ya ukaguzi wa abiria na mizigo kwa viwanja vya ndege vya Iringa na Songea; na ununuzi wa vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya viwanja vya ndege vya Arusha, Songea, Kahama, Mafia na Iringa.
 - (ix) **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa jengo la pili la abiria.
 - (x) **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na uhakiki kwa ajili ya ulipaji wa fidia na taratibu za awali za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.
 - (xi) **Kiwanja cha Ndege Tabora:** hatua iliyofikiwa ni kusainiwa kwa mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua, jengo jipya la abiria, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, barabara ya kiungio na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.
 - (xii) **Ufungaji wa Rada Nne za Kuongozea Ndege za Kiraia (JNIA, KIA, Mwanza na Songwe):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa miundombinu ya rada, ufungaji wa mitambo, kuendelea kwa majaribio ya mitambo kwa rada za kuongozea ndege za kiraia katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Mwanza. Rada ya Songwe itakamilishwa baadaya anga la Ufaransa kufunguliwa na wataalam wa mkandarasi kuruhusiwa kuja nchini.
 - (xiii) **Ununuzi wa Rada Tatu (3) za Hali ya Hewa:** hatua iliyofikiwa ni kulipa asilimia 90 ya mkataba wa ununuzi wa Rada tatu (3) za hali ya hewa zitakazofungwa Mtwara, Mbeya na Kigoma na kupokelewa kwa vifaa mbalimbali vya hali ya hewa. Rada ya Mtwara imewasili nchini na taratibu za kuifunga zitakamilishwa baada ya wataalamu wa mkandarasi kutoka

Marekani kuweza kuja nchini.

G. Nishati

Miradi ya Kufua Umeme

- (i) **Mradi wa Kinyerezi I Extension - MW 185:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ufungaji wa mitambo yote minne (4); na kuendelea na upanuzi (upgrade) wa njia ya msongo wa KV 132 kutoka Kinyerezi I hadi kituo cha kupoza umeme cha Gongo la Mboto ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85.
- (ii) **Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo - MW 80:** hatua iliyofikiwa ni kuendelea na kazi ya kufunga mitambo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52; kukamilika kwa milango ya kuingiza na kuchepusha maji (spillway and intake gates); kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi; na kukamilika kwa asilimia 56 ya kazi ya uchimbaji wa handaki la kupitishia maji. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 61.
- (iii) **Mradi wa Kakono - MW 87:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa kazi za usanifu wa mradi.
- (iv) **Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kikonge - MW 300:** kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa Tathmini ya Mazingira ya Kimkakati (Strategic Environmental & Social Assessment - SESA); na kuendelea na upembuzi yakinifu.
- (v) **Mradi wa Kufua Umeme wa Malagarasi - MW 45 (Kigoma):** hatua iliyofikiwa ni kukamilisha uhuishaji wa upembuzi yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme pamoja na uthamini katika kilomita 33 toka kijiji cha Mazungwe hadi Kidahwe.
- (vi) **Mradi wa Ruhudji - MW 358 (Njombe):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa uhuishaji wa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa mradi pamoja na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi.
- (vii) **Umeme wa Jotoardhi - Ngozi (Mbeya):** hatua iliyofikiwa ni kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa Mpango Kazi wa uchorongaji na kusimamia uchorongaji; usanifu wa visima; uainishaji wa vigezo vya mitambo kwa ajili ya uchorongaji; kununua mtambo wa uchorongaji wa visima; kubainisha njia ya miundombinu ya barabara na maji pamoja na kukamilisha usanifu wa awali wa miundombinu.

Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme

- (i) **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Makambako - Songea:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa

- msongo wa kV 220, yenye urefu wa kilomita 250 kutoka Makambako hadi Songea kupitia Madaba pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Madaba na Songea na upanuzi wa kituo cha Makambako; na kukamilika kwa kazi ya kufunga *reactor* na *distribution panel* katika kituo cha Madaba.
- (ii) **Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendu Kasi (Standard Gauge Railway - SGR) Awamu ya Kwanza (Lot I) kV 220:** kazi zilizofanyika ni pamoja na kujengwa kwa misingi ya minara 444 kati ya 456 ya umeme (Tower Foundations) na minara (Towers erections) 404 kati ya 456; uvutaji wa nyaya kwa urefu wa kilomita 88 kati ya 160 na kulipa fidia wananchi waliopisha mradi ambapo utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 89.
- (iii) **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 - North West Grid Extension (Iringa - Mbeya - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Nyakanazi):** hatua iliyofikiwa ni kukamilisha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kuwaunganishia umeme wateja 5,000 katika mkoa wa Kigoma; na kukamilika kwa tathmini na kuanza kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi katika kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe. Vile vile, kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Sumbawanga - Mpanda - Kigoma kV 400 taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa ripoti ya mazingira zinaendelea.
- (iv) **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Geita - Nyakanazi (North West Grid):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upimaji wa udongo na usanifu wa mradi; kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa kituo cha kupoza umeme.
- (v) **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Bulyanhulu - Geita:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi; ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme pamoja na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme umefikia asilimia 82 na kazi ya kuvuta nyaya kwa ajili ya usambazaji wa umeme vijijini imefikia asilimia 92. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 85.
- (vi) **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji - Chalinze - Dodoma:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi.
- (vii) **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida - Arusha - Namanga:** hatua iliyofikiwa ni kujengwa kwa nguzo (Tower) 621 kati ya 1,072 ambapo utekelezaji wa mradi wote umefikia asilimia 67. Aidha, utekelezaji wa mradi huu unaenda sambamba na utekelezaji wa mradi wa Backbone awamu ya pili (Backbone Phase II) unaolenga kuongeza uwezo

(Upgrade) wa vituo vya kupoza umeme kutoka kV 220 mpaka kV 400 katika mikoja ya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 83.

- (viii) **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Kinyerezi - Chalinze:** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi.
- (ix) **Mradi kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini na Makao Makuu ya Wilaya (REA - III):** hatua iliyofikiwa ni kuunganishiwa umeme kwa vijiji 7,094 na hivyo kufanya vijiji vilivyopatiwa umeme nchini kote kufikia 9,112.

Miradi ya Kusambaza Gesi Asilia Viwandani

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia (trunk-lines) yenye urefu wa kilomita 18 yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 10,000 wa majumbani na viwandani katika Mkoa wa Dar es Salaam katika maeneo ya Sinza, Mlalakuwa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ubungo Msewe na nyumba za Polisi Kurasini ambapo hadi kufikia Aprili, 2020, jumla ya wateja wapatao 500 wa majumbani na viwanda 48 vimeunganishwa na gesi asili.

Utafiti katika Vitalu vya Eyasi - Wembere na Mnazi Bay Kaskazini

Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha tathmini ya taarifa za kijiolojia na kijiiofizikia na kumpata Mtaalamu Mshauri wa uchorongaji katika kitalu cha Mnazi Bay; na kukamilisha uchorongaji wa visima viwili (2) vifupi katika maeneo ya Kining'inila - Igunga na Nyaranja - Meatu katika Kitalu cha Eyasi - Wembere.

3.3.4.2 Ardhi na Maeneo ya Uwekezaji na Biashara

(a) Progamu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa upimaji wa viwanja 37,351 katika halmashauri za Mbeya Jiji 521, Kahama 3,526, Shinyanga 308, Msalala 302, Bariadi 1,446, Ilemela 1,200, Sengerema 1,800, Misungwi 71, Magu 1,535, Ukerewe 1434, Geita 2,100, Chato 2,528, Bukombe 2,767, Iringa 375, Sumbawanga 254, Njombe 4,048, Simanjiro 978, Halmashauri ya Mji wa Nzega 2,463, Wilaya ya Nzega 4,000, Songea 138, Namtumbo 4,659, Kondo 172, na Gairo 799; kuzinduliwa rasmi kwa Mipango Kabambe ya Jiji la Dodoma na Mji wa Tunduma na kuidhinishwa kwa Mipango Kabambe ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa za Kigoma/ Ujiji, Bukoba, Shinyanga na Sumbawanga na Miji ya Geita, Njombe na Babati; kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi kwa kuanzisha ofisi za ardhi za mikoja 26; kuandaliwa na kuidhinishwa kwa michoro ya Mipango Miji 334 ya urasimishaji yenye jumla ya viwanja 148,000 na kutoa hatimiliki 3,469 kupitia mfumo wa kielektroniki katika Jiji la Dar es

Salaam; kuandaliwa kwa mipango - kina ya vitovu vya vijiji katika vijiji vitano (5) katika Wilaya ya Morogoro na kutoa hati ya Hakimiliki za Kimila 5,845.

Vile vile, vipande vya ardhi 134,239 vilitambuliwa na leseni za makazi 868 zilitolewa katika jiji la Dar es Salaam; kutatuliwa kwa migogoro ipatayo 1,544 kiutawala ambapo jumla ya vijiji 920 kati ya 975 vilivyokuwa na migogoro ya matumizi ya ardhi na maeneo ya hifadhi na mapori vilihalalishwa ardhi rasmi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

(b) Programu ya Umilikishaji wa Ardhi

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuandaliwa kwa taarifa 59 za Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kijiji na taarifa za Mipango Kina ya Makazi ya Vijiji 86; kuchapishwa kwa Hati za Hakimiliki ya Kimila (CCRO) 20,841 katika Wilaya za Kilombero (7,191), Ulanga (7,523) na Malinyi (6,127); kusajiliwa kwa CCRO 35,497 katika Wilaya za Kilombero (9,154), Ulanga (14,418) na Malinyi (11,925); na kuchukuliwa kwa CCRO 43,897 na wamiliki katika Wilaya za Kilombero (15,707), Ulanga (11,736) na Malinyi (16,454).

Vile vile, kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Ardhi za halmashauri za wilaya za Kilombero (asilimia 90), Ulanga (asilimia 70) na Malinyi (asilimia 60); na kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Baraza la Ardhi na Nyumba ya Wilaya ya Kilombero.

(c) Maeneo ya Uwekezaji

Hatua iliyofikiwa ni kutenga jumla ya hekta 854,821.59 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo.

(d) Mipaka ya Kimataifa

Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kufanyika kwa vikao vya wataalam (Joint Technical Committee) kati ya Tanzania na nchi za Kenya na Burundi. Matokeo ya vikao hivyo ni makubaliano ya kuimarisha mipaka ambapo kwa Tanzania na Kenya kilometa 128 kutoka Ziwa Natron hadi Namanga zitakamilishwa. Kwa upande wa Tanzania na Burundi, kilometa 100 zitakamilishwa kutoka Kagunga hadi Manyovu.

3.3.4.3 Huduma za Fedha, Biashara na Masoko

A. Huduma za Fedha

(a) Benki ya Maendeleo ya TIB

Hatua iliyofikiwa ni Benki ya Maendeleo ya TIB kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 554.68 na TIB Corporate Bank kutoa mikopo yenye thamani ya

shilingi bilioni 165.6 mwaka 2019 kwa ajili ya shughuli mbalimbali zilizohusiana na kilimo, viwanda, madini, biashara na watu binafsi. Aidha, mapato ya benki ya Maendeleo ya TIB kwa mwaka 2019 yalikuwa shilingi bilioni 79.92.

(b) Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB

Hatua iliyofikiwa ni: kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 59.59 katika kipindi cha mwaka 2019 ambapo imewanufaisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa wa mazao na wafugaji katika mnyororo wa thamani; kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 36.37 kupitia benki za biashara nane (8) na kuwanufaisha wakulima wadogo wapatao 5,808 kupitia Mfuko wa Dhamana kwa wakulima wadogo; kutolewa mafunzo kwa wakulima wadogo wapatao 20,399 toka benki ilipoanza huduma zake mwaka 2016; na kufunguliwa kwa ofisi moja ya kanda za nyanda za juu kusini katika mkoa wa Mbeya.

(c) Masoko ya Mitaji na Dhamana

Hatua iliyofikiwa ni Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kuimarisha udhibiti na usimamizi wa masoko ya mitaji kwa kutumia Mfumo wa Usimamizi unaozingatia Vihatarishi (RBS), kutoa jumla ya leseni 76 kwa waombaji waliokidhi matakwa ya sheria na kuchambua na kuidhinisha hatifungani ya Benki ya Biashara ya NMB na hivyo kufanikisha kuuzwa kwa hatifungani za shilingi bilioni 83.30. Vile vile, Mamlaka iliidhinisha uuzwaji wa hisa 588,000,070 za kampuni ya Vodacom Tanzania kwa Shilingi bilioni 499.80 ambapo Serikali ilipata kodi ya shilingi bilioni 146.

B. Biashara

Kazi zilizotekelezwa ni kuanzishwa kwa vituo vinane (8) vya kutolea huduma za pamoja mipakani; kurahisishwa kwa taratibu za kufanya biashara rasmi nchini kwa kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili wa Majina ya Biashara, makampuni, alama za biashara na huduma, hataza, leseni za viwanda na leseni za biashara kwa njia ya mtandao (online registration); na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la maabara ya kisasa - Dar es Salaam (TBS Test House).

(a) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE)

Kazi zilizotekelezwa ni kuwezesha wajasiriamali 38 kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Nairobi nchini Kenya.

C. Masoko

Kazi zilizotekelezwa ni kukamilika kwa Mwongozo wa Mauzo Nje; kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi ikijumuisha wanachama wa Umoja wa Wazalishaji wa

Mafuta ya Alizeti (TASUPA) katika maonesho ya bidhaa za mafuta ya alizeti mjini Nampula, Msumbiji; na kuratibu na kusimamia Maonesho ya wiki ya Viwanda ya SADC katika jiji la Dar es Salaam ambapo wafanyabiashara 574 walishiriki.

(a) Kuchochea Uongezaji Thamani wa Bidhaa za Kilimo na Kuimarisha Miundombinu ya Masoko

Hatua iliyofikiwa ni: kutolewa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani katika ununuzi wa zao la ufuta katika mikoa ya Lindi na Mtwara; ufuatiliaji wa matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani katika mikoa ya Mtwara, Lindi, na Ruvuma; kukusanya taarifa za bei za mazao ya kilimo kwa mikoa 26 na taarifa za bei za mifugo kwa minada 53; na kuridhiwa kwa Itifaki ya Marrakesh ya mwaka 2013 inayolenga kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa ajili ya watu wasioona, wenye uoni hafifu na ulemavu unaofanya mtu kushindwa kusoma.

3.3.4.4 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

(a) Mradi wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Balizi

Shughuli zilizotekelezwa ni: ujenzi wa uzio katika kiwanja kilichopo Nairobi Kenya; ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi katika Ubalizi wa Tanzania uliopo Kinshasa - Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Khartoum - Sudan; ukarabati wa majengo ya makazi ya watumishi wa Ubalizi wa Tanzania, Lusaka - Zambia; na kuendelea na ukarabati wa makazi ya Balizi wa Tanzania Ottawa - Canada.

(b) Upanuzi na Uboreshaji wa Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa vyumba tisa (9) vya madarasa.

3.3.4.5 Miradi Mingine Inayotekelezwa katika Halmashauri

Hatua iliyofikiwa ni utekelezaji wa miradi 38 ya kimkakati ambapo miradi 13 katika Halmashauri 11 za Wilaya za Ruangwa, Chato, Kakonko na Nanyumbu; Halmashauri za Manispaa za Ilemela, Ubungo, Kinondoni, Ilala, Moshi; Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam; na Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Aidha, miradi mingine 9 ya kimkakati inaendelea kutekelezwa katika Halmashauri 8 za Wilaya za Maswa, Momba, Songwe, Kakonko, Buhigwe, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Halmashauri ya Mji wa Kibaha na Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

3.3.4.6 Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi

Serikali imekamaliza mkakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara Nchini (BluePrint) na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya

utekelezaji. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

- (a) Kufutwa na kupunguzwa kwa ada na tozo 54 zilizokuwa zikitozwa na Wizara, Wakala, Idara na taasisi zinazojitegemea ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanya biashara na wawekezaji;
- (b) Serikali imeandaa *Information Memorandum* kwa viwanda vilivyo rudishwa serikalini baada ya kubinafsishwa kwa ajili ya kutoa taswira halisi ya viwanda na fursa zilizopo kwa wawekezaji wapya;
- (c) Kutambua na kuiwezesha sekta isiyo rasmi kwa kutoa vitambulisho maalum ili kuiwezesha kushiriki shughuli za ujenzi wa uchumi wa taifa;
- (d) Kuongeza uzalishaji wa umeme na kuunganisha mikoa iliyokuwa inatumia umeme wa jenereta katika gridi ya taifa ili kuwa na umeme wa uhakika na hivyo wawekezaji kuondokana na gharama kubwa ya kutumia majenereta katika viwanda vyao;
- (e) Kuendelea kujenga miundombinu wezeshi ya barabara, maji, umeme na mawasiliano katika maeneo yaliyotengwa na halmashauri zote nchini kwa ajili ya wafanyabiashara;
- (f) Kufanyika kwa mikutano ya mara kwa mara na wadau wa sekta binafsi ili kujadili na kutatua changamoto zinazowakabili;
- (g) Kuboresha sekta ya usafiri na usafirishaji kwa kufufua baadhi ya njia za garimoshi ya Tanga - Moshi - Arusha, kuongeza safari za ndani na nje ya nchi kwa shirika la ndege ATCL na hivyo kuwawezesha wafanyabiashara na wawekezaji kusafiri na kusafirisha kwa urahisi na kwa gharama nafuu; na
- (h) Upanuzi na uboreshaji wa bandari ikiwemo ya Dar es Salaam kumewezesha muda wa kupakia na kupakua mizigo kuwa rahisi na pia kuondoa madalali kumewezesha urahisi katika biashara na uwekezaji.

3.3.4.7 Viwanda vya Sekta Binafsi

Uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini kwa mwaka 2019/20 umekuwa na matokeo chanya kama ifuatavyo:

- (a) Kuzinduliwa na kuanza uzalishaji kwa kiwanda cha *Pipe Industries Co. Limited* cha kutengeneza mipira na mabomba ya plastiki kilichopo Vingunguti, Dar es salaam;
- (b) Kuanza uzalishaji kwa Kiwanda cha Chai cha Kabambe (Njombe) chenye uwezo wa kuchakata tani 50 za chai kwa siku;
- (c) Kuanza ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho cha *Yalin Cashewnut Company Ltd* (Mikindani - Mtwara) chenye uwezo wa kubangua tani 10,000 kwa mwaka;
- (d) Kuanza uzalishaji kwenye kiwanda cha *21st Century Food and Packaging* chenye uwezo wa kusaga mahindi tani 300 na ngano tani 1,240 kwa siku

- kilichopo Kurasini, Dar es Salaam;
- (e) Kuanzishwa kwa kiwanda cha kusaga mahindi cha Kampuni ya *Mohamed Enterprises Tanzania Limited* (MeTL) chenye uwezo wa kusaga mahindi tani 100 kwa siku kilichopo Songea, Ruvuma;
 - (f) Kuanza uzalishaji kwenye kiwanda cha bidhaa za plastiki cha *Plasco Pipelines Co LTD* kinachozalisha mabomba kilichopo Chang'ombe, Dar es Salaam;
 - (g) Kuanzishwa kwa kiwanda cha *Rungwe Avocado* chenye uwezo wa kufungasha tani 60 za maparachichi kwa siku kilichopo wilayani Rungwe, Mbeya; na
 - (h) Kuingiwa kwa makubaliano kati ya Serikali na viwanda vinne (4) vinavyosindika maziwa yanayokaa muda mrefu bila kuharibika (Ultra Heat Treatment - UHT) vya *ASAS LTD*, *Tanga Fresh Ltd*, *MilkCom Ltd* na *AZAM Dairy Products* kwa lengo la kuongeza usindikaji wa maziwa kutoka lita 154,100 hadi lita 284,500 kwa siku.

3.3.4.8 Uwekezaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma

Uwekezaji wa mtaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma umekua kwa asilimia 7.85 kutoka shilingi bilioni 55,178.3 mwaka 2017/18 hadi shilingi bilioni 59,511.1 mwaka 2018/19 na kuweza kuongeza mapato Serikalini.

Vile vile, Serikali imerejesha jumla ya viwanda 31 ambavyo havifanyi kazi, ikiwa ni katika kuwachukulia hatua wawekezaji waliokiuka masharti ya mikataba ya mauziano. Aidha, Serikali imeendelea na jitihada za kutafuta wawekezaji ili viwanda vilivyorejeshwa Serikalini viweze kuendelezwa. Katika jitihada hizo viwanda vya *Utegi Dairy Farm*, kiwanda cha Chai Mponde na *Lindi Cashew nuts* vimepata wawekezaji na viwanda vya *Shinyanga Meat Plant*, *TPL Mbeya*, *Mwanza Tanneries Ltd* na *Kilimanjaro Paddy Hulling Co. Ltd.* wawekezaji wameonesha nia ya kuvichukua. Sanjari na hatua hiyo, Serikali imeandaa "Information Memorandum" (Company Profile) ili kutoa taswira halisi ya viwanda na fursa zilizopo ili kuvutia wawekezaji wapya.

3.3.4.9 Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Serikali imeendelea kujenga uwezo kwa wataalam wa uibuaji na utekelezaji wa miradi ya PPP kutoka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na Sekta Binafsi kuhusiana na uibuaji na utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ambapo imechangia kuongezeka kwa miradi ya ubia. Miradi mikubwa ya PPP iliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni pamoja na:

- (a) **Miradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Dawa Muhimu na Vifaa Tiba itakayotekelezwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika Mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya:** kuendelea na taratibu za kutafuta wabia wa mradi;
- (b) **Mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo kasi Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza:** kukamilika kwa upembuzi yakinifu; na kuandaliwa kwa nyaraka za zabuni kwa ajili ya watoa huduma;
- (c) **Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Kituo cha Kibiashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere:** kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa miradi;
- (d) **Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano, Kituo cha Kibiashara na Jengo la Watu Mashuhuri katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro:** kukamilisha hatua za kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kuandaa taarifa ya upembuzi yakinifu;
- (e) **Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara:** kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa awali na kuendelea na hatua za kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kuandaa upembuzi yanikifu;
- (f) **Ujenzi wa Reli ya Tanga - Arusha - Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu ya *standard gauge*:** kukamilisha hatua za kumpata Mshauri Elekezi (Transaction advisor) kwa ajili ya kuandaa nyaraka na kumpata Mwekezaji kwa mfumo wa Ubia baina ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP);
- (g) **Mradi wa ujenzi wa reli ya Mtwara - Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga ya *Standard Gauge*:** kukamilika kwa hatua za kumpata Mshauri Elekezi (*Transaction advisor*) kwa ajili ya kuandaa nyaraka na kumpata mwekezaji;
- (h) **Mradi wa Ujenzi wa Hosteli za Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi za Dodoma na Dar es Salaam:** kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa mradi;
- (i) **Mradi wa Ujenzi wa Hosteli ya Chuo cha Maendeleo Vijijini (IRDP):** hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa mradi; na
- (j) **Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo:** Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

3.3.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango

3.3.5.1 Ufuatiliaji wa Miradi katika Mwaka 2019/20

A. Hatua za utekelezaji

Katika mwaka 2019/20, Serikali ilifuatilia miradi ya maendeleo katika mikoa ya Tabora, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Iringa, Songwe, Mbeya, Mwanza na Geita. Miradi iliyofuatiliwa ilijumuisha ya Umma na Sekta Binafsi katika sekta za Nishati, Maji, Elimu, Madini, Kilimo, Viwanda, Utalii, Afya, Ujenzi, Uvuvi, Mifugo, Utawala bora na Uchukuzi. Baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyofuatiliwa ni kama ifuatavyo:

(a) Ujenzi na Upanuzi wa Chuo Kikuu Mzumbe – Kampasi ya Mbeya

Ujenzi wa jengo la utawala na madarasa katika Chuo Kikuu Mzumbe, Kampasi ya Mbeya ulianza Septemba 2016. Hadi kufikia Oktoba 2019 shughuli zilizokuwa zinaendelea kukamilishwa ni pamoja na kupaka rangi, kuweka marumaru, kufunga madirisha, kufunga milango, kufunga mifumo ya maji, kutandaza mifumo ya umeme na mtandao na kuweka mifumo ya kuzima moto.



Jengo la ofisi na madarasa la Chuo Kikuu cha Mzumbe – Kampasi ya Mbeya

(b) Kiwanda cha Kusindika Mpunga Ruaha Milling - Iringa

Kiwanda kilianzishwa mwaka 2018 kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la mpunga. Kiwanda kina uwezo wa kukoboa tani 60 hadi 80 za mpunga kwa siku. Aidha, hadi Oktoba 2019 kiwanda kilikuwa kinakoboa tani 40 za mpunga kwa siku.

Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 12 (ajira za kudumu) na kutoa fursa za masoko kwa wakulima takribani 6,000 kutoka katika vikundi viwili vya wakulima (Idodi na Luganda).



Sehemu ya kiwanda cha Mpunga Ruaha milling ya kupokelea mpunga na kuchambua mchele

(c) Kiwanda cha Saruji Mbeya

Kiwanda kinazalisha na kuuza saruji aina ya Tembo. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 385,000 za saruji na tani 262,000 za klinka kwa mwaka. Kiwanda kinatoa ajira za kudumu 200 na ajira za muda kwa wakandarasi na wasafirishaji wapatao 540. Vile vile, kiwanda kimenufaisha watu 580 wa moja kwa moja na zaidi ya 1000 wasio wa moja kwa moja kupitia utoaji wa huduma za jamii kama vile maji, mashamba ya kilimo, huduma za afya, mafunzo ya uanagenzi na utunzaji wa mazingira.



Mitambo ya kiwanda cha Saruji Mbeya

(d) Kituo cha Kusambaza Umeme katika Kijiji cha Serewa - Songwe

Mradi umejenga kituo chenye uwezo wa kusambaza umeme wa msongo wa kV 33 katika miji minne ya Kamsamba, Mlowo, Vwawa, na Tunduma pamoja na mji mdogo wa Mpemba mpaka Ileje ili kupunguza athari ya kukosekana kwa umeme pindi itokeapo hitilafu katika gridi ya Taifa. Shughuli zilizokamilika ni: ujenzi wa jengo la mitambo ya kusambaza umeme; ujenzi wa miundombinu ya umeme katika kituo; ujenzi wa njia ya kuunganisha umeme kuingia na kutoka kwenye kituo; ujenzi wa uzio wa kituo; na kuendelea na kazi ya kusawazisha eneo la kituo ikiwa ni pamoja na kumwaga kokoto.



Kituo cha kusambaza umeme katika kijiji cha Serewa - Songwe

(e) Ukarabati wa Meli ya MV Victoria na MV Butiama

Mradi unahusisha ukarabati wa meli ya MV Victoria kutokana na uchakavu na hivyo kushindwa kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi. Mradi huu ulianza kutekelezwa Machi, 2019 ambapo hadi Desemba 2019 utekelezaji umefikia asilimia 75. Aidha, ukarabati wa meli ya MV. Butiama umefikia asilimia 70. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: ukataji wa chuma kilichooza, uondoaji kutu kwa njia ya mchanga (*sand blasting*), usafi na upakaji rangi baadhi ya maeneo kwa maandalizi ya ufungwaji wa mitambo mipya na vifaa vipya zikiwemo injini za kuendesha meli na jenereta za kufua umeme na mashine saidizi.



Picha ya MV Victoria inayokarabatiwa.

(f) Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ilemela

Mradi wa ujenzi wa hospitali ya Ilemela ni sehemu ya mradi mkubwa wa kitaifa wa ujenzi wa hospitali za wilaya 67 kwa Halmashauri mbalimbali nchini. Mradi huu ulianza kutekelezwa Machi 2018 ambapo hadi Oktoba 2019 utekelezaji umefikia asilimia 98 ikijumuisha ujenzi wa majengo saba ambayo ni wodi ya wazazi, jengo la mionzi, stoo ya dawa, jengo la utawala, jengo la wagonjwa wa nje, maabara na jengo la kufulia. Shughuli zinazoendelea ni upachikaji wa vioo, kumalizia kufunga mfumo wa maji na uwekaji wa milango. Jumla ya wakazi wapatao 457,000 wanatarajiwa kunufaika na mradi huu.



Jengo la mionzi katika hospitali ya Wilaya ya Ilemela.

(g) Ujenzi wa Gati katika Bandari ya Nyamirembe - Geita

Mradi huu unahusisha ujenzi wa gati lenye urefu mita 132 na miundombinu yake ikiwemo jengo la mizigo na la abiria, uzio na vyoo katika bandari ya Nyamirembe iliyopo katika Ziwa Victoria. Ujenzi wa gati ulianza Agosti 2018 ambapo hadi Oktoba 2019 utekelezaji wa mradi ulifikia asilimia 85. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa gati, *water tower*, jengo la mizigo, jengo la abiria, jengo la jenereta na *gate house*.



Sehemu ya ujenzi wa gati katika bandari ya Nyamirembe.

(h) Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa Kv 220 kutoka Bulyanhulu - Geita (Km 55)

Mradi huu unahusu ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220, kilometa 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita na ujenzi wa miundombinu ya kusambazia umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa km 71 katika vijiji 10 katika mkoa wa Geita. Mradi huu ulianza Januari, 2019 ambapo kazi zilizokamilika ni: kusafisha na kusawazisha viwanja vya vituo vya kupozea umeme na uchimbaji wa misingi ya jengo la kuongozea mitambo, transfoma na vifaa vingine. Shughuli zinazoendelea ni umwagaji wa zege kwenye misingi kwa vituo vya Bulyanhulu na Geita; usukaji wa vyuma na umwagaji wa zege; kusafisha njia za kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220; na kuanza kwa kazi ya uchimbaji wa misingi ya nguzo za kusafirisha umeme kwa upande wa Bulyanhulu.



Ujenzi wa Kituo cha kupoza Umeme wa 220/33kV cha Geita

(i) Kituo cha Uchenjuaji Madini kwa Wachimbaji Wadogo –Katente

Ujenzi wa kituo cha mfano cha uchenjuaji madini kwa wachimbaji wadogo – Katente unatekelezwa kupitia mradi wa SMMRP ambao unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali. Ujenzi ulianza Desemba 2018 ambapo hadi Oktoba 2019 ulifikia asilimia 95. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa ufungaji wa mitambo yote na kufanyiwa majaribio.



Sehemu ya kituo cha uchenjuaji madini kwa wachimbaji wadogo Katente- Bukombe

(j) Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo – EP4R Bukombe, Geita.

Utekelezaji wa mradi wa EP4R katika halmashauri ya Bukombe ulianza Januari, 2019 ambapo ujenzi wa baadhi ya majengo kama vile mabweni, vyumba vya madarasa na bwalo upo katika hatua za mwisho za kukamilika.



Muonekano wa Bwalo linalojengwa kupitia mradi wa EP4R katika Shule ya Sekondari Bukombe

(k) Shamba la Mbogamboga na Matunda (Masifio Farm - Ifunda)

Mradi huu unahusika na uzalishaji na usambazaji wa mbogamboga za aina mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ndani na hivyo kuchangia kupunguza uagizwaji wa mboga kutoka nje. Hadi Oktoba 2019, mradi uliweza kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo la hekta kumi (10) ambapo hekta tano (5) zimekamilika na hekta nyingine tano (5) zinatarajiwa kufunguliwa. Vile vile, shamba hili linahusisha hekta moja (1) ya kitalu nyumba chenye vyumba nane (8) vya kuzalishia uyoga, *cauliflower*, *broccoli*, letusi, nyanya na tango. Shamba hili limeweza kutoa ajira za kudumu 70 na ajira za muda mfupi kati ya 35 hadi 70.



Shamba la umwagiliaji la mbogamboga na kitalu nyumba- Masifio Farm.

SURA YA NNE

MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2020/21

4.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha kwa kifupi maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21. Maeneo hayo yamezingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 kama vilivyoainishwa katika Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango huo. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 ni wa tano katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21.

4.2 Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

4.2.1 Misingi ya Mpango wa Mwaka 2020/21

Misingi iliyozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo:

- (a) Kuendelea kuimarisha na kudumisha amani, usalama, utulivu na umoja wa ndani na nchi jirani;
- (b) Kutengamaa kwa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii na kijamii kama vile Pato la Taifa;
- (c) Kuendelea kuimarika kwa utekelezaji wa sera za fedha na za bajeti;
- (d) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa; na
- (e) Hali nzuri ya hewa ndani ya nchi na katika nchi jirani.

4.2.2 Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

Shabaha kuu za uchumi katika mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo:

- (a) Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa unatarajiwa kupungua kutoka maoteo ya awali ya asilimia 6.9 na kufikia asilimia 5.5 mwaka 2020 ikilinganishwa asilimia 7.0 mwaka 2019. Hii ni kutokana na athari za ugonjwa wa COVID-19 ulioenea katika nchi nyingi ambazo ni washirika wetu wakubwa wa kibiashara;
- (b) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki katika wigo wa tarakimu moja kati ya wastani wa asilimia 3 hadi 5 kwa mwaka 2020/21;
- (c) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.7 ya Pato la Taifa mwaka 2020/21 kutoka matarajio ya asilimia 14.0 mwaka 2019/20;
- (d) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 22.1 ya Pato la Taifa mwaka 2020/21;

- (e) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.6 mwaka 2020/21 ikiwa ni chini ya asilimia 3.0 kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- (f) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.0.

4.3 Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2020/21

4.3.1 Miradi ya Kielelezo

Ili kufikia malengo tarajiwa ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/21, msukumo wa kipekee unaelekezwa katika kutekeleza miradi ya kielelezo ifuatayo:

(a) Ujenzi wa Reli ya Kati ya *Standard Gauge*

Shilingi trilioni 2.1 zimetengwa kwa ajili ya: kukamilisha ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300); kuendelea na ujenzi wa kipande cha Morogoro - Makutupora (km 422); kuendelea na taratibu za upatikananaji wa mkandarasi kwa vipande vya Makutupora - Tabora (km 376.5), Tabora - Isaka (km 162) na Isaka - Mwanza (km 311.3); kuendelea na taratibu za upatikanaji wa washauri elekezi na utoaji wa ardhi kwa vipande vya Tabora - Kigoma (km 411), Kaliua - Mpanda - Karema (km 320), Uvinza - Msongati (km 240) na Isaka - Rusumo (km 371).

(b) Mradi wa Kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere - MW 2,115

Kazi zitakayofanyika ni kuendelea na: ujenzi wa bwawa; ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji; ujenzi wa eneo la kufunga mitambo ya kufua umeme; na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme ambapo shilingi trilioni 1.44 fedha za ndani zimetengwa.

(c) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania

Shilingi bilioni 450 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kununua ndege moja ya mizigo na moja ya abiria aina ya Boeing 787-8 Dreamliner; kukamilisha malipo ya ndege mbili (2) aina ya Airbus A220-300; kununua vifaa vya kuhudumia ndege na abiria viwanjani; kulipa madeni ya Shirika; na kukarabati *Hangar* za KIMAFa (KIA) na JNIA.

(d) Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma

Shughuli zilizopangwa ni kuhakiki mali za wananchi watakaopisha mradi pamoja na uperembaji na tathmini ya mradi ambapo shilingi milioni 110 fedha za ndani zimetengwa.

(e) Kiwanda cha Kufua Chuma cha Liganga

Shughuli zilizopangwa ni kuhakiki mali za wananchi watakaopisha mradi pamoja na uperembaji na tathmini ya mradi ambapo shilingi milioni 120 fedha za ndani zimetengwa.

(f) Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)

Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha majadiliano ya mikataba ikiwemo ya Nchi Hodhi na Wawekezaji, mkataba wa ubia, mkataba wa bandari, mkataba wa pango la ardhi na kulipa fidia ambapo shilingi bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa.

(g) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia - Lindi

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na tafiti mbalimbali za kitaalam pamoja na majadiliano ya mradi ambapo shilingi bilioni 2.6 fedha za ndani zimetengwa.

(h) Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi

Shilingi bilioni 5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya uendelezaji wa kanda maalum za kiuchumi. Shughuli zitakazotekelezwa ni:

(i) Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo: kukamilisha uandaaji wa nyaraka za kisheria kwa ajili ya mradi; kukamilisha taratibu za umilikishaji ardhi katika eneo lililolipiwa fidia; kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu wezeshi katika eneo la kituo cha Teknolojia Bagamoyo; kujenga barabara katika eneo lililojengwa viwanda 11, ambapo shilingi bilioni 4 fedha za ndani zimetengwa.

(ii) Eneo Maalum la Uwekezaji la Ukanda Huru wa Bandari ya Mtwara: kujenga jengo la Kituo cha Pamoja cha Huduma na uzio ambapo shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

(iii) Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini: shilingi bilioni 2.2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wakazi watatu ambao awali nyumba zao hazikufanyiwa thamini; kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuliendeleza eneo na tathmini ya athari za kijamii na mazingira.

(i) Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi (I na II)

Shughuli zitakazotekelezwa ni: **Mkulazi I** - kuendelea na upanuzi wa kitalu cha miwa kufikia hekta 250 na maandalizi ya ujenzi wa kiwanda; **Mkulazi II** - kuzalisha tani 2,300 za sukari; kuendelea na ujenzi wa mifumo ya umwagiliaji, vyanzo vya maji na barabara katika eneo la shamba; na ujenzi wa mabwawa madogo sita (6) yenye mita za ujazo 250,000 na makubwa matatu (3) yenye mita za ujazo 1,000,000.

(j) Kusomesha kwa Wingi Wataalam kwenye Fani na Ujuzi Adimu.

Kuendelea kugharamia mafunzo kwa wanafunzi katika fani mbalimbali zinazohitajika kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya viwanda na watu nchini. Fani hizo ni pamoja na mafuta na gesi, afya hususan udaktari bingwa kwa ngazi za uzamili na uzamivu katika nyanja zote za magonjwa ya upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu, upandikizaji figo, ini na uboho (*bone marrow*), tiba za ndani za moyo, na uhudumiaji wa wagonjwa wa dharura na mahututi (*Emergency medicine and critical care*).

4.3.2 Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

4.3.2.1 Viwanda

(a) Kiwanda cha Kuunganisha Matrika ya URSUS - TAMCO, Kibaha

Shughuli zilizopangwa ni: kuzalisha zana za kilimo; kukamilisha ujenzi wa kiwanda kipyacha kuunganisha matrika; na kusimamia matengenezo ya matrika nchini ambapo shilingi milioni 280 zimetengwa.

(b) Eneo la Kongane za Viwanda - TAMCO, Kibaha

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi katika eneo la mradi; na kutangaza eneo kwa wawekezaji ambapo shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

(c) Mradi wa Magadi Soda - Bonde la Engaruka

Shughuli zilizopangwa ni: kusimamia ujenzi wa miundombinu wezeshi; na kutangaza eneo kwa wawekezaji ambapo shilingi milioni 50 fedha za ndani zimetengwa.

(d) Kiwanda cha Matairi - Arusha

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa andiko la mpango wa kibiashara wa mradi; na kuendeleza mashamba ya mpira ya Kihuhwi na Kalunga pamoja na kuanzisha mashamba mapya ambapo shilingi milioni 100 fedha za ndani zimetengwa.

(e) Maeneo Mengine Maalumu ya Uwekezaji

Shilingi bilioni 2.4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza kanda maalumu za uwekezaji kama ifuatavyo:

- (i) Eneo Maalum la Uwekezaji Kahama, Songwe, Dodoma, Tunduma, Arusha :**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa Mpango Kabambe na uendelezaji wa miundombinu wezeshi (barabara, maji, umeme).

- (ii) **Uanzishwaji wa Maeneo Maalum Uwekezaji ya Kimkakati kwa Maendeleo ya Taifa.** Shughuli zitakazotekelezwa ni: kutenga maeneo maalum ya uwekezaji ya kimkakati ya *Songwe Logistic Centre and Agro-processing industry* na Arusha SEZ.
- (iii) **Eneo Maalum la Uwekezaji Dodoma.** Shughuli zitakazotekelezwa ni kufanya tathmini ya athari za mazingira na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi.
- (iv) **Eneo Maalum la Uwekezaji Benjamin William Mkapa.** Shughuli zilizopangwa ni ukarabati wa miundombinu katika eneo ikijumuisha barabara, maji, mifereji ya majitaka na umeme.
- (v) **Kongane ya Viwanda vya Ngozi (Zuzu- Dodoma):** Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa Mpango Kabambe; kuandaa *Layout Plan and Detailed Design*; kufanya upembuzi yakinifu; kufanya tathmini ya athari ya mazingira; kuandaa Mpango wa Biashara; na ujenzi wa majengo ya viwanda.

(f) Kuboresha Shirika la Nyumbu

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendeleza programu za utafiti na uhawilishaji wa teknolojia ambapo kiasi cha shilingi bilioni 7.5 zimetengwa.

4.3.2.2 Utafiti wa Teknolojia na Bidhaa za Viwandani

(a) Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini - CAMARTEC

Shughuli zilizopangwa ni: kuingiza nchini na kutohoa teknolojia ya kuvuna matunda ya chikichi; kubuni na kuunda teknolojia ya kutenganisha maganda na kiini cha mbegu ya chikichi; kubuni na kuunda teknolojia rahisi ya kupandia mbegu za mafuta; kufanya usanifu wa teknolojia za kulima, kupanda na kuchakata mazao; kufanya tathmini ya mahitaji ya teknolojia ya uchimbaji wa madini kwa wachimbaji wadogo katika mikoa ya Geita na Shinyanga; kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Wajasiriamali wabunifu na watengenezaji wa zana za kilimo; kufanya mradi wa majaribio wa teknolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu vijijini; ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika kijiji cha Mtego wa Simba wilayani Karatu; na kununua vifaa, mitambo na mashine, ambapo Shilingi milioni 300 fedha za ndani zimetengwa.

(b) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha upatikanaji wa ithibati ya maabara ya Kemia na Mazingira; na kuongeza vigezo vya uhakiki wa maabara ya bidhaa za chakula kutoka vitano (5) hadi 20 ambapo shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

(c) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo - TEMDO

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na matengenezo ya mitambo na ukarabati wa majengo ya karakana; kuendeleza teknolojia ya uchakataji wa mbegu za mafuta; kuendeleza teknolojia ya uchakataji wa mazao ya korosho, miwa, muhogo, na zabibu; na kuendeleza teknolojia ya uchakataji wa mazao ya mkonge na pamba ambapo shilingi bilioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

(d) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo - SIDO

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kujenga majengo ya viwanda katika mikoa ya Katavi, Simiyu, Morogoro, Pwani, Kigoma, Singida, Ruvuma, Njombe, Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa na Shinyanga; na kuongeza mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara (NEDF) ambapo shilingi bilioni 4.8 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.2.3 Kilimo

(a) Kilimo cha Kahawa

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza tija na uzalishaji wa kahawa kufikia tani 90,000 kutoka tani 55,979; kuongeza upatikanaji wa miche bora ya kahawa kutoka miche 7,059,835 mwaka 2019/20 hadi miche 20,000,000 kwa mwaka 2020/2021; itaanzisha mashamba darasa 80 na kusambaza nakala 5,743 za vipeperushi vya kanuni za kilimo bora cha kahawa katika Halmashauri 69; kuimarisha vyama vya ushirika 400 kwa kutoa elimu ya masoko; kutangaza kahawa ya Tanzania katika masoko ya kimataifa; kuongeza soko la ndani kwa kuhamasisha unywaji wa kahawa ya ndani; na kuandaa mikakati ya kutegeneza chapa ya bidhaa bora ya kahawa; na kutangaza kahawa ya Tanzania katika masoko ya kimataifa ili kuongeza soko; kuhamasisha matumizi sahihi ya *Central Pulpuly Unit - CPU* ili kuongeza ubora wa kahawa; kuongeza thamani ya kahawa kwa asilimia 16; na kusajili na kutoa vitambulisho kwa wakulima wa kahawa.

(b) Kilimo cha Chai

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 38,000 mwaka 2019/2020 hadi tani 40,000 mwaka 2020/2021; kuongeza ubora wa majani mabichi ya chai kutoka asilimia 60 mwaka 2019/2020 hadi asilimia 70 mwaka 2020/2021; kufufua mashamba makubwa ya chai yaliyotelekezwa katika Wilaya za Njombe, Lushoto, Bukoba, Muleba na Kilolo; kuzalisha miche 1,000,000 ya chai kwa ajili ya wakulima wadogo; kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima wadogo wa chai kwa kuongeza maafisa ugani wa TSHTDA kutoka 17 hadi 37; na kuanzisha mnada wa chai (DSM) pamoja na kanzidata ya wakulima wa chai.

(c) Kilimo cha Tumbaku

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza uzalishaji kutoka tani 63,000 mwaka 2019/2020 hadi kufikia tani 65,000, tija kutoka tani 1.4 kwa hekta hadi kufikia tani 1.5 kwa hekta na ubora wa tumbaku kutoka asilimia 93 hadi asilimia 94; kuaandaa mwongozo wa upandaji miti na kuchimba visima ili kutoa elimu ya kupanda na kutunza miti; kuhifadhi mazingira pamoja na kupata maji ya kumwagilia hususan wakati wa kiangazi; kusajili wakulima wa tumbaku na kutoa vitambulisho; kuimarisha soko la tumbaku, na kuanzisha makampuni madogomadogo ya ndani kwa ajili ya kununua tumbaku ili kupunguza utegemezi wa makampuni makubwa.

(d) Kilimo cha Miwa

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza uzalishaji wa sukari katika viwanda vilivyopo kutoka tani 298,948.61 mwaka 2019/20 hadi tani 424,663; kuongeza tija kutoka tani 50 kwa hekta mwaka 2019/20 hadi tani 60 kwa hekta mwaka 2020/21; kuanzisha viwanda vikubwa, vya kati na vidogo; na kuhamasisha viwanda vya ndani kuzalisha sukari ya viwandani takriban tani 50,000.

(e) Kilimo cha Pamba

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza uzalishaji kutoka tani 348,882 mwaka 2019/20 hadi tani 400,000 mwaka 2020/21; kusambaza chupa 8,000,000 za viuadudu na vinyunyizi 20,000,000 moja kwa moja kwa wakulima kupitia AMCOS; kusambaza mbegu bora tani 18,318 aina ya UKM 08; kuhamasisha matumizi ya kanuni za kilimo bora; kutumia mfumo wa ununuzi wa pamoja wa viuadudu ili kuongeza upatikanaji na kupunguza bei; kufufua vinu saba (7) vya kuchambulia pamba ili kuongeza thamani ya pamba kabla ya kuuzwa nje ya nchi; na kukamilisha taratibu za kisheria za kubadili umiliki wa vinu na kuunda upya mfumo wa uendeshaji.

(f) Kilimo cha Korosho

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza uzalishaji kutoka tani 232,000 mwaka 2019/20 hadi tani 300,000 mwaka 2020/21 na tija kutoka wastani wa kilo 10 za korosho ghafi kwa mti kwa mwaka hadi kufikia kilo 15; usambazaji wa mbegu na miche bora ya mikorosho 15,000,000; kununua tani 30,000 za salfa na lita 350,000 za viuatilifu kwa mfumo wa pamoja na kusimamia usambazaji; na mafunzo ya kilimo bora cha korosho kwa wakulima na maafisa ugani; na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kubangua korosho vidogo na vya kati.

(g) Kilimo cha Mkonge

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza uzalishaji wa mkonge kutoka tani 35,551 mwaka 2019/20 hadi tani 125,428 mwaka 2020/21 na tija kutoka tani 1.1 hadi tani 2.5

kwa hekta; kuanzisha vitalu vya mkonge katika Wilaya 5 za Kishapu, Bariadi, Meatu, Serengeti na Same; kuongeza bidhaa za mkonge kutoka tani 5,701 hadi tani 11,500; na kuhamasisha matumizi ya bidhaa za mkonge ndani ya nchi vikiwemo vifungashio kama vile magunia na ujenzi wa viwanda vya kutengeneza bidhaa mpya za mkonge katika Wilaya za Korogwe na Handeni.

(h) Kilimo cha Pareto

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza uzalishaji wa pareto kutoka tani 2,600 mwaka 2019/20 hadi tani 2,800 mwaka 2020/21; kuhamasisha kanuni za kilimo bora; kufanya utafiti wa aina 10 za mbegu bora ili kupata aina bora za pareto; na kuweka mtaalamu wa maabara katika kiwanda cha pareto Mufindi ili kuthibitisha kiwango cha sumu kutoka kwenye maua ya pareto.

(i) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji

Shughuli zilizopangwa ni: kukamilisha ujenzi na ukarabati wa skimu 17 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 8,536 kupitia ASDP II; kukamilisha ujenzi na ukarabati wa skimu tano (5) za Kigugu - Mvomero (hekta 195), Msolwa Ujamaa (hekta 40), Njage (hekta 75) - Kilombero, Mvumi (hekta 249) na Kilangali Seed farm (hekta 400) - Kilosa kupitia mradi wa ERPP; kutoa mafunzo kwa wakulima na wakulima viongozi 1,000 katika uandaaji wa mipango ya matunzo na uendeshaji wa skimu pamoja na usimamizi wa rasilimali maji katika skimu 50; kukamilisha upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa nyaraka za zabuni katika skimu ya Mkombozi (Iringa vijijini-hekta 10,000) pamoja na upembuzi yakinifu na Usanifu wa mabwawa na skimu za Luiche (Ujiji, Kigoma - hekta 3,000) na Ibanda (Sengerema/Geita - hekta 1,200); na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu katika skimu za Ilemba (Sumbawanga - hekta 800) na Makwale (Kyela - hekta 3,500) pamoja na mabwawa ya Nyisanzi (Chato - hekta 260), Kisese (Kondoa - hekta 2,000), Msia (Mbozi - hekta 100) na Idudumo (Nzega - hekta 200).

(j) Ujenzi wa Maghala na Kuboresha hifadhi ya Taifa ya Chakula

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza uwezo wa NFRA kuhifadhi nafaka kwa kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa maghala sita (6) na vihenge nane (8) vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 250,000; kukarabati maghala matano (5) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 37,500; kujenga vihenge tisa (9) vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 94,000 za nafaka na maghala mawili (2) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za nafaka Mwanza na Dodoma; kujenga karantini na maabara ya uchunguzi ili kudhibiti magonjwa na uchafuzi wa mazao unaosababishwa na sumukuvu; kujenga maabara kuu ya kilimo katika jiji la Dodoma; kujenga maghala 12 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,000 kila moja katika wilaya za Kasulu, Kibondo,

Itilima, Nzega, Bukombe, Chemba, Babati, Gairo, Kiteto, Nanyumbu, Buchosa na Namtumbo kwa lengo la kudhibiti sumukuvu; na kutoa mafunzo kwa vijana 400 kuhusu teknolojia ya kutengeneza vihenge vya kisasa.

(k) Uzalishaji wa Mbegu Bora za Mazao

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 1,436 hadi tani 5,000 kwa kupanua eneo la uzalishaji kutoka hekta 1,017 hadi hekta 2,800; kuzalisha miche ya michikichi 1,000,000, miche ya matunda 560,000 na pingili za muhogo 1,800,000; kuongeza upatikanaji wa mbegu za ufuta na alizeti kufikia tani 1,325; kujenga na kuboresha miundombinu ya uzalishaji wa mbegu ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza eneo (ASA) la kuzalisha mbegu la umwagiliaji kutoka hekta 600 hadi hekta 850; kukarabati na kujenga ofisi na maghala ya kuhifadhi mbegu, kununua matrekta na zana za kilimo na magari ya kusambaza mbegu; kuzalisha mbegu na kusambaza kwa wakulima na makampuni binafsi ya mbegu kiasi cha tani 3,627 kati ya hizo tani 301.88 ni mazao ya nafaka, tani 326.48 mazao jamii ya mikunde na tani 290.204 ni mazao ya mafuta; na kuzalisha miche, pingili na vikonyo 21,000,000 kwa mazao ya korosho (miche 629,629) muhogo (pingili 7,682,674), mkonge (miche 440,548), viazi vitamu (vikonyo 723,664), viazi mviringo (vikonyo 1,000,000), miwa (miche 393,698), migomba (miche 2,936,984), nazi (miche 587,396), zabibu (miche 1,405,477) na michikichi (miche 5,000,000).

(l) Tafiti za Kilimo

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kufanya utafiti ili kugundua mbegu bora 15 za mazao ya nafaka, jamiii ya mikunde, mazao ya mizizi na mbegu za mafuta; kuendelea kutunza aina 520 za mbegu za asili za mpunga; kufanya utafiti wa kusafisha mbegu aina ya Super Magugu katika Wilaya ya Babati; kuendelea kufanya utafiti wa kahawa aina fupi ya Arabica chotara na Robusta; kuzalisha na kusambaza miche bora ya kahawa 15,042,975; kutoa mafunzo kuhusu kanuni bora za utunzaji wa kahawa kwa wakulima 2,581, wakulima wahamasishaji 69, vikundi vya wakulima wa kahawa 57 na maafisa ugani 288; kuongeza eneo la bustani ya kuzalisha miche ya kahawa katika kanda sita (6); kuendeleza utafiti wa matumizi ya chokaa (*application of lime*) katika kurekebisha rutuba ya udongo; kufanya utafiti wa kugundua teknolojia tano (5) za usindikaji wa mazao ya korosho, muhogo, viazi vitamu na zabibu; na kununua na kufunga mashine ya kufanyia utafiti wa usindikaji wa korosho katika kituo cha TARI Naliendele.

(m) Miundombinu ya Utafiti wa Kilimo

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukarabati ofisi na kuvipatia vifaa muhimu vituo

vitano (5) vya utafiti vya Ukiriguru, Ilonga, Kihinga, Selian na Tumbi; kuboresha miundombinu ya mashamba ya uzalishaji wa mbegu ya vituo vya Ilonga, Uyole, Ukiriguru, Selian na Kihinga; kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ya Vituo vya Utafiti vya Ilonga, Naliendele, Ukiriguru na miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika vituo vya Uyole, Ilonga na Seliani; kujenga kituo cha TARI Kihinga Kigoma kwa ajili ya utafiti wa zao la chikichi ikijumuisha ujenzi wa miundombinu ya utafiti, uzalishaji wa miche na kununua matrekta saba (7); kujenga Makao Makuu ya TARI Dodoma; na kuwajengea uwezo watafiti kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu (5 Shahada ya Kwanza, 10 Shahada ya Uzamili na 5 Shahada ya Uzamivu).

(n) Huduma za Upimaji wa Matabaka na Ubora wa Udongo

Shughuli zilizopangwa ni: kuhakiki na kuandaa ramani za udongo za kiikolojia katika mashamba ya uwekezaji ya wakulima wadogo katika mikoa nane (8) ya Morogoro, Singida, Katavi, Kigoma, Lindi, Rukwa, Tabora na Mtwara; kuimarisha kanzidata ya ardhi ya kilimo; kufanya utafiti ili kugundua teknolojia tano (5) za kuhifadhi rutuba ya udongo; kuhifadhi udongo na maji na teknolojia tatu (3) za viwango vya matumizi ya mbolea; kupima sampuli 4,000 za udongo kutoka katika maeneo mbalimbali ili kubaini na kupendekeza viwango vya matumizi ya mbolea katika maeneo husika; na kuboresha ramani za udongo zilizopo zinazoonesha virutubishi vya *Carbon* na PH.

(o) Soko la Bidhaa Tanzania - TMX

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza mauzo ya mazao ya kimkakati hususan korosho, chai na kahawa; kutoa elimu kwa umma kuhusu uendeshaji na manufaa ya soko; kuboresha mfumo wa mauzo wa kielektroniki ili kuongeza ufanisi wakati wa mauzo, ulipaji na uondoshaji bidhaa ghalani; kuweka mfumo wa kisasa wa utoaji wa taarifa za bei na masoko ya bidhaa kwa manufaa ya wakulima waishio vijijini; na kufanya tathmini ya maghala na kubainisha mahitaji mapya ya ghala ili kuendana na shughuli za soko la bidhaa.

4.3.2.4 Mifugo

(a) Kuimarisha Tiba na Udhhibiti wa Magonjwa ya Mifugo

Shilingi bilioni 1.95 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda cha Chanjo za Mifugo cha Serikali (Kibaha) ili kuzalisha chanjo 13 za magonjwa ya kipaumbele zinazohitajika hapa nchini; kuimarisha Vituo nane (8) vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo kwa kukarabati majengo, kununua vifaa vya uchunguzi wa magonjwa na vitendea kazi; kujenga majosho 20 katika halmashauri za wilaya 20; kukarabati majosho 75 katika halmashauri mbalimbali nchini; na kujenga kliniki na maabara 10 za mifugo katika halmashauri za wilaya 10.

(b) Kuendeleza Vyanzo vya Maji katika Maeneo ya Wafugaji

Shilingi bilioni 1.93 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bwawa la Mbangala; kuchimba visima virefu vinne (4) katika halmashauri za Manyoni (Mpapa), Iringa DC (Usolanga), Tanganyika (Tanganyika) na Tunduru (Mkowela); na kukarabati malambo 10 yaliyopo katika halmashauri za Longido (Kemokoa), Simanjiro (Narakauo), Bukombe (Bukombe), Butiama (Bukabwa), Igunga (Igunga), Kiteto (Kimana), Kishapu (Mwalata), Chunya (Isewe), Kilindi (Lengusero) na Meatu (Isebanda).

(c) Kutenga na Kupima Maeneo ya Malisho

Shilingi milioni 130 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuainisha, kutenga na kupima maeneo ya malisho yaliyotambuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ufugaji endelevu na kutangaza hekta 500,000 kwenye Gazeti la Serikali.

(d) Kuimarisha huduma za Utafiti, Ugani na Mafunzo ya Mifugo

Shilingi milioni 375 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kujenga jengo la Wizara katika uwanja wa Maonesho ya Nanenane Nyakabindi (Simiyu); kuanzisha Mashamba Darasa 50; na kufundisha Maafisa Ugani 54 kuhusu kuanzisha mashamba darasa katika halmashauri 30.

(e) Kuboresha Huduma ya Uhimilishaji Mifugo na Upatikanaji wa Mitamba ya Ng'ombe Bora wa Maziwa

Shilingi milioni 245 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kununua mitamba 53 ya Boran (wazazi) kwa ajili ya shamba la kuzalisha mitamba Nangaramo; kununua madume matano (5) ya Friesian (wazazi) kwa ajili ya shamba la kuzalisha mitamba Kitulo; na kuwezesha kambi za uhimilishaji kuhimilisha ng'ombe 100,000.

(f) Kuboresha Mazingira ya Biashara ya Mifugo

Shilingi milioni 899.6 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa minada ya upili ya Meatu - Simiyu na Buzirayombo - Chato pamoja na mnada wa mpakani Mtukula - Kagera; na kuwezesha uendelezaji, usimamizi na uendeshaji wa minada 26 ya upili na mpakani.

4.3.2.5 Uvuvi

(a) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi

Shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa bandari awamu ya kwanza.

(b) Kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)

Shughuli zilizopangwa ni: Ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi (Long liner na Purse Seiner) kwa ajili ya uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu na meli moja ya mizigo ambapo shilingi bilioni 75.93 fedha za ndani zimetengwa na shilingi bilioni 4.2 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kununua meli moja (1) ya uvuvi kwenye maji ya ndani; mtambo wa kuzalisha barafu; ghala la ubaridi na gari maalum la kuhifadhia samaki.

(c) Ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Uvuvi (Mialo na Masoko ya Uvuvi)

Shilingi bilioni 1.4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa mialo 20 na masoko ya uvuvi 14.

(d) Ujenzi na Ukarabati Miundombinu ya Ufugaji wa Viumbe Maji

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ujenzi wa vituo viwili (2) vya Rubambagwe - Geita na Nyegedi - Lindi, kuanzishwa kwa mashamba darasa manne (4) katika halmashauri nne (4) za Mbarali, Meatu, Mkuranga na Malinyi na ukarabati wa Kituo cha Ruhila - Songea, ambapo shilingi bilioni 2.6 fedha za ndani zimetengwa. Aidha, shilingi bilioni 1.7 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Baharini cha Kunduchi.

(e) Kuimarisha na Kuendeleza Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira:

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuimarisha vituo tisa (9) vya doria kwa kuvipatia vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa Maafisa Uvuvi, Polisi, Mahakimu na Vikundi Shirikishi vya Ulinzi wa Rasilimali za uvuvi; kuwezesha uendeshaji wa doria kwa maeneo ya maji na nchi kavu pamoja na mipakani; kufanya operesheni maalum kila robo mwaka; na kuwezesha Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Kupambana na Uhalifu wa Kimazingira kufanya operesheni 10 katika maji yote ambapo shilingi bilioni 1.9

fedha za ndani zimetengwa.

4.3.2.6 Maliasili na Misitu

(a) Mradi wa Kujenga Uwezo kwenye Mapori ya Akiba

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ukarabati wa nyumba 58 za watumishi katika mapori 24 ya akiba; kuboresha miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na ofisi katika mapori ya akiba; na kuwajengea uwezo askari wanyamapori katika kulinda na kusimamia rasilimali za wanyamapori ambapo shilingi milioni 300 fedha za ndani zimetengwa.

(b) Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kupambana na Ujangili

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa Mkakati wa Kuwezesha Upatikanaji wa Rasilimali za Kutekeleza Mpango wa Kudhibiti Ujangili; kutoa mafunzo ya udhibiti wa matukio ya ujangili kwa vikundi tisa (9) vya kikanda vinavyoratibu shughuli za kupambana na matukio ya ujangili; na kutoa mafunzo ya uhifadhi kwa watumishi 70 ya sekta ndogo kuhusu mbinu mpya za kudhibiti ujangili wa maliasili ambapo shilingi milioni 583.77 fedha za nje zimetengwa.

(c) Programu ya Misitu na Uendelezaji wa Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu (FORVAC)

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji sita (6) vya mradi; kuwezesha mnyororo wa thamani kwa mazao ya misitu katika vijiji 20 ndani ya wilaya sita (6) za Mpwapwa, Kilindi, Handeni, Nachingwea, Liwale na Ruangwa; kujenga uwezo wa maafisa wa halmashauri kuhusu utekelezaji wa mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii; kuwezesha uandaaji wa mkakati wa misitu wa ugani na mawasiliano; kuboresha mfumo wa taarifa za misitu na nyuki; na kuwezesha mafunzo kwa maafisa sheria kuhusu usimamizi wa sheria, utawala bora na biashara ya mazao ya misitu ambapo shilingi bilioni 7.1 fedha za nje zimetengwa.

(d) Mradi wa Panda Miti Kibiashara

Shughuli zilizopangwa ni: kujenga uwezo kwa Taasisi za Mafunzo zilizo chini ya Idara ya Misitu na Nyuki; kuwezesha wakulima wadogo wa miti katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Njombe kupanda miti kibiashara; kufanya mapitio ya sera, kanuni na miongozo mbalimbali; kuongeza ubora wa mazao ya Misitu yaliyo kwenye mnyororo wa thamani; kujenga uwezo kwa wakulima wa miti katika kupambana na matukio ya moto; na kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo na wa kati katika biashara na mnyororo wa mazao ya misitu ambapo shilingi bilioni 6.3

fedha za nje zimetengwa.

(e) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kusimamia Rasilimali za Misitu na Nyuki

Shughuli zilizopangwa ni: kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Nyuki ya Mwaka 1998; na kuwezesha taasisi za utafiti ya mafunzo ambazo ni Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki - Tabora, Chuo cha Mafunzo ya Misitu Olmotonyi na Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI) ambapo shilingi milioni 200 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.2.7 Utalii

Mradi wa Kuendeleza Utalii Ukanda wa Kusini - REGROW: shughuli zitakazotekelezwa zitajikita katika kuboresha Hifadhi za Taifa za Nyerere, Ruaha, Mikumi na Udzungwa kwa kujenga miundombinu ya barabara (km 1,259, trail km 132.5) na viwanja vya ndege nane (8), mabanda ya kupokelea wageni na malango ya kuingilia watalii; kutekeleza mkakati wa masoko ya utalii; na kufanya utafiti wa masuala mbalimbali yanayohusu wanyamapori; kuhamasisha uhifadhi katika vijiji 15 vinavyozunguka hifadhi. Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni kuboresha skimu za umwagiliaji za Madibira na Mbarali kwa kujenga mfumo wa utunzaji maji na umwagiliaji; kuwajengea uwezo watumiaji wa maji katika maeneo ya mto Mswiswi, Gwiri, Chimala na Mlowo; kusimamia na kuendeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji vitatu (3) katika wilaya za Mbarali, Makete na Wanging'ombe; na kuwezesha usimamizi na utunzaji wa vyanzo sita (6) vya maji katika wilaya sita (6) za Mbeya, Mbarali, Mufindi, Wanging'ombe, Makete na Iringa Vijijini ambapo shilingi milioni 200 fedha za ndani na shilingi bilioni 30.2 fedha za nje zimetengwa.

4.3.2.8 Madini

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP)

Shughuli zilizopangwa ni: ujenzi wa ofisi nane (8) za maafisa madini wakazi katika mikoa ya Songwe, Manyara, Katavi, Kigoma, Iringa, Rukwa na Tanga; kuanza ujenzi wa kituo kimoja (1) cha umahiri; kujenga ghala la kuhifadha sampuli za miamba chorongwe (core shed); ununuzi wa magari ya kufanyia shughuli za utafiti wa ikolojia; kuendeleza mgodi wa makaa ya mawe Kiwira; kujenga ghala la kuhifadha sampuli za miamba chorongwe (core shade); na ununuzi wa vifaa vya maabara na utafiti ambapo shilingi bilioni 8.5 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.3 Kufungamanisha Uchumi na Maendeleo ya Watu

4.3.3.1 Elimu, Sayansi na Teknolojia

A. Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari

(a) Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu

Shughuli zilizopangwa ni: kuboresha vyuo vya ualimu vya Mhonda na Dakawa kwa kukarabati na kujenga miundombinu katika vyuo hivyo ili kukidhi mahitaji ya sasa na kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji; kukamilisha ujenzi wa hosteli, bwalo la chakula na mifumo ya maji katika Chuo Kikuu cha Mzumbe ili kuwezesaji upatikanaji wa malazi na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji; kukarabati nyumba za wakufunzi katika vyuo vya ualimu; na kuendelea kuratibu ujenzi wa ofisi 55 za Uthibiti Ubora wa Shule ngazi ya wilaya ambapo shilingi bilioni 9.1 fedha za nje zimetengwa.

(b) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi (MEMM)-KKK

Shilingi bilioni 40.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha Vituo vya Walimu (TRC) kutekeleza Mpango wa mafunzo endelevu kazini (CPD); kuandaa mwongozo kwa ajili ya Waratibu wa Vituo vya Walimu ili kuendana na Mpango wa Mafunzo Endelevu Kazini (CPD); kuwezesha mafunzo ya Waratibu wa TRC na Maafisa Elimu kata 966; kuandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa walimu wa shule za Msingi kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu; kuandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa wawezeshaji wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA) kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu; kuwezesha mafunzo kwa wawezeshaji wa MEMKWA wenye mahitaji maalum ngazi ya mikoa na halmashauri; kuwezesha uandaaji, uchapaji na usambazaji wa vitabu vya wanafunzi wa Darasa la VI na VII pamoja na kiongozi cha mwalimu kwa masomo yote; kuandaa miongozo na kuboresha mihtasari kwa ajili ya MEMKWA na kufanya upimaji; na kuwezesha mafunzo kazini kwa walimu wenye mahitaji maalum kuhusu mtaala, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu.

(c) Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa moduli na Mwongozo wa Elimu Jumuishi pamoja na kutoa mafunzo ya elimu jumuishi kwa walimu wa Shule za Sekondari za Serikali ili kuwajengea uelewa zaidi kuhusu elimu jumuishi; kuandaa na kutekeleza mkakati wa upatikanaji wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati; kuandaa mwongozo kwa ajili ya kufanya tathmini ya ujifunzaji kwa Elimu ya Sekondari;

kuandaa mwongozo wa ufundishaji wa TEHAMA na kutoa mafunzo kwa walimu 1,000 kutoka shule za Sekondari 500 kuhusu moduli za TEHAMA; na kuboresha vituo vya kutolea Elimu nje ya mfumo rasmi ili kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ambapo shilingi bilioni 19.1 fedha za nje zimetengwa.

(d) Programu ya Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni - SWASH

Shilingi milioni 955.8 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kufuatilia na kutathmini ujenzi wa miundombinu ya vyoo na maji awamu ya pili katika shule za msingi 946; kujenga miundombinu ya maji na vyoo katika vyuo vya ualimu vitano (5) vya Katoke, Nachingwea, Kinampanda, Shinyanga na Murutunguru ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu; na kutoa elimu elekezi kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa SWASH kwa Maafisa Elimu na Wathibiti Ubora wa Shule.

(e) Mamlaka ya Elimu Tanzania - TEA

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuwezesha: ujenzi wa madarasa 180 katika shule 50 za msingi na sekondari 10; ujenzi wa nyumba 100 za walimu katika shule 25 za sekondari zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu; ujenzi wa mabweni 15 ya wanafunzi wa kike katika shule 15 za sekondari zenye mazingira magumu; ujenzi wa matundu 432 ya vyoo katika shule 13 za msingi na sekondari tano (5); ujenzi wa awamu ya kwanza wa shule ya msingi ya kisasa itakayofundisha kwa lugha ya Kiingereza jijini Dodoma; ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na uboreshaji wa miundombinu katika Chuo Kikuu kimoja - Zanzibar; na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi nne (4) ambapo shilingi bilioni 12.0 fedha za ndani zimetengwa.

(f) Elimumsingi bila Ada

Shilingi bilioni 298.13 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza utoaji wa elimumsingi bila ada ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 137.63 zitatumika kwa shule za msingi na shilingi bilioni 160.49 zitatumika kwa shule za sekondari.

B. Elimu ya Ufundi na Ualimu

(a) Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Shilingi bilioni 54.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 7.88 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kuanzisha vituo vya mafunzo ya ufundi stadi; kuendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi na huduma vya mikoa ya Geita, Simiyu, Rukwa, Njombe na Kagera na vyuo 27 vya Mafunzo ya Ufundi Stadi vya wilaya; kukarabati, kununua na kuweka vifaa vipya vya kujifunzia katika vyuo 29 vya mafunzo ya ufundi stadi;

ujenzi wa karakana 12 kwenye vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi; kuanzisha kitengo cha unenepeshaji wa ng'ombe kwenye Kituo cha Mafunzo na kiwanda cha nyama katika Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma - Dodoma; kukamilisha uanzishwaji wa Kituo cha Uchapaji kwenye Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Chang'ombe - Dar es Salaam; kujenga mabweni sita (6) katika Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Namtumbo (2), Mbeya, Dakawa, Mara na Makete; Ujenzi wa nyumba 23 za watumishi kwenye vituo vya mafunzo ya ufundi stadi vya Makete (6), Ulyankulu (10), Busokelo (2) na Namtumbo (5); ukarabati wa nyumba saba (7) za Watumishi wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi - Dar es Salaam; kukamilisha ununuzi wa nyumba 10 katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma - Manyara; na ununuzi wa magari 15 kwa ajili ya Makao Makuu ya VETA, Kanda, na vyuo vipya vya Wilaya.

(b) Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu

Shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi wa kumbi za mihadhara, ununuzi wa vifaa vya maktaba na ukarabati wa jengo la utawala katika Kampasi ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima - Morogoro; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo vya ualimu vinne (4) vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali ambapo shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani na fedha za nje 5.50 zimetengwa.

(c) Chuo cha Ufundi Arusha

Shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja na maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000; kukarabati madarasa, mabweni, barabara za ndani, majengo ya ofisi, mfumo wa maji safi na majitaka, mfumo wa mawasiliano wa ndani na nyumba za makazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji; kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja litakalokuwa na maabara, madarasa na ofisi za walimu; na kuendeleza Kituo cha Mafunzo ya Nishati Jadidifu cha Kikuletwa kuwa Kituo cha Umahiri.

(d) Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kununua vifaa vya maabara ya sayansi, TEHAMA, vitabu vya kiada vya shule za msingi na sekondari, vitabu vya kiada na ziada kwa vyuo vya ualimu 35 vya Serikali; kukarabati maabara nne (4) za sayansi, tano (5) za TEHAMA na maktaba sita (6) katika vyuo vya ualimu vya Serikali; kuwezesha mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Ualimu, uchapishaji na usambazaji na miongozo kwa ajili ya uendeshaji wa mafunzo kazini kwa masomo 21 na moduli sita (6) za mkakati jumuishi; kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa vyuo 35 vya

ualimu ikijumuisha vya maabara; na kutoa mafunzo kazini kwa vyuo vya ualimu 35 katika maeneo ya utawala na matumizi ya TEHAMA kwa watumishi 1,300, matumizi ya vifaa visaidizi na TEHAMA kwa walimu na wakufunzi 300 wenye mahitaji maalumu, matumizi ya lugha ya alama kwa walimu wa shule 350 za msingi na sekondari 150, mbinu za ufundishaji kwa wakufunzi 570 hususan masomo ya Sayansi, Hisabati, Biashara, Kilimo, Taaluma ya Maendeleo na Elimu ya Michezo, Uraia na Sanaa ambapo shilingi bilioni 28.4 fedha za nje zimetengwa.

C. Elimu ya Juu

(a) Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu: shilingi bilioni 464.0 zimetengwa kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi 145,000 ambapo wanafunzi 54,000 ni wa mwaka wa kwanza na 91,000 ni wanaoendelea na masomo; na kuendelea na kazi ya ukusanyaji wa shilingi bilioni 190 kutoka kwa wanufaika 162,000 ambao mikopo yao imeiva.

(b) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili yakukamilisha upanuzi wa Hosteli za Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuongeza ghorofa mbili (2) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280; kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Shule Kuu tarajiwa ya Uchumi katika Kampasi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere lenye ghorofa sita(6); na kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la kituo cha wanafunzi.

(c) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa - MUCE: shughuli zitakazotekelezwa ni kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kupanua maabara ya Baiolojia yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 kwa wakati mmoja; na kukarabati majengo ya maabara mbili (2) za sayansi (Fizikia na TEHAMA), ukumbi wa mihadhara, madarasa manne (4), jengo la utawala na hosteli ambapo shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

(d) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam - DUCE: shughuli zilipongwa ni kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala ili kuongeza ofisi hamsini (50) za wafanyakazi na vyumba vya utafiti na kujenga jengo la maabara za sayansi na vyumba vya kujifunzia ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo; kuimarisha miundombinu kwa kukarabati mabweni na kumbi za mihadhara, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na ujenzi wa mfumo wa ukusanyaji wa maji taka; kujenga hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na kuiwekea samani; kuboresha hosteli za wanafunzi (NSSF Mtoni Kijichi) zenye uwezo wa kuchukua jumla wanafunzi 500; na kujenga madarasa katika shule ya Msingi ya Mazoezi Chang'ombe na Shule ya Sekondari ya

Chang'ombe pamoja na maabara nne (4) za sayansi ili kuongeza fursa za kupata elimu ambapo shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

(e) Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia: Shilingi bilioni 11.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili kukarabati miundombinu katika kampasi ya Oswald Mang'ombe; na kuandaa michoro na mpango wa matumizi ya ardhi ya chuo.

(f) Ukarabati na Ujenzi wa Chuo Kikuu Mzumbe: shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa madarasa, ofisi, ukumbi, uwekaji wa samani na miundombinu ya TEHAMA katika jengo la Kampasi Kuu (Maekani); kukarabati na kuweka samani katika jengo la wanafunzi wa Shahada za Uzamivu; na ujenzi wa maktaba, bwalo la kulia chakula na ukarabati wa miundombinu ya kampasi ya Tegeta - Dar es Salaam ambapo shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

(g) Ujenzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Ardhi: shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Ardhi na kuunganishwa na mfumo wa maji safi; ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA na kuweka samani katika mabweni ya wanafunzi; na kuendeleza ujenzi wa mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592 kwa wakati mmoja.

(h) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili: shughuli zilizopangwa ni kukamilisha ujenzi wa kituo cha umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu katika Kampasi ya Mloganzila; na kuanza mpango wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto, ili kuimarisha mazingira ya kufundishia, kutafiti na kutoa huduma za tiba ambapo shilingi bilioni 1.50 fedha za ndani na shilingi bilioni 5.34 fedha za nje zimetengwa.

(i) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi: shilingi bilioni 1.50 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukaraba na kufanya upanuzi wa Chuo; kujenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa wakati mmoja; na kujenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja.

(j) Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha: shughuli zilizopangwa ni kuendelea na ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500, kituo cha utafiti na kituo cha afya na upanuzi wa maabara; kutekeleza miradi 21 ya kitafiti na ubunifu kwa kufadhili wanafunzi na kulipa gharama za kiutafiti kwa wanafunzi na wanataaluma; na kuendelea na taratibu za

awamu ya pili ya ujenzi wa *Estate Building* ambapo shilingi bilioni 1.50 fedha za ndani zimetengwa.

(k) Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - DIT: shughuli zilizopangwa ni kutengeneza mtambo maalumu wa kuwezesha mazingira rafiki ya kilimo mjini; kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa umwagiliaji kwa kutumia nguvu za jua kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia maji ya kisima; kuboresha teknolojia ya mfumo wa usimamizi wa hospitali; kutengeneza mfumo wa mawasiliano yasiyo tumia nyaya kwenye magari yasiyo na dereva; kukamilisha utengenezaji wa mashine ya kuchakata kahawa kwa kigezo cha rangi utakaosaidia wakulima wa kahawa kuongeza mnyoro wa thamani; kutengeneza injini itakayotumia mfumo wa gesi asilia; kujenga mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 na jengo la ghorofa 12 la kituo cha umahiri wa TEHAMA katika Kampasi ya Dar es Salaam; na kuanza ujenzi wa mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 na jengo la ghorofa sita (6) la kituo cha umahiri wa teknolojia ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi katika Kampasi ya Mwanza ambapo shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

(l) Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya: shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la maktaba lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500; ujenzi wa majengo mawili (2) ya hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja; ujenzi wa jengo la madarasa la Ndaki ya Usanifu na Teknolojia ya Majengo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja; na kuanzisha Kituo cha Teknolojia Vijijini katika Kampasi ya Rukwa ili kuchochea matumizi ya teknolojia stahiki katika maeneo ya vijijini.

(m) Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo - SUA: shughuli zilizopangwa ni kukarabati vyumba 17 vya madarasa, mabweni matano (5), nyumba 30 za wafanyakazi katika Kampasi kuu na Kampasi ya Solomon Mahlangu, majengo ya ofisi na maabara katika Idara za DFRAM na DEC, majengo ya idara ya mimea vipando (Crop Science), mabweni na hosteli tano (5), Horticulture shed house (Crop museum) pamoja na kukarabati majengo na kununua samani kampasi ya Tunduru; kukarabati miundombinu Kampasi ya Katavi, kituo cha mafunzo ya kilimo kwa wakulima kilichopo Mgeta, kiwanda cha samani Vuyisile - SMC; na kufunga mfumo wa kisasa wa umwagiliaji kwenye shamba la mafunzo lililopo Kampasi Kuu ambapo shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

D. Ujuzi na Utafiti

(a) Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi kwa Ajili ya Shughuli za Kuzalisha na Kukuza Uchumi

Shughuli zilizopangwa ni kuendelea na utekelezaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za Kazi kwa kutoa ruzuku kwa ushindani kwa taasisi za mafunzo; kuwezesha karakana na maabara za wabunifu kwa kuzipatia vifaa vya kisasa ili kuboresha mazingira ya uendelezaji ubunifu na ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo; kuendelea kutoa fedha za kuziwezesha taasisi za mafunzo ya ufundi kununua vifaa na kuboresha mitaala kupitia maandiko ya kiushindani ili kuendana na mahitaji ya kijamii; kujenga na kukarabati miundombinu ya taasisi zinazotoa mafunzo ya ufundi ikiwemo VETA; kutoa ufadhili kwa vijana ili kuwawezesha kupata ujuzi; kuwezesha ujenzi wa maktaba tano (5) mpya katika mikoa ya Singida, Shinyanga, Simiyu, Dodoma na katika Chuo cha Maktaba - Bagamoyo; na kuimarisha vyuo vya VETA na elimu ya ufundi kwa kutoa mafunzo ya uanagenzi ambapo shilingi bilioni 54.58 fedha za nje zimetengwa.

(b) Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH

Shilingi bilioni 3.50 fedha za ndani na shilingi bilioni 1.69 fedha za nje zimetengwa kugharamia miradi mipya nane (8) ya utafiti; kuboresha mfumo ya ubunifu na kuwaendeleza wabunifu; kubiasharisha matokeo ya tafiti tano (5) ili ziweze kutumika na kuleta tija kwa maendeleo ya nchi; kuratibu mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya mwaka 2021 ili kutambua, kuendeleza na kurasimisha matokeo ya ubunifu; kusimamia uanzishwaji wa mfumo na miongozo ya kuzijengea uwezo taasisi zinazofanya tafiti nchini katika kulinda viwango vya utekelezaji wa utafiti; na kuboresha mfumo wa udhibiti na utoaji vibali vya utafiti.

(c) Maabara ya Mionzi ya Nguvu za Atomiki - Arusha:

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maabara ya Tume; kuanza ujenzi wa maabara za kanda ya Zanzibar na mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza; kuanzisha ofisi za Tume katika kanda za Kati - Dodoma, Nyanda za Juu Kusini - Mbeya na Kusini -Mtwara; kuanzisha kituo cha mafunzo cha usalama na kinga ya mionzi katika ngazi ya stashahada, cheti na mafunzo ya muda mfupi; kupima kiasi cha mionzi katika sampuli 20,000 za vyakula na mbolea; na kuimarisha upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 620 ambapo shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

E. Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

Upanuzi na Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

Shilingi bilioni 1.50 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya nishati mbadala ya majumbani kwa ajili ya vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi; na ununuzi wa vifaa vipya vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia.

4.3.3.2 Afya na Ustawi wa Jamii

A. Afya

(a) Mradi wa Kupunguza Vifo vya akina Mama Vinavyotokana na Uzazi

Shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa vituo 6 vya kukusanyia damu salama katika mikoa ya 12 yenye uhitaji mkubwa ya Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Geita, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Tabora, Dodoma, Pwani, Arusha na Kagera.

(b) Hospitali za Rufaa za Mikoa

Shughuli zilizopangwa ni uboreshaji na upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za tiba; kuanzisha na kuboresha vitengo vya dharura, wagonjwa mahututi, maeneo ya kutakasia vifaa, upasuaji na maeneo ya huduma za mama na mtoto katika hospitali za rufaa za mikoa; kuendelea na ujenzi wa hospitali mpya za rufaa za mikoa ya Katavi, Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Kwangwa – Mara; kuendelea kukamilisha ujenzi kwenye hospitali nane (8) za rufaa za mikoa za Mount Meru (Arusha), Mbeya, Sekou Toure (Mwanza), Mwananyamala (Dar es Salaam), Kibaha - Tumbi, Maweni (Kigoma), Manyara na Mawenzi (Kilimanjaro); kuboresha miundombinu katika hospitali nne (4) za mikoa ya Kigoma (Maweni), Tanga (Bombo), Tabora (Kitete) na Manyara; na kuwezesha upatikanaji wa damu salama kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama ambapo shilingi bilioni 14 fedha za ndani na shilingi bilioni 1.7 fedha za nje zimetengwa.

(c) Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi

Shilingi bilioni 200 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya nchini na ugomboaji wa dawa za msaada; na kugharamia huduma za uchunguzi.

(d) Taasisi ya Saratani Ocean Road

Shilingi bilioni 4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya PET/SCAN na CYCLOTRON ya kufanya uchunguzi wa saratani.

(e) Hospitali ya Moyo ya Jakaya Kikwete

Shughuli zilizopangwa ni kufanya ukarabati wa Wodi namba moja na tatu; na upanuzi wa chumba cha kutakasia ili kuimarisha huduma za upasuaji wa moyo ambapo shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

(f) Hospitali ya Rufaa Bugando

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa wodi ya wagonjwa wa saratani ambapo shilingi bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa.

(g) Hospitali ya Rufaa Kibong'oto

Shilingi bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Maabara ya ngazi ya 3 (nbio safety level 3) ili kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa ya kuambukiza.

(h) Hospitali ya Rufaa Mbeya

Shughuli zilizopangwa ni ununuzi wa vifaa tiba, kuendelea na ujenzi wa jengo la X-ray na jengo la Wazazi – Meta ambapo shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa.

(i) Kujenga hospitali ya Kanda ya Ziwa- Burigi

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ukamilshaji wa majengo ya hospitali ambapo shilingi bilioni 3 fedha za ndani zimetengwa.

(j) Hospital ya Rufaa Mtwara

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya Hospitali ambapo shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa.

(k) Hospitali ya Taifa Muhimbili

Shughuli iliyopangwa ni kuendelea na ujenzi wa jengo la wodi la wagonjwa wanaojigharamia pamoja na ununuzi wa vifaa tiba ambapo shilingi bilioni 4 fedha za ndani zimetengwa.

(l) Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

Shilingi billioni 5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa mkopo wa ujenzi kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; kununua vifaa tiba (vipandikizi); kuwajengea ujuzi wataalam wa upasuaji; na ujenzi wa kituo cha huduma za utengamao.

(m) Uimarishaji wa Huduma za Chanjo

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuimarisha huduma za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kupitia huduma za chanjo ambapo shilingi bilioni 51.5 fedha za ndani zimetengwa.

(n) Kuimarisha Vyuo vya Mafunzo ya Afya

Shughuli zitakazotekelezwa ni kugharamia mafunzo a uzamili kwa wataalam katika Sekta ya Afya; kufanya upanuzi na ujenzi wa majengo na ukarabati kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Afya vya Uguzi nchini ambapo jumla ya shilingi bilioni 6.1 fedha za ndani zimetengwa

(o) Hospitali za Halmashauri

Shilingi bilioni 32.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa wodi tatu (3) katika hospitali 67 za halmashauri; shilingi bilioni 27.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya katika halmashauri za wilaya 27; shilingi bilioni 27.75 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati tatu (3) katika kila halmashauri; na shilingi bilioni 32.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali 67 za halmashauri.

B. Maendeleo ya Jamii

(a) Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kujenga hosteli ya wasichana; na kujenga kumbi za mihadhara katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ambapo shilingi bilioni 2.7 fedha za ndani zimetengwa.

(b) Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kutoa mafunzo ya ujasiriamali, ufugaji na kilimo cha mbogamboga kwa wanawake wajasiriamali; kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali kupitia asilimia 4 ya mapato ya ndani ya halmashauri na Dawati la Wanawake katika Benki ya Posta.

(c) Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango

Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na: kuendesha kampeni ya kutokomeza ukatili wa kijinsia na ukeketaji; kuratibu uingizwaji wa masuala ya jinsia katika mipango na mikakati ya kissekta; kuratibu uanzishwaji wa Dawati la Jinsia katika vyuo vya elimu ya juu na vya kati; na kuimarisha madawati ya jinsia na watoto kwenye vituo vya polisi, magereza na TAKUKURU ambapo shilingi bilioni 1.6 fedha za nje zimetengwa.

(d) Uhai na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kutekeleza afua za Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto na Agenda ya Taifa ya Kuwekeza kwenye Afya na Maendeleo ya Vijana; kuratibu uanzishwaji wa vikundi vya malezi katika jamii; kuratibu ujenzi wa vituo vya awali vya kulea watoto wadogo ngazi ya jamii; na kuratibu uanzishwaji wa madawati ya kuzuia ukatili katika shule za msingi na sekondari ambapo shilingi milioni 617 fedha za nje zimetengwa.

(e) Huduma za Ustawi wa Jamii

Shughuli zilizopangwa ni: kuendelea na ujenzi wa Makao ya Taifa ya Watoto Mkoani Dodoma; kukarabati Makazi ya Wazee ya Kibirizi ambayo yatabadilishwa kuwa Mahabusu ya Watoto; ujenzi wa Shule ya Maadilisho katika Mkoa wa Geita; kuendelea na kukarabati Makazi ya Wazee; na kuendelea na ujenzi wa Mahabusu ya Watoto Mtwara, ambapo shilingi bilioni 1.3 fedha za ndani na shilingi milioni 503 fedha za nje zimetengwa.

4.3.3.3 Maji na Usafi wa Mazingira

(a) Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini

Shughuli zilizopangwa ni: kujenga na kukarabati mabwawa makubwa mawili (2) ya Farkwa na Ndembera/Lugoda na ya ukubwa wa kati matatu (3) ya Itobo, Nkiniziwa na Enguikmet; kulipa fidia kwa maeneo yanayowekewa mipaka na kutangazwa kwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji; ujenzi na ukarabati wa ofisi tano (5) za mabonde ya maji ya Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Mto Rufiji, Wami/Ruvu na Mto Pangani na maabara za maji ambapo shilingi bilioni 11.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 28.0 fedha za nje zimetengwa.

(b) Kuwezesha Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II)

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maji nchini; kufanya tafiti na kuandaa Sera na mikakati ya utekelezaji ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.54 fedha za ndani na shilingi milioni 933 fedha za nje zimetengwa.

(c) Ufuatiliaji na Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II)

Shilingi bilioni 3.96 fedha za ndani na shilingi bilioni 6.37 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya madarasa, mabweni na maabara katika Chuo cha Maji; kuratibu utekelezaji wa Programu kwa kuendesha mikutano

ya wadau kwa mujibu wa makubaliano ya usimamizi wa WSDP II; na kuandaa kanuni za utekelezaji wa sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019.

(d) Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia

Shughuli zitakazotekelezwa ni ununuzi wa vifaa na kemikali za maabara 16; kutekeleza mkakati wa teknolojia ya kuondoa madini ya *floride* kwenye maji; na kutekeleza mkakati wa usimamizi wa ubora wa maji na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji ambapo shilingi bilioni 2.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.5 fedha za nje zimetengwa.

(e) Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa

Shilingi bilioni 47.3 fedha za ndani na shilingi bilioni 38.21 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira katika miji mikuu ya Wilaya 29, miji midogo mitano (5) pamoja na maeneo yanayohudumiwa na miradi sita (6) ya kitaifa.

(f) Kuboresha Huduma za Maji Vijijini

Shughuli zilizopangwa ni kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea; na kukarabati miradi ya maji na kujenga vituo vipya vya kuchotea maji vijijini ambapo shilingi bilioni 212.75 fedha za ndani na shilingi bilioni 111.63 fedha za nje zimetengwa.

(g) Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa

Shilingi bilioni 25.3 fedha za ndani na shilingi bilioni 76.42 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa ikiwemo miji ya Kigoma, Lindi, Babati, Mwanza, Lamadi, Misungwi, Magu, Geita, Morogoro, Arusha, Dodoma, Tanga, Mtwara na Shinyanga.

(h) Mradi wa Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa Mipya

Shughuli zitakazotekelezwa ni ukamilishaji na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Njombe, Katavi na Songwe ambapo shilingi bilioni 5.1 fedha za ndani zimetengwa.

(i) Mradi wa Maji Masasi - Nachingwea

Shughuli zilizopangwa ni ujenzi wa chujo la maji; kuendelea na uunganishaji wa huduma ya maji kwa wateja ; na kujenga vituo 50 vya kuchotea maji katika vijiji 20

ambapo shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

(j) Mradi wa Maji Same - Mwanga - Korogwe

Shilingi bilioni 11.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 18.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika miji ya Same na Mwanga, pamoja na baadhi ya vijiji vya wilaya za Mwanga, Same na Korogwe.

(k) Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Igunga, Nzega na Tabora

Shilingi milioni 500 fedha za ndani na shilingi bilioni 5.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi wa maji kwenye miji ya Tinde na Shelui na kukamilisha ujenzi katika miji ya Nzega, Igunga, Uyui na Tabora pamoja na vijiji vilivyopo kando ya bomba kuu la kusafirisha maji.

(l) Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama - Shinyanga

Shilingi bilioni 4.48 fedha za ndani na shilingi bilioni 22.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayolenga kuboresha huduma ya maji safi kutoka katika Ziwa Victoria kwenda Miji ya Malampaka, Sumve, Malya, Lagangabilili, Busega, Bariadi na Mwanhuzi kwa kujenga chanzo cha maji (intake), kuanza ulazaji wa bomba kuu, kujenga matanki ya kuhifadhi maji na kulipa fidia kwa wananchi watakaohamishwa ili kutekeleza mradi.

(m) Kuboresha Huduma za Maji Jiji la Dar es Salaam (DAWASA)

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni usanifu na ujenzi wa mradi wa usambazaji maji safi katika maeneo ambayo miundombinu haipo pamoja na ujenzi wa mitambo ya kutibu maji taka maeneo ya Kurasini, Mbezi beach na Jangwani na miundombinu ya kuondoa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam ambapo shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 43.0 fedha za nje zimetengwa.

(n) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuanza ujenzi wa bwawa la Kidunda ambapo shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

(o) Mradi wa Maji wa Mpera na Kimbiji

Shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha uchimbaji wa visima 20 vya Kimbiji na Mpera na kuendeleza visima hivyo kwa kulaza bomba na ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji katika maeneo karibu na visima hivyo.

4.3.3.4 Ujuzi na Uwezesaji

(a) Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini

Shilingi bilioni 9.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukuza ujuzi na stadi kazi kwa kupitia uanagenzi katika kilimo, viwanda, biashara na TEHAMA. Maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa ni pamoja na kurasimisha ujuzi na kutoa mafunzo ya uanagenzi kwa vijana 10,000; kutoa mafunzo ya vitendo kazini kwa vijana 5,000 waliohitimu ngazi mbalimbali za elimu; kutoa mafunzo ya ujasiriamali na vifaa kwa vijana ili kuongeza ufanisi na ujuzi katika sekta isiyo rasmi; na kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi kwa vijana 10,000.

(b) Mfuko wa Maendeleo ya Vijana

Shughuli zilizopangwa ni: kuwawezesha vijana mitaji na mikopo nafuu kwa miradi 100 kupitia SACCOS; na kuandaa mkakati wa kisekta wa usimamizi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambapo shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani na shilingi milioni 65.0 fedha za nje zimetengwa.

(c) Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini katika Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III): shughuli zilizopangwa ni kuendelea na utekelezaji wa kipindi cha pili cha TASAF III kwa kuongeza maeneo ya utekelezaji kutoka 161 ya sasa hadi maeneo 187 katika halmashauri zote Tanzania Bara na wilaya zote Zanzibar ambapo shughuli za miradi 2,505 ya kutoa ajira za muda na kuendeleza miundombinu zitatekelezwa Tanzania Bara na miradi 204 zitatekelezwa Zanzibar ambapo shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani na shilingi bilion 97.6 fedha za nje zimetengwa.

4.3.3.5 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

(a) Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

Shughuli zilizopangwa ni: ukarabati na ufungaji wa mitambo katika studio za redio na televisheni jijini Dodoma, ujenzi wa makao makuu ya TBC katika eneo la Vikonje jijini Dodoma; ununuzi wa mitambo na vifaa vya urushaji matangazo mubashara; ufungaji wa mitambo ya kuongeza usikivu katika Wilaya za Same, Sikonge, Bunda, Kahama, Nkasi, Kasulu na Karagwe; ujenzi na ukarabati wa studio za redio (TBC Taifa, TBC FM na TBC International); na ufungaji wa mitambo na vifaa vya kisasa vya kidijitali vitakavyowezesha urushaji wa maudhui na matangazo kwenye mitandao ya kijamii ambapo shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani zimetengwa.

(b) Habari kwa Umma

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukusanya, kuchakata, kuandaa na kusambaza

taarifa kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa Miradi na Programu zinazotekelezwa na Serikali; na kununua vitendea kazi muhimu kwa ajili ya ukusanyaji, uchakataji na usambazaji wa taarifa kwa wananchi ambapo shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

(c) Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika

Shughuli zilizopangwa ni: ukarabati wa maeneo yenye kumbukumbu kuhusu harakati za ukombozi wa Bara la Afrika ikiwemo majengo yaliyotumika katika harakati hizo; na kufanya tafiti, kuhifadhi na kutangaza urithi wa ukombozi wa bara la Afrika unaoshikika na usioshikika ambapo shilingi milioni 515 fedha za ndani zimetengwa.

(d) Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi na utunzaji wa uwanja wa ndani wa Taifa katika eneo Changamani la Michezo la Taifa lililopo Dar es Salaam ambapo shilingi milioni 650 zimetengwa.

(e) Ujenzi wa Chuo cha Michezo cha Malya

Shilingi milioni 300 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu (3), bwalo pamoja na kuweka samani.

(f) Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa)

Shughuli zilizopangwa ni ukarabati wa madarasa, maktaba na studio ya kufundishia kwa vitendo pamoja na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambapo shilingi milioni 250 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.3.6 Utawala Bora na Huduma Bora kwa Wananchi

(a) Azma ya Serikali Kuhamia Dodoma

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na taratibu za ujenzi wa mji wa Serikali Mtumba awamu ya pili; na kuendelea na ujenzi wa barabara za lami km 40 ambapo shilingi bilioni 49 fedha za ndani zimetengwa.

(b) Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu

Shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi wa uzio wa nje wenye urefu wa kilomita tano (5) ambapo shilingi bilioni 2.37 fedha za ndani zimetengwa.

(c) Kuimarisha Mfuko wa Mahakama

Kuimarisha shughuli za Mfuko wa Mahakama hususan kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mahakama ambapo shilingi bilioni 59.0 zimetengwa, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 30.0 fedha za ndani na bilioni 28.0 fedha za nje. Miradi itakayotekelezwa ni:

- (i) **Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama za Wilaya:** shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi wa Mahakama za wilaya 15 na kuziwekea vifaa ambapo shilingi bilioni 5.2 fedha za ndani zimetengwa;
 - (ii) **Mradi wa Upanuzi wa Majengo ya IJA:** shughuli zilizopangwa ni kukamilisha awamu ya tatu ya ujenzi wa Bweni IJA - Lushoto ambapo shilingi milioni 900 fedha za ndani zimetengwa;
 - (iii) **Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama za Mwanzo:** shilingi bilioni 3.1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo;
 - (iv) **Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama Kuu:** shughuli zitakazotekelezwa ni ukarabati wa Mahakama Kuu Songea na Tabora; na ujenzi wa Mahakama kuu katika Mkoa wa Kilimanjaro ambapo shilingi bilioni 3.2 fedha za ndani zimetengwa;
 - (v) **Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo:** shughuli zilizopangwa ni ujenzi wa nyumba za majaji eneo la Chimala; na ujenzi wa nyumba mbili (2) Dodoma ambapo shilingi bilioni 2.6 fedha za ndani zimetengwa;
 - (vi) **Ujenzi wa Mahakama Kuu Dodoma:** Shughuli zilizopangwa ni ujenzi wa majengo ya mahakama kuu Dodoma ambapo shilingi bilioni 24.0 fedha za ndani zimetengwa.
 - (vii) **Mradi wa "Citizen Centric Judiciary Modernisation Project":** shilingi bilioni 28.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Vituo sita (6) Jumuishi vya Haki - IJC; na ujenzi wa mahakama 33 za wilaya; na
 - (viii) **e - Judiciary na e - Justice:** kuimarisha mifumo ya uendeshaji wa shughuli za mahakama na utoaji haki kwa kuweka mifumo ya kielektroniki (e - Judiciary na e-justice) pamoja na kusimika kanzidata ya Wanasheria katika utumishi wa umma ambapo shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.
- (d) **Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge**
- (i) **Ukarabati wa Ukumbi wa Bunge:** shughuli zitakazotekelezwa ni: usanifu wa paa jipya na miundombinu yake; ununuzi na uwekaji wa paa jipya la vigae kwenye Ukumbi wa Bunge; ukarabati wa miundombinu iliyoharibika katika ukumbi wa Bunge; marekebisho, ujenzi na upakaji rangi wa Jengo la Bunge ambapo shilingi bilioni 3.2 fedha za ndani zimetengwa;
 - (ii) **Ujenzi wa miundombinu ya Bunge:** shughuli zilizopangwa ni:

kufanya upembuzi yakinifu wa udongo na usanifu wa awali kwenye viwanja vya makazi ya viongozi; na ununuzi na ufungaji wa vifaa vya usalama kwenye majengo ya Bunge ambapo shilingi bilioni 1.8 fedha za ndani zimetengwa;

- (iii) **Mradi wa Kulijengea Bunge Uwezo Awamu ya Pili (LSP II):** shilingi bilioni 2.57 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya nyaraka muhimu za Bunge jipya; mafunzo elekezi kwa Wabunge wapya; na mafunzo kwa Wabunge na Watumishi katika masuala ya bajeti, uandaaji wa miswada, utungwaji wa Sheria, utafiti, ufuatiliaji na tathmini, mifumo ya TEHAMA na ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge;

- (e) **Ujenzi wa Majengo ya Utawala kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Shilingi bilioni 49.29 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya utawala ya ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tarafa na nyumba za viongozi katika mikoa, wilaya na tarafa.

- (f) **Vitambulisho vya Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea kutambua, kusajili na kutoa namba za utambulisho pamoja na Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi ambapo jumla ya watu 6,076,666 wanatarajiwa kusajiliwa ili kufikia lengo la kusajili wananchi 27,796,983 ifikapo Juni, 2021; kuendelea na usajili wa wageni wakaazi, walowezi na wakimbizi Tanzania bara na Zanzibar; kuunganisha Wilaya 16 za Tanzania Bara na Zanzibar katika mtandao wa mawasiliano ili kusafirisha taarifa za usajili na utambuzi wa wananchi kutoka wilayani kwenda kituo cha kuchakata na kutunza taarifa; kuendelea na ujenzi wa ofisi 31 za usajili za wilaya Tanzania Bara na Zanzibar, ujenzi wa jengo la Makao Makuu (Dodoma) pamoja na ghala la kuhifadhi vifaa na sehemu ya matengenezo ya vifaa; kuunganisha Taasisi 39 za Umma na Binafsi katika mfumo wa NIDA ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi; ununuzi wa kadi ghafi (*raw cards*) 12,556,657; ununuzi wa kompyuta 70, Router 20, magari matano (5), Server 20 na printer 26 ambapo shilingi bilioni 10.0 fedha za ndani na shilingi milioni 861.81 ni fedha za nje zimetengwa.

- (g) **Usalama wa Raia**

Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani na shilingi milioni 34.05 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kugharamia Mpango wa Ulinzi wa Haki za Mtoto na Ushirikishwaji; ujenzi wa kituo cha polisi Mkokotoni Zanzibar; ujenzi wa ofisi na nyumba za makazi - Byekera Kagera; ujenzi wa kituo cha polisi Mbalizi - Mbeya; na ujenzi wa nyumba

za makazi ya askari Meatu – Simiyu.

(h) Magereza

Shilingi bilioni 14.59 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: ujenzi wa jengo la ofisi ya Makao Makuu ya Magereza – Dodoma; ujenzi wa kiwanda cha mikate katika chuo cha TCTA; ukarabati mifumo ya maji taka katika magereza ya Njombe, Geita, Isupilo, Masasi, Nachingwea, Kahama, Karatu na Isanga; ujenzi wa miundombinu ya majisafi katika magereza ya Kitete, Mollo na Mwanga; na ukarabati wa mabweni ya gereza la Ukonga na sehemu ya kushonea nguo gereza Butimba.

(i) Zimamoto na Uokoaji

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ukarabati na upanuzi wa huduma za zimamoto ambapo shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa katika ujenzi wa kituo cha zimamoto na uokoaji katika wilaya za Chamwino na ununuzi wa magari matatu (3) ya zimamoto.

(j) Uhamiaji

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ujenzi wa ofisi za uhamiaji katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Geita, Manyara; ujenzi wa nyumba za makazi ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji ya Jijini Dodoma na Masaki, Dar es salaam; pamoja na kukamilisha ukarabati wa nyumba za makazi za watumishi katika Mkoa wa Shinyanga-Ibinzamata; na kuanza ujenzi wa ofisi za uhamiaji katika wilaya za Chato, Simanjiro, Rorya, Mufindi, Kyerwa na Mlele ambapo shilingi bilioni 4.45 fedha za ndani zimetengwa.

(k) Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na utekelezaji wa programu ya maboresho katika utumishi wa Umma kwa kujenga nyumba za Viongozi Wastaafu wa Kitaifa (Awamu ya II na IV); kuendelea na utekelezaji wa Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi, kuendelea na uimarishaji wa vituo vya kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya TEHAMA ya Serikali na kujikinga na majanga, kuongeza usalama wa mifumo na taarifa za Serikali; kuendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara (HCMIS); usanifu wa mfumo wa kidigitali wa upangaji wa Rasimalimali watu katika Taasisi za Umma - eHRP; na usanifu na utekelezaji wa Mfumo wa Kidigitali wa Mfumo Wazi wa Upimaji wa Utendajikazi – e-OPRAS ambapo shilingi bilioni 10.95 fedha za ndani zimetengwa.

(l) **Utawala wa Sheria**

- (i) **Mradi wa Kusaidia Sekta Mbalimbali katika Kulinda Haki za Mtoto (UNICEF Multisectorial Support):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Ulinzi na Uendelezaji wa Haki za Mtoto (*Child Protection*) nchini; na kusajili vizazi milioni tatu vya watoto wa umri chini ya miaka mitano ambapo shilingi milioni 236.25 fedha za nje zimetengwa;
- (ii) **Mradi wa Upatikanaji wa Haki za Binadamu (Access to Justice and Human Rights):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuweka mfumo wa kielektroniki wa kukusanya takwimu na ufuatiliaji wa taarifa za kuhifadhi na kulinda haki za binadamu pamoja na kutekeleza Mpango wa Pili wa Taifa wa Haki za Binadamu ambapo shilingi bilioni 3.5 fedha za nje zimetengwa;
- (iii) **Mpango Kazi Endelevu wa Kupambana na Rushwa (Building Sustainable Anti-Corruption Action Plan in Tanzania - BSAAT):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuimarisha mifumo ya Haki Jinai kwa kutumia TEHAMA ambapo shilingi milioni 730 fedha za nje zimetengwa; na
- (iv) **Mradi wa Kuboresha Uwajibikaji (Improving Accountability through fighting Corruption and Increased Access to Justice - IMPACT):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea kutekeleza Mkakati wa Huduma ya Msaada wa Sheria Nchini, ambapo shilingi bilioni 1.297 fedha za nje zimetengwa.

- (m) **Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo:** shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250; ujenzi wa jengo la utawala (Awamu ya Kwanza); ujenzi wa darasa na ofisi kampasi ya Dodoma Mjini; ununuzi wa vitanda na magodoro; na kukarabati mabweni, ofisi na nyumba za watumishi ambapo shilingi bilioni 1.6 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.3.7 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

- (a) **Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Ikolojia ili kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

Shughuli zilizopangwa ni kutoa mafunzo kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi na kutumia mifumo ya Ikolojia ili kukabiliana na athari hizo katika wilaya za Simanjiro, Mpwapwa, Mvomero, Kishapu na Kaskazini A (Zanzibar); ukarabati wa malisho na kuongeza uzalishaji na uhifadhi wa malisho endelevu katika maeneo ya

mradi; kuboresha lindimaji na kuongoa kwa kutumia mimea ya asili; kuboresha kingo za mito; kutekeleza na kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kilimo kinachozingatia njia bora za kilimo; na kuboresha uwezo wa jamii za vijijini kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kuwawezesha kiuchumi ambapo shilingi milioni 400 fedha za ndani na shilingi bilioni 4.64 fedha za nje zimetengwa.

(b) Mradi wa Kusimamia Uhifadhi na Matumizi Endelevu ya Bonde la Ziwa Nyasa

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuandaa programu za uelimishaji jamii kuhusu usimamizi endelevu wa Bonde la Ziwa Nyasa; kuongoa ardhi iliyoharibika kwa kupanda miti; kuongeza uwezo wa uzalishaji wa ardhi; kuboresha maisha ya watu wanaozunguka Bonde la Ziwa Nyasa; na kuwezesha sera na mifumo ya kitaasisi kuhusu usimamizi endelevu wa Ziwa Nyasa ambapo shilingi bilioni 1.3 fedha za nje zimetengwa.

(c) Mpango wa Ufuatiliaji na Udhhibiti wa Taka Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu

Shughuli zilizopangwa ni: kufanya uchambuzi wa kina pamoja na kutambua vyanzo vya takwimu za usimamizi wa kemikali; kuainisha mapungufu katika takwimu; kuandaa viashiria muhimu vya afya na mazingira kuhusu kuongezeka kwa ufanisi katika usimamizi wa kemikali; kufanya tathmini ya hali halisi, mahitaji na kujenga uwezo katika mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa kemikali; kufanya tathmini, kutambua wadau na mahitaji kwa ajili ya kuhodhi mfumo wa kiuchunguzi wa usimamizi wa kemikali; kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mazingira, afya, kemikali na wataalam wa mazingira waliopo katika vituo vya mipaka juu ya usimamizi wa kemikali; kuandaa nyenzo na miongozo ya ukusanyaji, ufuatiliaji na uchunguzi katika usimamizi wa kemikali; kuwezesha uandaaji wa kanzidata ya hali ya uchomaji wa taka usio salama na uzalishwaji wa kemikali sumu; kuandaa vitini na miongozo ya mbinu rafiki kwa mazingira za namna ya kuondoa au kupunguza uchomaji wa taka usio salama; na kusaidia wadau na manispaa zilizoteuliwa kwa ajili ya majaribio kuanzisha mipango mahsusni yenye mbinu rafiki kwa mazingira ya kupunguza taka zinazopelekwa kwenye madampo ambapo shilingi milioni 654.7 fedha za nje zimetengwa.

(d) Mradi wa Kudhibiti kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: Kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa mazingira na maafisa forodha kuhusu udhibiti wa kemikali; kuandaa mfumo madhubuti wa udhibiti wa kemikali; Kujenga uwezo wa kitaasisi katika kudhibiti na kusimamia kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; na Kutoa mafunzo kwa

mafundi mchundo wanahudumia vifaa vinavyotumia kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal ambapo kiasi cha shilingi milioni 21.3 fedha za nje zimetengwa.

4.3.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendeleza na kusimamia ujenzi na ukarabati wa miundombinu wezeshi ya biashara na uwekezaji na kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini kwa kuzingatia mapendekezo yaliyoainishwa katika *Blueprint*.

4.3.4.1 Miundombinu

A. Reli

- (a) **Mfuko wa maendeleo ya reli:** shilingi bilioni 289.68 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa reli ya kati ya *standard gauge*, kuboresha miundombinu ya reli iliyopo, kuboresha mfumo wa mawasiliano, kuendelea na uratibu wa ujenzi wa miundombinu ya usafiri wa treni za abiria katika majiji, kufufua njia za reli na ukarabati wa vitendea kazi ikiwemo vichwa vya treni na mabehewa ya mizigo na abiria; na
- (b) Shilingi bilioni 95.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa njia ya reli ya kutoka Dar es Salaam - Isaka (km 970).

B. Barabara na Madaraja

Barabara Zinazofungua Fursa za Kiuchumi

- (i) **Barabara ya Kidatu - Ifakara - Lupilo - Mahenge/Malinyi - Londo - Lumecha/Songea (km 499):** kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu - Ifakara (km 66.9) na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Ifakara - Lupiro - Malinyi - Londo - Lumecha/Songea (km 396) ambapo shilingi milioni 105.0 fedha za ndani zimetengwa.
- (ii) **Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke - Kibena (km 150):** shilingi bilioni 6.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kibena - Lupembe (km 50) kwa kiwango cha lami na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Ifakara - Kihansi (km 50) na Lupembe - Madeke (km 50).
- (iii) **Barabara ya Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 383):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Usesula - Komanga (km 115.5), Komanga - Kasinde (km 112.8) na Kasinde - Mpanda (km 111.7) ambapo shilingi bilioni 2.08 fedha za ndani na shilingi bilioni 31.44 fedha za nje zimetengwa.

- (iv) **Barabara ya Makutano - Natta - Mugumu/Loliondo - Mto wa Mbu (km 235):** shilingi bilioni 12.16 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami katika barabara ya Makutano - Sanzate (km 50) na Waso - Sale (km 50); na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Sanzante - Natta (km 40), Natta - Mugumu (km 35); Tarime - Mugumu (km 50); na Mbulu - Haydom (km 50).
- (v) **Barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora (km 259.7):** shughuli zitakazotekelezwa ni kulipa madai ya makandarasi na wahandisi washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni - Itigi - Chaya (km 89.35) na Tabora - Nyahua (km 85); na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyahua - Chaya (km 85.4) ambapo shilingi milioni 650 fedha za ndani na shilingi bilioni 22.71 fedha za nje zimetengwa.
- (vi) **Barabara ya Itoni - Ludewa - Manda (km 211):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha zege sehemu ya Lusitu - Mawengi (km 50) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Itoni - Lusitu (km 50) ambapo shilingi bilioni 12.0 fedha za ndani zimetengwa.
- (vii) **Barabara ya Handeni - Kibereshi - Kibaya - Singida (km 460):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi wa barabara ya Handeni - Kiberashi - Kijungu - Kibaya - Njoro - Olboloti - Mrojo Chini - Dalai - Bicha - Chambalo - Chemba - Kwa Mtoro - Singida (km 460) kwa kuanzia na sehemu ya Handeni - Kiberashi (km 50) kwa kiwango cha lami ambapo shilingi bilioni 6.0 fedha za ndani zimetengwa.
- (viii) **Barabara ya Dodoma - Iringa (km 267.1):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo wa Iringa (Iringa Bypass km 7.3) na kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa - Dodoma ambapo shilingi bilioni 3.02 fedha za ndani zimetengwa.
- (ix) **Barabara ya Dodoma - Babati (km 263.4):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Babati (*Babati Bypass* km 12) ambapo shilingi milioni 60.0 fedha za ndani zimetengwa.
- (x) **Barabara ya Mbeya - Makongolosi (km 267.90):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Chunya - Makongolosi (km 43); na kuanza ujenzi wa sehemu za Itigi - Mkiwa - Noranga (km 56), Mbalizi - Makongolosi (km 50) na Makongolosi - Rungwa - Noranga (km 356) ambapo shilingi bilioni 11.06 fedha za ndani zimetengwa.
- (xi) **Barabara ya Kigoma - Kidahwe - Uvinza - Kaliua - Tabora (km 389.7):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi sehemu za Urambo - Kaliua (km 28); na Kazilambwa - Chagu (km 42); na kuanza ujenzi kwa

- kiwango cha lami sehemu ya Uvinza – Malagarasi (km 51.1) ambapo shilingi bilioni 10.44 fedha za ndani na shilingi bilioni 15.0 fedha za nje zimetengwa.
- (xii) **Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (DD Review and Rehabilitation) (km 200):** shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami.
- (xiii) **Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 221):** shilingi bilioni 10.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi; sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) na maandalizi ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mnivata – Tandahimba (km 50).
- (xiv) **Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50):** shilingi bilioni 1.59 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilomita 10 kwa kiwango cha lami.
- (xv) **Barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130):** shilingi milioni 250.0 zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.
- (xvi) **Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 145):** shilingi bilioni 7.43 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Masasi – Nachingwea (km 45) na Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100) kwa kiwango cha lami.
- (xvii) **Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343):** shilingi bilioni 15.03 fedha za ndani na shilingi bilioni 7.89 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Mbinga – Mbamba Bay (km 66), Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na daraja la Mnywamaji.
- (xviii) **Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5):** shilingi bilioni 7.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 43.8 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani (km 50) kwa kiwango cha lami; kuanza ujenzi wa barabara ya Pangani – Mkange (km 124.5) kwa kiwango cha lami pamoja na Daraja la Pangani.
- (xix) **Barabara ya Kisarawe – Maneromongo (km 54):** shilingi bilioni 1.4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.
- (xx) **Barabara ya TAMCO –Vikawe – Mapinga (km 24):** shilingi milioni 950 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.
- (xxi) **Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7):** shilingi milioni 10 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi.
- (xxii) **Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119):** shilingi milioni 630 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.
- (xxiii) **Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6):** shilingi milioni 730 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara

kwa kiwango cha lami.

- (xxiv) **Barabara ya Nzega - Tabora (km 289.7):** shughuli zilizopangwa ni kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Nzega - Puge (km 58.6) na Puge - Tabora (km 56.1); kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Shelui - Nzega (km 110) kwa kiwango cha lami; na kuanza ujenzi wa barabara ya Nzega - Kagongwa (km 65) ambapo shilingi bilioni 2.02 fedha za ndani zimetengwa.
- (xxv) **Barabara ya Msimba - Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 376.8):** shilingi bilioni 8.96 fedha za ndani zimetengwa kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mbarali - Ubaruku (km 8.9) kwa kiwango cha lami; kuanza ujenzi wa barabara za Rujewa - Madibira - Mafinga (km 152); kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mafinga - Mgololo (km 78); na kukarabati barabara ya Morogoro - Iringa sehemu ya Tumbaku Jct. - Mangae/Melela - Mikumi - Iyovi (km 156.45).
- (xxvi) **Barabara ya Igawa - Songwe -Tunduma pamoja na Mchepuo wa Mbeya (Mbeya bypass) (km 273.4):** shilingi milioni 60 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Igawa - Songwe-Tunduma (km 218) pamoja na barabara ya mchepuo ya Mbeya (Uyole - Songwe km 48.9) na Iwambi - Mbalizi (km 6.5).
- (xxvii) **Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4):** shilingi bilioni 22.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe - Makete - Isyonje sehemu ya Njombe - Moronga (km 53.9) na Moronga - Makete (km 53.5); na kuanza ujenzi wa barabara ya Isyonje - Makete (km 50) kwa kiwango cha lami.
- (xxviii) **Barabara ya Makambako - Songea na barabara ya Mchepuo ya Songea (Songea bypass) (km 295):** shilingi milioni 20 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa kina wa barabara ya Mchepuo wa Songea (Songea Bypass) na maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Makambako - Songea.
- (xxix) **Barabara za kuelekea Mradi wa Kufua Umeme katika Maporomoko ya Mto Rufiji (km 348):** shilingi bilioni 3.18 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara za Bigwa - Matombo - Mvuha (km 70), Maneromango - Vikumburu - Mloka (km 100) na Kibiti - Mloka - Mtemele - Rufiji. Aidha, kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ubena Zomozi - Mvuha - Kisaki - Mtemele Junction (km 178).
- (xxx) **Barabara ya Dar es Salaam - Chalinze - Morogoro (km 152.3):** shilingi bilioni 3.81 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na matengenezo ya

dharura katika barabara ya Mlandizi - Chalinze (km 44); kufanya usanifu wa kina wa ukarabati (overlay) wa barabara ya Mlandizi - Chalinze (km 44.24); na ujenzi sehemu ya kwa Mathiasi - Msangani (km 8.3) katika barabara ya Morogoro kwa kiwango cha lami.

- (xxxix) **Barabara ya Dodoma - Manyoni (km 127) na Barabara ya Mchepuo Kuingia Manyoni Mjini(Km 4.8):** shilingi milioni 160 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi - Muhalala (Manyoni) na kulipa madai ya Mkandarasi wa mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (*Weigh in Motion - WIM*) uliojengwa Nala (Dodoma).
- (xxxii) **Barabara ya Dumila - Kilosa - Mikumi (km 141):** shilingi bilioni 13.52 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Rudewa - Kilosa (km 24); na kuanza ujenzi wa barabara ya Kilosa - Ulaya - Mikumi (km 50) kwa kiwango cha lami.
- (xxxiii) **Barabara ya Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105):** shilingi bilioni 8.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya fidia na kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.
- (xxxiv) **Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 189):** shilingi bilioni 5.42 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kibaoni - Majimoto - Inyonga (km 152) na Ntendo - Muze - Kilyamatundu sehemu ya Ntendo - Muze (km 37) kwa kiwango cha lami.
- (xxxv) **Barabara ya Kyaka - Bugene - Kasulo (km 222.1):** shilingi bilioni 2.01 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha mapitio ya usanifu wa barabara za Kumunazi - Bugene - Kasulo na Kyaka - Mutukula (km 124).
- (xxxvi) **Barabara ya Tabora - Ipole - Rungwa (Sehemu ya Ipole - Rungwa (km 172):** shilingi bilioni 1.15 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.
- (xxxvii) **Barabara ya Same - Mkumbara - Korogwe (km 147.5):** shilingi bilioni 6.06 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same - Himo (km 76) na Mombo - Lushoto (km 32) kwa kiwango cha lami; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Lushoto - Magamba - Mlola (km 34.5) na Same - Kisiwani - Mkomazi (km 97) sehemu ya Same - Kisiwani (km 5) kwa kiwango cha lami.

Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani

- (i) **Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 112):** shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 112) na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai -

- Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami ambapo shilingi bilioni 11.0 fedha za ndani zimetengwa.
- (ii) **Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai - Kamwanga /Bomang'ombe - Sanya Juu (km 84.8):** shilingi bilioni 1.7 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za kwa Sadala - Masama - Machame Junction (km 16) na Kiboroloni - Kiharara - Tsuduni - Kidia (km 10.8).
 - (iii) **Barabara ya Isaka - Lusahunga (km 392):** shilingi bilioni 2.74 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi - OSIS cha Nyakanazi; na kuanza ukarabati wa sehemu ya Lusahunga - Rusumo na Nyakasanza - Kobero (km 150).
 - (iv) **Barabara ya Nyakahura - Kumubuga - Rulenge - Kabanga Nickel (km 141):** shilingi milioni 30 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.
 - (v) **Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56):** shilingi bilioni 14.32 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mpanda - Ifukutwa - Vikonge (km 30) na kuanza ujenzi sehemu za Kibaoni - Sitalike (km 71) na Kizi - Lyambalyamfipa - Sitalike (km 86.3) kwa kiwango cha lami.
 - (vi) **Barabara ya Nyanguge - Musoma/ Usagara - Kisesa (km 202.25):** shilingi milioni 903 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Musoma - Makojo - Busekela (km 92); na kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge - Simiyu/Mara Border (km 100.4) kwa kiwango cha lami.
 - (vii) **Barabara ya Nyamuswa - Bunda - Kisorya (km 106):** shilingi bilioni 4.79 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Nansio - Kisorya - Bunda - Nyamuswa sehemu ya Kisorya - Bulamba (km 51) na Nyamuswa - Bunda - Bulamba (km 55) kwa kiwango cha lami.
 - (viii) **Barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 181.8):** shilingi bilioni 3.52 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Maswa - Bariadi (km 49.7) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Isabdula (Magu) - Kwimba Station - Ngudu - Ng'hungumalwa (km 10) kwa kiwango cha lami.
 - (ix) **Barabara ya Kidahwe - Kasulu - Kibondo - Nyakanazi (km 341.25):** shilingi bilioni 21.25 fedha za ndani na shilingi bilioni 23.72 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kidahwe - Kasulu (km 63) na kuendelea na ujenzi wa barabara za Nyakanazi - Kakonko (Kabingo) (km 50), Kanyani Junction - Mvugwe (km 70.5), Mvugwe - Nduta Junction (km 59.35), Nduta Junction - Kabingo (km 62.5) na Nduta Junction - Kibondo (km 25.9); na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibondo - Mabamba (km 35) kwa kiwango

cha lami.

- (x) **Barabara ya Mpemba - Isongole (km 51.2):** shilingi bilioni 5.31 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mpemba - Isongole (km 51.2) kwa kiwango cha lami; maandalizi ya ujenzi wa barabara za Ruanda - Iyula - Nyimbili (km 21); na kufanya usanifu na kujenga barabara ya Katumbasongwe - Kasumulu - Ngana - Ileje (km 90.1) kwa kiwango cha lami.
- (xi) **Barabara ya Usagara - Geita - Buzirayombo - Kyamyorwa (km 388):** shilingi bilioni 12.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Geita - Bulyanhulu *Junction* (km 58.3), Bulyanhulu *Junction* - Kahama (km 61.7), Geita - Nzera (km 54) na Uyogo - Nyamilangano - Nyandekwa - Kahama (km 54).

Barabara za Mikoa

Shilingi bilioni 48.5 fedha za ndani na shilingi milioni 380.96 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa kilomita 589.31 kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilomita 41.31 kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja/Makalavati makubwa 24.

Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 152.16)

Shilingi bilioni 7.07 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Banana - Kitunda - Kivule - Msongola (km 14.7) na Wazo Hill - Madale (km 6); kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba - Kisopwa - Kwembe - Makondeko (km 14.66) sehemu ya Mloganzila - Mloganzila Citizen (km 4), Ardhi - Makongo (km 5), Kongowe - Mjimwema - Kivukoni Ferry, Mji Mwema - Kimbiji - Pembamnazi (km 27) na Goba-Matosa - Temboni (km 6) pamoja na kuanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1) na Kongowe - Mji Mwema - Kivukoni (km 25.1).

Upanuzi wa Barabara ya Kimara - Kibaha (km 25.7) ikijumuisha upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji: shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na upanuzi wa barabara ya Kimara - Kibaha kuwa njia nane (8) sehemu ya Kimara - Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga ambapo shilingi bilioni 9.0 fedha za ndani zimetengwa.

Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka

Shilingi bilioni 7.87 fedha za ndani na shilingi bilioni 43.88 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka; kuanza ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka

awamu ya tatu na nne; kuboresha karakana ya DART iliyoko Jangwani; na kufanya mapitio ya usanifu wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya tano.

Ujenzi wa Barabara za Juu (*Flyover*) Jijini Dar es Salaam

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo; kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Kenyata na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jet); na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa *Mabey Flyovers* katika jiji la Dar es Salaam ambapo shilingi milioni 180.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 5.55 fedha za nje zimetengwa.

Barabara ya Chuo Kikuu cha Dodoma *University* na Barabara ya Mzunguko wa Dodoma

Shilingi bilioni 22.83 fedha za ndani na shilingi bilioni 18.27 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara ya kutoka Ihumwa kuelekea Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12) na barabara za Ikulu ya Chamwino; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma (*Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road*) sehemu ya Nala - Veyula - Mtumba - Ihumwa *Dry Port* (km 52.3), sehemu ya Ihumwa *Dry Port* - Matumbulu - Nala (km 60.0) na upanuzi wa barabara ya Bahi *Round About* - Image *Round About* - Ntyuka *Round About* - Makulu *Round About*. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Ntyuka *Junction* - Mvumi *Hospital* - Kikombo *Junction* (km 76.07) na barabara ya Kikombo *Junction* - Chololo - Mapinduzi (km 18). Aidha, mradi huu utahusisha upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katikati ya mji wa Dodoma (km 200) zinazohusisha barabara ya Dodoma - Morogoro (km 50); Dodoma - Iringa (km 50); Dodoma - Singida (km 50) na Dodoma - Arusha (km 50).

Barabara za Vijijini na Mijini

Shilingi bilioni 275.03 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za wilaya zilizopo vijijini na mijini zenye urefu wa km 23,175.11. Kati ya hizo, km 14,104.86 ni matengenezo ya kawaida, km 6,094.52 ni matengenezo ya maeneo korofi na km 2,975.73 ni matengenezo ya muda maalum; ujenzi na ukarabati wa madaraja 80, makalvati 2,052 na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa km 79.9; ujenzi wa barabara urefu wa km 35.3 kwa kiwango cha lami na ukarabati wa barabara urefu wa km 321 kwa kiwango cha changarawe.

Ujenzi wa Madaraja

- (i) **Ujenzi wa Madaraja Makubwa:** shilingi bilioni 19.46 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa Madaraja ya Magufuli (Morogoro), Magara (Manyara), Mlalakuwa (Dar es Salaam), Momba (Rukwa), Lukuledi (Lindi) na Mara (Mara). Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara); kuendelea na ujenzi wa Daraja la Sibiti (Singida) na barabara zake unganishi, Daraja Jipya la Wami (Pwani) lenye urefu wa mita 510 na barabara unganishi zenye urefu wa km 4.3, Daraja la Msingi (Singida), Daraja la Kitengule (Kagera) na Barabara Unganishi (km 18), Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), na Daraja la Sukuma (Mwanza). Aidha, kazi nyingine ni kufanya mapitio ya usanifu na ujenzi wa Daraja la Mirumba (Katavi); ujenzi wa Daraja la Simiyu (Mwanza), Daraja la Kiegeya (Morogoro), madaraja ya Sanza na Mkenda (Ruvuma). Vilevile, mradi huu utahusisha kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa madaraja ya Mtera na Godegode (Dodoma) na Daraja la Mitomoni (Ruvuma); kuanza upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina wa Daraja la Malagarasi Chini (Kigoma), Daraja la Mzinga, Daraja la Ugalla, na kununua vipuri vya daraja la vyuma la dharura.
- (ii) **Daraja Jipya la Selander (Dar es Salaam):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa daraja na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa km 5.2 ambapo shilingi bilioni 48.16 fedha za nje zimetengwa.
- (iii) **Daraja la Nyerere na Barabara Unganishi (km 6.9):** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi za Kigamboni (Daraja la Nyerere) – Vijibweni (km 1.5); kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mjimwema (km 1.6); na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani *Junction*/Tundwisongani – Kimbiji (km 41) ambapo shilingi bilioni 2.8 fedha za ndani zimetengwa.
- (iv) **Daraja la Kigongo - Busisi na Barabara Unganishi:** shilingi bilioni 21.3 fedha za ndani zimetengwa kuendelea na ujenzi wa daraja lenye urefu wa km 3.2 na barabara unganishi.

C. Ujenzi Nyumba za Serikali

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ujenzi wa nyumba za Makazi, Magomeni Kota Manispaa ya Kinondoni – DSM; ujenzi wa nyumba za Viongozi; kuwezesha utoaji huduma za usanifu, kuandaa michoro na kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano mkoani Dodoma; ukarabati/matengenezo ya nyumba za viongozi mkoa wa Dodoma; ukarabati wa karakana za Serikali (TBA) katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Dodoma, Tabora, Dar

es Salaam na Mbeya; ujenzi wa karakana mpya ya kisasa katika mkoa wa Dodoma; na kukamilisha ujenzi wa karakana (Awamu ya III) katika mkoa wa Manyara na ujenzi wa karakana mpya tano (5) za TEMESA katika mikoa mipya mitano (Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi) ambapo shilingi bilioni 66.87 fedha za ndani zimetengwa.

D. Usafiri Majini

- (a) **Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa:** shilingi bilioni 135.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 4.09 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kukamilisha malipo ya meli mpya inayoendelea kujengwa katika Ziwa Victoria; malipo ya awali ya ununuzi wa meli mpya katika Ziwa Tanganyika; kujenga meli ya mizigo (*ferry wagon*) katika Ziwa Victoria na meli nyingine ya mizigo katika Ziwa Tanganyika; kujenga meli ya kusafirisha mizigo katika Bahari ya Hindi; kuweka mifumo ya TEHAMA; na kukarabati meli za MV. Liemba, MV. Umoja, MV. Serengeti, MT. Sangara, MT. Ukerewe, na MT. Nyangumi.
- (b) **Vivuko**
- (i) **Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko:** shilingi bilioni 2.87 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa jengo la abiria na maegesho ya Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati - Mafia; ujenzi na ukarabati wa maegesho nane (8) ya Bugolora - Ukara, Rugezi - Kisorya, Kilambo - Namoto, Utete - Mkongo, Iramba - Majita, Nyakarilo - Kome, Kasharu - Buganguzi na Kigongo - Busisi; ujenzi wa ofisi, jengo la abiria na uzio kwenye vituo 10 vya vivuko (Bugolora, Ukara, Kome, Nyakaliro, Misome, Kaunda, Nkome, Kisorya, Musoma, na Kinesi) pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Ngara - Nyakiziba na Muleba - Ikuza.
- (ii) **Ununuzi wa Vivuko Vipya:** shilingi bilioni 6.75 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ununuzi na ujenzi wa vivuko vya Nyamisati - Mafia; Bugolora - Ukara, Kisorya - Rugezi; ununuzi wa vifaa vya karakana; na ununuzi wa boti moja (1) la uokozi kwa ajili ya Utete - Mkongo.
- (iii) **Ukarabati wa Vivuko:** shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ukarabati wa Vivuko vya MV Tegemeo (Mwanza), MV Musoma (Mara), MV Mara (Mara), MV Misungwi (Mwanza), MV Sengerema (Mwanza), MV Ujenzi (Mwanza), MV Kigamboni (Dar es Salaam), MV Kome II (Mwanza) na boti ya uokozi MV KIU (Mwanza). Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa MV Nyerere (Mwanza), MV Kilombero I (Morogoro) na MV Kilombero II

(Morogoro) ambapo shilingi bilioni 4.17 fedha za ndani zimetengwa.

E. Bandari

Shilingi bilioni 500 fedha za ndani na shilingi bilioni 200 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya:

- (a) Kukamilisha Mradi wa uboreshaji wa Gati Na. 5 - 7 katika Bandari ya Dar es Salaam;
- (b) Kukamilisha ujenzi wa Gati moja (multipurpose terminal) lenye urefu wa mita 300 katika Bandari ya Mtwara;
- (c) Kuendelea na Mradi wa kupanua na kuchimba Lango la kuingilia na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin) katika Bandari ya Tanga;
- (d) Kuanza utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Matanki ya kuhifadhia Mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam;
- (e) Kuanza kutekeleza Mradi wa kupanua na kuchimba Lango la kuingilia na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin) katika Bandari ya Dar es Salaam;
- (f) Kuendelea na ununuzi wa Mitambo na vifaa mbalimbali kwa Bandari zote;
- (g) Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA na mfumo wa usalama bandarini (Port Integrated Security System - ISS); na
- (h) Kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala, Ruvu.

F. Usafiri wa Anga

(a) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere - JNIA

Shilingi bilioni 13.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya mkandarasi na mshauri elekezi na kuanza maandalizi ya usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa Jengo la Pili la Abiria (Terminal II). Aidha, shilingi bilioni 13.4 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa karakana ya ndege - JNIA na ujenzi wa jengo la kutunzia vipuri vya ndege - *Terminal I*.

(b) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato

Shughuli zilizopangwa ni kuanza ujenzi na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi ambapo shilingi bilioni 20.05 fedha za ndani na shilingi bilioni 19.67 fedha za nje zimetengwa.

(c) Kiwanja cha Ndege cha Songwe (Awamu ya III na IV)

Shughuli zilizopangwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria, ufungaji wa taa za kuongozea ndege, ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara ya kiungio pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye

barabara ya kutua na kuruka ndege na ujenzi wa uzio wa usalama ambapo shilingi bilioni 8.9 fedha za ndani zimetengwa.

(d) Kiwanja cha ndege Mwanza - Awamu ya II

Shughuli zilizopangwa ni ujenzi wa jengo jipya la abiria, maegesho ya magari na uzio wa usalama ambapo shilingi bilioni 3.02 fedha za ndani zimetengwa.

(e) Kiwanja cha Ndege Kigoma

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka); ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege; na ujenzi wa uzio, jengo la kuongozea ndege na jengo la uangalizi wa hali ya hewa ambapo shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.76 fedha za nje zimetengwa.

(f) Kiwanja cha Ndege Tabora

Shughuli zilizopangwa ni ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani pamoja na maegesho ya magari ambapo shilingi milioni 134 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.76 fedha za nje zimetengwa.

(g) Kiwanja cha Ndege Mtwara

Shughuli zilizopangwa ni kuendelea na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio, maegesho ya ndege, kufunga taa za kuongozea ndege na maegesho ya magari ambapo shilingi bilioni 5.36 fedha za ndani zimetengwa.

(h) Kiwanja cha Ndege Sumbawanga

Shughuli zilizopangwa ni: ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uangalizi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na uzio wa usalama ambapo shilingi milioni 110 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.76 fedha za nje zimetengwa.

(i) Kiwanja cha Ndege Shinyanga

Shughuli zilizopangwa ni: ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uangalizi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari; ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na uzio wa usalama ambapo shilingi milioni 110 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.76 fedha za nje zimetengwa.

(j) Kiwanja cha Ndege Arusha

Shughuli zilizopangwa ni: kuongeza urefu wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita 200; na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege, uzio wa usalama, barabara mpya ya kuingilia kiwanjani na ukarabati wa maegesho ya magari ambapo shilingi milioni 200 fedha za ndani zimetengwa.

(k) Kiwanja cha ndege Bukoba

Shughuli zilizopangwa ni ujenzi wa jengo la watu mashuhuri (*VIP Lounge*) pamoja na ufungaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa mita 200 za barabara ya kuruka na kutua ndege ambapo shilingi milioni 10.0 fedha za ndani zimetengwa.

(l) Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa

Shilingi bilioni 17.79 fedha za ndani na shilingi milioni 450 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Geita na Simiyu; upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Iringa, Songea (Ruvuma), Lindi, Kiwanja cha Lake Manyara (Manyara), Tanga na Musoma (Mara); ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na barabara ya kufanyia ukaguzi kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma; na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Moshi.

(m) Kiwanja cha Ndege Mpanda

Shilingi milioni 10.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa uzio wa usalama pamoja na ujenzi wa barabara kwa ajili kufanyia ukaguzi.

G. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

(a) Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi

Shughuli zitakazotekelezwa ni: uwekaji wa nguzo na namba za nyumba katika halmashauri zenye makao makuu ya Mikoa ya Lindi, Mbeya, Kagera, Arusha, Mtwara, Ruvuma, Songwe, Kigoma, Mara, Simiyu, Katavi, Tabora, Singida, Iringa, Mjini Magharibi, Kusini Pemba na miji ya Chato na Kibaha, halmashauri za wilaya za Chamwino, Geita na Bahi, Manispaa za Ilemela, Moshi, Morogoro, Shinyanga na Majiji ya Dodoma, Tanga na Mwanza; kuhuisha ramani, *Mobile Apps* na kanzidata; kufanya mapitio na kuhuisha Sera ya Taifa ya Posta na Mkakati wa Utekelezaji; na kufanya ufuatiliaji na tathmini ambapo shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

(b) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa inayohusisha kufikisha huduma za mkongo hadi makao makuu ya wilaya; kufikisha

huduma za Mkongo wa Taifa katika nchi za Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; ujenzi wa miundombinu ya mkongo kwa watumiaji wa mwisho ambazo ni taasisi za Serikali mijini na vijijini; usanifu wa mfumo wa taarifa za miundombinu na TEHAMA nchini utakaounganisha mifumo yote ya Serikali ili kurahisisha utumaji wa data na taarifa kutoka mfumo mmoja kwenda mwingine; ujenzi wa miundombinu ya *broadband* kwenye maeneo ya huduma za jamii; na kuandaa mpango kabambe na mwongozo kwa kituo cha data, na kwa watumiaji wa mwisho kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo kiasi cha shilingi bilioni 8.0 fedha za ndani zimetengwa.

H. Nishati

(a) Miradi ya Kuzalisha Umeme

Miradi ifuatayo imepangwa kutekelezwa:

- (i) **Ruhudji - MW 358 (Njombe): shughuli zitakazofanyika ni pamoja na:** kukamilisha uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu; usanifu wa awali wa mradi; na kumpata Mkandarasi wa kujenga mradi ambapo shilingi bilioni 252.58 zimetengwa;
- (ii) **Mtwara Power Project - MW 300:** shughuli itakayofanyika ni kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi ambapo shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.
- (iii) **Kinyerezi I Extension - MW 185:** shughuli zitakazotekelezwa ni ukamilishaji wa utekelezaji wa mradi ambapo shilingi bilioni 138.0 fedha za ndani zimetengwa;
- (iv) **Rumakali - MW 222:** shughuli zitakazofanyika ni kukamilisha kuhusha Upembuzi Yakinifu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa mradi ambapo shilingi bilioni 23.03 zimetengwa;
- (v) **Mradi wa Rusumo - MW 80:** shughuli zitakazofanyika ni kuendelea na ufungaji wa mitambo pamoja na ujenzi wa mfumo wa kupitisha maji; ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme; ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme; na kukamilisha miradi ya kijamii kwa wananchi wanaozunguka eneo la mradi (Local Area Development Plan - LADP na Livelihood Restoration Program - LRP) ambapo shilingi bilioni 13.84 fedha za nje zimetengwa;
- (vi) **Mradi wa Kikonge - MW 330:** shughuli zitakazofanyika ni kukamilisha upembuzi yakinifu; kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; na kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi ambapo shilingi bilioni 1.03 fedha za nje zimetengwa;
- (vii) **Mradi wa Kakono - MW 87:** shughuli zilizopangwa ni: kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kukamilisha Tathmini ya Athari za Kimazingira

ambapo shilingi bilioni 1.56 zimetengwa.

(b) Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

- (i) **Mradi wa Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 - North - West Grid Extension (Iringa - Mbeya - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Nyakanazi):** ulipaji wa fidia wananchi watakaopisha mradi; kuhuisha Tathmini ya Athari za Kimazingira; kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vinne (4) (Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga) vya kupoza umeme ambapo shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa. Aidha, kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kigoma hadi Nyakanazi kazi zitazotekelezwa ni kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha upembuzi yakinifu; na kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi ambapo shilingi bilioni 34.28 zimetengwa.
- (ii) **Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa Kv 220, Geita - Nyakanazi:** kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi na kituo cha kupozea umeme cha Nyakanazi; upanuzi wa kituo cha kupozea umeme cha Geita; na kusambaza umeme katika vijiji na mitaa 32 vitakavyopitiwa na mradi ambapo shilingi bilioni 25.33 zimetengwa
- (iii) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida - Arusha - Namanga:** kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme vya Dodoma na Singida ambapo shilingi bilioni 30.21 fedha za nje zimetengwa.
- (iv) **Mradi wa Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji - Chalinze - Dodoma:** kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; kumpata Mkandarasi wa ujenzi; na kuanza ujenzi wa mradi ambapo shilingi bilioni 8.14 fedha za ndani zimetengwa.
Kwa upande wa **Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Chalinze hadi Kinyerezi:** kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi; kuanza kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi ambapo shilingi bilioni 3.89 zimetengwa.
- (v) **Umeme wa Jotoardhi - Ngozi (Mbeya):** kukamilisha shughuli za uchorongaji wa visima vitatu (3) vya utafiti kwa ajili ya uhakiki wa rasilimali ya jotoardhi ambapo shilingi milioni 419 zimetengewa
- (vi) **Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini na Makao Makuu ya Wilaya:** kuendelea na utekelezaji wa mradi ambapo shilingi bilioni 363.10 fedha za

ndani na shilingi bilioni 51.16 fedha za nje zimetengwa.

(c) Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika Vitalu vya Mnazi Bay Kaskazini na Eyasi - Wembere

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuchoronga visima vya utafutaji na uhakiki na kukamilisha rasimu ya Mkataba kati ya Serikali na TPDC kuhusu utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini ambapo shilingi bilioni 102 zimetengwa. Kwa upande wa **Eyasi - Wembere**: shughuli zitakazotekelezwa ni kuchoronga kisima kifupi cha utafutaji katika eneo la Luono - Singida; kukusanya, kuchakata na kutafsiri data za kijiokemia; kutayarisha moduli ya 3D ya *Airbone Gravity Gradiometry* (AGG); kukamilisha taarifa za kimaabara za sampuli zilizokusanywa kutoka visima vitatu (3); na kuendelea na Tathmini ya Athari za Kimazingira na kukusanya data za mitetemo za 3D ambapo shilingi milioni 500 zimetengwa.

(d) Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea kukamilisha upatikanaji wa mshauri mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu ambapo shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

(e) Usambazaji wa Gesi Asilia kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira; na kumpata Mkandarasi (EPC contractor) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji katika maeneo ya Mwanambaya na Mkiu; kulipa fidia ya kutwaa ardhi kwa ajili ya maeneo yatakayowekwa mradi wa CNG katika maeneo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na kufanya Tathmini za Athari za Kimazingira katika mkuza wa miundombinu pamoja na ujenzi wa bomba kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach na kutoka Tegeta (Wazo Hills) hadi Bagamoyo ambapo shilingi bilioni 1.1 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.4.2 Ardhi na Maeneo ya Uwekezaji na Biashara

(a) Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuimarisha Mfuko wa Fidia; kuendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya Kurasimisha Makazi na Kuzuia Ujenzi wa Makazi holela katika mikoa yote na kuwapatia wananchi hatimiliki; kupanga, kupima na kutoa hati za kumiliki ardhi 150,000 na hatimiliki za kimila 420,000; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo yanayopitiwa na ukanda wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge), bomba la mafuta na bwawa la ufuaji umeme; na ufuatiliaji

wa utekelezaji wa mradi ambapo shilingi bilioni 7.0 fedha za ndani zimetengwa.

(b) Uboreshaji wa Milki za Ardhi

Shughuli zilizopangwa ni: kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo ya miji na vijiji kwa kutoa hati za hakimiliki, hati za hakimiliki za kimila na leseni za makazi; kupima mipaka ya vijiji na kutoa vyeti vya ardhi ya kijiji; kujenga ofisi za ardhi za mikoa na kufunga Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi; uboreshaji wa miundombinu ya upimaji na ramani; kuimarisha mifumo ya kitaasisi kwa kufanya mapitio ya Sera na Sheria za Ardhi pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi na kujenga jengo la kutunza kumbukumbu na nyaraka za ardhi; na kununua vifaa vya TEHAMA ambapo shilingi bilioni 2.3 fedha za ndani na shilingi bilioni 34.8 fedha za nje zimetengwa.

(c) Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuimarisha mipaka minne (4) ya kimataifa (Tanzania - Kenya; Tanzania - Zambia; Tanzania - Burundi; Tanzania - DRC/Burundi/ Zambia); kuandaa kanzidata ya taarifa ya mipaka ya kimataifa; kupima mipaka ya nchi katika maziwa; kukusanya na kutunza taarifa za upimaji majini; na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi ambapo shilingi bilioni 5.4 fedha za ndani zimetengwa.

(d) Uboreshaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa ramani za msingi kwa ajili ya kurahisisha upimaji ardhi nchini; kujenga vituo vya upimaji katika miji mikuu ya mikoa yote na kuongeza alama 300 za upimaji nchini ambazo zitawezesha upimaji na umilikishaji ardhi nchini; na kujenga kanzidata ya taarifa za kijiografia pamoja na mifumo ya kulinda na kusambaza taarifa kwa watumiaji ambapo shilingi milioni 500 fedha za ndani na bilioni 31.49 fedha za nje zimetengwa.

(e) Ujenzi na Ukarabati wa Majengo

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) ili kuwezesha udahili wa wanachuo 1,500 na kupunguza uhaba wa watendaji katika sekta ya Ardhi; ujenzi wa mabweni mawili (2) ya Chuo cha Ardhi Morogoro; na kukamilisha ukarabati wa majengo ya ofisi za Wizara pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi ambapo shilingi bilioni 1.1 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.4.3 Huduma za Fedha, Biashara na Masoko

(a) Huduma za Fedha

Shughuli zilizopangwa ni: kuimarisha huduma jumuishi za fedha; kuhakikisha ulinzi kwa mtumiaji wa huduma za fedha; kulinda uhimilivu wa mfumo wa fedha; kuimarisha sekta ya fedha ili iweze kugharamia mipango ya maendeleo ya muda mrefu; kuhamasisha utafiti ili kusaidia maendeleo ya sekta ya fedha; kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya fedha; na kuboresha sera, sheria na muundo wa usimamizi kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya fedha.

- (i) **Benki ya Maendeleo - TIB:** shughuli zilizopangwa ni kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 50. Kwa upande wa TIB Corporate Bank shughuli zilizopangwa ni kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 190.6.
- (ii) **Benki ya Maendeleo ya Kilimo - TADB:** shughuli zilizopangwa ni: kuongeza utoaji wa mikopo kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji, miradi ya mfumo wa nyuklasi (nucleus farms), miradi ya maghala, kuanzisha vituo vya huduma na zana za kilimo; kuendelea kutoa mikopo katika sekta ya kilimo kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo; na kuendelea kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo wakulima wadogo kupitia mafunzo ya usimamizi wa fedha, uundaji wa vikundi na vyama, utunzaji wa kumbukumbu na uandaaji wa miradi inayokidhi masharti ya mikopo kutoka katika benki na taasisi za fedha.
- (iii) **Soko la Mitaji na Dhamana:** shughuli zilizopangwa ni: kuendelea kuimarisha usimamizi wa masoko ya mitaji kwa kutumia mfumo unaozingatia vihatarishi; kuendelea na kusimamia biashara katika masoko ya mitaji kwa kuzingatia taratibu na miongozo; kuendelea kuongeza bidhaa katika masoko ya mitaji; kuendelea kuongeza idadi ya wataalamu wa masoko ya mitaji wanaokidhi viwango vya kimataifa; na kuendelea kutoa elimu kwa umma.
- (iv) **Huduma Ndogo za Fedha:** Shughuli zilizopangwa ni kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha katika mikoa yote nchini; kuanzisha jukwaa la wadau wa sekta ndogo ya fedha kwa ajili ya kujadili masuala yanayowahusu kwa lengo la kuratibu na uhamasishaji wa sekta ndogo ya fedha; na kuundwa kwa Kamati ya kushauri kuhusu masuala ya uratibu wa sekta ndogo ya fedha na utekelezaji wa sheria.

(b) Biashara

- (i) **Uboreshaji wa mazingira ya kufanyia biasharana na kuongeza fursa za biashara:** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na majadiliano ya biashara baina ya Tanzania na nchi zingine na kuingia nazo mikataba ya

ufunguaji wa masoko katika maeneo ya kipaumbele; majadiliano ya biashara kikanda (EAC, SADC, AfCFTA) na kimataifa (WTO); kufanya makongamano ya biashara na nchi nyingine ili kukutanisha wazalishaji wa nchi hizo na wazalishaji wa ndani; kuimarisha Dirisha la Taifa la Biashara (National Business Portal - NBP) kwa ajili ya kutoa leseni na taarifa za biashara kwa njia ya mtandao; kuimarisha mfumo wa usajili wa makampuni kupitia mtandao; kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini; na kuratibu mikutano ya majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania.

- (ii) **Kuboresha na kuongeza huduma zitolewazo na TanTrade:** shughuli zitakazotekelezwa ni kuongeza wigo wa huduma kwa kutangaza na kuendeleza fursa za mazao ya kimkakati kama vile bidhaa za viungo, chumvi, mwani, dagaa, utalii, sanaa na utamaduni; na kuboresha na kuimarisha Kituo cha Ushauri wa Biashara (Business Clinic).
 - (iii) **Kuimarisha Sekta Ndogo ya Biashara (SMEs):** shughuli zitakazotekelezwa ni kutolewa kwa mafunzo na ushauri wa kibiashara hususan katika usimamizi wa biashara na masoko; kurasimisha biashara zisizo rasmi nchini; na kuviwezesha vikundi vya uzalishaji kufikia masoko endelevu.
 - (iv) **Kuboresha na Kuimarisha Chuo cha Biashara (CBE):** shughuli zitakazotekelezwa ni kufanya upembuzi yakinifu wa kuboresha makazi ya watumishi katika eneo la Oysterbay Dar es Salaam; ukarabati wa mifumo ya TEHAMA; miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Kampasi ya Dar es Salaam na Dodoma; na kuanza ujenzi wa Kampasi ya Mbeya.
- (c) **Masoko**
- (i) **Kuwaunganisha Wazalishaji, Wasindikaji na Wafanyabiashara na Masoko ya Ndani na Nje ya Nchi:** shughuli zitakazotekelezwa ni kufanya uchambuzi wa taarifa za masoko na kubaini mahitaji ya soko la ndani na la nje ya nchi; kufanya utambuzi wa kampuni za ununuzi na uuzaji wa mazao na bidhaa za ndani na nje ya nchi na kuyaunganisha na wazalishaji na wasindikaji wa ndani; kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya kutengeneza vifungashio kwa wajasiriamali wadogo na wa kati; kushirikisha Balozi za Tanzania kutambua fursa za masoko mbalimbali ya mazao na bidhaa za kilimo na viwandani; kuhamasisha na kuwezesha kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania; kuhamasisha ujenzi wa masoko ya mipakani; kuwezesha Sekta Binafsi kushiriki Maonesho ya Kimataifa; na kuwezesha Sekta Binafsi kushiriki Maonesho ya Biashara ya Kikanda.
 - (ii) **Kupanua wigo wa Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala:** shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea kuhamasisha na kusimamia matumizi ya

mfumo wa stakabadhi za ghala kwenye mazao ya kimkakati na mazao mchanganyiko; kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya masoko ikiwa ni pamoja na maghala na vihenge vya kuhifadhia mazao; na kuendelea na usajili wa maghala na kutoa leseni kwa waendesha ghala katika mazao ya kimkakati na mazao mchanganyiko.

- (iii) **Kuimarisha masoko ya mipakani kwa ajili ya wajasiriamali wadogo waweze kuuza nje ya nchi:** shughuli zitakazotekelezwa ni kuimarisha na kuongeza wigo wa matumizi ya Soko la Bidhaa nchini; kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini; kushirikisha sekta binafsi kujenga miundombinu ya masoko na maghala bora ya kuhifadhia mazao mbalimbali hususan vijijini kwa kutoa elimu na kuondoa vikwazo vya utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani; na kuratibu ujenzi wa masoko ya kimkakati katika maeneo ya mipaka ya nchi ili kuwapa wakulima fursa ya kuuza mazao yao nje ya nchi.
- (iv) **Kufanya utafiti wa masoko ya ndani na nje ya nchi kwa bidhaa na mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini yanayozalishwa nchini:** shughuli zitakazotekelezwa ni kufanya tathmini ili kubaini mahitaji ya mazao ya kilimo katika viwanda vinavyoongeza thamani nchini na kufanya tafiti katika masoko ya nje ili kubaini fursa za kiushindani wa bidhaa na mazao katika masoko hayo. Tafiti hizo zitafanyika katika soko la Kenya, Sudani ya Kusini, Uholanzi, China, Vietnam, India, Afrika Kusini na Demokrasia ya Jamhuri ya Watu wa Kongo.
- (v) **Kuimarisha utoaji wa taarifa za Biashara na Intelijensia ya Masoko:** shughuli zitakazotekelezwa ni kuanzisha mifumo ya taarifa za biashara; kuanzisha vituo vya taarifa za masoko ili kutengamanisha biashara katika mikoa mbalimbali nchini kwa kuanzisha vituo katika mikoa ya Dodoma, Mbeya na Mwanza ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa za uzalishaji wa mazao na bidhaa, wanunuzi na bei katika ngazi ya wilaya, mkoa na Taifa; na kulipia vyanzo mbalimbali vya taarifa za biashara duniani.
- (vi) **Kuendeleza Miundombinu ya Biashara na Maonesho:** shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha mchakato wa umilikishwaji wa ardhi katika maeneo ya kimkakati ili kuwekeza miradi mbalimbali ya uendelezaji wa viwanja vya maonesho na miundombinu ya biashara katika Kanda za (Nyanda za Juu Kusini - Songwe; Kati - Dodoma, Kaskazini - Siha (Kilimanjaro), Ziwa Tanganyika - Kigoma, Kusini (Mtwara) na Zanzibar; na ujenzi wa mradi wa soko la nafaka wilayani Gairo - Morogoro ambapo shilingi bilioni 15.0 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.4.4 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

(a) Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Balozi

Shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi katika balozi za Moroni (Comoro), Kinshasa (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), Lilongwe (Malawi), Harare (Zimbabwe), Washington (Marekani), Kigali (Rwanda), Maputo (Msumbiji), Bujumbura (Burundi), Riyadh (Saudi Arabia), Abuja (Nigeria), Nairobi (Kenya), Muscat (Oman) ambapo shilingi bilioni 17.62 fedha za ndani zimetengwa.

(b) Upanuzi na Uboreshaji wa Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia

Shughuli zilizopangwa ni kuendelea na ujenzi wa vyumba tisa (9) vya madarasa; ofisi nne (4) za wakufunzi; vyumba vinne (4) vya kuhifadhia vifaa na vyumba vinne (4) vya mapokezi ambapo shilingi bilioni 2.38 fedha za ndani zimetengwa.

4.3.4.5 Ushiriki wa Sekta Binafsi, Mashirika na Taasisi za Umma

(a) Sekta Binafsi

Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- (i) Kuendelea na maboresho ya kimuundo na kiutendaji yatakayolenga kuimarisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika fursa zilizopo na za baadaye;
- (ii) Kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi ili kuongeza mchango wa sekta binafsi katika uchumi; na
- (iii) Kuongeza kasi ya uwekezaji katika miundombinu wezeshi hususan kwenye maeneo ya bandari, barabara, mawasiliano, reli na viwanja vya ndege, nishati na uendelezaji miji kwa kuwashirikisha wadau wa maendeleo.

(b) Mchango wa Serikali katika kuimarisha Ushiriki wa Sekta binafsi

Serikali imepanga kuimarisha na kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/21. Mikakati hiyo ni pamoja na:

- (i) Mkakati wa kuboresha mazingira wezeshi ya kikodi na yasio ya kikodi na vivutio vya kipekee yatakayowezesha sekta binafsi kuwekeza katika fursa zilizopo;
- (ii) Mkakati wa utekelezaji wa changamoto zinazoibuliwa wakati wa majadiliano kati ya serikali, sekta binafsi na wawekezaji ili kurahisisha uwekezaji nchini; na
- (iii) Mpango wa utekelezaji wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta

Binafsi (PPP) Sura 103 katika kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(c) Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

- (i) Miradi ya uzalishaji wa Dawa Muhimu na Vifaa Tiba katika mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya: shughuli zitakazotekelezwa ni kutafuta wabia wa ujenzi wa viwanda vitatu vya uzalishaji wa dawa muhimu na vifaa tiba na kuanza ujenzi;
- (ii) Mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza: shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea kutafuta mbia wa kutoa huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka kwa lengo la kuboresha huduma;
- (iii) Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Kituo cha Kibiashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere: shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea kutafuta mbia;
- (iv) Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara: shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na upembuzi yakinifu na kuutangaza mradi ili kupata mbia;
- (v) Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Mtwara - Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga ya *standard gauge*: shughuli itakayotekelezwa ni kukamilisha upembuzi yakinifu na kuendelea kukamilisha taratibu za kumpata mwekezaji kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli;
- (vi) Miradi ya Ujenzi wa Hosteli za wanafunzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara (Kampasi za Dar es Salaam na Dodoma), Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) na Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI): shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea kutangaza mradi ili kumpata mbia; na
- (vii) Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Tanga - Arusha - Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu ya *standard gauge*: shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na hatua za kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa nyaraka na kumtafuta Mbia.

SURA YA TANO

UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2020/21

5.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa kifupi vyanzo mbalimbali vya ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2020/21 kwa kuzingatia Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21. Vyanzo hivyo ni mapato ya ndani, mikopo na misaada, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na uwekezaji wa mashirika ya umma. Aidha, makadirio ya gharama za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 yamezingatia hali halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

5.1 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2020/21

5.1.1 Vyanzo vya Ndani

Katika mwaka 2020/21, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kuimarisha vyanzo vya mapato vilivyopo na kuibua vyanzo bunifu katika kuongeza mapato ili kugharamia miradi ya maendeleo. Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, Serikali itaendelea kutekeleza yafuatayo: kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi; kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari na kupanua wigo wa kodi kupitia ukusanyaji kutoka vyanzo na kanzidata mbalimbali za taarifa za walipakodi wapya; kuendelea kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA; kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali; kutekeleza Mfumo wa Dirisha Moja la Kielektroniki la Tanzania (TeSWs) ili kurahisisha upitishaji wa mizigo katika vituo vya mipaka pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini; kuharakisha usambazaji wa Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG); kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali; na kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa michango stahiki ya Mashirika kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali inawasilishwa kwa wakati. Aidha, katika mikopo ya ndani, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zilizopo za uwekezaji pamoja na uendeshaji wa minada ya dhamana za Serikali ili kupanua wigo wa wawekezaji.

5.1.2 Vyanzo vya Nje

Serikali itaendelea: kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano na Washirika wa

Maendeleo (Development Cooperation Framework - DCF) pamoja na Mpango Kazi wake; kuimarisha usimamizi wa fedha za Washirika wa Maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja katika miradi ya maendeleo pamoja na kusimamia uwasilishwaji wa taarifa za fedha hizo kwa wakati kupitia Mfumo wa D-fund; kuboresha majadiliano na Washirika wa Maendeleo ili kupata misaada na mikopo nafuu kwa wakati; na kukopa mokopo yenye masharti ya kibiashara kwa kuzingatia viwango vya uhimilivu wa deni na kuelekeza fedha hizo katika miradi itakayokuwa na matokeo makubwa kiuchumi na kijamii.

5.1.3 Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje ya Nchi (FDI)

Kwa kuzingatia msukumo uliowekwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21, Serikali itaendelea kuweka mazingira bora na wezeshi ili kuvutia uwekezaji ambapo msisitizo umelekezwa katika viwanda vya kuongeza thamani vya malighafi zinazopatikana nchini, uunganishaji wa magari na mitambo, uzalishaji wa mafuta ya kula, dawa na vifaa tiba. Vile vile, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya taratibu na sheria, kutangaza fursa za uwekezaji wa moja kwa moja na kuandaa miongozo kwa ajili ya vivutio vya wawekezaji katika miradi ya maendeleo.

5.1.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Serikali itaendelea na jitihada za kuibua, kuchambua na kutekeleza miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) kwa kuzingatia Sheria ya PPP Sura ya 103 (R.E 2018). Katika kuimarisha Mfuko wa Uwezeshaji Miradi ya Ubia, Serikali itaendelea na utaratibu wa uanzishaji wa Kituo cha Ubia (*PPP centre*) ili kusimamia mfuko huo ambao utagharamia maandalizi ya miradi na kutoa mafunzo kwa Wizara, Idara na Taasisi za Umma ili kuziwezesha Mamlaka za Serikali kuibua na kutekeleza miradi ya Ubia kwa ufanisi.

5.1.5 Mifuko ya Kimataifa ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira

Kwa upande wa fedha za mifuko mbalimbali ya kimataifa inayohusika na hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, mwaka 2020/21 Serikali inategemea kupata takribani Shilingi bilioni 56.0 kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Environmental Facility - GEF*) ambao upo katika awamu ya saba (7) (*GEF Seventh Replenishment Cycle*) ili kugharamia miradi mbalimbali ya kuhifadhi mazingira na maendeleo endelevu. Ili kuwezesha upatikanaji wa fedha hizi, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuandaa miradi pamoja na kufanya majadiliano na Washirika wa Maendeleo ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kutoka mifuko mbalimbali inayohusiana na hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Serikali imewasilisha miradi kwa ajili ya kupata ufadhili kwenye mfuko wa

Global Environmental Facility (GEF) kwa kipindi cha miaka mitano (2019 – 2023) ambapo Tanzania inatarajia kupata takriban dola za kimarekani milioni 108.3 kwenye programu hiyo.

5.2 Gharama za Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2020/21

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2020/21 utaendelea kujikita katika maeneo ya kipaumbele makuu manne yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 ambayo ni: Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Kufungamanisha Uchumi na Maendeleo ya Watu; Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji; na Kuboresha Utekelezaji wa Mpango. Hivyo ni azma ya Serikali ya awamu ya Tano kuendelea kutekeleza maeneo haya ya kipaumbele ili kufikia malengo ya Mpango.

Katika mwaka 2020/21, matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 12,899.4, sawa na asilimia 37.0 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10,163.4 zinatarajiwa kutoka vyanzo vya ndani sawa na asilimia 82.3 ya bajeti ya maendeleo na shilingi bilioni 2,736.0 fedha za nje sawa na asilimia 17.7 ya bajeti ya maendeleo.

Sehemu kubwa ya bajeti itaelekezwa katika miradi ya kimkakati inayoendelea ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Reli Mpya ya Kati ya Standard Gauge (SGR); ujenzi wa Mtambo wa Kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere; kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); uendeshaji wa jengo la III la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; usambazaji wa umeme vijijini; miundombinu ya umwagiliaji; upanuzi wa Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga; na ujenzi wa Vivuko vipya, Meli na Magati kwenye Maziwa Makuu. Matumizi mengine ni pamoja na: utekelezaji wa miradi yenye kuongeza mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; utoaji wa elimumsingi bila ada; ujenzi wa barabara za juu Ubungu; utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; utoaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi; na upatikanaji wa huduma ya maji.

Miradi mingine ya maendeleo hususan ya viwanda na uwekezaji mkubwa itaendelea kutekelezwa kupitia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka sekta binafsi na kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

SURA YA SITA

UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

6.1 Utangulizi

Mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo umelezwa kwa kina kwenye Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021. Mfumo huo, pamoja na mambo mengine, umeainisha mgawanyo wa majukumu katika ufuatiliaji na tathmini ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya kila mwaka. Vile vile, utaratibu wa uandaaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango umeainishwa kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021, pamoja na Sheria ya Bajeti Sura 439 ya mwaka 2015. Sura hii, inaainisha malengo, mfumo, mkakati, utoaji taarifa na mgawanyo wa majukumu katika ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021 kama ifuatavyo:-

6.2 Malengo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma zinatakiwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango ili kufikia malengo yafuatayo:-

- (a) Kupima mwelekeo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na malengo yake; malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21 na Dira ya Taifa 2025;
- (b) Kubainisha mafanikio, ufanisi, changamoto na dosari katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti;
- (c) Kubainisha hatua za kuchukua ili kurekebisha dosari zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti;
- (d) Kubainisha hatua za kuchukua ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti;
- (e) Kubainisha vihatarishi katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti;
- (f) Kubainisha masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu; na
- (g) Kujiridhisha kama fedha zilizotolewa na Serikali zimeelekezwa kwenye maeneo ya kimkakati, miradi au kazi zilizokusudiwa.

6.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa 2020/21

Katika mwaka 2020/21, Serikali itaendelea kuzingatia miongozo mbalimbali ya ufuatiliaji na tathmini ya Mipango na Bajeti, hususan Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21; Mwongozo wa Mpango na Bajeti; Sheria ya Ununuzi wa Umma; Sheria ya Bajeti; Sheria ya Fedha za Umma; na Sheria ya Ukaguzi wa Umma. Aidha, kila Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoza, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma zinalazimika kuandaa Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini ya Mpango, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kila robo mwaka, kuainisha masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa ufuatiliaji na tathmini, kuandaa na kutenga rasilimali fedha, watu na vifaa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini na kuwajengea watumishi uwezo wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango. Vile vile, kila taasisi itazingatia mgawanyo wa majukumu katika uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango. Kila taasisi inatakiwa kuwasilisha Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini, pamoja na taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya Mpango za kila robo, nusu na mwaka Wizara ya Fedha na Mipango kwa uchambuzi, majumuisho, kumbukumbu na rejea.

6.4 Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango

Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango umejielekeza katika kuweka utaratibu wa wazi, wianishi, jumuishi na shirikishi ili kurahisisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mipango mbalimbali ya Maendeleo ya Taifa. Vile vile, Mpango unalenga kuimarisha usimamizi na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti. Mbinu zitakazotumika katika ufuatiliaji na tathmini ya Mpango ni pamoja na kudhibiti, kukagua, kutembelea maeneo ya miradi na kufanya mapitio na mahojiano na wadau juu ya mwelekeo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021. Wizara ya Fedha na Mipango itashirikiana na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali zinazotekeleza miradi ya maendeleo kuratibu na kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya Mpango.

Katika kufanikisha utekelezaji wa Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021, Serikali inazielekeza Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali zinazotekeleza miradi ya maendeleo kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- (a) Kuimarisha mifumo ya ndani ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo;
- (b) Kutafsiri malengo na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21 katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/2021;

- (c) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo kila robo mwaka;
- (d) Kuwajengea watumishi uwezo katika tasnia ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na
- (e) Kuandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na programu, na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango.

6.5 Utoaji Taarifa

Taarifa za utekelezaji wa mpango na miradi ya maendeleo zitaandaliwa na kusambazwa kwa kuzingatia Mkakati wa Mawasiliano wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021. Wadau na wananchi wataelimishwa kuhusu wajibu na ushiriki wao katika kushiriki katika hatua mbalimbali za uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Aidha, taarifa zitabainisha mafanikio, fursa, dosari na changamoto katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa Mpango, ikiwa ni pamoja na hatua za kukabiliana na dosari na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Serikali itatumia njia mbalimbali katika kuhakikisha kuwa, taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinawafikia wananchi kwa wakati. Njia hizo ni pamoja na mikutano ya hadhara, maonesho ya Kitaifa na Kimataifa (Saba Saba na Nane Nane), tovuti za Serikali, magazeti, vipeperushi, vyombo vya habari (televisheni na radio) pamoja na vikao vya wadau. Vile vile, wananchi watapewa fursa ya kutoa maoni na mapendekezo yao juu ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali, hususan katika mikutano ya hadhara na mahojiano ya ana kwa ana.

6.6 Mgawanyo wa Majukumu

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi nyingine za Umma, Sekta Binafsi na Wananchi ni wadau muhimu katika ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Mgawanyo wa kazi ya ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango ni kama ifuatavyo:-

6.6.1 Wizara ya Fedha na Mipango

Wizara ya Fedha na Mipango imekasimiwa jukumu la kuratibu kazi ya utafuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kielelezo, kimkakati na inayotekelezwa na Sekta Binafsi kwa kushirikiana na Wizara, Idara, Taasisi na Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali. Aidha, Wizara itachambua taarifa za ufuatiliaji na tathmini, na kuainisha maeneo ya kuboresha utekelezaji miradi ya kitaifa ya kimkakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Vile vile, Wizara itawajibika kuandaa na kutoa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mpango wa

Maendeleo kwa miradi yote inayotekelezwa na Wizara, Idara, Taasisi, Wakala za Serikali na Sekta Binafsi.

6.6.2 Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali

Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali zitawajibika kuandaa Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini, taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kila robo mwaka, nusu na mwaka na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Vitengo vya ufuatiliaji na tathmini vinasisitizwa kuwa na Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ili kuendana na matakwa ya Mpango Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021. Vile vile, Wizara, Idara na Wakala za Serikali zinasisitizwa kuviwezesha na kuvijengea uwezo Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini ili kutekeleza majukumu ya ufuatiliaji na tathmini kwa ufanisi. Aidha, Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma umeainisha masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa ufuatiliaji na tathmini, ambayo ni upimaji wa malengo na matumizi ya rasilimali fedha, kuainisha changamoto, vihatarishi na ushirikishwaji wa wadau.

6.6.3 Ofisi ya Rais – TAMISEMI

Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu na kutoa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinawajibika kuandaa Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini, ikiwa ni pamoja na kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo, nusu na mwaka Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itachambua na kuandaa taarifa jumuiishi na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua stahiki. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itatumia fursa ya kuandaa taarifa jumuiishi kutoa maoni, mapendekezo na ushauri kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

6.6.4 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itaendelea kuhakikisha kuwa Vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti vina rasilimali watu ya kutosha, yenye weledi, uadilifu na uwezo wa kutekeleza majukumu ya ufuatiliaji na tathmini kwa ufanisi.

6.6.5 Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Ofisi ya Taifa ya Takwimu itakuwa na jukumu la kuandaa miongozo mbalimbali ya ukusanyaji, uchambuzi, uchakataji na uandaaji wa taarifa rasmi za ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma, pamoja na Sekta Binafsi zitatakiwa kuzingatia miongozo hiyo wakati wa kukusanya, kuchambua, kuandaa na kutoa taarifa za kitakwimu za mwenendo na matokeo ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Vile vile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itakuwa na jukumu la kuwajengea wadau, pale inapohitajika, uwezo wa kukusanya, kuchambua, kuchakata, kuandaa na kutoa taarifa za kitakwimu za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali.

6.6.6 Sekta binafsi

Sekta Binafsi itawajibika kutoa taarifa muhimu zitakazohitajika katika kufanya mapitio ya mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi ili kuboresha mazingira ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Aidha, kwa kuzingatia Mwongozo wa Mawasiliano baina ya Sekta Binafsi na Umma, Sekta Binafsi itawajibika kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za Uwekezaji wa Sekta hiyo. Taarifa hizo zitaainisha mwenendo wa uwekezaji wa Sekta Binafsi ikilinganishwa na malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021; mafanikio, fursa, changamoto na dosari zilizopo katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021. Vile vile, Sekta Binafsi itatakiwa kutoa maoni na mapendekezo ya hatua za haraka za kuchukua ili kukabiliana na changamoto na dosari zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango wa maendeleo.

SURA YA SABA

VIHATARISHI KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO

7.1 Utangulizi

Katika utekelezaji wa miradi iliyoanishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21, vipo vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na kusababisha athari zitakazopekelea utekelezaji wa miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati. Sura hii inaainisha vihatarishi, madhara yatokanayo na vihatarishi hivyo pamoja na kupendekeza mikakati ya kukabiliana na vihatarishi hivyo. Vihatarishi hivyo ni pamoja na: uharibifu wa mazingira sanjari na mabadiliko ya tabianchi; mtikisiko wa uchumi wa kikanda na dunia; majanga asilia; migogoro ya ndani na hali ya siasa isiyo imara katika maeneo mbalimbali ikiwemo nchi jirani, kikanda na katika mataifa makubwa duniani; uhalifu wa kimtandao; upatikanaji wa rasilimali fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo; mchakato mrefu wa kubadili umiliki wa ardhi katika maeneo ya miradi na migogoro ya ardhi, ushiriki hafifu wa sekta binafsi; rushwa; na mabadiliko ya teknolojia.

Vihatarishi hivi vimegawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni vihatarishi vya ndani na vya nje. Vihatarishi vya ndani ni vile ambavyo udhibiti wake upo ndani ya uwezo wa Serikali na vihatarishi vya nje ni vile ambavyo udhibiti wake upo nje ya uwezo wa Serikali.

7.2 Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo

Jedwali 7.1: Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo

NA.	KIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA NA KIHATARISHI
1.	Upatikanaji wa rasilimali fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo	<ul style="list-style-type: none">• Ucheleweshaji wa utekelezaji wa mikataba na hivyo kuongeza gharama kwa Serikali kutokana na kuongezeka kwa malipo ya riba; na	<ul style="list-style-type: none">• Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kuharakisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ili kuongeza wigo wa mapato;• Kulinda (ringfence) fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili kugharamia shughuli zilizopangwa kwa

NA.	KIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA NA KIHATARISHI
		<ul style="list-style-type: none"> • Kuchelewa kukamilika kwa miradi. 	<p>wakati;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha sekta ya fedha ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya kibiashara kutoka katika taasisi za fedha zilizopo nchini; na • Kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (Development Cooperation Framework - DCF) na mpango wa utekelezaji.
2.	Ushiriki mdogo wa Sekta Binafsi katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango	<ul style="list-style-type: none"> • Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi inayokusudiwa kutekelezwa kwa mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi; • Kupungua kwa kasi ya ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji; • Kuzorota kwa utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kutokana na kutegemea vyanzo vya mapato ya Serikali katika utekelezaji wa miradi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuhamasisha na kuimarisha mazingira wezeshi ya maandalizi ya miradi kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP); • Kuboresha huduma za kifedha ili kuwezesha sekta binafsi kukopa zaidi kwa ajili ya uwekezaji; • Kuendelea kuvutia uwekezaji kwa kufanya majadiliano ya mara kwa mara na Sekta Binafsi ili kutatua changamoto za wawekezaji; na • Kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya biashara ili kupunguza gharama za uwekezaji.
3.	Rushwa	<ul style="list-style-type: none"> • Miradi kutekelezwa chini 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wanaobainika

NA.	KIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA NA KIHATARISHI
		<p>ya viwango;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Upotevu wa fedha za umma; na • Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi. 	<p>kuhusika na vitendo vya rushwa;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama; • Kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini; na • Kuimarisha mfumo wa utoaji motisha kwa watoaji taarifa zinazohusiana na rushwa.
4.	Mchakato mrefu wa kupata na kubadili umiliki wa ardhi katika maeneo ya miradi na migogoro ya ardhi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchelewesha utekelezaji wa miradi kwa ufanisi hususan wakati wa ulipaji fidia; • Ukosefu wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji; na • Kuharibiwa kwa miundombinu ya miradi. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa mipango miji inayoendana na kasi ya ukuaji wa miji na shughuli za maendeleo ili kurahisisha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii; • Kutenga maeneo maalum ya uwekezaji yenye hati miliki na miundombinu wezeshi; na • Kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika maeneo ya miradi ili wafahamu umuhimu wa miradi hiyo.
5.	Mifumo ya ukusanyaji wa Takwimu na Utoaji taarifa	<ul style="list-style-type: none"> • Mifumo kutoa taarifa zinazokinzana hivyo kupelekea ugawaji wa rasilimali usio sahihi; na • Kukosekana kwa thamani halisi ya fedha kwenye miradi ya maendeleo. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuoanisha mifumo ya utoaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini za miradi ili iweze kutoa taarifa sahihi na zinazowiana; • Uanzishaji wa kanzidata ya miradi ya maendeleo; na • Kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini kwa kutenga rasilimali za kutosha.
6.	Uharibifu wa	<ul style="list-style-type: none"> • Kupungua kwa 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuhamasisha matumizi bora ya

NA.	KIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA NA KIHATARISHI
	Mazingira	<p>uzalishaji hususan katika sekta ya kilimo;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Magonjwa ya milipuko ambayo yanaweza kusababisha kuongeza gharama za utoaji huduma za afya kwa Serikali; • Kutoweka kwa bioanuai; na • Uharibifu wa miundombinu ya miradi. 	<p>ardhi ikiwemo kilimo rafiki kwa mazingira;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuhamasisha shughuli mbadala za uzalishaji kipato na matumizi ya nishati mbadala; • Kuhamasisha matumizi sahihi ya teknolojia katika kutekeleza shughuli za maendeleo ili kupunguza uharibifu wa mazingira; • Kujenga uelewa wa wananchi juu ya utunzaji wa mazingira; • Kutunza na kurejesha uoto wa asili; na • Kuimarisha kamati za usimamizi wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya maji na misitu.
7.	Uhalifu wa mtandaoni	<ul style="list-style-type: none"> • Uwezekano wa fedha za Serikali kuibiwa na wadukuaji hivyo kupelekea miradi ya maendeleo kushindwa kutekelezwa kwa wakati; • Uwezekano wa taarifa za mipango/fedha za Serikali kudukuliwa na kupotoshwa na watu wasiohusika; na • Mifumo ya utoaji 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mifumo ya taarifa ya kieletroniki ya Serikali; • Kuimarisha maeneo ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali za Serikali (Data recovery sites); • Kuimarisha utekelezaji na usimamizi wa sera ya udhibiti wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha za umma; • Kuendelea kuhakikisha kuwa mawasilisho ya taarifa za serikali kwa njia za kielektroniki yanafanyika kwenye mifumo rasmi inayosimamiwa na Serikali; na • Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam wa mifumo ya

NA.	KIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA NA KIHATARISHI
		wa taarifa kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.	TEHAMA wa Serikali/taasisi zinazosimamia mifumo ya TEHAMA namna ya kukabiliana na uhalifu wa kimtandao.

7.3 Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana navyo

Jedwali 7.2: Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana navyo

NA.	VIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA NA KIHATARISHI
1.	Mtikisiko wa kiuchumi wa kikanda na dunia	<ul style="list-style-type: none"> • Kupungua kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi; • Kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni; • Kupungua kwa mikopo ya nje ya kibiashara inayotarajiwa kutekeleza miradi ya maendeleo; • Kupungua kwa fedha za kutekeleza miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo; na • Kupungua kwa uwekezaji. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na jitihada za kujenga viwanda vya kuongeza thamani na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ili kuimarisha akiba ya fedha za kigeni; • Kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na maendeleo ya kiuchumi ya kikanda; • Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuharakisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ili kupunguza utegemezi; • Kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kuhimili ushindani; • Kuimarisha usimamizi wa rasilimali zinazopatikana nchini ili ziweze kuchangia katika

NA.	VIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA KIHATARISHI
			<p>mapato ya Serikali na kukidhi mahitaji; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kuimarisha sekta ya fedha ya ndani ili iweze kuchangia katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo.
2.	Majanga asilia na Mabadiliko ya tabianchi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuathirika kwa rasilimali asili na ikolojia na kupunguza uzalishaji; • Kuharibika kwa miundombinu ya uzalishaji na usafirishaji; • Kuathirika kwa nyumba, makazi ya watu; • Kuchelewa kukamilika kwa miradi kutokana na kubadilika kwa ratiba za utekelezaji; • Kupungua kwa uwekezaji; na • Kupungua kwa nguvu kazi; na • Kupungua kwa uzalishaji kutokana na mabadiliko ya tabianchi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha mifumo ya kukabiliana na majanga; • Kuimarisha taasisi za kitaalamu zinazohusika na utabiri wa hali ya hewa ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa za majanga tarajiwa kwa wakati; • Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa ajili ya utoaji tahadhari ya mapema kuhusu uwezekano wa kutokea kwa majanga ya asili; • Kuwekeza kwenye teknolojia za kisasa za kupambana na majanga asilia; • Kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya kukabiliana na majanga asilia; na • Kuimarisha Taasisi za usimamizi wa majanga (disaster preparedness). • Kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao

NA.	VIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA KIHATARISHI
			<p>katika maeneo yanayokabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi - Climate Smart Agriculture; • kuhamasisha matumizi sahihi ya teknolojia katika kutekeleza shughuli za maendeleo ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi; • Kutunza na kurejesha uoto wa asili; • Kuendelea kuwahamisha wananchi wanaoishi katika maeneo hatarishi kama vile kwenye mabonde; na • Kutekeleza na kuendelea kuridhia itifaki za kimataifa kuhusu utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.
3.	Migogoro na hali ya Siasa isiyo imara katika maeneo mbalimbali ikiwemo nchi jirani, kikanda na kimataifa;	<ul style="list-style-type: none"> • Kukosekana kwa masoko nje ya nchi kwa ajili kuuza bidhaa zinazozalishwa nchini; • Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi hususan inayotumia vifaa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi; 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano ili kuzuia matukio yanayoweza kuhatarisha amani nchini, kikanda na kimataifa; • Kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi jirani

NA.	VIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA KIHATARISHI
		<ul style="list-style-type: none"> • Kupungua kwa uwekezaji (FDIs); • Kupungua kwa mikopo na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; na • Kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu katika soko la dunia kama mafuta, mashine na mitambo. 	<p>na kikanda ili kukuza masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa viwandani;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuvutia uwekezaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa kutumia teknolojia na malighafi za ndani ili kupunguza uagizaji wa bidhaa nje ya nchi; na • Kujenga uwezo wa nchi kushiriki katika majadiliano ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kupunguza athari za migogoro itokanayo na kuyumba kwa ushirikiano kati ya nchi na nchi.
4.	Mabadiliko ya Kiteknolojia	<ul style="list-style-type: none"> • Kuwa na uwezo mdogo wa kiushindani katika soko la kikanda na kimataifa; • Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi kutokana na uhitaji wa zana zinazotumia teknolojia mpya; na • Mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi isiyoendana na mabadiliko ya kiteknolojia. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga mazingira wezeshi ya kukabiliana na mabadiliko ya kiteknolojia; na • Kuendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza ujuzi, uhawilishaji wa teknolojia na kuhamasisha ubunifu wa teknolojia kwa wataalam wa ndani.; na • Kuboresha mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi ili iendane na mabadiliko ya

NA.	VIHATARISHI	MADHARA YATOKANAYO NA KIHATARISHI	MIKAKATI YA KUKABILIANA KIHATARISHI
			kiteknolojia.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Miradi ya Kielelezo		
Ujenzi wa Reli ya Kati kwa <i>Standard Gauge</i>	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa reli kutoka Dar es salaam - Morogoro (km 300); • Ujenzi wa reli kutoka Morogoro - Makutupora (km 422); na • Ujenzi wa reli ya Isaka - Rusumo (km 371). 	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 76.63; • kipande cha Morogoro - Makutupora (km 422), utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 28; na • Jitihada za utafutaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora - Tabora (km 294), Tabora - Isaka (km 133), Isaka - Mwanza (km 249), Isaka - Rusumo (km 371), Tabora - Kigoma (km 411), Keza - Ruvubu (km 36), Kaliua - Mpanda hadi Karema (km 321) zinaendelea.
Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania	<ul style="list-style-type: none"> • Ununuzi wa ndege moja aina ya Boeing 787 - 8 Dreamliner; • Ununuzi wa ndege moja mpya aina ya Bombadier Dash 8 Q400; na • Kulipa bima, gharama za uendeshaji wa ndege (start up cost), mafunzo ya marubani, wahandisi na wahudumu pamoja na ulipaji wa madeni. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kupokelewa kwa ndege mbili ambazo ni Boeing 787-8 Dreamliner na Bombadier Dash 8 Q400; • Kusainiwa kwa mikataba na kufanyika kwa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege mpya tatu ambapo mbili (2) ni aina ya Airbus A220-300 na moja (1) ni aina ya De Havilland Dash 8 - 400; • Serikali imegharamia mafunzo ya marubani (78), wahandisi (120) na wahudumu (125); • kulipa bima za ndege na gharama za awali za kuendesha ndege tatu zilizopokelewa; • ukarabati wa karakana ya ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) hususan katika mfumo wa umeme, mfumo wa kupambana na majanga ya moto na ufungaji wa jenereta na kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Karakana ya Matengenezo ya Ndege; na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> • Shirika limeongeza idadi ya vituo vya safari za ndani kufikia 11 na nje kufikia vituo saba ambavyo ni Hahaya (Comoro), Entebbe (Uganda), Bujumbura (Burundi), Mumbai (India), Lusaka (Zambia) Johannesburg (Afrika Kusini) na Harare (Zimbabwe).
Mradi wa Kufua Umeme wa Maji Bonde la Mto Rufiji - MW 2,115	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa bwawa, kuanza ujenzi wa njia za kupitisha maji; na • Kukamilisha ujenzi wa njia ya pili ya umeme msongo wa kV 33 kutoka Gongo la Mboto 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa bwawa (main dam); • Kukamilika kwa asilimia 24.74 kwa ujenzi wa handaki la kuchepusha maji (diversion tunnel); • Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu wezeshi ikijumuisha: njia ya kusafirisha umeme; barabara kwa kiwango cha changarawe; mifumo ya maji; mawasiliano ya simu; na nyumba za kuishi Mkandarasi; • Kazi zingine zinazoendelea ni maandalizi ya mgodi wa kufua umeme, njia za maji kwenda kwenye mitambo na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya mradi.
Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma Mradi wa Vanadium, Titanium na chuma Liganga	<ul style="list-style-type: none"> • kulipia leseni za uchimbaji wa makaa ya mawe; • kulipa fidia ya mali za wananchi watakaopisha eneo la mradi baada ya tathmini kukamilika; • kuratibu na kufuatilia kazi za mradi; • kusimamia ujenzi wa mgodi wa makaa ya mawe na msongo wa umeme wa Mchuchuma – Liganga; • kulipia leseni za mashapo; • kusimamia ujenzi wa mgodi wa chuma na kiwanda cha chuma; na • kusimamia ujenzi wa miundombinu 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa uhakiki wa mali za wananchi watakaopisha ujenzi wa miradi hiyo ambapo kiasi cha shilingi bilioni 11.037 kinatarajiwa kulipwa kama fidia kwa wananchi 1,145 kwa maeneo yote ya miradi. • upitiaji mikataba kati ya NDC na mwekezaji unaendelea; na • kulipwa kwa ada za leseni za kuchimba madini (<i>Primary Mining Licence – PML</i>) katika maeneo yaliyo chini ya NDC katika eneo la mradi.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	wezeshi.	
Mradi wa kuendeleza kituo cha biashara na usafirishaji Kurasini	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha malipo ya fidia kwa wakazi watatu (3) ambao nyumba zao hazikuthaminiwa awali • Kuwezesha utekelezaji wa mradi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa uthamini wa nyumba; • Kukamilika kwa upimaji wa eneo; • Kuendelea na taratibu za kupata hati miliki ambazo zipo katika hatua za mwisho.
Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi	<ul style="list-style-type: none"> • Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo: Kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu wezeshi katika eneo la kituo cha Teknolojia Bagamoyo; kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya ndani kwa eneo lililolipwa fidia pamoja na kukamilisha majadiliano na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa Bagamoyo; kukamilisha hatua zote za utwaaji wa Ardhi na kufanya upimaji wa eneo ili kupata hati miliki ya eneo lililokwisha lipiwa fidia. • Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini: Kukamilisha hatua zote za utwaaji ardhi ili kupata hati; kufanya upembuzi yakinifu; kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi (masterplan) kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya ndani; kuweka uzio eneo la mradi; kununua gari la mradi 	<p>Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo: Kufanyika kwa uwekezaji wa viwanda 11 (<i>Seif For Tobacco Trade Limited, Fujian Hexingwang Industry Company Limited, Siparcoci International Limited, Hua Teng Metalurgical Company Limited, Wegmar Paking Limited, Jambo Food Products Limited, Phiss Tannery Limited, Tube Limited, Ramky Tanzania Limited, Tanfroz Limited, na Africa Dragon Enterprises Limited</i>). Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) ambavyo ni <i>Africa Dragon Enterprises Limited na Phiss Tannery Limited</i> vimeanza uzalishaji na kuzalisha ajira za moja kwa moja 120 na ujenzi wa viwanda tisa (9) unaendelea. Aidha, andiko la uendelezaji na makisio ya gharama za kuweka miundombinu wezeshi katika eneo lililolipiwa fidia limekamilika.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Eneo Maalum la Uwekezaji Kigoma: kukamilika kwa upembuzi yakinifu na Mpango Kabambe wa uendelezaji wa eneo (<i>Master Plan</i>) na ugawaji wa viwanja kwa ajili ya kupewa wawekezaji; kuendeleza miundombinu kwa kufungua barabara zenye jumla ya km 28.46 na kuweka alama za mipaka 106; kupatikana kwa wawekezaji watatu ambao watakofanya kazi zifuatazo: ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa jua (<i>Next Gen Solowazi Limited</i>), ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki (<i>Third Man Limited</i>) na ujenzi wa kiwanda cha kuchakata zao la michikichi na ghala (<i>SGC Investment Limited</i>).

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	pamoja na kulipia gharama za mashauri elekezi.	<ul style="list-style-type: none"> • Eneo Maalum la Uwekezaji la Ukanda Huru wa Bandari ya Mtwara: kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara za ndani ya eneo la mradi yenye urefu wa kilomita tatu.
Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia - Lindi	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha majadiliano ya mradi na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; • Kuendelea kwa tafiti za namna ya kuzalisha na kusafirisha gesi kutoka bahari kuu hadi eneo la mradi; na • Kuendelea na majadiliano ya Mikataba Hodhi (Host Government Agreement - HGA) baina ya Serikali na Kampuni za utafutaji na uendelezaji zitakazotekeleza mradi.
Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha majadiliano ya mkataba wa Ubia (SHA) kati ya nchi washirika na kampuni zilizowekeza katika mradi; na • Kulipa fidia wakazi watakaohamishwa kupisha eneo la mkuza litakapopita bomba 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na • Kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa maeneo ya pembezoni mwa eneo la mradi.
Miradi ya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Masingi wa Uchumi wa Viwanda		
Uzalishaji Viwandani		
Kuunganisha Matrikta, TAMCO, Kibaha	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea na maboresho ya kiwanda; • ujenzi wa kiwanda kipya cha kuunganisha matrikta; • kusimamia shughuli za kufanya matengenezo ya matrikta nchini; na • kusimamia na kulipia gharama za uingizaji matrikta na zana zake bandarini na kuyapeleka eneo la mradi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa Kiwanda kipya cha kuunganisha Matrikta ambapo ujenzi wa jengo la kiwanda umekamilika; • matrikta 822 kati ya 2,400 aina ya URSUS yameingizwa nchini kutoka Poland yakiwa katika vipande (semi <i>knocked down</i>); na • matrikta 717 yameuzwa ambapo matrikta 676 yameuzwa kwa mkopo na 41 kwa fedha taslimu.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Kuendeleza Kongane ya Viwanda TAMCO – Kibaha	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi katika eneo la mradi; na • kuendelea kutangaza eneo kwa wawekezaji. 	<ul style="list-style-type: none"> • kukamilika kwa asilimia 98 ya ujenzi wa barabara ya urefu mita 580 kwa kiwango cha lami; • kupatikana kwa mtaalam mwelekezi kwa ajili ya usanifu wa ujenzi wa kituo cha umeme; na • kuendelea na maandalizi ya Mpango Kabambe wa kuendelea eneo la ekari 201.6 ili kuvutia uwekezaji
Mradi wa Magadi Soda - Bonde la Engaruka	<ul style="list-style-type: none"> • kufanya upembuzi yakinifu wa barabara za ndani na za kufikia eneo la mradi; • kujenga miundombinu wezeshi katika eneo la mradi; • kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii; • kufanya utafiti wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya mradi wa wananchi; na • kulipia leseni za uchimbaji 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa uthaminishaji wa ardhi na mali za wananchi pamoja na uhakiki uthaminishaji; na • kuendelea kufanya <i>Techno-Economic Study</i> inayojumuisha Upembuzi Yakinifu katika eneo la Magadi Soda, Tathmini ya Athari za Kimazingira – EIA na Utafiti wa masoko ya Magadi Soda na kuendelea kutangaza mradi ili kuvutia wawekezaji.
Utafiti wa Teknolojia na Bidhaa za Viwandani		
Kituo cha zana za Kilimo na Ufundi Vijijini - CAMARTEC	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea kufanya utafiti wa mahitaji ya teknolojia za kilimo na teknolojia zinazohitajika vijijini na kujua hali ya matumizi ya teknolojia hizo katika maeneo mingine ambayo utafiti huo bado haujafanyika; • kufanya utafiti na kuunda teknolojia zinazolenga kuongeza tija katika shughuli za kilimo vijijini; • kuunda na kuzalisha sampuli kifani za 	<ul style="list-style-type: none"> • Kubuni, kutengeneza na kufanyia majaribio ya awali mashine za kubangua korosho inayoendeshwa kwa kutumia miguu ambapo jumla ya mashine 36 zimetengenezwa; • Kubuni na kutengeneza mashine ya kubangua na kutenganisha mbegu za chikichi; • Kufanya utafiti wa awali uliosaidia kutengeneza mashine ya kuvunja na kutenganisha maganda ya chikichi inayoendeshwa kwa mkono; na • kubuni njia rahisi ya kuzifanya mbegu za pamba zenye manyoya kuweza kutumika kwa urahisi katika Kipandio cha

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>teknolojia za kilimo na teknolojia nyingine zinazotumika vijijini;</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuhamasisha utengenezaji wa mashine za kilimo, zana za kilimo na teknolojia nyingine za ufundi vijijini; na • kuendelea kuimarisha miundombinu ya kituo ili kuweza kufanya utafiti kwa ufanisi zaidi 	<p>ng'ombe bila kukwama</p>
<p>Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO</p>	<ul style="list-style-type: none"> • kuanzisha na kukidhi vigezo vya kupata ithibati kwa maabara ya mafuta na gesi asilia, makaa ya mawe na maabara ya vipimo vya chuma ngumu; • kuhuisha teknolojia ya kutumia <i>sensor</i> kufuatilia uzalishaji viwandani kwa wajasiriamali; • kukamilisha vigezo vya upatikanaji wa ithibati na kuboresha maabara ya chakula, mazingira, kemia, na maabara ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa; na • kukamilisha Jengo la Utawala na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa sekta ya ngozi kuhusu utunzaji wa mazingira. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na kazi za utafiti wa teknolojia za ubanguaji Korosho na usindikaji wa Michikichi, na kununua vifaa mbalimbali vya maabara kwa ajili ya tafiti mbalimbali.
<p>Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo - TEMDO</p>	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea na uboreshaji wa karakana na ofisi ya usanifu pamoja na miundombinu ya Taasisi kwa ujumla; 	<ul style="list-style-type: none"> • Kubuni na kutengeneza Chasili cha Mtambo wa kukausha mazao, kubuni na kutengeneza Chasili cha kutengeneza brikwiti kutokana na vumbi la Makaa ya Mawe kwa lengo la kupata

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • kubuni na kuendeleza utengenezaji wa mtambo wa kuweka baridi; • kubuni na kuendeleza chasili ya kusindika chai; • kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo mdogo wa kutengeneza brikwiti kutokana na vumbi la makaa ya mawe; • kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kukausha mazao ya kilimo; • kuhawilisha teknolojia na kuhamasisha uzalishaji wa kibiashara wa mitambo iliyobuniwa; • kutoa huduma za kiufundi kwa viwanda; kujenga miundombinu ya kiatamizi cha teknolojia na biashara; • kuanzisha na kuwezesha mpango wa kusambaza viwanda nchini kwa utaratibu wa kiwanda kimoja kila wilaya; na • kuanza ujenzi wa ofisi Dodoma 	<p>teknolojia bora ya nishati na yenye gharama nafuu katika kukausha korosho; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuimarisha maabara za utafiti kwa kununua mitambo na vifaa vya kisasa. Aidha, TEMDO imeweza kupata mtambo mdogo wa kuchakata mafuta ya mawese tani 1.25 kwa siku, mtambo huu umenunuliwa kwa ajili ya kudurufu.
Uendelezaji wa Viwanda Vidogo – SIDO	<ul style="list-style-type: none"> • kuboresha miundombinu wezeshi ya barabara, maji, umeme, uzio, mfumo wa maji taka na TEHAMA katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Iringa, Mwanza, Morogoro, Lindi, Mtwara, na Kagera; kujenga majengo ya viwanda 	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea na ujenzi wa ofisi nne (4) za Simiyu, Katavi, Geita na Chato; • ujenzi wa majengo ya viwanda (<i>Industrial Shades</i>) kumi na mbili (12) katika mitaa ya viwanda ya SIDO iliyopo mikoa ya Dodoma (3), Manyara (3), Kagera (1), Mtwara (1) na Geita (4) ambapo mitambo ya viwanda 29 imefungwa katika majengo hayo na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	katika mikoa ya Pwani, Ruvuma, Katavi, Mwanza, Tabora na Morogoro; kuongeza mtaji kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali - NEDF ambao unatoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo	kutoa ajira 648; na <ul style="list-style-type: none"> • SIDO ilitoa mikopo 16,954 yenye thamani ya shilingi bilioni 25.289 kwa wajasiriamali, ambapo asilimia 52 ya mikopo ilitolewa kwa wanawake na asilimia 48 kwa wanaume. Aidha, asilimia 38 ya mikopo hiyo ilitolewa kwa maeneo ya vijijini na asilimia 62 maeneo ya mijini. Vile vile, miradi iliyoanzishwa kupitia mikopo hiyo imechangia kutoa jumla ya ajira 40,998, kati ya ajira hizo asilimia 54 ni kwa wanawake na asilimia 46 kwa wanaume.
KILIMO		
Kilimo cha Mpunga	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendesha mashamba ya mfano 1,200 ya kilimo shadidi cha mpunga kutoka skimu za umwagiliaji 40; • Kutoa mafunzo kwa wakulima, viongozi na maafisa ugani; na • Kuendesha siku ya mkulima kwa wakulima 280 kutoka skimu 10 zilizofanya vizuri. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa mafunzo kwa wakulima 1,463 (wanawake 835 na wanaume 628) kuhusu matumizi ya pembejeo na kilimo shadidi; • Kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya Wakala wa Mbegu za Kilimo; na • Kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 66 kuhusu uzalishaji wa mbegu na kulinda ubora na teknolojia ya uzalishaji mpunga.
Kilimo cha Miwa	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo cha miwa kupitia mashamba darasa yaliyopo Kilombero, Mtibwa, Kagera, Mbigiri, Bagamoyo, Geita, Chamwino, Manyara - Kiru Valley, Singida, Ikungi, Katavi, Kalambo na Songea; kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutolewa kwa mafunzo ya kilimo bora cha miwa kwa maafisa ugani wa Mbigiri (Mkulazi) na Dabalo (Chamwino); • Kufikiwa kwa makubaliano baina ya Bodi ya Sukari na TEMDO ya kutengeneza “hot water treatment plants” ili kuwezesha wakulima wadogo kupata mbegu safi na salama; • Kuzalishwa kwa tani 234,727.63 za sukari; na • Kusajiliwa kwa wakulima 7,034.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>katika maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya uwekezaji wa miradi mipya ya sukari, katika maeneo ya Kasulu, Kibondo, Rufiji, Geita, Kilombero, Karagwe, Pangani, Bagamoyo na Morogoro;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha ekari 100 za vitalu vya mbegu za miwa katika maeneo ya miradi ya kati na midogo katika halmashauri za wilaya za Geita, Chamwino, Mpanda, Nsimbo na Mlele; na • Ukarabati wa mitambo ya kiwanda kidogo cha sukari Lumuma ambapo Shilingi bilioni 6.1 fedha za ndani zimetengwa. 	
Kilimo cha Chai	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha na kutunza mashamba mama 45 katika halmashauri za wilaya saba (Njombe, Mufindi, Kilolo, Ludewa, Tarime, Bumbuli na Korogwe) kwa kutumia mbegu bora (clones) za chai kutoka TRIT; • Kufufua kiwanda cha chai Mponde (Ludewa) kuzalisha miche bora ya chai 2,500,000 kwa ajili ya wakulima wadogo wa chai katika halmashauri za wilaya tano (Tarime, Bumbuli, 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuongezeka kwa uzalishaji wa chai kavu kufikia tani 11,185 ambapo wakulima wadogo walizalisha kilo 415 za chai kavu kwa hekta na wakulima wakubwa kilo 522 kwa hekta; • Kuongezeka kwa wastani wa ubora wa majani mabichi na kufikia asilimia 60 kutokana na ukaguzi na uhamasishaji; • Kuandaliwa kwa mikakati ya kuanzisha kituo cha pamoja cha wadau wa sekta ndogo ya chai kwa lengo la kupunguza gharama na muda; na • Kuongezeka kwa uzalishaji wa chai iliyochanganywa na kufungwa kwenye vikasha kufikia tani 2,700.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>Korogwe, Mufindi na Bukoba); na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuwezesha usafirishaji na upandaji wa miche bora ya chai 650,000 kutoka vitaluni kwenda mashambani katika wilaya za Tarime na Mufindi. 	
Kilimo cha Kahawa	<ul style="list-style-type: none"> • Kuongeza uzalishaji wa Kahawa kutoka tani 65,000 hadi tani 80,000 kwa kuzalisha na kusambaza miche bora ya kahawa 10,000,000 katika wilaya 42 zinazolima kahawa; • Kutoa mafunzo kwa wakulima 4,000, maafisa ugani 500 na wakulimaviongozi 300; • Kufanya maboreshoya maabara ya kuonjea kahawa na ununuzi wa mtambo wa kukaanga kahawa; • Kuendesha minada ya kahawa katika kanda nne za uzalishaji wa kahawa ambazo ni Bukoba-kagera, Songwe-Mbeya, Mbinga -Ruvuma, Moshi-Kilimanjaro; na • Kuendesha kampeni ya kufufua mashamba ya zamani na upandaji wa miche mipya. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuzalishwa kwa kahawa tani 55,979 ambapo kahawa aina ya Robusta ni tani 22,320, Arabika laini tani 32,057, na Arabika ngumu tani 1602; kuzalishwa kwa miche 3,692,780; • Kutolewa mafunzo kwa wakulima 62,523, Maafisa ugani 58, na wakulima viongozi; • Kuuzwa kwa tani za kahawa 21,929 katika minada 17 ya Kanda, zenye thamani ya Dola za Marekani 47,666,919; • Kuuzwa kwa tani 25,574 kupitia soko la moja kwa moja zenye thamani ya Dola za Marekani 39,860,860; • Kutolewa kwa mikopo ya mbolea kwa wakulima wadogo 286,297 (asilimia 89.5) na wakubwa 101 (asilimia 100) walisajiliwa, kupitia viwanda vya kukobolea kahawa na taasisi za fedha; • Uboreshwaji wa maabara za kahawa kwa kununua vifaa vya kisasa; • Utolewaji wa mafunzo kwa wanafunzi 50 wa cheti cha ubora wa kahawa na biashara (CQT) katika Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU); • Kuandaliwa kwa maonesho ya uhamasishaji wa unywaji wa kahawa katika nchi za Afrika, na kushiriki maonesho ya kimataifa ya SCAJ 2019, Tokyo - Japan na kuwezesha ongezeko la wanunuzi wawili (2) wakubwa wa kahawa ya Tanzania; na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa mapitio ya vigezo vya utoaji wa vibali vya ufungashaji kahawa ili kuongeza thamani ya bidhaa za kahawa kwa ajili ya soko la ndani
Kilimo cha Pamba	<ul style="list-style-type: none"> • Kununua, kuchakata na kusambaza tani 18,000 za mbegu za pamba zilizoondolewa manyoya kwa ajili ya kupanda; • Kuongeza upatikanaji wa mbegu kutoka tani 22,000 hadi kufikia 40,000; • Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya viudadu na vinyunyuzi; • Kuwasajili wakulima 500,000 wa pamba kidigitali; • Kutengeneza, kusambaza, na kuhamasisha matumizi ya teknolojia rahisi katika uzalishaji wa pamba; • Kuwezesha ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji na uchakataji; • Kuwezesha usimamiaji wa shughuli za mfuko wa kuendeleza zao la pamba; kununua na kusambaza ekapaki 10,000,000 za viudadu vya pamba kwa wakulima; na • Kutoa mafunzo kwa wadau wa pamba kuhusu kanuni za kilimo bora cha pamba na kuwezesha shughuli za 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuongezeka kwa uzalishaji wa pamba kutoka tani 222,725 za msimu wa 2018/19 hadi tani 350,000 katika msimu wa mwaka 2019/20; • Kuongezeka kwa matumizi ya kamba za kupandia pamoja na mbegu bora na hivyo kuongeza tija kwa mkulima kutoka wastani wa tani 250 hadi 316 kwa hekta; • Kusajiliwa kwa wakulima 568,000; • Kuimarika kwa usafi na ubora wa pamba; • Kuongezeka kwa daraja la Ganny ya juu kutoka asilimia 43 hadi asilimia 45; • Kuzalishwa kwa mbegu bora za kupanda kiasi cha tani 38,078 na kusambazwa kwa tani 17,942 za mbegu bora; na • Kukamilika kwa Mpango wa uendelezaji wa zao la Pamba pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 20 pamoja na kuboresha miundombinu ya TEHAMA.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	maendeleo na utafiti katika taasis za utafiti (Ukiriguru na Ilonga).	
Kilimo cha Tumbaku	<ul style="list-style-type: none"> • Kutengeneza kanzi data ya usajili na kusajili wakulima wa tumbaku wapatao 60,000 kutoka vyama vyote vya msingi vya ushirika; • Kukagua na kusajili vituo vya kuchambulia na kufungia tumbaku vipatavyo 1,972 na vya kuuzia 790; • Kufanya tathmini ya wingi na ubora wa zao shambani ili kubaini idadi ya kaya na wakulima walioshiriki kilimo, eneo lililopandwa tumbaku, uzalishaji na ubora tarajiwa katika vyama vyote; • Kuendesha mafunzo kwa wataalam wa masoko wa zao la tumbaku; • Kuendesha tafiti za zao la tumbaku ili kupata mbegu bora; na • Kuelimisha wakulima kupanda na kutunza miti na kuboresha mabani kuwa majiko banifu katika wilaya 25 katika vyama 298 na kukagua uzingatiaji wa taratibu za hifadhi ya mazingira na matumizi ya mabani yenye majiko sanifu na banifu katika vyama 298 kwenye wilaya 25. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuuzwa kwa tani 70,087 za tumbaku zenye thamani ya shilingi 230,367,073; • Kufanyika majaribio kwa aina nne (4) za mbegu za tumbaku ya mvuke kutoka nchini China; • Kufanyika usajili wa wakulima wa tumbaku 30,000; • Kupatikana kwa wanunuzi wapya wanne (4) wa tumbaku ambao ni kampuni za Grand Tobacco Co Ltd, Magefa Growers Ltd, Petrobena East Africa Ltd, na Pachetc Co Ltd; • Kufanyika ukaguzi na usajili wa vituo 1,578 vya kuchambua na kufungia tumbaku, na vituo 632 vya kuuzia tumbaku; • Kutolewa mafunzo ya kilimo bora cha tumbaku kwa wakulima 50,000; • Kufanyika maandalizi ya awali ya ujenzi wa kiwanda kipya katika Halmashauri ya wilaya ya Urambo ambacho kitajengwa kwa ushirikiano wa wakulima na Serikali; na • Kuimarika kwa ubora wa tumbaku ambapo tumbaku isiyo na dosari ni asilimia 93 na yenye dosari ni asilimia 7.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Upatikanaji wa Mbegu na Pembejeo za kilimo	<ul style="list-style-type: none"> • Kuzalisha mbegu za alizeti tani 200, pamba tani 200, miche ya michikichi milioni 5 na miche ya korosho milioni 1; • Kukarabati vituo 36 vya Afya ya mimea na vituo 8 vya ukaguzi wa mazao; • Kuagiza na kusambaza tani 625,000 za mbolea; • Kukarabati ghala moja (1) lenye uwezo wa kuhifadhi tani 20,000 za mbolea katika wilaya ya Tabora; • Kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchanganya mbolea kwa uwiano katika mkoa wa Dar es Salaam; • Kununua na kusambaza lita 300,000 na kilo 3,000 za viuatilifu; • Kukarabati na kununua vifaa katika maabara mbili (2) za kupimia viuatilifu ili zipate ithibati ya kimataifa; • Kutoa mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu na uhifadhi wa taka zake kwa wakulima na maafisa ugani 1,200 katika kanda za Mashariki, Kaskazini, Kati na Magharibi; • Kuanzisha kituo kimoja (1) cha zana za kilimo kwa ajili ya kutoa huduma za kiufundi kwa lengo kusogeza huduma 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanyika kwa tathmini kuhusu gharama za ukarabati wa ghala la Tabora kupitia Wakala wa Majengo Tanzania kanda ya Tabora; • Kupatikana kwa eneo la kujenga kiwanda cha kuchanganya mbolea (Fertilizer blending plant) katika wilaya ya Kisarawe lenye ukubwa wa mita za mraba 40,404; • Kuingizwa nchini mbolea ya DAP (tani 28,500), na mbolea ya UREA (tani 65,850); na • Kutolewa kwa vibali 209 vya uagizaji wa mbolea kiasi cha tani 215,417 na lita 85,018.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	karibu na wakulima katika kanda ya ziwa.	
Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ujenzi wa mabwawa ya Lwanyo, Kongogo na Nyisanzi; • Kujenga miundombinu mipya ya umwagiliaji katika skimu za Lupilo (Ulanga), Bugwema (Musoma), Mara, Ngono, Nyisanzi na Kongogo; kujenga mabwawa mapya ya Borenga (Bonde la Mara), Kalebe (Bonde la Ngono) na Luiche-Kigoma; • Kukarabati miundombinu ya skimu za umwagiliaji za Kigugu-Mvomero, Mvumi-Kilosa, Msolwa Ujamaa na Njage-Kilombero; ukarabati wa miundombinu 88 ya umwagiliaji katika kuingia katika skimu za Mvumi (km 8) na Njage (km 7); • Kukamilisha upembuzi kuingia katika skimu za Mvumi (km 8) na Njage (km 7); • Kukamilisha upembuzi yakinifu kwa skimu ya Luiche (Ujiji Kigoma) na Ibanda (Sengerema/Geita); kufanya yakinifu kwa skimu ya Luiche (Ujiji Kigoma) na Ibanda (Sengerema/Geita); • Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufikia asilimia 60 kwa ujenzi wa mradi wa Edagana; • Kukamilika kwa skimu 8 za umwagiliaji (Soko - Moshi; Kituani, Mwenzae na Kwemgiriti - Lushoto; Katela Ntaba - Busokelo; Ngongowele na Nanganga - Ruangwa; Mwalunili - Igunga; na Njage - Simanjiro); kuendelea na ujenzi wa skimu za Kinyope - Lindi, Mwisu - Korogwe, Nyatwali na Maliwanda - Bunda, Nyida - Shinyanga, Mwamkulu - Igunga na Orumwi (Moshi) kufikia asilimia 78 ya utekelezaji; • Kukamilika kwa ukarabati wa skimu ya Dakawa kupitia programu ya Feed the Future; na • Kutolewa kwa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya skimu kwa wakulima viongozi 402 kutoka skimu za Njage na Msolwa Ujamaa (Kilombero).

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>wa kina katika skimu nne (4) za Mwamkulu (Mpanda), Mkombozi (Iringa), Msia (Mbozi) na Luhafwe (Tanganyika); na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Lwanyo, Kirya, Igenge, Endagaw (Hanang^o), Rudewa (Kilosa) na Nyamitita (Serengeti). 	
Uzalishaji wa Mbegu Bora za Mazao	<ul style="list-style-type: none"> • Kuzalisha na kusambaza mbegu bora za awali tani 200, za msingi tani 1,000, na mbegu zilizothibitishwa tani 3,000 za mazao ya aina ya nafaka, mikunde, mboga mboga, mafuta na miche milioni 20 ya mazao ya mizizi; • Kuzalisha tani 2,000 za mbegu za Alizeti na kuzisambaza kwa wakulima; • Kuboresha miundombinu ya umwagiliaji kwa mashamba ya Arusha, Mwere, Bugagana na Dabaga; kuboresha na kujenga maghala ya kuhifadhia mbegu za, kilimo kwa shamba la Msimba na Kilangali; na • Kufanya tathmini ya afya ya udongo katika mashamba 8 ambapo Shilingi bilioni 6.3 fedha za ndani zimetengwa. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuzalishwa kwa miche 10,305,427 ya mazao ya korosho, miwa, migomba, nazi, zabibu na katani; • Kuzalishwa kwa vikonyo 1,649,379 vya viazi vitamu na pingili 4,064,620 za muhogo; • Kuongeza uzalishaji kupitia makampuni binafsi kwenye ardhi ya ASA kutoka tani 2584.8 kufikia tani 3037.47; kuongeza maeneo ya uzalishaji kutoka hekta 9,890 kufikia hekta 10,500 zinazofaa kulimwa; • Kuoteshwa kwa mbegu 61,384 za michikichi; • Kuzalisha vipando bora vya muhogo pingili 7,000,000; na • ununuzi wa zana mpya zikiwemo trekta 3 (trekta 2 za HP 95 na moja la HP 125), mashine 2 za kupanda, majembe mawili, mashine 3 za kunyunyiza dawa na mashine ya kulainisha udongo.
Tafiti za Kilimo	<ul style="list-style-type: none"> • Kutafiti, kugundua na kusambaza aina 	<ul style="list-style-type: none"> • Kugunduliwa kwa aina 22 za mbegu bora za mazao (muhogo (9),

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>15 za mbegu bora za mazao ya nafaka, mizizi, mbegu za mafuta, migomba, mikunde na mazao ya bustani;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kugundua na kusambaza teknolojia bora za kilimo zikiwemo teknolojia za agronomia 20; • Kukamilisha majaribio ya mbegu mpya za NARITAs Hybrid zenye ukinzani mkubwa wa wadudu na magonjwa katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya na Kagera; na • Kupunguza harubu katika kilimo tano (5) na usindikaji, kuzuia upotevu wa mazao baada ya kuvuna na uhifadhi wa mazao 15 kwa ajili ya kuimarisha usalama wa chakula na lishe. 	<p>alizeti (2), mahindi (2), mpunga (2), ulezi (1) na viazi vitamu (6)). Mbegu zilizogunduliwa zinatarajiwa kuongeza uzalishaji;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuzalishwa kwa tani 940.94 za mbegu bora za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta (mbegu mama tani 228.2, mbegu za awali tani 521.75, mbegu za msingi tani 59.656 na mbegu zilizothibitishwa tani 131.332); na • Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 84 wa katika vyuo mbalimbali chini ya ufadhili wa wadau mbalimbali wa maendeleo (34 ni wa shahada ya uzamivu, 23 shaada ya uzamili, 26 shahada ya kwanza na mmoja (1) stashahada).
Miundombinu ya Utafiti wa Kilimo	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha na kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa kukarabati ofisi na kuvipatia vifaa muhimu vituo vinne (4) vya utafiti vya Ukiriguru, Ilonga na Tumbi; • Kuboresha miundombinu ya mashamba ya uzalishaji wa mbegu kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora; • Kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ya vituo vya utafiti vya Ilonga, Naliendele, Ukiriguru na 	<ul style="list-style-type: none"> • Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika vituo vya Uyole, Ilonga na Selian; na kufanyika kwa maandalizi ya awali ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ya vituo vya Ilonga, Naliendele na Ukiriguru.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika vituo vya Uyole, Ilonga na Seliani itaboreshwa;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kujenga Makao Makuu ya TARI pamoja na kituo cha Biosayansi, kituo cha TARI Kihinga Kasulu kwa ajili ya utafiti; • Kuendeleza zao la michikichi kwa kujenga miundombinu ya utafiti na uzalishaji wa miche na vitendea kazi; na • Kufanya ukarabati wa miundombinu ya kituo cha ukusanyaji na utunzaji nasabu za mimea (NPGRC). • 	
Maghala na Kuboresha Hifadhi ya Taifa ya Chakula	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ujenzi wa maghala matano (5) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 na vihenge nane (8) vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 190,000 za nafaka; • Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa maghala matano (5) kwa ajili ya kuhifadhi mahindi katika Halmashauri za Wilaya za Buchosa (1), Mkalama (1), Kasulu (1), Itilima (1) na Ileje (1); ujenzi wa maghala matano (5) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 6,700 za mpunga 	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa ghala katika Skimu mbalimbali unaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 60 kwa Skimu ya Msolwa Ujamaa, Skimu ya mbogo kwa Mtongo (asilimia 20), Skimu ya Mvumi (asilimia 72), na Skimu ya Njage (asilimia 55); • Kuchakatwa kwa tani 160 za mahindi kwa siku (Dodoma tani 60, Iringa tani 55, na Arusha tani 45); • Kufanya mashine za kukamua alizeti Kizota Dodoma umefikia asilimia 95; • Kununuliwa kwa mazao katika mikoa ya Iringa, Njombe, Songwe na Dodoma kiasi cha tani 11,113.57 za mahindi, tani 165 za alizeti na tani 29.273 za maharage; na • Kuuzwa kwa jumla ya tani 610.299 za korosho zilizobanguliwa.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>katika skimu tano (5) za umwagiliaji za Njale (1,700), Msolwa Ujamaa (1,700), Kigugu (1,000), Mvumi (1,300) na Mbogokomtonga (1,000) katika mkoa wa Morogoro; ukarabati wa kituo cha udhibiti wa magonjwa ya kibaolojia (Kibaha);</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kusindika tani 29,000 za mahindi ili kuzalisha tani 17,400 za unga wa mahindi na tani 4,350 za pumba za mahindi kwa ajili ya chakula cha mifugo; • Kusindika tani 15,000 za alizeti ili kuzalisha lita 3,461,000 za mafuta na tani 10,350 za mashudu ya alizeti; na kukoboa tani 27,000 za mpunga zitakazozalisha tani 8,100 za mchele na tani 4,000 za pumba. 	
Huduma za Upimaji wa Matabaka na Ubora wa Udongo	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kupima na kuwezesha upatikanaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila; • Kufanya tathmini ya ubora wa udongo na kuandaa ramani za udongo kwenye maeneo ambayo ardhi ya kilimo imetambuliwa kwa ajili ya vijana katika Halmashauri za wilaya za Singida na Morogoro; na 	<ul style="list-style-type: none"> • Kupimwa kwa mashamba makubwa 43 katika mkoa wa Tanga yenye jumla ya hekta 124,924.13; • Kuhakiki mashamba yaliyobatilishwa umiliki ambapo mashamba 17 yapo mkoani Morogoro, 13 Tanga na 15 Arusha; na • Kutolewa elimu kwa wakulima kuhusu teknolojia za matumizi bora ya ardhi ikiwemo hifadhi ya udongo na maji mashambani. •

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanya tathmini katika vijiji vinavyozunguka mashamba saba (7) ya uwekezaji katika Bonde la Mto Rufiji (Lukulilo, Muhoro na Tawi) na mashamba mengine ya Mkulazi, Pangani, Kitengule na Bagamoyo ili kupata taarifa na ramani zitakazowezesha kuchagua mazao yatakayolimwa pamoja na matumizi sahihi ya mbolea. 	
<p>Huduma za Ushauri kuhusu Utafiti, Mafunzo na Usambazaji Taarifa za Kilimo na Sayansi Shirikishi</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuandaa mashamba ya mfano 50 kwa teknolojia ya mazao mbalimbali; • Kutoa machapisho 1,000 ya aina 20 za teknolojia za mazao ya nafaka, mizizi, mikunde, pamba, na mboga mboga na kuzisambaza kwa wakulima; • Kuandaa kanzidata ya kielektroniki ya teknolojia zote zilizozalishwa na vituo vya utafiti na kuziunganisha na simu za mkononi za wakulima ili wapate taarifa kwa urahisi; na • Kutoa elimu kwa wakulima 2,000 na wagani 200 katika utumiaji wa teknolojia mpya ikiwa ni pamoja na matumizi ya mbegu bora, udhibiti wa magonjwa na matumizi ya madawa ambapo Shilingi milioni 500 fedha za 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya pembejeo na kilimo shadidi kwa wakulima 1,463 (wanawake 835 na wanaume 628); • Kutoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu bora na usimamizi wa teknolojia ya uzalishaji wa zao la mpunga kwa Maafisa ugani 66; kutolewa kwa machapisho 15 ya tafiti za kilimo pamoja na kupatiwa ufadhili wa shilingi 11,987,842 kwa ajili ya kugharamia uandaaji wa maandiko ya miradi 25. •

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	ndani zimetengwa.	
Mkakati wa uzalishaji wa zao la Mchikichi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuzalishaa miche ya michikichi 5,000,000 kutakofanywa na taasisi za TARI kwa kushirikiana na ASA, Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza, Sekretarieti za Mikoa na Sekta Binafsi; • Kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Bugaga (Kasulu); na • Kujenga kituo kipya cha TARI Kihinga kwa ajili ya utafiti wa zao la michikichi. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuzalishwa kwa mbegu 1,129,429 za michikichi ambapo mbegu 790,611 zimeoteshwa katika halmashauri 6 za mkoa wa Kigoma na taasisi nyingine za Serikali; na kuzalishwa na kusambazwa kwa miche 35,975 ya michikichi kwa wakulima.
MIFUGO		
Kuimarisha Vituo vya Uhimilishaji Kitaifa na Kanda	<ul style="list-style-type: none"> • Kununua mtambo mpya wa Naitrojeni wenye uwezo wa kuzalisha lita kumi (10) za kimiminika baridi cha hewa ya Naitrojeni kwa saa moja; • Kununua mitungi 70 ya kuhifadhi kimiminika baridi cha hewa ya Naitrojeni yenye ujazo wa lita 35 kwa kila mtungi na kuisambaza kwenye halmashauri 70; • Kununua mtungi wa kuhifadhi kimiminika cha hewa baridi ya Naitrojeni wenye ujazo wa lita 200 kwa ajili ya kituo cha NAIC Arusha; • Kununua chupa 75,000 za homoni; 	<ul style="list-style-type: none"> • Kununuliwa kwa jumla ya mitungi 20 ya kuhifadhi kimiminika cha hewa baridi ya Naitrojeni yenye ujazo wa lita 35 kila mmoja na kuisambaza kwa wahimilishaji; • Kununuliwa kwa chupa za homoni 10,000; • Kuanzisha kambi za kuendesha uhimilishaji katika Mikoa ya Simiyu, Katavi na Dodoma; • Kutoa mafunzo ya uhimilishaji kwa wahimilishaji 48 wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Njombe, Mtwara, Dodoma, Songwe, Mbeya na Tanga; • kujenga uwezo wa vitendo kuhusu uhimilishaji kwa wahimilishaji 37 katika Halmashauri 8; • Kuzalishwa kwa mbegu bora za madume dozi 31,931 na Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa cha NAIC; na • Kusambazwa kwa wafugaji kwa ajili ya kuboresha mifugo.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa elimu ya uhimilishaji kwa wahimilishaji 600 kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Katavi, Mwanza na Geita; na • Kununua darubini 2 kwa ajili ya vituo viwili vya uhimilishaji vya mikoa ya Pwani na Dodoma. 	
Kutenga Maeneo ya Malisho na Upatikanaji wa Maji	<ul style="list-style-type: none"> • Uendelezaji wa miundombinu ya majosho na malisho; • Kuendelea kutenga na kupima maeneo ya malisho na kuandaa miongozo ya utumiaji na usimamizi wa maeneo hayo; • Kusimamia na kudhibiti ubora wa vyakula vya mifugo kwa kufanya ukaguzi wa viwanda, maeneo ya kuuzia na kutoa mafunzo kwa wakaguzi na watengenezaji; • Kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za malisho kwa kuimarisha na kupanua mashamba saba (7) ya Serikali; • Kuchimba na kujenga visima 50 katika maeneo mbalimbali nchini; na • Ukarabati wa malambo sita (6) katika mikoa ya Manyara, Pwani, Simiyu, 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutengwa, kupimwa na kuweka alama zinazoonekana kwenye maeneo yaliyotengwa kwa malisho ya mifugo kwenye mashamba 8 yenye ukubwa wa hekta 23,066.94 ya Hanga ngadinga (Ruvuma) (4,200), Mahukuru Lilahi (Ruvuma) (3,100), Chibe (Shinyanga) (2,054), Shishiyu (Simiyu) (3,170), Mkwese (Singida) (5,036), Kinyangiri (Singida) (3,419.94), Nachingwea (Lindi) (1,497) na Kelema (Dodoma) (590). • Kutengwa jumla ya hekta 2,818,687.17 kwa ajili ya malisho na kupimwa kwa hekta 108,427.49 katika Halmashauri za Wilaya; na • Kuanzishwa kwa mashamba darasa 20 ya malisho, kati ya hayo, mashamba darasa matano (5) yapo Wilaya ya Monduli na 15 yapo katika halmashauri zote za mkoa wa Singida.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	Arusha, Geita na Tabora.	
Kuimarisha Tiba na Udhhibiti wa Magonjwa ya Mifugo	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga uwezo Kiwanda cha Chanjo za Mifugo cha Serikali kilichopo Kibaha ili kiweze kuzalisha aina saba (7) za chanjo za magonjwa; • Kuwezesha Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania kuzalisha dozi milioni 111 za chanjo za mifugo ikiwa ni pamoja na dozi milioni 100 za chanjo ya Mdondo ya TEMEVAC 12, milioni 5 za CBPP, milioni 3 za Kimeta na milioni 3 za Chambavu; na • Kuanza majaribio ya kuzalisha chanjo dhidi ya ugonjwa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (CCPP), dhidi ya Kichaa cha Mbwa na Mapele ya Ngozi. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa jengo la kuzalisha chanjo za bakteria katika Kituo cha Kuzalisha Chanjo cha Kibaha (TVI) ambapo kwa sasa umefikia asilimia 75; na • Kuzalisha na kusambaza dozi 47,347,700 za chanjo ya Ugonjwa wa Mdondo, dozi 320,800 za Ugonjwa wa Kimeta, dozi 86,600 za ugonjwa wa Chambavu, dozi 513,200 za Ugonjwa wa Mapafu ya Ng'ombe, dozi 27,725 za Ugonjwa wa Kutupa Mimba na dozi 31,750 za chanjo zenye muunganiko wa <i>Blackquarter vaccine</i> na <i>Anthrax vaccine - TECOBLAX</i>.
UVUVI		
Kusimamia na Kuhamasisha Uwekezaji katika Uvuvi na Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Uvuvi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha vituo vya ubora na uthibiti wa mazao ya uvuvi na kuanzisha vituo vipya vitatu vya Singida, Kisesya na Murusagamba; • Kufanya kaguzi 7,200 za ubora wa samaki na mazao yake wakati wa kusafirisha nje ya nchi; • Kufanya kaguzi 120 za kina kwenye 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzishwa kwa vituo vitano (5) vya usimamizi wa rasilimali za Uvuvi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali ambavyo ni Gozba, Rorya, Bwawa la Nyumba ya Mungu, Bwawa la Mtera na Ziwa Rukwa pamoja na vituo vya ubora na uthibiti wa mazao ya uvuvi vya Singida, Kisesya na Murusagamba; • Kufanyika kwa kaguzi 2,904 za samaki na mazao ya uvuvi katika viwanda vya uchakataji wa Samaki, maghala ya kuhifadhia samaki na magari ya kusafirisha samaki pamoja na kaguzi 191 za

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>viwanda vinavyochakata samaki, maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi, mialo na masoko ya samaki;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha maabara za samaki za Nyegezi (Mwanza) na ya viuatilifu Dar es Salaam kwa kuzipatia vitendea kazi, watumishi na mafunzo kwa Wataalam; na • Kufanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli 4,800 za minofu ya samaki, maji, udongo, masalia ya madawa ya mimea, asidi, alikali na madini tembo ili kuhakiki usalama wa mazao ya uvuvi. 	<p>kina katika viwanda vinavyochakata samaki na masoko;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuimarishwa kwa Maabara za samaki za Nyegezi (Mwanza) na ya viuatilifu Dar es Salaam kwa kupatiwa vitendea kazi ikiwemo madawa na vifaa ya kufanyia uchunguzi wa sampuli; • Kuweka mazingira wezeshi katika uvuvi wa bahari kuu kwa kuweka vivutio kwa wawekezaji wa ndani ya nchi na nje, kufuatia kutungwa kwa Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2020; • Kuhamasisha sekta binafsi kwa kuiunganisha na taasisi za kifedha ili iwekeze katika ujenzi wa viwanda vya uchakataji wa mazao ya uvuvi; na • Kuanzishwa kwa Dawati la Sekta Binafsi kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji wa Sekta Binafsi, kusaidia kuondoa changamoto za biashara na uwekezaji na upatikanaji wa mitaji. Aidha, Dawati limehamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya Wavuvi na Wakuzaji Viumbe Maji katika mikoa ya Mwanza, Tanga, Kagera, Geita, Mbeya, Ruvuma, Songwe na Mara. Vile vile, dawati limeunganisha Vyama vya Ushirika 86 vya Wavuvi na taasisi za kifedha ili waweze kupata mikopo, na kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 510 kutoka Taasisi za kifedha hususan Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambapo mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 22 ipo katika hatua mbalimbali za uthamini na inategemewa kutolewa pindi uthamini utakapokamilika.
<p>Kuimarisha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi; • Kuboresha mfumo wa ufuatiliaji wa 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ambao umependekeza maeneo matatu yanayofaa kwa ujenzi wa bandari hiyo: Mbegani-Bagamoyo, Kilwa Masoko na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
na Bahari Kuu	<p>meli za uvuvi wa Baharini;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kununua meli ya doria kwa ajili ya kufanya operesheni mbalimbali kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari kuu; na • Kununua meli mbili (2) za uvuvi (Long line na Purse Seiner). 	<p>Lindi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuhuishwa kwa mfumo wa kufuatilia mienendo ya meli kwa kununua mtambo wa Automatic Identification System-AIS; • Kutungwa kwa Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2020 ambayo imezingatia mahitaji ya sasa; na • Kuwajengea uwezo waangalizi 11 wa shughuli za uvuvi melini kutoka katika Mamlaka na Idara za Uvuvi (SMT na SMZ).
Kuimarisha Tafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya uvuvi	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanya utafiti wa samaki wapya wa kufugwa; • Kufanya utafiti wa vyakula vya samaki na kuongeza ubora wa mbegu za samaki wa kufugwa na mwani; na • Kufanya tafiti za kujua wingi wa rasilimali za uvuvi zilizo katika ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanya utafiti wa kuangalia wingi wa samaki katika Ziwa Victoria kupitia taasisi ya TAFIRI ambapo matokeo yanaonyesha kuongezeka kwa samaki aina ya Sangara kutoka tani 553,770 mwaka 2018/19 hadi tani 816,694 mwaka 2019/20. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za kupiga vita uvuvi haramu; • Utoaji wa huduma za ugani juu ya uvuvi endelevu, uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi, ufugaji bora wa samaki na umuhimu wa uanzishwaji wa vyama vya ushirika kwa wadau 3,266; na • Kuanzishwa na kupatiwa mikopo kutoka taasisi za kifedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa vyama 16 vya ushirika.
Kuongeza Upatikanaji wa Vifaranga vya Samaki	<ul style="list-style-type: none"> • Kuwezesha Vituo vitatu (3) vya samaki wa maji baridi vya Ruhila, Kingolwira na Mwamapuli na kujenga kituo kimoja (1) cha Nyamirembe ili kuzalisha vifaranga milioni 15 vya samaki; • Kuboresha matumizi ya teknolojia za uzalishaji, kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya viumbe vya 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuzalishwa kwa vifaranga 15,041,401 ambapo vifaranga 950,401 ni kutoka vituo vya Serikali na vifaranga 14,088,000 kutoka vituo binafsi; • Kutoa mafunzo ya ufugaji wa samaki kwa wananchi 3,595 sawa na asilimia 89.88 ya lengo lililokusudiwa; • Kununuliwa kwa matanki 27 yenye uwezo wa kuhifadhi vifaranga 324,000 kwa wakati mmoja na kupelekwa katika vituo vya Ruhila, Kingolwira na Mwamapuli;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>majini; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuunda kanda 3 za ufugaji wa vizimba katika Ziwa Victoria na kanda 2 za ukuzaji viumbe wa maji bahari katika mikoa ya Pwani na Mtwara 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufungwa kwa <i>happa nets</i> 50 katika vituo vya Ruhila (30), Mwamapuli (20) kwa ajili ya kukuzia wazazi kukusanya mayai; • Kupandikiza samaki wazazi wapatao 27,640 katika vituo vya Ruhila (2,100), Mwamapuli (5,900), Kingolwira (11,640) na Mtama/Nyengedi (8,000) na kuunganisha umeme katika vituo vya Mwamapuli na Ruhila; • Kukarabati mabwawa 11 katika vituo vya Mtama/Nyengedi (8) na Kingolwira (8); • Kukarabati mabwawa matatu (3) na nyumba moja (1) ya mtumishi katika kituo cha Kingolwira; na • Kununuliwa kwa mashine mbili (2) za kusukuma maji kwa ajili ya vituo vya Ruhila na Mwamapuli.
<p>Kuimarisha na Kuendeleza Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha vituo 27 vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi vilivyopo na kuanzisha kanda na vituo katika maeneo ya maji na nchi kavu; • Kufanya doria za kawaida za kudhibiti uvuvi na biashara haramu; na • Kufanya operesheni za kila robo ya mwaka za kudhibiti Uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanyika kwa operesheni na doria zenye jumla ya siku kazi 5,788 katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu, na katika Bahari ya Hindi ambazo ni sawa na asilimia 89 ya lengo la mwaka lililokuwa na Siku kazi 6,500; na • Kutolewa kwa vitendea kazi katika vituo 27 vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi na kuanzishwa kwa vituo viwili (2) vya Mtera na Nyumba ya Mungu.
<p>Kuimarisha Miundombinu na Kukuza Biashara ya Mazao ya Uvuvi</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kukarabati mialo ya kupokelea samaki na masoko ya samaki (Mialo) ya Sota, Marehe, Kigangama, Kahunda, Ikumbaitale, Bwai, Nyamisati, Igombe, Ihale, Mafia, Kilwa, Kirumba na Feri. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanya tathmini katika masoko manne (4) na mialo 26 ikiwemo ya Sota, Marehe, Kigangama, Kahunda, Ikumbaitale, Bwai, Nyamisati, Igombe, Ihale, Mafia, Kilwa ili kupata hali halisi na changamoto za uendeshaji; na • Soko la Samaki la Feri - Dar es Salaam limeboreshwa kwa kujengwa ofisi mbili (2), stoo mbili (2) na choo cha kisasa chenye

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		matundu 12 na mabafu nane (8).
MALIASILI, MISITU NA UTALII		
Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili	<ul style="list-style-type: none"> • Kusaidia Halmashauri za Ngorongoro na Serengeti katika masuala ya Sera, Sheria na taratibu zinazohusu mgawanyo wa faida zitokanazo na uhifadhi wa maliasili; na • Kuzijengea uwezo Halmashauri za Ngorongoro na Serengeti katika kutatua migogoro inayotokana na mwingiliano kati ya wanyamapori na wananchi. 	<ul style="list-style-type: none"> • kujengwa kwa maboma ya kujilinda na wanyama wakali wakati wa usiku katika vijiji 10 vya Wilaya ya Serengeti; • kutoa mafunzo kwa maafisa mazingira na uhifadhi katika ngazi ya Kata na Vijiji katika wilaya ya Ngorongoro; • kuandaliwa kwa mwongozo wa uwindaji wa Simba na Chui kwa kuzingatia mahitaji ya Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya viumbe vilivyo katika hatari ya kutoweka; • kuandaa mpango wa usimamizi wa Pori la Akiba la Kijereshi na kubainisha maeneo ya uwekezaji na uendelezaji utalii; • kuendelea na maandalizi ya Mpango wa Usimamizi wa Pori la Akiba la Mkungunero; • kuandaliwa kwa mpango shirikishi ya usimamizi wa misitu na sheria ndogo katika vijiji sita (6) katika Wilaya ya Serengeti na Ngorongoro; na • kufanya ufuatiliaji na mafunzo rejea kwa vikundi 6 vya kuweka na kukopa vya ufugaji wa nyuki kibiashara.
Mradi wa Kuimarisha Misitu Asilia, Mapori Tengefu na Vitendo vya Kupambana na Ujangili Nchini	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, nyumba na watumishi; • Kuwezesha halmashauri za Wilaya na Vijiji vinavyozunguka misitu ya mazingira asilia kufanya doria za mara kwa mara kwa kuvipatia vifaa; na 	<ul style="list-style-type: none"> • kujengwa kwa barabara za msituni (km 85.53) katika Hifadhi zote za Misitu ya Asili; • kujengwa kwa njia za msituni (km 37.3) katika hifadhi za misitu asilia ya Udzungwa Scarp, Kilombero, Mlima Hanang na Minziro; • kuanzishwa kwa manzuki, vitalu vya miche, ufugaji samaki kwa jamii zinazopakana na hifadhi za misitu asilia ya Chome,

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kuweka alama za kudumu kuzunguka misitu yote ya mazingira asilia. 	<p>Mkingu, Minziro, Kilombero, Mlima Rungwe, Mlima Hanang na Magamba;</p> <ul style="list-style-type: none"> • ushirikishwaji wa jamii zinazozunguka hifadhi katika Hifadhi za Misitu Asilia ya Minziro, Chome, Magamba, Mlima Rungwe na Mkingu; na • kutangaza shughuli za utalii ikolojia kwa nia ya kuongeza idadi ya watalii na kuongeza mapato.
Mradi wa Kusaidia Uendelezaji wa Misitu Binafsi na Mnyororo wa Thamani	<ul style="list-style-type: none"> • Kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na mipango ya usimamizi wa misitu ya hifadhi ya vijiji katika wilaya nane (8) za mikoa ya Tanga, Lindi Mtwara na Ruvuma; • Kutoa elimu kwa Kamati za Maliasili za vijiji, sekta binafsi kuhusu umuhimu wa rasilimali na namna ya kuongeza thamani mazao ya misitu; • Kutoa elimu na uraghibishi kwa Kamati za Maliasili za vijiji, watumishi wa halmashauri na Asasi zisizo za Serikali; na • Kuwezesha Kamati za Mazingira za vijiji katika kufanya doria mbalimbali kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji kwa kuvipatia vifaa. 	<ul style="list-style-type: none"> • kuandaliwa kwa Mipango 25 ya Matumizi Bora ya Ardhi; • kusambaza miche 230,000 ya mitiki katika vinne (4) vya Wilaya ya Nyasa kwa ajili ya kupanda kwenye mashamba yao; • kuchapishwa kwa nakala 3,500 za Kitabu cha Usimamizi wa Misitu ya Jamii; • kupatiwa mafunzo kwa waandishi wa habari 27 kuhusu mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na uandishi wa habari za kiuchunguzi; • kufungwa kwa mfumo wa utoaji na upashanaji wa taarifa; • kuanzisha Misitu ya Vijiji 32 yenye ukubwa wa hekta 32,245; • kuandaa mtaala wa kuongeza thamani mazao ya misitu, mifumo ya masoko na kuendeleza biashara; • kuanzisha mfumo wa Taarifa wa Programu ya FORVAC ikiwa ni pamoja na kuanzisha Tovuti ya Programu; • kuandaa mwongozo wa kuandaa Mpango wa Usimamizi wa misitu ya Asili Tanzania; • kuunda na kujenga uwezo wa Kamati za Hifadhi ya Mazingira za vijiji 12; • kuunda na kutoa mafunzo kwa vikundi 10 vya ujasiriamali vyenye jumla ya wanachama 520; na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
<p>Mradi wa kuwezesha Wananchi Kunufaika na Rasilimali za Misititu kwa Maendeleo ya Kiuchumi</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha mipango ya usimamizi wa misitu ya hifadhi ya vijiji 33 vya mradi; • Kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 36 na kutoa hati miliki za kimila; • Kuandaa mpango wa uendelezaji wa matokeo ya mradi, uwekezaji na mambo ya kujifunza yaliyotokea kwenye kila uwanda; na • Kujenga uwezo kwa wataalam ngazi ya kijiji kusimamia shughuli za mradi. 	<ul style="list-style-type: none"> • kuandaa mtaala wa ongezeko la thamani ya mazao ya misitu, mifumo ya masoko na maendeleo ya biashara. • kutolewa kwa hati za kimila 3,500 za umiliki wa ardhi; • kukamilika kwa Mipango 29 ya Matumizi Bora ya Ardhi; • kutolewa mafunzo kwa timu za Mradi za Wilaya na Vijiji na Kamati za Mialo kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Maliasili na Sheria ndogo; • kuandaliwa kwa mipango ya usimamizi na uvunaji wa misitu kwa vijiji nane (8) katika wilaya za Kibondo na Kasulu; • kuanzisha hifadhi za misitu ya vijiji katika vijiji 28 vyenye jumla ya misitu 39 na ukubwa wa hekta 39,449; • kuanzisha Kamati za fukwe tatu (3) za Mtanga, Kagalye na Kalalangabo; • kuanzisha vikundi vitano (5) vya wavuvi katika vijiji vya Kasisi, Mtego wa noti, Malagarasi, Itebula na Chagu; • kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuongeza thamani katika asali na samaki kwa wajumbe 86 wa timu za uendeshaji mradi za wilaya na vikundi 73 vya uzalishaji mali; • kuwezesha vikundi vidogo vya uzalishaji mali 25 kutekeleza miradi ya kuhifadhi maliasili; na • kuwezesha upatikanaji wa mitumbwi ya kisasa 23 kwa ajili ya doria, ufuatiliaji na uvuvi wa samaki katika Ziwa Nyamagoma na Ziwa Sagara.
<p>Mradi wa kuendeleza Utalii Ukanda wa Kusini - REGROW</p>	<p>Kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa babarara, viwanja vya ndege, mabanda kwa ajili ya kupokea wageni katika hifadhi zilizo kusini mwa Tanzania.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • kuandaliwa kwa maandiko kwa ajili ya kuwajengea uwezo wananchi wanaopakana na Hifadhi ya Taifa Ruaha kwenye skimu ya umwagiliaji ya Madibira katika wilaya ya Mbarali ili kulinda hifadhi dhidi ya uharibifu wa mazingira;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> • kukamilika kwa tathmini ya kuandaa mpango mkakati wa masoko ya utalii katika maeneo ya kusini; • ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kufanya doria katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Mikumi, na Udzungwa; • kutangaza na kutoa elimu kuhusu vivutio vya utalii kupitia maonesho ya Karibu Kusini yaliyofanyika mkoa wa Iringa; • kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo ili kujua mapungufu yaliyopo kwa wakulima katika vyama vya umwagiliaji; • kufanya mapitio ya katiba na ada za huduma ya umwagiliaji kulingana na Sheria ya Umwagiliaji; na • kusajili na kuzindua chama kimoja (1) cha watumiaji wa maji wa Mto Mbarali wa Chini.
MADINI		
Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini - SMMRP	<ul style="list-style-type: none"> • Kuwezesha shughuli za utafiti wa madini ili kuongeza taarifa za kijilojia na kuvutia uwekezaji; • Kuhamasisha uongezaji thamani madini nchini; • Kufanya mapitio na kuandaa mkakati wa Sera ya madini ya Mwaka 2009; • Uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini; • Usimamizi wa masuala ya mazingira, afya na usalama migodini; • Uendelezaji wa masoko ya madini; na • Ufuatiliaji na tathmini ya sekta ya madini. 	<ul style="list-style-type: none"> • kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya mfano vya uchenjuaji madini vya Katente (Bukombe) na Lwamgasa (Geita); • kukamilika kwa utafiti wa kina wa jiosayansi kwa lengo la kubaini uwepo na kiasi cha madini kinachopatikana katika maeneo sita (6) ya wachimbaji wadogo ya Kapanda (Mpanda), Buhemba (Musoma), Katente (Bukombe), Itumbi (Chunya), Kyerwa (Kagera) na Kange (Tanga); • kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne (4) vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni; • kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Mpango wa Utunzaji wa Mazingira; • kukamilika kwa ufungaji wa miundombinu ya umeme na taa katika jengo la Kituo cha Pamoja (one stop centre) Mirerani na kuendelea na ufungaji wa kamera za ulinzi (CCTV) kuzunguka

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		eneo la ukuta; • kuendelea na ujenzi wa vituo vya umahiri vya Songea, Mpanda na Chunya; na • kuendelea na ujenzi wa kituo cha uchenjuaaji madini cha Itumbi (Chunya).
Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia - TEITI	<ul style="list-style-type: none"> • Kuelimisha umma kuhusu matumizi ya takwimu za taarifa za TEITI katika kuhoji ufanisi wa ukusanyaji na mapato yanayotokana na rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia; na • Kuanzisha rejista ya taarifa na majina ya watu wanaomiliki hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia. 	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea na ukamilishaji wa taarifa ya TEITI ya mwaka 2016/17 na 2017/18; • kuelimisha umma kupitia redio na runinga kuhusu matumizi ya takwimu za taarifa za TEITI katika kuhoji ufanisi wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia ambapo zaidi ya wananchi 500 wameelimishwa; na • kuanzishwa kwa Rejesta ya Taarifa na majina ya watu wanaomiliki hisa katika kampuni 37 za madini, mafuta na gesi asilia.
KUFUNGAMANISHA MAENDELEO YA VIWANDA NA MAENDELEO YA WATU		
Elimu, Sayansi na Teknolojia		
Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu)	<ul style="list-style-type: none"> • Kununua magari 65 kwa ajili ya kuimarisha uthibiti ubora wa shule; • Kujenga ofisi 55 za wathibiti ubora wa shule; • Kununua magari 10 kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu; • Kutoa motisha kwa shule 400 za msingi na sekondari zilizoongeza kiwango cha ufaulu katika mitihani ya Taifa ya Darasa la Saba na Kidato cha Nne 2018; • Kutoa motisha kwa halmashauri 184 	<ul style="list-style-type: none"> • Kununuliwa kwa magari 39 na kusambazwa katika vyuo vyote vya ualimu vya Serikali; • Kuendelea kwa taratibu za ununuzi wa magari 65 kwa ajili ya kuimarisha uthibiti ubora wa shule pamoja na magari matano na Malori mawili kwa ajili ya Baraza la Mitihani la Taifa; • kuendelea na taratibu za ujenzi wa ofisi 55 za wilaya za uthibiti wa ubora wa shule ili kuimarisha mazingira ya utendaji kazi; • kuendelea na taratibu za ujenzi wa shule ya sekondari ya mfano jiji la Dodoma; • kuboresha miundombinu na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kukarabati Vyuo vya Ualimu 26 na kujenga

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>kutokana na utekelezaji wa vigezo vilivyokubalika kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kununua magari matano (5) na malori mawili (2) kwa ajili ya Baraza la Mitihani la Taifa; na • Ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya mfano mkoani Dodoma kwa ajili ya kidato cha 1 – 6. 	<p>upya chuo kimoja (1) kati ya vyuo 35 vya Serikali; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • kukamilisha ujenzi wa ofisi mpya 100 za Uthibiti Ubora wa Shule za Wilaya.
<p>Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi (MEM) –Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK)</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuandaa, kuchapisha na kusambaza vitabu vya mwanafunzi na kiongozi cha mwalimu kwa masomo yote vya darasa la VI na VII; • Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu; • Kugharamia matengenezo ya magari ya wathibiti ubora wa shule kwa ajili ya kazi za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Kiunzi cha uthibiti ubora wa shule; • Kuwezesha uendeshaji na uratibu wa Programu ya LANES na ukaguzi wa ndani na nje; • Kuwajengea uwezo waratibu wa Vituo vya Walimu; na • Kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum 	<ul style="list-style-type: none"> • Kubainishwa kwa shule zenye upungufu wa vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa ajili ya kufanya manunuzi kulingana na mahitaji; na • Kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa LANES awamu ya pili baina ya Serikali na Ubalizi wa Sweden.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Elimumsingi bila ada	<ul style="list-style-type: none"> • kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi bila ada 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi bila ada ambapo katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019, jumla ya shilingi bilioni 128 zimetolewa kugharamia elimumsingi bila ada ikijumuisha posho ya madaraka kwa walimu wakuu na maafisa elimu kata.
Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni - SWASH	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa miundombinu ya maji na vyoo katika shule za msingi 200; na • Kuendelea kutoa mafunzo kuhusu utumiaji wa mwongozo wa programu kwa wathibiti ubora wa shule na waratibu wa programu katika ngazi ya halmashauri. 	<ul style="list-style-type: none"> • kuwezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 9,712 (Wasichana matundu 5,539, Wavulana matundu 3,645 na Walimu matundu 528), miundombinu ya maji, matanki ya maji 911 pamoja na miundombinu ya kunawia mikono katika shule za Msingi 602.
Mamlaka ya Elimu Tanzania - TEA	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa nyumba 20 za walimu wa sekondari katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi; • Ujenzi wa madarasa 75 katika shule za Msingi na Sekondari zenye uhaba mkubwa wa madarasa; • Ujenzi wa mabweni 16 ya wanafunzi wa kike katika shule za sekondari; • Ujenzi wa vyoo katika shule 10 zenye upungufu mkubwa; ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na uboreshaji wa miundombinu katika vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu 2 vya Zanzibar; 	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 (madarasa matatu (3) kwa kila shule) katika shule za msingi 23 na shule za sekondari nne (4) zenye uhitaji mkubwa; • kuendelea na ujenzi wa mabweni matatu (3) katika shule 3 za msingi, ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa na chumba maalum (Audiology room); na • Kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa nyumba 40 katika shule 10 za sekondari ambazo ziko katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ukarabati wa majengo katika shule kongwe 4 za Sekondari za Serikali (Mwenge, Msalato, Nganza na Mzumbe); • Ukarabati wa shule za msingi 5 katika jiji la Dodoma; na • Ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa shule 10 za msingi na sekondari 	
Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga karakana tano (5) katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi katika mikoa ya Lindi (1), Pwani (1), Manyara (2) na ujenzi wa karakana ya "Mechatronics" katika chuo cha TEHAMA-Kipawa, Dar es Salaam; • Kujenga jengo la utawala, uzio na kufanya marekebisho katika bweni moja na madarasa mawili katika Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC); • Kujenga bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 200 katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Mkoa wa Mbeya; • Kujenga karakana ya mitambo mizito katika Chuo cha Ufundi Stadi cha 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma katika mikoa ya Kagera, Geita, Rukwa, Njombe na Simiyu; • Ujenzi wa vyuo 33 vya Wilaya za Buhigwe, Butiama, Chemba, Chunya, Ikungi, Igunga, Kishapu, Kwimba, Monduli, Mbarali, Mafia, Pangani, Ulanga, Uvinza, Kilindi, Korogwe, Longido, Masasi, Mkinga, Ukerewe, Uyui, Bahi, Iringa, Lushoto, Rufiji, Kongwa, Ruangwa, Nyasa, Chato, Karagwe, Ileje, Newala, Simanjiro; • Ujenzi wa karakana za uungaji vyuma katika vyuo vya ufundi stadi na huduma Pwani na Manyara na karakana za viyoyozi, majokofu na ubunifu na ushonaji wa mavazi katika Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Lindi; • Kufikiwa kwa asilimia 90 kwa kazi ya utengenezaji wa samani kwa ajili ya Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Kihonda, Morogoro na kazi ya ufundi bomba na uwashi katika chuo cha Lindi;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>Mwanza;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kujenga nyumba 10 za watumishi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Ulyankulu; • Ununuzi wa nyumba 10 za watumishi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Manyara; • Kujenga karakana katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro (MVTTC); na • Kununua vifaa vya kisasa kwa Vyuo vitatu vya Ufundi Stadi vya TEHAMA Kipawa-Dar es Salaam, Mtwara na Lindi. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa uunganishaji wa Mkongo wa Taifa kwa vyuo 27 vya mafunzo ya ufundi stadi kwa ajili ya kuimarisha teknolojia ya habari na mawasiliano; • Kukamilika kwa ujenzi wa vyuo nane (8) vya mafunzo ya ufundi stadi katika Wilaya za Kilindi (Mabalanga), Babati (Gorowa), Ngorongoro (Samunge), Urambo (Chekereni), Nkasi (Paramawe), Kasulu (Nyamidaho) Muleba (Ndolage), Itilima (Kanadi); • Ujenzi wa karakana ya zana za kilimo katika Chuo cha Ufundi Stadi Arusha; na • Kuendelea kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Chuo cha Ufundi Arusha kwa kujenga jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu.
<p>Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi na huduma vya mikoa ya Geita na Rukwa; • Kujenga mabweni mawili (2) katika chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro; • Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara, ugavi na ofisi za walimu katika Chuo cha Ufundi Arusha; 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro; • Kuendelea na Ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma vya Mikoa ya Geita, Simiyu na Rukwa; • Kuendelea na taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha Ufundi Stadi kwa Mkoa wa Njombe; • Kuendelea na ujenzi katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa kwa kujenga bweni, nyumba za watumishi, bwalo na Jengo la TEHAMA; • Kuendelea na ujenzi wa maabara na jengo la TEHAMA katika

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kulaza wanachuo 576, jengo la ghorofa 2 lenye madarasa 6 na ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 1,500, na jengo la jiko katika Chuo cha Ualimu Dakawa; • Kujenga nyumba nne (4) za walimu katika Chuo cha Ualimu Marangu; kujenga bweni la ghorofa moja (1), nyumba nane (8) za walimu na kukarabati jengo la utawala katika Chuo cha Ualimu Butimba; • Kujenga maabara ya ghorofa moja (1), bweni la ghorofa moja (1) kwa ajili ya wanafunzi 576 katika Chuo cha Ualimu Tabora; • Kujenga bwalo la chakula, bweni la ghorofa moja (1) la wanafunzi wa kike 176, maabara ya ghorofa moja (1) na nyumba mbili (2) za walimu katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa; • Kununua na kufunga vifaa kwa ajili ya programu ya vito na usonara katika Chuo cha Ufundi Arusha; na • Kununua na kufunga vifaa vya <i>Biomedical</i> katika maabara ya uhandisi ya ujenzi na umwagiliaji katika Chuo 	<p>vyuo vya ualimu vya Kleruu, Marangu na Butimba; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na upanuzi wa miundombinu katika Vyuo vya Ualimu vitano (5) ambavyo ni Mpwapwa, Kleruu, Marangu, Tabora na Dakawa.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	cha Ufundi Arusha.	
Ukarabati na Upanuzi wa Chuo cha Ufundi Arusha	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga bweni moja (1) la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 250; • Kuendelea na utafiti wa kuzalisha umeme Wilayani Mbulu chini ya ufadhili wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA); na • Kujenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 1,000 na bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 250. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa kituo cha mafunzo ya kufua umeme kwa kutumia nguvu ya maji cha Kikuletwa; • Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu; • Kutoa ushauri wa kitaalam katika usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi, upimaji wa udongo, upimaji lami na usanifu na ufungaji wa taa za kuongozea magari barabarani katika Jiji la Arusha. • Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kuzalisha umeme wa kW 70 na kuhudumia vijiji viwili vya Kwermusl na Amoa; na • kuendelea na utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa Nishati Jadidifu ambao kwa sasa umefikia asilimia 40.
Kuendeleza Elimu ya Ualimu	<ul style="list-style-type: none"> • Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa vyuo 35 vya ualimu; • Kununua vitabu vya rejea vya kielektroniki kwa ajili ya vyuo vya ualimu 35 na kusambaza vifaa vya TEHAMA; • Kutoa mafunzo ya TEHAMA na teknolojia saidizi kwa wakufunzi /walimu 150 wenye mahitaji maalum; • Kuboresha miundombinu ya TEHAMA katika vyuo vya ualimu na 	<ul style="list-style-type: none"> • Kununuliwa kompyuta 480, vifaa vya kudurufu 35, kompyuta mpakato 43 katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali; • Kuendelea na kazi ya usanifu kwa ajili uunganishaji wa Vyuo 35 vya Ualimu katika Mkongo wa Taifa kwa lengo la kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA; • Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga; • Kukamilika kwa mtaala wa elimu ya ualimu; • Kutolewa kwa mafunzo kazini kwa walimu 771 (Msingi 451 na Sekondari 320) katika Halmashauri 20 zenye ufaulu wa chini katika somo la Hesabu kwenye mitihani ya Kitaifa; • Kutoa mafunzo kazini kwa walimu 269 kutoka shule 23 za

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>kuviunganisha na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu cha Kabanga; • Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji 300 wa kitaifa kuhusu mtaala wa umahiri; • Kutoa mafunzo ya programu ya wakufunzi wa chuo kwa wakufunzi 1,300 wa vyuo vya ualimu; • Kutoa mafunzo ya Hisabati kwa walimu waliopo kazini katika halmashauri 20 zenye ufaulu hafifu; • Kuanzisha vituo vya kitaalam vya Hisabati na kuandaa vifaa vya mafunzo kwa somo la Hisabati; na • Kutoa mafunzo kwa walimu 500 (350 Msingi na 150 Sekondari) kuhusu lugha ya alama na mbinu sahihi za ufundishaji kwa wanafunzi viziwi 	<p>sekondari nchini;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kutoa mafunzo kazini ya TEHAMA na Teknolojia saidizi kwa Walimu 125 na Wakufunzi 9 wenye ulemavu; • Kununuliwa vifaa vya maabara za sayansi kwa vyuo 11 ili kuwawezesha walimu tarajali kujifunza kwa vitendo; • Kununua na kusambaza katika vyuo vya Ualimu vya Serikali aina 449 za vitabu zenye jumla ya nakala 25; • Kutoa mafunzo kazini ya TEHAMA kwa wakufunzi 530 wa kutoka katika vyuo 17 vya Ualimu; na • Kuandaa miongozo ya mafunzo ya TEHAMA na Teknolojia saidizi kwa Wakufunzi na Walimu wenye mahitaji maalumu (Competence Based Curriculum).
Kuimarisha Taasisi ya Elimu Tanzania	<ul style="list-style-type: none"> • Kuandika muhtasari wa kufundishia lugha ya Kichina kidato cha Tano na Sita ambayo inafundishwa katika shule za Sekondari 16; • Kuandaa mtaala na muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za msingi na sekondari za nchi za Afrika ya Kusini na nchi nyingine zitakazowasilisha 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchapishwa na kusambazwa kitabu cha kiongozi cha mwalimu (nakala 41,642) kwa Darasa la I na II na vitabu vya kiada vya elimu ya Awali ((nakala 719,905)) na moduli za mafunzo kazini katika Halmashauri zote nchini; • Kukamilika kwa uandishi wa vitabu 15 vya masomo ya sayansi (Fizikia, Kemia na Baiolojia), Kiswahili na <i>Basic Applied Mathematics</i> kwa kidato cha tano (5) na sita (6); • Kuandaa Mwongozo wa kufundishia Elimu ya Awali na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>maombi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuhuisha mtaala wa elimu ya sekondari ili uzingatie mahitaji ya wanafunzi viziwi; • Kuendelea na uandishi wa vitabu vya kiada kwa Darasa la VI, VII, Kidato cha I - VI na moduli kwa Elimu ya Ualimu pamoja na kuandaa maudhui ya kielektroniki; • Kuchapa vitabu vya kiada vya Darasa la VI - VII, Kidato cha I - VI na vitabu vya Elimu ya Ualimu; • Kurusha hewani vipindi vya Taasisi ya Elimu Tanzania vyenye kubeba maudhui ya kielektroniki kwa lengo la kukuza stadi za Kazi; • Kutoa mafunzo kazini kwa walimu wa shule za msingi (darasa la V - VII) kwa mtaala ulioboreshwa; na • Kuendelea kuandika vitabu vya hadithi kwa ajili ya shule za msingi. 	<p>miongozo mitano ya kufundishia kwa kutumia mbinu za michezo (Play and Learn);</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuchapishwa na kusambazwa kwa vitabu vya kiada kwa ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I - III kwa ajili ya shule zinazotumia lugha ya kiingereza; • Kuandaliwa kwa muhtasari wa kufundishia lugha ya kichina kwa kidato cha kwanza (1) hadi cha nne (4). • Kuchapa na kusambaza nakala 8,750 za vitabu vya kiada vya maandishi kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu; • Kuandaa na kusambaza nakala 272,000 za Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo yote nane (8); • Kuchapa na kusambaza nakala za vitabu 1,359,350 vya masomo yote kwa ngazi ya Elimu Awali na Msingi Darasa la I-V; • Kuandika vitabu vya kiada vya masomo 05 kwa Darasa la VI kwa shulezinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia; • Kuandika, kuchapa na kusambaza nakala 11,402 zavitabu vya kiada vya nukta nundu (Braille) aina 18 kwa Darasa la I, II, na V kwa ajili ya wanafunzi wasioona; • Kuchapa katika maandishi ya nukta nundu (braille); na • Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu kupitia huduma ya makataba mtandao (TIE- online library) ambapo wanafunzi wanapata vitabu vya kiada, ziada, na machapisho mengine ya TET kwa ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na vyuo vya Ualimu.
Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 450 kwa wanafunzi 128,285 ambapo wanafunzi 45,485 ni 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutolewa kwa mikopo ya Shilingi bilioni 266.43 kwa wanafunzi 130,072 ambapo wanafunzi 49,493 ni wa mwaka wa kwanza na 80,579 wanaoendelea na masomo;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>wa mwaka wa kwanza;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kukusanya Shilingi bilioni 221.5 kutoka kwa wanufaika ambao mikopo yao imeiva; • Kuanzisha na kuimarisha ofisi mbili (2) za kanda katika mikoa ya Mbeya na Mtwara; • Kuendeleza utekelezaji wa mkakati wa uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA ili kuunganisha mifumo ya Bodi ya Mikopo na ya wadau wengine; na • Kutekeleza kampeni za uelimishaji kuhusu huduma zinazotolewa na Bodi ya Mikopo, vigezo, utaratibu, wajibu wa wanufaika na waajiri katika urejeshaji wa mikopo. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukusanywa kwa mikopo iliyoiva ya thamani ya shilingi bilioni 95.13 sawa na asilimia 83.74 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 113.6; na • Kutambuliwa kwa wadaiwa wapya 14,731 wenye mikopo iliyoiva yenye thamani ya shilingi bilioni 100.7.
Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga hosteli mbili (2) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kila moja na maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja; na • Kuimarisha kitengo cha masomo ya uzamili, utafiti na huduma kwa jamii. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza kwa ujenzi wa hosteli mbili (2) za wanafunzi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kila moja na maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja; na • Kufanyika kwa ukarabati wa majengo ya zamani.
Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala; na • Kununua vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi 57 wenye 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala; na • Kuanza ujenzi wa maabara za sayansi na vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari ya mazoezi.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	mahitaji maalum pamoja na vifaa vya utafiti kwa wanataaluma.	
Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia	<ul style="list-style-type: none"> • Kukarabati miundombinu katika Kampasi ya Oswald Mang'ombe; na • Kukamilisha upatikanaji wa hati ya maeneo ya chuo hususan, Kisangura - Mugumu katika Wilaya ya Serengeti na Kinesi - Wilaya ya Rorya. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kupatikana kwa hatimiliki ya hekari 95 ya kampasi ya chuo ya Kinesi - Rorya; na • Kuandaliwa na kuidhinishwa kwa mitaala 29 ya masomo mbalimbali kwa ngazi ya Shahada ya kwanza.
Ujenzi na Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe	<ul style="list-style-type: none"> • Kuweka samani katika hosteli za wanafunzi Kampasi Kuu eneo la Maekani. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ukarabati wa hosteli mbili za wanafunzi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 256 katika Kampasi ya Mbeya; • Kukamilika kwa hosteli tatu Kampasi Kuu na nyumba kumi za watumishi; kuendelea na ujenzi wa madarasa Kampasi Kuu; na • Kuendelea na uwekaji wa samani katika majengo Kampasi ya Tegeta - Dar es Salaam.
Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Ardhi	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ardhi pamoja na kuweka samani, maabara itakayokuwa na matumizi zaidi ya moja, mabweni ya wanafunzi, ukumbi wa mihadhara, mifumo ya maji taka, na miundombinu ya TEHAMA; • Kukarabati karakana, madarasa, hosteli ya wanafunzi, bwalo la chakula na nyumba za watumishi; • Kuanza ujenzi wa jengo la usanifu majengo, kuandaa michoro ya ujenzi wa karakana, bwalo la chakula na kituo cha Afya; na 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa bwani la wanafunzi lenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 592.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kununua magari matatu (3), jenereta moja (1), samani na vifaa vya TEHAMA. 	
Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ujenzi wa kituo cha umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu katika Kampasi ya Mloganzila; na • Kukarabati kituo cha kufundishia na tafiti cha Bagamoyo. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu; na • Kufanya maboresho katika shule ya meno hususan chumba kwa ajili ya kutolea huduma binafsi.
Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja; na • Kujenga hosteli za wanafunzi. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa kafeteria moja kwa ajili ya kuongeza maeneo ya utoaji wa huduma ya chakula kwa wanafunzi na wafanyakazi katika kampasi ya Moshi; na • kukamilika kwa ujenzi wa ukuta wenye urefu wa mita 200.
Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga hosteli za wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kupatikana kwa Mshauri Elekezi na kuendelea na taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa hosteli za wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar.
Ujenzi wa Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha (NM - AIST)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja; na • Kutekeleza miradi 33 ya kitafiti na ubunifu kwa kufadhili wanafunzi na kulipa gharama za kiutafiti kwa wanafunzi na wanataaluma. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa hosteli kwa ajili ya wanafunzi 500; • Kuwezesha awamu ya pili ya ujenzi wa jengo miliki (estate building); na • Kuendelea kuboresha miradi ya utafiti katika kilimo, maji, TEHAMA na usalama wa chakula kama vile uzalishaji wa miche bora ya ndizi inayohimili magonjwa ya kitropiki na kuondoa sumu kuvu katika nafaka.
Jengo la Kufundishia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam -	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha upanuzi wa jengo la maktaba kwa kutumia mapato ya ndani 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanya upanuzi wa jengo la maktaba ili kuweza kuhudumia wanafunzi 450 kwa wakati mmoja;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
DIT	<p>lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuweka samani za ndani na miundombinu ya TEHAMA katika jengo la DIT Teaching Tower; na • Kuendelea kutafuta maeneo ya ardhi kwa ajili ya kuanzisha kampasi mpya mikoa ya Pwani na Jijini Dodoma. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuweka samani na miundombinu ya TEHAMA katika jengo la maktaba; • Kupima ubora wa vifaa vya ujenzi katika miradi miwili mikubwa ya kimkakati mradi wa kufua umeme wa maji (Julius Nyerere Hydropower) na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (standard gauge railway); • Kuratibu ujenzi wa mabweni manne (4) ya wanafunzi na majengo mawili (2) ya vituo vya umahiri katika kampasi za Mwanza na Dar es Salaam; • Ujenzi wa jengo la maabara ya Kompyuta, darasa na bwalo la chakula katika Kampasi ya Myunga; • Kukarabati miundombinu ya Kampasi ya Mwanza ikiwemo maabara na ununuzi wa mashine ya kuchakata na kutengeneza bidhaa za ngozi; na • Upanuzi wa jengo la maktaba (Vertical Extension of DIT Library) pamoja na kuweka samani na miundombinu ya TEHAMA katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam.
Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine - SUA	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga kumbi mbili (2) za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila mmoja, ukumbi mmoja (1) wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 1,000 na madarasa manne (4) yenye uwezo wa kuchukua watu 50 kila moja; • Kuendelea na ujenzi wa hosteli moja (1) Kampasi ya Solomon Mahlangu, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 700; 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la maabara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja ambao umefikia asilimia 90; • Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la utafiti wa wanyama na wadudu; • Kuendelea na ukarabati wa madarasa ambao umefikia asilimia 92; • Kuboresha shamba la Chuo kwa kupanda mazao ya Taifa ya kimkakati; • Kuanzishwa kwa kampasi mpya ya Mizengo Kayanza Peter

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga maabara mtambuka katika kampasi kuu; na • Kukarabati miundombinu iliyochakaa ikijumuisha vyumba 17 vya kufundishia, mabweni sita (6), nyumba 30 za watumishi na barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 10 katika Kampasi Kuu na Solomon Mahlangu na ofisi na madarasa Kampasi ya Tunduru na Kampasi kuu na Solomon Mahlangu. 	<p>Pinda katika kijiji cha Kibaoni, Katavi; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ukarabati wa karakana za uhandisi kilimo na kukamilika kwake kutawapa fursa wanafunzi kufanya mafunzo kwa vitendo.
<p>Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la maktaba lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja; • Kuanza ujenzi wa jengo la ukumbi wa mihadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa wakati mmoja; • Kuendelea kukarabati miundombinu ya majengo ya madarasa, hosteli na nyumba za watumishi; • Kufanya tathmini ya mali za wananchi katika eneo la Kitalu Na. 2 lenye hekta 511 (Mbeya Vijijini) litakalotumika kwa ajili ya upanuzi wa chuo; na • Kufanya tathimini ya mali za wananchi katika eneo ambalo limeainishwa kuongezwa katika kampasi ya Rukwa 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ambao umefikia asilimia 97; • Ukarabati wa ofisi za wafanyakazi wa Chuo; • Kuweka samani (viti) katika madarasa matano (5) ili kuboresha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	ili kufikia hekta 500	
Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha awamu ya kwanza na kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa kituo cha wanafunzi; • Kuanza ujenzi wa Ndaki ya Tiba za Afya - Mbeya; • Kufanya upanuzi wa hosteli za Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ghorofa mbili zaidi; • Kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la Kituo cha Afya cha Chuo; • Kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Shule Kuu ya Uchumi na ukarabati wa nyumba za walimu; • Kukarabati mabweni ya wanafunzi, barabara za ndani; na • Kuanza ujenzi wa jengo la ofisi na vyumba vya madarasa katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari pamoja na ujenzi wa jengo la Taasisi ya Sayansi za Bahari lililopo Buyuni Zanzibar. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa kituo cha huduma za kijamii kwa wanafunzi ambapo ujenzi umefikia asilimia 70; • Kukamilika kwa ukarabati mkubwa wa nyumba tano za watumishi; kukarabati bweni Na. I Kitalu G linalotumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalum lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 63; na • Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia ambao umefikia asilimia 50.
Kukuza Stadi za Kazi kwa Ajili ya Shughuli za Kuzalisha na Kukuza Uchumi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na utekelezaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za Kazi kwa kutoa ruzuku kwa ushindani kwa taasisi za mafunzo; 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na awamu ya pili ya ukarabati wa Vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi (FDC); • Kuanza ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika halmashauri za Ruangwa, Kongwa, Kasulu Mji na Nyasa;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi (VETA) katika halmashauri za Ruangwa, Kongwa, Kasulu TC na Nyasa; • Kukarabati vyuo vya maendeleo ya wananchi na kuvinunulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia; • Kuendelea na ukarabati wa vyuo 14 vya Maendeleo ya Wananchi; • Kutoa mafunzo ya uanagenzi katika vyuo vya Ufundi Stadi na Elimu ya Ufundi; na • Kuendelea na ujenzi wa chuo cha ufundi Dodoma chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 5,000 kwa wakati mmoja. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuwezesha vijana 2,534 kupata mafunzo ya uanagenzi katika Taasisi mbalimbali; na • Kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa watumishi 318 wanaosimamia stadi za ujuzi katika taasisi za TEA, TCU, NACTE, HESLB na VETA.
Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH	<ul style="list-style-type: none"> • Kugharamia miradi mipya 8 ya utafiti kulingana na vipaumbele vya utafiti vya Taifa; • Kuboresha mifumo ya ubunifu na kuwaendeleza wabunifu nchini ili waweze kujijiri; • Kubiasharisha matokeo ya utafiti nchini ili ziweze kutumika na kuleta tija kwa maendeleo ya nchi; • Kuandaa mfumo wa uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje, 	<ul style="list-style-type: none"> • Kubaini mahitaji ya bunifu na kutoa mafunzo katika nyanja za ulinzi miliki bunifu, ujasiriamali, ubiasharishaji na usimamizi wa mikataba kwa wabunifu 60 ambao ni washindi wa Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU); na • Kuendelea kugharamia uanzishaji wa kituo kimoja cha mfano kwa ajili ya uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>pamoja na uhakiki wa teknolojia zinazoibukia;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha mfumo wa udhibiti na utoaji vibali vya utafiti nchini; na • Kuendesha mafunzo, semina, mijadala, na mikutano mbalimbali kuhusiana na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. 	
<p>Ujenzi wa Maabara ya Mionzi ya Nguvu za Atomiki</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maabara ya Tume; • Kuanza ujenzi wa maabara za kanda ya Zanzibar na mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza; • Kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa kutengeneza madawa ya kuchunguza na kutibu saratani pamoja na kinu cha tafiti za kinyuklia; • Kupima kiasi cha mionzi katika sampuli 16,357 za vyakula na mbolea; na • Kuimarisha upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 50. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukaguliwa kwa migodi miwili ya Buzwagi ambayo iko kwenye hatua za mwisho za ufungwaji; • kukaguliwa na kuhakikiwa kwa vituo 384 vya vyanzo vya mionzi nchi nzima ambapo ukaguzi huo ulibaini kuwa vituo 369 vilikuwa vinaendeshwa kwa kufuata taratibu husika na vituo 15 vilikuwa vinatumia vyanzo vya mionzi bila kufuata utaratibu wa kiusalama; • Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maabara ya kupima mionzi; • Kufunguliwa kwa ofisi moja (1) ya mipakani katika wilaya ya Bagamoyo; • Kusajiliwa kwa vituo vipya 58 kwa ajili ya kuanza kutumia vyanzo vya mionzi na hivyo kufikia jumla ya vituo vya mionzi 985 vilivyosajiliwa; • Kupima sampuli 19,462 na kutoa vibali 29,613 vilivyojumuisha sampuli za vyakula 16,563, na mbolea 363 na sigara na matumizi mengine kama chakula cha mifugo zilikuwa sampuli 2,536; na • Kununua vifaa viwili (2) vya kupima mionzi (Sodium Iodide Detector) kwa ajili ya ofisi mbili (2) za kanda na vifaa vingine mbalimbali vya maabara kwa ajili ya ofisi 18 za mipakani ili

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		kusaidia kuongeza kasi ya utoaji wa vibali ndani ya siku moja ili kulinda usalama wa wananchi.
Upanuzi na Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDCs	<ul style="list-style-type: none"> Kujenga na kukarabati miundombinu katika vyuo 34 vya maendeleo ya wananchi na ununuzi wa vifaa vipya vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia. 	<ul style="list-style-type: none"> Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi; na Kuendelea na awamu ya pili ya ukarabati wa vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs).
AFYA NA MAENDELEO YA JAMII		
Mradi wa Kupunguza Vifo vya kina Mama Vinavyotokana na Uzazi	<ul style="list-style-type: none"> Kujenga vituo 12 vya damu salama katika Mikoa 12; Kukarabati na kujenga wodi maalum kwa ajili ya watoto wachanga (<i>Neonatal Care Units</i>) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 7; na Kufanya upanuzi wa wodi za wazazi na kutenga vyumba vya wagonjwa mahututi wanaotokana na uzazi katika hospitali za Rufaa za mikoa 5. 	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi wa kituo cha damu salama katika mkoa wa Njombe; Kuendelea na ukarabati wa vituo vya afya kwa ajili ya kuboresha huduma za uzazi ikiwemo huduma ya upasuaji katika vituo vya afya vya Bunju (Kinondoni MC), Mbande (Kongwa DC), Mtera (Mpwapwa DC), Katoro (Geita DC), Ilemela (Chato DC), Mogitu (Hanang' DC), Masinono (Msoma DC), Magoma (Tarime DC), Kisasi (Morogoro DC), Kibila HC (Magu DC), Msanga (Kisarawe DC), Chibumanga (Manyoni DC), Shelui (Iramba DC) na Nyahua HC (Sikonge DC).
Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa	Ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za tiba katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, kuanzishwa na kuboresha vitengo vya dharura (Emergency Units) katika Hospitali za Rufaa za mikoa, ujenzi wa hospitali mpya za mikoa katika mikoa ya Katavi, Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Mara.	<ul style="list-style-type: none"> Kuboreshwa kwa miundombinu ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na mtandao kiambo katika hospitali sita (6) za rufaa za mikoa (Temeke, Geita, Njombe, Dodoma, Bombo na Mbeya); Kuendelea na ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma katika hospitali za mikoa ya Mara (Kwangwa), Mwanza (Sekou Toure), Mbeya, Ruvuma (Songea), Lindi (Sokoine), Mtwara (Ligula), Kilimanjaro (Mawenzi), Arusha (Mount Meru), Manyara, Tabora (Kitete),

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<p>Pwani (Tumbi), Singida, Shinyanga na Dar es Salaam (Mwananyamala). Aidha, katika mikoa mipya ya Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Katavi ujenzi wa Hospitali za Rufaa unaendelea katika hatua mbalimbali ambapo kwa mikoa ya Njombe, Geita na Simiyu huduma zimeanza kutolewa; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa majengo ya huduma za dharura katika hospitali za rufaa za mikoa ya Songwe, Mawenzi, Njombe, Tabora, Sumbawanga, Songea na Mbeya.
Ujenzi wa Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa hospitali za wilaya (67); na • Kuendelea na upanuzi na ukarabati wa vituo vya afya ili kuviongezea ubora ikiwemo uwezo wa kufanya upasuaji wa akina mama wenye uhitaji ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto vitokanavyo na uzazi. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa Hospitali mpya za Wilaya 71 zikijumuisha hospitali tatu za Uhuru (Dodoma), Mji wa Tunduma (Songwe) na Manispaa ya Ubungo (Dar es Salaam) ambapo utekelezaji katika baadhi ya hospitali umefikia asilimia kati ya 50 hadi 90, baadhi ya halmashauri ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji ikijumuisha kupaka rangi, kuunganisha umeme, maji na kuweka milango na madirisha. Aidha, ujenzi wa vituo vya afya 133 umekamilika.
Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Dawa	Kununua na kusambaza Dawa, Chanjo, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi kwa ajili ya Vituo vya Umma vya kutolea huduma za afya nchini.	<ul style="list-style-type: none"> • Bohari Kuu ya Dawa imeendelea kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kwa kutumia Mfumo wa Ugavi ujulikanao kama Ugavi Shirikishi. Hadi Desemba 2019, asilimia 99 ya vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za Afya vimesambaziwa dawa na vifaa tiba muhimu;
Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya	Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa la kufungwa kwa vifaa vya uchunguzi vya X – ray na kununua vifaa tiba	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ghorofa mbili (2) la huduma za uchunguzi wa mionzi (Radiolojia) na kuanza kutumika; na • Kuendelea na ujenzi wa jengo la wazazi.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu - Kibong'oto	<ul style="list-style-type: none"> • Kununua mashine ya CT - SCAN kwa ajili ya uchunguzi wa kifua kikuu; na • Kujenga mtambo wa kuzalisha hewa ya Oxygen. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa michoro ya eneo itakapowekwa mashine ya CT - Scan na taratibu za ununuzi zinaendelea; • Kununuliwa kwa mashine nne (4) za uchunguzi wa madhara yatokanayo na dawa na mashine moja ya <i>ultrasound</i> kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa; • Kutolewa mafunzo ya kudhibiti magonjwa ambata ya Kifua Kikuu na Kisukari kwa wataalam 89 katika mikoa mitatu ya Iringa, Dar es Salaam na Kilimanjaro; na • Kukabidhi mashine 27 aina ya HbA1c Analyser kwa vituo vya afya 27 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa wenye magonjwa ambata ya Kifua Kikuu na Kisukari.
Hospitali ya Rufaa Bugando	kuendelea na awamu ya pili ya Mradi wa Saratani kwa kujenga wodi ya kulaza wagonjwa wa Saratani.	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na awamu ya pili ya mradi wa Saratani kwa kujenga wodi ya kulaza wagonjwa wa Saratani ambapo mkandarasi ameanza maandalizi ya kupeleka vifaa eneo la mradi (mobilization); • Kuanza kuzalisha maji tiba ambapo chupa 38,000 za maji tiba ya aina tisa tofauti za ujazo wa nusu lita kwa kila moja zimezalishwa; na kuzalisha mitungi 11,098 ya <i>oxygen</i> kupitia mitambo miwili iliyofungwa hospitalini.
Mradi wa Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza	kununua na kusambaza chanjo kulingana na mahitaji ya nchi kwa ajili ya kuwakinga watoto chini ya mwaka mmoja; na kuimarisha huduma za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza.	<ul style="list-style-type: none"> • Ununuzi na usambazaji wa chanjo na vifaa vya kutolea huduma za chanjo nchini kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa ya kuambukiza kama vile Surua, Dondakoo, Ugonjwa wa kupooza; • Kutolewa chanjo ya kukinga ugonjwa wa Polio na chanjo ya PENTA-3 inayozuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini na Homa ya Uti wa Mgongo kwa watoto 1,027,566 wenye umri chini ya mwaka mmoja, sawa na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		asilimia 98 ya lengo; <ul style="list-style-type: none"> • Watoto 8,082,861 walipata chanjo ya kuzuia ugonjwa wa Surua na Rubella sawa na asilimia 112; na • Watoto 4,040,654 sawa na asilimia 114 wamepatiwa chanjo ya kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa nchi nzima kupitia kampeni ya Chanjo ya Kuzuia Surua na Ugonjwa wa Kupooza.
Hospitali ya Taifa ya Muhimbili - MNH	Kuendelea na ujenzi wa jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa wa kulipia	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la watoto wanaohitaji uangalizi maalum ikijumuisha watoto njiti, watoto wachanga siku 0 - 28 (Neonatal ICU), na ICU ya watoto (Peadriatic ICU); • Kukamilika kwa mchoro wa jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa binafsi (Private wing); • Kuendelea na mradi wa ujenzi wa jengo la kuwahudumia wagonjwa wenye magonjwa ya kuambukiza (Isolation Unit) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; • Kukamilika kwa upanuzi wa jengo la Huduma za Dharura (EMD) kwa kuweka mashine na vitendea kazi; • Kugharamia mafunzo ya shahada za uzamili katika tiba kwa wataalam 81; • Kuendelea na maandalizi ya kuanzisha huduma za kupandikiza uloto (bone marrow transplant) ambapo mashine na vitendea kazi vya kutolea vimenunuliwa; • Kupandikizwa figo wagonjwa 8 na kufikia jumla ya wagonjwa 51 ambao wametibiwa tangu Hospitali ianze kutoa huduma hiyo • Kupandikizwa vifaa vya usikivu kwa wagonjwa 9 na kufikia jumla ya wagonjwa 30 waliopata matibabu tangu huduma hii ianze kutolewa

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> • Kupatiwa huduma ya matibabu kwa wagonjwa 133 ya “interventional radiology” ili kuruhusu upasuaji wa shingo na kichwa, kuondoa uvimbe kwenye sehemu ya kinywa, uso na shingo, kuweka mirija kwenye figo, kuzibua mirija ya nyongo iliyoziba, kuzibua mirija ya uzazi na kuondoa usaha ndani ya tumbo. Hadi sasa jumla ya wagonjwa 691 wamepatiwa huduma hiyo tangu ilipoanza kutolewa Oktoba 2017.
Taasisi ya Mifupa Muhimbili - MOI	<ul style="list-style-type: none"> • Kulipa mkopo wa ujenzi kutoka NHIF • Kununua mitambo, vifaa tiba vya kisasa na vipandikizi kwa ajili ya jengo jipya • Kuwaongezea ujuzi wataalam wa upasuaji 	<ul style="list-style-type: none"> • kukamilika chumba cha wagonjwa wenye uangalizi maalum na kuweka vitanda vipya na vya kisasa 16 na monita zake; • Kufungwa kwa vifaa vya kisasa kwa kiwango cha kimataifa katika kitengo cha wagonjwa mahututi; • Kuendelea kujenga chumba maalum cha kisasa kwa ajili ya kufanya matibabu ya ubongo kupitia mishipa ya damu (Angio Suite) na mitambo ya kisasa kwa ajili ya huduma hiyo tayari imenunuliwa; kupelekwa kwa madaktari watatu (3) na wauguzi wawili (2) kupata mafunzo maalum ya kutumia mitambo na teknolojia ya Angio Suite nchini China; na • Kuwasili kwa mitambo ya maabara ya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu (Angio Suite) nchini kutoka Ujerumani.
Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete - JKCI	Kununua vifaa tiba	<ul style="list-style-type: none"> • kutolewa matibabu kwa wagonjwa 610 kwa kufanyiwa upasuaji wa moyo kupitia tundu dogo kwa kutumia mtambo maalum “Catheterization Laboratory”; na upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na upasuaji wa mishipa ya damu kwa wagonjwa 289, ambapo 140 walikuwa watu wazima na 149 watoto. • Kuanza kwa upembuzi yakinifu wa mradi wa kupanua eneo la Mlongazila awamu ya pili kwa ajili ya wagonjwa wa moyo

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		nchini.
Ukarabati na Ujenzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii	kukarabati majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Mlale, Uyole na Misungwi	<ul style="list-style-type: none"> kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa hosteli za wasichana na wavulana, mabwalo, nyumba za watumishi, maktaba na miundombinu ya umeme, vyoo na maliwato katika vyuo vinne vya Maendeleo ya Jamii vya Ruaha, Misungwi, Monduli na Uyole; Kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Kidigitali cha Ubunifu katika Chuo cha Misungwi.
Programu ya Kuwezesha Wanawake Kiuchumi	<ul style="list-style-type: none"> Kuratibu na kuhamasisha utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake. 	<ul style="list-style-type: none"> Kutoa Shilingi 3,890,123,401 kwa wanawake wajasiriamali 14,295 kutoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri; Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali kupitia Dirisha la Wanawake lililoanzishwa katika Benki ya Posta Tanzania (TPB) ambapo mikopo yenye thamani ya Shilingi 3,586,400,000.00 imetolewa kwa wanawake wajasiriamali 14,271.
Maendeleo ya Awali ya Mtoto	<ul style="list-style-type: none"> Kutokomeza ukatili dhidi ya watoto katika mikoa yote nchini; Kutoa elimu ya malezi chanya kwa jamii ili kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto; Kuanzisha vikundi vya malezi 	<ul style="list-style-type: none"> kuanzishwa kwa vikundi vya malezi 1,186 kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii katika kuzuia ukatili dhidi ya watoto; Kuanzishwa kwa madawati 18 Shule za Msingi na madawati nane (8) Shule za Sekondari katika Mkoa wa Rukwa kwa ajili ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto; Kuanzishwa kwa vituo 126 vya kijamii vya malezi na makuzi

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>chanya kwa watoto; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa mabaraza ya watoto katika mikoa na halmashauri. 	<p>ya awali ya watoto wadogo; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuandaa Taarifa ya Sita (6) ya Nchi ya Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto - CRC.
<p>Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha miundombinu katika makazi ya wazee, mahabusu za watoto na makao ya watoto; • Kuwezesha upatikanaji wa vitambulisho vya matibabu kwa wazee; • Kuwezesha huduma za msingi kwa watoto walio katika mazingira hatari, walio katika mkinzani na sheria waliopo katika makao ya Taifa ya Watoto Kurasini, Shule ya Maadilisho ya Irambo, na watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani; • Kuwezesha huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza walio katika makazi 17 ya wazee; • Kutoa usuluhishi wa migogoro ya ndoa katika familia; • Kuwezesha upatikanaji wa huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana; • Kuwezesha huduma za malezi ya 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutambuliwa kwa watu wa kuaminika 295 ili kuimarisha mfumo wa ulinzi na usalama wa watoto walio katika mazingira hatari, ambapo jumla ya watoto 527 walio katika mazingira hatari wanalelewa na watu wa kuaminika; • Kujenga uwezo kwa Maafisa Ustawi wa Jamii kutoka katika Halmashauri 15 kuhusu Mfumo wa Kieletroniki wa Takwimu za Watoto walio katika mkinzani wa sheria; na • Kuboreshwa kwa viashiria muhimu kutoka katika mfumo wa kieletroniki wa utoaji wa taarifa kwa kuandaa <i>Score Card</i> kwa lengo la kutoa taarifa muhimu juu ya watoto walio katika mazingira hatari na watoto waliokinzana na sheria.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>kambo na kuasili kwa watoto walio katika mazingira hatarishi; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kusajili makao ya watoto walio katika mazingira hatarishi. 	
Mradi wa Kupunguza Vifo vya kina Mama Vinavyotokana na Uzazi	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga vituo 12 vya damu salama katika Mikoa 12; • Kukarabati na kujenga wodi maalum kwa ajili ya watoto wachanga (<i>Neonatal Care Units</i>) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 7; na • Kufanya upanuzi wa wodi za wazazi na kutenga vyumba vya wagonjwa mahututi wanaotokana na uzazi katika hospitali za Rufaa za mikoa 5. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya Afya na kununuliwa kwa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji katika mikoa ya Mara (7), Mwanza(6), Simiyu(6) na Geita (6); na • Kuendelea na ujenzi wa kituo cha damu salama katika mkoa wa Njombe ambapo ujenzi umefika hatua ya kupaua.
Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa	Ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za tiba katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, kuanzishwa na kuboresha vitengo vya dharura (Emergency Units) katika Hospitali za Rufaa za mikoa, ujenzi wa hospitali mpya za mikoa katika mikoa ya Katavi, Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Mara.	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboreshwa kwa miundombinu ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na mtandao kiambo katika hospitali sita (6) za rufaa za mikoa (Temeke, Geita, Njombe, Dodoma, Bombo na Mbeya); • Kuendelea na ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma katika hospitali za mikoa ya Mara (Kwangwa), Mwanza (Sekou Toure), Mbeya, Ruvuma (Songea), Lindi (Sokoine), Mtwara (Ligula), Kilimanjaro (Mawenzi), Arusha (Mount Meru), Manyara, Tabora (Kitete), Pwani (Tumbi), Singida, Shinyanga na Dar es Salaam (Mwananyamala). Aidha, katika mikoa mipya ya Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Katavi ujenzi wa hospitali za rufaa unaendelea ambapo kwa mikoa ya Njombe, Geita na Simiyu huduma zimeanza kutolewa; na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi wa majengo ya huduma za dharura katika hospitali za rufaa za mikoa za Songwe, Mawenzi, Njombe, Tabora, Sumbawanga, Songea na Mbeya.
Ujenzi wa Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi wa hospitali za wilaya 71; na Kuendelea na upanuzi na ukarabati wa vituo vya afya ili kuviongezea ubora ikiwemo uwezo wa kufanya upasuaji wa akina mama wenye uhitaji ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto vitokanavyo na uzazi. 	<ul style="list-style-type: none"> Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya afya 133; Kuendelea na ujenzi wa Hospitali mpya za Wilaya 71 zikijumuisha hospitali tatu za Uhuru (Dodoma), Mji wa Tunduma (Songwe) na Manispaa ya Ubungo (Dar es Salaam) ambapo utekelezaji katika baadhi ya hospitali umefikia asilimia kati ya 80 hadi 99, baadhi ya Halmashauri ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji ikijumuisha kupaka rangi, kuunganisha umeme, maji na kuweka milango na madirisha.
Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Dawa	Kununua na kusambaza Dawa, Chanjo, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi kwa ajili ya Vituo vya Umma vya kutolea huduma za afya nchini.	<ul style="list-style-type: none"> Usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo hadi Machi, 2020 asilimia 91.4 ya vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za Afya vilisambaziwa dawa na vifaa tiba muhimu; na Kununuliwa na kusambazwa kwa mashine 4 za X-ray za kidigitali katika hospitali za rufaa za Manyara, Mt. Meru (Arusha), Songwe na Mwananyamala (Dar es Salaam).
Taasisi ya Saratani Ocean Road	Ununuzi wa vifaa tiba.	<ul style="list-style-type: none"> Kununuliwa kwa majokofu manne (4) kwa ajili ya maabara; kufunga mashine mpya yenye uwezo wa kupima vipimo vya kemia; Kununuliwa kwa mashine tisa (9) za oksijeni concentrators kwa ajili ya wagonjwa wanaolazwa wakiwa na wenye uhitaji maalum wa hewa ya oksijeni; Kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa wodi ya kulaza wagonjwa wa saratani;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa vipimo vya radiolojia 9,897 ikiwa ni sawa na asilimia 141.4 zaidi ya lengo kwa mwaka; • Kufanyika kwa uchunguzi na tiba za dawa ya nyuklia kwa kutumia mashine za Gamma Camera; • Kununuliwa kwa mashine za kuchunguza matokeo ya tiba ya saratani kwa njia ya damu (tumor markers); • Kutibu wagonjwa 22,462 kwa kutumia tiba za mionzi na kemia, wagonjwa 14,384 tiba kemia na wagonjwa 21,362 walipata tiba ya kemia na mionzi; • Kutoa mafunzo kwa Wanafunzi 52 kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Mionzi; na • Kuendelea na ukarabati wa miundombinu ikiwemo mfumo wa majitaka ya jengo la wodi, stoo ya dawa maalum, dawa za tiba ya saratani katika wodi ya tiba kemia.
Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya	Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa la kufungwa kwa vifaa vya uchunguzi vya X – ray na kununua vifaa tiba.	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi na kuanza kutumika kwa jengo la ghorofa mbili (2) la huduma za uchunguzi wa mionzi (Radiolojia); • Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa jengo la kutolea huduma za dharura; na • Ujenzi wa jengo la wazazi umefikia asilimia 50.
Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini - Mtwara	Kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje.	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa awamu ya pili ya jengo la wagonjwa wa nje (OPD) umefikia asilimia 45.
Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC)	<ul style="list-style-type: none"> • Ununuzi wa vifaa tiba • Ujenzi wa wodi maalumu za wagojwa wa saratani. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kununuliwa na kufungwa kwa mitambo mipya ya MRI, CT scan, Digital X-ray ambapo hadi februari, 2020 wagonjwa 670 walifanyiwa vipimo vya MRI, wagonjwa 4,137 vipimo vya CT Scan, wagonjwa 12,502 vipimo vya Ultrasound na wagonjwa 12,754 vipimo vya X-ray;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> • Kunuliwa kwa kinu cha kufua hewa ya Oksijeni chenye uwezo wa kuzalisha mitungi 400 kwa siku; • Ujenzi wa wodi maalumu ya wagonjwa wa saratani umefikia asilimia 70; na • Ujenzi wa vyumba vinne vya upasuaji umefikia asilimia 50.
MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA		
Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa mabwawa makubwa ya Kidunda (Morogoro), Farkwa (Dodoma), Ndembera (Iringa) na Dongo (Manyara); • Kuandaa na kutekeleza mipango ya utunzaji wa vyanzo vya maji katika mabonde ya maji nchini; • Kukusanya taarifa za rasilimali za maji na kuandaa mahitaji ya mfumo wa kielektroniki wa rasilimali za maji; na • Kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde ya maji. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutambuliwa kwa vyanzo 35 vya maji; kuweka mipaka katika vyanzo 22 vya maji na kutangazwa kwa vidakio 6 vya maji katika gazeti la Serikali; • Kupandwa kwa miche 16,400 ya miti rafiki ya maji na kuundwa kwa jumuiya 13 za Watumia Maji; • Kuanza maandalizi ya ujenzi wa bwawa la Farkwa ambapo wananchi 2,612 kati ya 2,868 wanaostahili fidia wamelipwa; na • Kukarabatiwa kwa vituo 53 vya kukusanyia takwimu za rasilimali za maji.
Kuimarisha Huduma za Ubora wa Maji	<ul style="list-style-type: none"> • Kuwezesha maabara 16 kufanya kazi kwa kununua kemikali na kutekeleza mkakati wa teknolojia ya kutoa madini ya <i>fluoride</i> kwenye maji. • Kuendelea kutekeleza mipango ya usalama wa maji yanayosambazwa mijini na vijijini ambapo jumla ya sampuli 4,713 za maji safi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ukarabati, ujenzi na uimarishaji wa ofisi za maji za mabonde na maabara za maji ikijumuisha Bonde la Kati (asilimia 99), Ruvuma na Pwani ya Kusini (asilimia 95), Ziwa Rukwa (asilimia 70), Ziwa Nyasa (asilimia 65), Rufiji Makao Makuu (asilimia 30), Rufiji Kimani na Mkoji (asilimia 85) na Wami-Ruvu (asilimia 60); • Kukusanywa na kuhakikiwa usalama kwa sampuli za maji 2,667 ambapo asilimia 95.8 zilikidhi viwango vinavyokubalika;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	zilichunguzwa kati ya sampuli 10,000 zilizokusanywa	<ul style="list-style-type: none"> • Kusambazwa kwa mitambo 200 ya kuondoa madini ya <i>Fluoride</i> katika maji ya kunywa na kupikia kwa kutumia chengachenga za mkaa wa mifupa ya Ng'ombe katika Mkoa wa Manyara maeneo ya Minjingu na Olasiti itakayonufaisha wananchi wapatao 1,600.
Mradi wa Maji wa Kimbiji na Mpera	Kukamilisha uchimbaji wa visima 20 vya Kimbiji na Mpera na kuendelea na utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo ya Kimbiji na Mpera.	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa visima 19 kati ya 20 vilivyopangwa kuchimbwa katika eneo la Kimbiji na Mpera; na • Kuanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza huduma ya maji kwa wananchi kutoka katika visima vitano (5) vya awali vya Kimbiji.
Kuboresha Huduma za Maji Vijijini	Kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea; pamoja na kukarabati miradi ya maji na kujenga vituo vipya vya kuchotea maji vijijini katika kila Halmashauri.	Kuendelea na utekelezaji wa miradi 802 ya huduma za maji ambapo kati ya miradi hiyo, miradi 75 imekamilika na imeanza kutoa huduma za maji kwa wananchi.
Mradi wa Maji Kahama - Nzega - Tabora	<ul style="list-style-type: none"> • kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye Miji ya Tinde, Nzega, Igunga, Uyui, Tabora na Sikonge pamoja na Vijiji vilivyopo kando kando ya bomba kuu. • kupeleka maji katika vijiji 33 vya nyongeza 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ulazaji wa mabomba makubwa ya kusafirisha maji kutoka Kijiji cha Solwa - Nzega, Nzega - Tabora na Nzega - Igunga kwa umbali wa kilomita 290.7; • Kukamilika kwa ujenzi wa matanki 17 • Ulazaji wa mabomba ya matawi umefikia asilimia 86; na • Ulazaji wa mabomba ya usambazaji mijini na vijijini umefikia asilimia 98.6.
Mradi wa Maji Masasi - Nachingwea	<ul style="list-style-type: none"> • kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Masasi - Nachingwea pamoja na uunganishaji wa wateja na • ujenzi wa vituo vya kuchotea maji. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ukarabati wa mradi ambapo wananchi 24,077 wanapata huduma ya maji; • kukamilika kwa taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kutibu na kusafisha maji.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • ujenzi wa mtambo wa kutibu maji 	
Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Usambazaji wa Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa	Kuboresha huduma za maji katika miji ya Kigoma, Lindi, Babati, Mwanza, Lamadi, Misungwi, Magu, Geita, Morogoro, Arusha, Dodoma, Tanga, Mtwara na Shinyanga.	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kwa ujenzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa mipya ambapo Geita umekamilika, Njombe (asilimia 95); Songwe (asilimia 95); Kigoma (asilimia 93); • kukamilika kwa rasimu ya usanifu wa kina wa miundombinu ya kuboresha huduma za maji jijini Dodoma; na • kukamilika kwa mradi wa usambazaji wa maji katika mji wa Serikali.
Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha maji, ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji, mtambo wa kusafisha maji na matenki; na • Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika mji wa Mwanga. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kwa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji ambapo katika miji ya Same utekelezaji umefikia asilimia 73 na Mwanga asilimia 38; na • ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji umefikia asilimia 81.
Maji kutoka Ziwa Victoria – Shinyanga na Kahama	Kutekeleza miradi inayolenga kuboresha huduma ya maji katika miji ya Kagongwa, Isaka, Magu, Sumve, Malya, Lagangabilili, Busega, Bariadi, Mwanhuzi, Kolandoto na Maganzo	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ulazaji wa bomba la kusambazaji maji katika miji ya Isaka, Tinde na Kagongwa; na • Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji katika vijiji vya Mwasekagi na Mwakatola.
Kuboresha Huduma za Maji Dar es Salaam	<ul style="list-style-type: none"> • ukarabati wa miundombinu ya usambazaji maji ili kupunguza upotevu wa maji; • ujenzi, ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji wa majisafi; 	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea na usambazaji wa maji kutoka mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini katika jiji la Dar es salaam na maeneo ya Bagamoyo, Kibaha na Mlandizi; • kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa dira za maji pamoja na vifaa vya uboreshaji wa huduma za maji;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • ujenzi wa mfumo wa maji kutoka Kibamba hadi Kisarawe; • Kukamilisha malipo ya mradi wa maji wa Ruvu Chini; • Kuanza mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam; na • Upanuzi wa mtambo, ulazaji wa bomba kuu la kusambaza maji, ujenzi wa matanki na kulipa fidia kwa wananchi. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa bomba la maji kutoka Kibamba kwenda Kisarawe ambapo utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 74; • Ukamilika kwa ufungaji wa mita mpya 8,022 na matengenezo ya mita 5,231; na • Ubadilishaji wa mabomba ya zamani kilomita 62 na kuongeza mtandao wa usambazaji.
VIJANA NA AJIRA		
Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha nguvu kazi iliyo katika Soko la ajira kiujuzi ili kuwezesha kufikiwa kwa uchumi wa viwanda kwa kuongeza ufanisi na tija katika uzalishaji mali na utoaji wa huduma; na • Kuwezesha vijana kujiajiri au kuajirika katika soko la ndani na nje na hivyo kufikia mahitaji ya nchi ya uchumi wa kipato cha kati 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutolewa kwa mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa vijana 8,900 kupitia teknolojia ya kitalu nyumba ambapo Vitalu Nyumba vya Mafunzo 87 vimejengwa katika Halmashauri 84 za Mikoa 12 nchini na mafunzo ya ujasiriamari kwa vijana 1,390 kwa lengo la kuwapatia ujuzi ili waweze kujiajiri na kuajiriwa; • Kutolewa kwa mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo kupitia watathmini kutoka vyuo vya ufundi visivyomilikiwa na VETA (asilimia 65), watathmini kutoka vyuo vya VETA (asilimia 31) na watathmini (asilimia 3) kutoka maeneo ya kazi hususan Viwandani; • Kutolewa kwa mafunzo ya ujuzi utokanao na maendeleo ya teknolojia na mbinu mpya za uzalishaji na utendaji kazi kwa wafanyakazi 450 waliopo sekta rasmi kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania; na • Kutolewa kwa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wa elimu ya juu 2,297 mahali pa kazi katika fani mbalimbali ikiwemo katika

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		Mamlaka ya Mapato Tanzania.
Mfuko wa Maendeleo ya Vijana	<ul style="list-style-type: none"> • Kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu; • Kuimarisha utoaji wa Mikopo kwa Vijana mmoja mmoja au vikundi vya uzalishaji mali ili kukuza mitaji kwa ajili ya kuimarisha au kuanzisha miradi mipya ya kiuchumi inayowawezesha kupata kipato na hivyo kujitegemea kwa kujiajiri wenyewe. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutolewa kwa mikopo nafuu kwa miradi 46 ya vikundi vya vijana katika Halmashauri za wilaya 184 Tanzania Bara; • Kuendelea na ufuatiliaji, tathmini na usimamizi wa SACCOS; na • Kukamilika kwa mapitio ya Mwongozo Sanifu wa Stadi za Maisha kwa vijana walio nje ya mfumo wa elimu.
HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO		
Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha Chaneli ya Utalii kwa kununua vifaa na mitambo vikiwemo kamera za kawaida, kamera maalum magari na vifaa vingine muhimu kwa ajili ya kuandaa vipindi maalum vya utalii ndani ya hifadhi na maeneo ya vivutio; • Kuboresha mifumo ya TEHAMA ya utangazaji wa redio na televisheni kwa kuunganisha katika Mkongo wa Taifa ili kuongeza ufanisi katika urushaji wa matangazo; na • Ununuzi wa vifaa vya utangazaji pamoja na mitambo ya kurushia matangazo mubashara. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kununuliwa kwa vifaa kwa ajili ya Chaneli ya Utalii zikiwemo kamera (12), Drones (2), Kompyuta mpakato maalum mbili (2), na vifaa vya kurushia matangazo mubashara (Transmitter 2); • Kununuliwa kwa magari mawili (2) na kuyafanyia marekebisho maalum ili yaendane na matakwa ya uandaaji wa vipindi vya utalii maeneo ya hifadhi; • Kuingizwa katika kisimbuzi cha DSTV Chaneli ya Tanzania Safari; • Kupokelewa na kufungwa kwa vifaa kwa ajili ya mfumo wa TEHAMA; na kukamilika kwa ukarabati wa jengo la studio; • Kupatikana kwa mtaalam wa kusaidia kuweka maelezo ya makala na filamu kwa tafsiri ya lugha mbalimbali za kimataifa; na • Kukamilika kwa maainisho ya kiufundi ya maeneo yote yatakayojengwa mitambo ya kurushia matangazo ya redio.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Habari kwa Umma	<ul style="list-style-type: none"> • Kuhabarisha Umma kuhusu utekelezaji wa sera na kazi za serikali; na • Kuhabarisha umma kuhusu maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuhabarisha Umma kupitia vyombo vya habari mbalimbali vikiwemo redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii kuelezea mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na • Kununuliwa kwa vifaa mbalimbali vya kukusanya, kuchakata na kutoa habari kwa Umma.
HIFADHI YA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI		
Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendeleza uhifadhi endelevu wa bonde la Ziwa Nyasa 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanyika kwa warsha ya kukuza uelewa wa usimamizi endelevu wa ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa; • Kupatiwa mafunzo kwa vikundi vya wakulima kuhusu uandaaji wa bustani za miche ya miti, utengenezaji wa mizinga ya nyuki na uhifadhi wa misitu; • Kupatiwa mafunzo kwa vikundi vya wakulima katika kijiji cha Utengule kuhusu njia bora za kilimo cha ngano katika chuo cha Utafiti Uyole; na • Kupatiwa mafunzo wakulima wa kijiji cha Kipangala ya usimamizi wa mashamba ya korosho.
Kuimarisha Mifumo ya Ikolojia ili Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha mifumo ya ikolojia ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa tathmini ya athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwenye maeneo yote ya utekelezaji wa mradi; • Kupatiwa mafunzo wadau 54 ambao ni viongozi na wataalam mbalimbali wa Serikali, Taasisi za Elimu ya Juu, Asasi za Kiraia na sekta binafsi kuhusu namna ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya Ikolojia; • Kufanyika kwa utafiti kwenye wilaya zinazotekeleza mradi (Mvomero, Kishapu, Simanjiro, Mpwapwa na Kaskazini A) kuhusu kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi; na • Kuanza kwa maandalizi ya mfumo wa kuhimili mabadiliko ya

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Kujenga Uwezo wa Taasisi Kusimamia na Kupunguza Athari za Mazingira kwa Jamii za Vijijini Katika Sehemu Zenye Ukame	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga uwezo wa taasisi kusimamia na kupunguza athari za mazingira kwa jamii za vijijini katika sehemu zenye ukame 	<p>tabianchi kwa kutumia nyenzo rahisi zinazopatikana.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa mradi; • Kuendelea na taratibu za kupata wakandarasi wa kujenga skimu mbili za usambazaji wa maji katika Wilaya ya Mwanga na Kukarabati mita 1800 za njia za umwagiliaji katika Wilaya ya Same; • Kupatiwa mafunzo vikundi vya wakulima vyenye jumla ya watu 50 kuhusu uendeshaji endelevu wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika vijiji vya Mabilioni, Jipe, Makuyuni na Kambi ya Simba katika Wilaya ya Same; na • Kuendelea na taratibu za kumpata Mtaalam Elekezi wa kufanya utafiti wa awali kuhusu uwezekano wa kupata athari za mabadiliko ya tabianchi.
Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Upunguzaji wa Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga uwezo wa kitaifa na kimataifa wa kutekeleza Sheria ya Mazingira 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuandaliwa kwa andiko la awamu ya pili ya Mpango wa Kuondosha Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni ifikapo 2030; • Kufanyiwa mapitio kwa Kanuni za Mwaka 2007 za Udhubiti wa Kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni pamoja na vifaa vinavyotumia kemikali hizo ili kujumuisha marekebisha ya Kigali; na • Kutolewa mafunzo kwa Maafisa forodha na Wasimamizi wa Sheria nchini kuhusu Kanuni za Usimamizi wa Mazingira na Utekelezaji wa Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal.
Kutekeleza Mpango wa Ufuatiliaji na Udhubiti wa Taka Zinazodumu Katika Mazingira	<ul style="list-style-type: none"> • Kuongoa maeneo ya ikolojia yaliyoharibika na kuhifadhi baianuai 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuandaliwa kwa Mkakati wa Usimamizi wa Kemikali na Taka Hatarishi nchini; • Kuandaliwa kwa Mfumo wa kimtandao wa upatikanaji wa

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
kwa Muda Mrefu		<p>taarifa za kemikali na taka nchini na taarifa ya hali halisi ya kemikali nchini;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa Mpango Kazi wa uelimishaji jamii kuhusu kemikali ya <i>Polychlorinated Biphenyl</i> - PCB, 2019; kuandaliwa vipeperushi, mabango, vipindi vya redio na runinga kwa ajili ya kuelimisha jamii na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa TANESCO; • Kuelimisha jamii na wafanyakazi wa TANESCO juu ya madhara yatokanayo na kemikali za PCB katika mikoa tisa (9) nchini; na • Kuandaliwa kwa Kanuni za Usimamizi wa Zebaki nchini.
Miradi ya Ujenzi wa Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji		
MIUNDOMBINU		
RELI		
Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli	<ul style="list-style-type: none"> • Kuondoa reli zote nyepesi na kuweka reli mpya zenye uzito wa ratili 80 kwa yadi kati ya Dar es Salaam na Isaka. 	<ul style="list-style-type: none"> • Dar es Salaam – Kilosa (km 283) na Kilosa - Isaka (km 687) ambapo kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 86. Ukarabati unatarajiwa kukamilika Juni 2020
Ufufuaji wa Njia ya Reli ya Tanga - Arusha (km 439)	<ul style="list-style-type: none"> • Kufufua njia ya reli ya Tanga - Arusha (km 439) 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa kipande cha Tanga - Moshi (km 353) ambacho kimeanza kufanya kazi ya kusafirisha abiria na mizigo; na • Kukamilika kwa ukarabati wa kipande cha Moshi - Arusha (km 86) kwa kubadili reli na mataruma, kurejesha madaraja, makalavati, stesheni na kufungua mifereji ya maji ya mvua.
Ukarabati wa Mabehewa	<ul style="list-style-type: none"> • Ukarabati wa mabehewa 240 	<ul style="list-style-type: none"> • kukarabatiwa kwa mabehewa 133 kati ya lengo la mabehewa 240 yatakayotumika kwenye njia kuu ya reli ya kati ambapo mabehewa 200 ni mfuko wa reli na mabehewa 40 yamekarabatiwa kwa makubaliano ya kibiashara na WFP.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Ukarabati wa Miundombinu ya Reli ya TAZARA	<ul style="list-style-type: none"> • Ukarabati na uimarishaji wa miundombinu ya njia kuu ya reli iliyopo; kununua <i>Traction Motor</i> 90 kwa ajili ya injini 15 zitakazokarabatiwa; • Matengenezo na ukarabati wa vichwa vya treni vilivyopo, mitambo, mabehewa ya mizigo na ya abiria; • Ukarabati wa majengo ya karakana ya Dar es Salaam, mitambo, vifaa na mashine mbalimbali ikijumuisha karakana ya Mbeya, kiwanda cha kokoto na uzalishaji wa mataruma ya zege cha Kongolo; • ukarabati wa mabehewa 21 ya kusafirisha abiria katika treni za mjini Dar es Salaam na treni ya Udzungwa inayo hudumia kati ya stesheni za Mlimba - Kidatu - Makambako; na • kufanya upembuzi yakinifu wa kujenga mchepuko wa njia ya reli kati ya Mlowo na Magamba. 	<ul style="list-style-type: none"> • kukamilika kwa ufungaji wa mitambo (Excavator, Dumper Track na Drill Rig) ambayo imeanza kufanya kazi; na • kununuliwa kwa vipuri vya injini saba (7) ambapo <i>traction motors</i> 12 zimepokelewa. • Ununuzi wa vichwa vipya vinne (4) vya Treni ya njia kuu, vichwa vinne (4) vya sogeza, mabehewa mapya 18 ya abiria, ukarabati wa mabehewa 400 ya mizigo, uboreshaji wa Kituo cha Reli cha Fuga na nyumba Nyumba nane (8) za watumishi kwa ajili ya kuhudumia Mradi mkubwa wa Umeme wa Mto Rufiji.
BARABARA NA MADARAJA		
Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi		
Barabara ya Kidatu - Ifakara - Lupilo - Mahenge /Malinyi - Londo - Lumecha/Songea (km 499)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi sehemu ya Kidatu - Ifakara (km 66.9); na kuanza taratibu za ujenzi sehemu ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Taweta/Madeke (km 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu - Ifakara (km 66.9) ambapo ujenzi umefikia asilimia 12.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	220.22) na Ifakara - Lupiro - Mahenge /Malinyi - Londo - Lumecha/Songea (km 396).	
Barabara ya Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 370)	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi wa barabara sehemu za Usesula - Komanga (108), Komanga - Kasinde (km 108) na Kasinde - Mpanda (km 105.4). 	<ul style="list-style-type: none"> Kukamilika kwa sehemu ya Tabora - Sikonge (km 30); Kuendelea na utekelezaji katika sehemu za Usesula - Komanga (km 108) ambapo ujenzi umefikia asilimia 40; Komanga - Kasinde (km 108) asilimia 56; na Kasinde - Mpanda (km 108) asilimia 44.5.
Barabara ya Makutano - Natta - Mugumu (km 125)/Loliondo - Mto wa Mbu (km 213)	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi wa sehemu za Makutano - Sanzate (km 50) na Waso - Sale Junction (km 49); na kuanza ujenzi sehemu ya Sanzate - Natta (km 40), Natta - Mugumu (km 45), Karatu - Mbulu - Hydrom - Sibiti River - Lalago -Maswa (km 389) sehemu ya Mbulu - Hydrom (km 50). 	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi sehemu ya Makutano - Sanzate (km 50) ambapo ujenzi umefikia asilimia 82.5; Mto wa Mbu - Loliondo sehemu ya Wasso - Sale Junction (km 49) asilimia 46; na Ujenzi wa barabara kwa sehemu ya Sanzate - Natta - Mugumu (km 85) upo katika hatua ya kumpata Mkandarasi.
Barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora (km 259.7)	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi sehemu ya Nyahua - Chaya (km 85.4). 	<ul style="list-style-type: none"> Kukamilika kwa ujenzi sehemu za Tabora - Nyahua (km 85) na Manyoni - Itigi - Chaya (km 89.35); na Ujenzi kwa sehemu ya Nyahua - Chaya (km 85.4) umefikia asilimia 65.
Barabara ya Itoni - Ludewa - Manda (km 211)	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Lusitu - Mawengi (km 50) kwa kiwango cha zege. 	<ul style="list-style-type: none"> Ujenzi wa kiwango cha lami na zege katika sehemu ya Lusitu - Mawengi (km 50) unaendelea, ambapo utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 42.4.
Barabara ya Dodoma - Mtera - Iringa (km 260)	<ul style="list-style-type: none"> Kuanza ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Iringa (Iringa Bypass km 7.3) 	<ul style="list-style-type: none"> Mradi umekamilika; na Kazi za ujenzi katika barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3) zimeanza.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Barabara ya Mbeya - Makongolosi - Rungwa - Itigi - Mkiwa (km 577.90)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi sehemu ya Chunya - Makongolosi (km 43); na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mkiwa - Itigi - Noranga (km 56.9) na Mbalizi - Makongolosi (km 50). 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa sehemu za Chunya - Makongolosi (km 43) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 61.
Barabara ya Kigoma - Kidahwe - Uvinza - Kaliua - Tabora (km 389.7)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi sehemu ya Urambo - Kaliua (km 28); kuanza ujenzi sehemu ya Uvinza - Malagarasi (km 51.1) na sehemu ya Kazilambwa - Chagu (km 42). 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Urambo - Kaliua (km 28) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; • Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Uvinza - Malagarasi (km 51.1) anaendelea na kazi ya kufanya mapitio ya usanifu na nyaraka ya zabuni za kazi za ujenzi; na • Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Chagu - Kazilambwa (km 36) umesainiwa na Mkandarasi ameanza maandalizi ya kuanza kazi.
Barabara ya Mtwara -Mingoyo - Masasi - Songea - Mbamba Bay (km 1,470.9)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa barabara za Mbinga - Mbamba Bay (km 66) na Masasi - Newala - Mnivata (sehemu ya Mtwara - Mnivata km 50); • Kuanza ujenzi wa barabara za Masasi - Nachingwea (km 50), Mtwara - Newala - Masasi (sehemu ya Mnivata - Tandahimba km 50), Likuyufusi - Mkenda (km 122.5) na Kitai - Lituhi (km 90); • Kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nanganga - Ruangwa - 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Mbinga - Mbamba Bay (km 66) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52; • Sehemu ya Mtwara - Mnivata (km 50) asilimia 76; na • Kukamilika kwa kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 107).

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>Nachingwea (km 100), ukarabati wa barabara ya Mtwara - Mingoyo - Masasi (km 200); na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Nachingwea - Liwale (km 130). 	
Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani		
Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 112)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi sehemu iliyobaki kati ya Matai - Kasanga Port (km 32); na • Kuanza ujenzi wa barabara ya Matai - Kasesya (km 50). 	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 112) umefikia asilimia 95.
Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai - Kamwanga /Bomang'ombe - Sanya Juu (km 330.31)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa barabara za Kwasadala - Masama - Machame Junction (km 16), Kiboroloni - Kikarara - Tsuduni - Kidia (km 10.8), Kijenge - Usa River (Nelson Mandela AIST: km 14); • Kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mianzini - Ngaramtoni (km 18), upanuzi wa barabara ya Arusha - Moshi - Himo - Holili (sehemu ya Tengeru - Moshi - Himo (km 105) na ujenzi wa mizani ya Himo. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu - Elerai (km 32.2); Kiboroloni - Kiharara - Tsuduni - Kidia (km 10.8), Kwa Sadala - Masama - Machame Junction (km 16); na • Ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa 3 zilizobaki kati ya kilometa 14 za barabara ya Kijenge - Usa River unaendelea na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Mianzini - Ngaramtoni (km 18) yanaendelea.
Barabara ya Isaka - Lusahunga (km 533)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ukarabati sehemu ya Ushirombo - Lusahunga (km 110); • Ujenzi wa kituo cha Pamoja cha 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ukarabati wa sehemu ya Ushirombo - Lusahunga (km 110); na • Matengenezo ya dharura katika sehemu korofi kwenye sehemu

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>Ukaguzi (<i>One Stop Inspection Station - OSIS</i>) cha Nyakanazi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Ukarabati wa barabara ya Lusahunga - Rusumo (km 92); na • Kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nyakahura - Kumubuga - Murusagamba/ Rulenge - Murugarama na barabara ya Rulenge - Kabanga nickel (km 141). 	<p>ya Lusahunga - Rusumo (km 92) yanaendelea.</p>
<p>Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 517.4)</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mpanda - Mishamo (km 100) sehemu ya Mpanda - Ifukutwa - Vikonge (km 30); • Kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Kibaoni - Sitalike (km 71), Kizi - Lyambalyamfipa - Sitalike (km 86.31); • Kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Vikonge - Magunga - Uvinza (km 159); na • Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Namanyere - Katongoro - New Kipili Port (km 64.8). 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mpanda - Mishamo (km 100) sehemu ya Mpanda - Ifukutwa - Vikonge (km 35) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87.
<p>Barabara ya Nyanguge - Musoma, na Michepuo ya</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kufunga taa za barabarani katika mradi wa upanuzi wa barabara ya 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na taratibu za malipo ya mkandarasi wa upanuzi wa barabara ya kuelekea uwanja wa ndege wa Mwanza (km

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Usagara - Kisesa na Bulamba - Kisorya (km 495.9)	<p>kwenda uwanja wa ndege wa Mwanza (km 12);</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi barabara ya Nansio - Kisorya - Bunda - Nyamuswa (sehemu ya Kisorya - Bulamba km 51); • Kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Nyamuswa - Bunda - Bulamba (km 55), Musoma - Makojo - Busekela (km 92); na • Kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara za Nyanguge - Simiyu/Mara Boarder (km 100.4) na Makutano - Sirari (km 83). 	<p>12);</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nansio - Kisorya - Bunda - Nyamuswa sehemu ya Kisorya - Bulamba (km 51) ambapo ujenzi umefikia asilimia 84.
Barabara ya Mwigumbi - Maswa -Bariadi - Lamadi (km 265.8)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi sehemu ya Maswa - Bariadi (km 49.7); na • Kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara za Kolandoto - Mwanhuzi (km 10), Lalago - Ng'oboko - Mwanhuzi (km 74) na Isabdula (Magu) - Bukwimba - Ngudu - Ng'hungumalwa (km 10). 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Maswa - Bariadi (km 49.7) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 77.6.
Barabara ya Kidahwe - Kasulu - Kibondo - Nyakanazi (km 413)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi sehemu za Kidahwe - Kasulu (km 63) na Nyakanazi - Kakonko/Kabingo (km 50); • Kuanza ujenzi sehemu ya Kakonko 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujezi wa barabara sehemu za Kidahwe - Kasulu (km 63) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.5 na Nyakanazi - Kibondo (km 50) asilimia 78; na • Kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kabingo - Kibondo - Kasulu - Manyovu (km 260)

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	(Kabingo) - Kibondo - Kasulu - Manyovu (km 260) na barabara ya Nduta Junction - Kibondo mjini (km 25.6).	na barabara sehemu ya njia panda ya Nduta - Kibondo Mjini (km 25.6).
Barabara ya Usagara - Geita - Buzirayombo - Kyamyorwa (km 230)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa barabara za Geita - Bulyanhulu Junction (km 58.3); • Bulyanhulu Junction - Kahama (km 61.7); na • Kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyamirembe Port - Katoke (km 50). 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Geita - Bulyanhulu Junction (km 58.3), Bulyanhulu Junction - Kahama (km 61.7) na Nyamirembe Port - Katoke (km 50).
Barabara za Mikoa	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga km 40.81 za barabara za mikoa kwa kiwango cha lami; • Kukarabatiwa km 486.07 kwa kiwango cha changarawe na kujenga madaraja 12. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kujengwa kwa km 24.23 za barabara kwa kiwango cha lami; • Kukarabatiwa kwa km 255.21 kwa kiwango cha changarawe; na • Ujenzi wa madaraja upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.
Barabara za Vijijini na Mijini	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 21,525.04; • Matengenezo ya makalvati madogo 2,403, madaraja 113, makalvati makubwa 273 na mifereji yenye urefu wa mita 82,627.81; • Ujenzi wa kilomita 15.1 za barabara za lami, ukarabati wa kilomita 185.7 za barabara za changarawe; na • Ujenzi wa madaraja 23. 	<ul style="list-style-type: none"> • Matengenezo ya barabara km 4,998.60 (matengenezo ya mara kwa mara km 2,872.03, maeneo korofi km 1,396.38 na matengenezo ya muda maalum km 730.19); • Ujenzi wa kilomita 31 za barabara za lami, madaraja 57, makalvati 238 pamoja na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 9.3; na • Kuanza ujenzi wa barabara za Mji wa Serikali - Mtumba kwa kiwango cha lami zenye urefu wa km 40.
Barabara za Kupunguza	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa km 4 kwenye 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Kibamba - Kisopwa -

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 169.66)	barabara ya Kibamba - Kisopwa - Kwembe - Makondeko (km 14.66), Banana - Kitunda - Kivule - Msongola (km14.7), Mji Mwema - Kimbiji - Pemba Mnazi (km 30), Goba - Makongo (km 5), na Wazo Hill - Madale (km 9) na kuanza maandalizi ya upanuzi wa barabara za Mwai Kibaki (km 9) na Kongowe - Mji Mwema - Kivukoni (km 25.1).	Kwembe - Makondeko (km 14.66) sehemu ya Kibamba - Mloganzila (km 4.0) na barabara ya Ardhi - Makongo - Goba (km 9) sehemu ya Goba - Makongo (km 4); <ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa barabara ya Banana - Kitunda - Kivule - Msongola (km 14.7) sehemu ya Kitunda- Kivule (km 3.2) umefikia asilimia 40; • Kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni umekamilika kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Mjimwema - Kimbiji (km 27.0) na Kongowe - Mjimwema - Kivukoni (km 25.1); na • Upanuzi wa barabara ya Kimara - Kibaha (km 19.2) kuwa njia nane, ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80.
Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka jijini Dar es salaam kwa awamu ya pili (km 20.3) na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zilizopangwa awamu ya tatu (km 23.6) na ya nne (km 25.6). 	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa awamu ya pili (Lot 1) unaohusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 20.3 umefikia asilimia 3.3; na • Lot 2 inayohusisha ujenzi wa majengo (vituo 2, yadi 1 na vituo mlisho 4) ujenzi umefikia asilimia 22.
Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyover) Jijini Dar es Salaam	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa Ubungo <i>Interchange</i>; • Kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya barabara katika maeneo ya <i>Fire, Morocco, Mwenge, Magomeni</i> Tabata/Mandela, 	Kuendelea na ujenzi kwa mradi wa <i>Interchange</i> katika makutano ya Ubungo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 77.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>Buguruni, makutano ya barabara Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/<i>UN Road Junction</i>); na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa <i>Mabey Flyovers</i> katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. 	
UJENZI WA MADARAJA		
Ujenzi wa Madaraja Makubwa	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa daraja la Ruhuhu (Ruvuma), daraja jipya la Wami (Pwani), daraja la Magara (Manyara), daraja la Kitengule (Kagera), na barabara unganishi katika daraja la Sibiti; • Kuanza ujenzi wa daraja la Kigongo/Busisi (Mwanza), daraja la Sukuma (Mwanza) na daraja la Msingi (Singida); kuanza maandalizi ya ujenzi wa daraja la Mkenda (Ruvuma), daraja la Simiyu (Mwanza), na daraja la Mzinga (Dar es salaam); kuanza maandalizi ya ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara); kufanya usanifu na kuanza ujenzi wa daraja la Godegode (Dodoma); na • Kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja la Mtera (Dodoma), 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa madaraja ya Mara (Mara), na Magara (Manyara); na • Kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Ruhuhu (asilimia 86), Mitomoni (asilimia 75), Kitengule (asilimia 50), Msingi (asilimia 40), Selander (asilimia 38.2) na <i>New Wami</i> (asilimia 39).

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	daraja la Mkundi (Morogoro), daraja la Malagarasi Chini (Kigoma), daraja la Ugalla (Katavi), na daraja la Mitomoni (Ruvuma); na ununuzi wa vipuri vya daraja la dharura (<i>emmergency Steel Bridge Parts</i>).	
USAFIRI MAJINI		
Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na kazi ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni; • Ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome; • Ujenzi wa maegesho ya Nyamisati; ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda; na • Ukarabati wa maegesho ya Bugolora – Ukara, Rugezi – Kisorya, Kilambo – Namoto na Utete – Mkongo. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika kivuko cha Lindi – Kitunda; na • Kuanza kwa Awamu ya Pili ya upanuzi wa jengo la abiria na maegesho ya kivuko cha Kigamboni – Magogoni na ujenzi wa maegesho ya Bukondo.
Ununuzi wa Vivuko Vipya	Kukamilisha malipo ya ununuzi wa kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni na kivuko kipya cha Nyamisati – Mafia, kivuko kipya cha Bugolora – Ukara, boti moja (1) ya uokozi kwa ajili ya usafiri wa majini kati ya Lindi na Kitunda, boti nne (4) kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba, na Ghana) na Magogoni – Kigamboni.	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza ujenzi wa vivuko vipya vya Nyamisati-Mafia (asilimia 40), Bugolora-Ukara (asilimia 70); • Ununuzi wa boti mpya za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Ghana), Magogoni - Kigamboni pamoja na boti moja ya uokozi kwa kivuko cha Lindi – Kitunda unaendelea; na • Kununuliwa kwa vitendea kazi kwa ajili ya karakana 15 katika mikoja ya Dar es Salaam (Vingunguti), Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara, Iringa, Njombe, Katavi, Kigoma, Mwanza,

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		Dodoma, Singida na Wilaya za Kahama na Ifakara pamoja na karakana ya MT (Depot Dar es Salaam).
Ukarabati wa Vivuko	Kukarabati vivuko vya MV Sengerema, MV Kigamboni na MV Misungwi, MV Kome II, MV Ujenzi, MV KIU, MV Mara, MV Musoma, MV Tegemeo.	Kukamilika kwa ukarabati wa kivuko cha MV Kigamboni na kuendelea na ukarabati wa vivuko vya MV Sengerema (asilimia 60); MV Misungwi (asilimia 35);kuendelea na taratibu za kupatamkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa MV Tegemeo, MV Ujenzi, MV Musoma, MV KIU na MV Mara.
Ununuzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa meli mpya katika ziwa Victoria na Tanganyika; na • Kuendelea na ukarabati wa meli za MV Victoria, MV Butiama, MV Liemba, MV Umoja, MV Serengeti na MV Songea 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa meli mpya (MV Mwanza) yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 60; • Ujenzi wa chelezo umefikia asilimia 96.5; ukarabati wa meli ya MV Victoria umefikia asilimia 98 na MV Butiama asilimia 98. • Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV. Umoja na MV. Serengeti zilizopo katika ziwa Victoria wamepatikana na maandalizi ya mikataba kwa ajili ya ukarabati wa meli hizo yamekamilika; • Ujenzi wa meli moja mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 katika Ziwa Nyasa umekamilika.
BANDARI		
Bandari ya Dar es Salaam	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na kazi ya kuboresha Gati Na. 1 hadi 7; na kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia na kutokea meli, pamoja na kuongeza kina cha sehemu ya kugeuzia meli 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa magati Na. 1, Na. 2, Na. 3 na Na. 4; • Kukamilika kwa ujenzi wa gati ya kupakia na kupakua magari (Ro-Ro); na • Kuendelea na ujenzi wa Gati Na. 5 hadi 7 ikijumuisha utengenezaji wa vifaa mbalimbali vinavyotumika katika kujenga na kuimarisha magati hayo.
Bandari ya Tanga	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha kwa ukarabati na kuongeza kina cha Gati Namba 2, 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa asilimia 40 ya kazi ya uboreshaji wa bandari Awamu ya Kwanza unaojumuisha uchimbaji wa lango la

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	ukarabati wa barabara kuelekea lango Na. 2; na • Kukamilisha mapitio ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya Mwambani.	kuingilia meli, utafiti wa athari za kimazingira na ununuzi wa mitambo; na • Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya Gati la mafuta ghafi kutoka Uganda.
Bandari ya Mtwara	• Kuendelea na ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300.	• Kuendelea na ujenzi wa gati lenye urefu wa mita 300 la kuhudumia shehena mchanganyiko ambapo utekelezaji umefikia asilimia 61.
Bandari za Maziwa Makuu	• Kukamilisha ujenzi na ukarabati wa magati katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na miundombinu ya usalama.	• Ziwa Victoria: kukamilika kwa ujenzi wa gati la Magarine ambapo lipo kwenye hatua ya uangalizi; kuendelea na ujenzi wa gati Nyamirembe ambalo limefikia asilimia 72; kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Gati ya Majahazi (Dhow Wharves) katika bandari ya Mwigobero; kukamilisha uongezaji kina katika Bandari ya Nansio na <i>Mwanza South</i> ; kukamilisha kuboresha sehemu ya kushukia abiria <i>Mwanza North</i> na Ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya <i>Mwanza South</i> ; na kuendelea na ujenzi wa ofisi na jengo la abiria katika bandari ya Bukoba ambao umefikia asilimia 25. • Ziwa Tanganyika: kukamilika kwa uboreshaji wa Bandari ya Kipili; Ujenzi wa gati la Sibwesa asilimia 98; ujenzi wa gati la Kabwe asilimia 56; kuendelea na ujenzi wa gati la Lagosa ambao umefikia asilimia 53; kuendelea na maboresho ya bandari ya Kasanga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati la Karema, Kigoma ili kuunganishwa na Bandari ya Kalemie nchini Kongo (DRC). • Ziwa Nyasa: ujenzi wa sakafu ngumu kwa ajili ya maegesho

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		katika bandari ya Kiwira unaendelea ambapo umefikia asilimia 35; Kukamilika kwa mchakato wa zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuboresha gati la Ndumbi; na upembuzi Yakiniifu wa Ujenzi wa Gati za Mbamba Bay, Manda na Matema upo katika hatua za mwisho.
Bandari kavu katika eneo la Ruvu	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi wa bandari kavu katika eneo la Ruvu. 	<ul style="list-style-type: none"> kuendelea na ujenzi wa yadi, njia ya reli na ofisi za muda kwenye eneo la hekta tano (5) pamoja na Usanifu wa Matumizi Bora ya eneo la Bandari Kavu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 58.
USAFIRI WA ANGA		
Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro	Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza maandalizi ya kukarabati barabara za kuruka na kutua ndege, kufunga taa za kuongoza ndege na kukarabati eneo la kuegesha magari.	Kuendelea na taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa tabaka la juu la barabara ya kuruka na kutua ndege, kufungwa kwa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa maegesho ya magari.
Kiwanja cha Ndege cha Mwanza	Ujenzi wa jengo jipya la abiria, uzio wa kiwanja, mfumo wa maji safi, mfumo wa kuondoa maji taka na maji ya mvua kiwanjani, maegesho ya magari na kufunga taa za kuongozea ndege.	Kukamilika kwa upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo, uzio wa kiwanja, jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani na kufunga taa za kuongozea ndege.
Kiwanja cha Ndege cha Mtwara	Kuendelea na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio, maegesho ya ndege, kufunga taa za kuongozea ndege, maegesho ya magari na barabara za kuingia na kutoka kiwanjani.	Kuendelea na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, ujenzi wa barabara ya kuingilia kiwanjani na maegesho ya magari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 33.
Viwanja vya Ndege vya	Ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka	Kusainiwa kwa mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Sumbawanga	ndege, viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongoza ndege, jengo la uangalizi wa hali ya hewa, maegesho ya magari na barabara za kuingia na kutoka kiwanjani.	ajili ya: <ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa; • Ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari; na • Ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.
Kiwanja cha Ndege Kigoma	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga jengo la abiria na miundombinu yake ikijumuisha maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara za kuingia na kutoka kiwanjani; ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege; ujenzi wa uzio wa kiwanja, jengo la kuongozea ndege, na jengo la uangalizi wa hali ya hewa. 	Kuendelea na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege pamoja na miundombinu yake (mitambo ya kuongozea ndege), ujenzi wa kituo kidogo cha umeme, ujenzi wa kituo cha uangalizi wa hali ya hewa pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingilia uwanjani na maegesho ya magari.
Kiwanja cha Ndege Shinyanga	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongoza ndege, jengo la uangalizi wa hali ya hewa, maegesho ya magari na barabara za kuingia na kutoka kiwanjani; na • Ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na uzio wa kiwanja. 	Kusainiwa kwa mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.
Viwanja vya Ndege vya Mikoa	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa viwanja vya ndege katika 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa barabara ya kutua na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>mikoa ya Geita na Simiyu;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Upanuzi wa viwanja vya ndege vya mikoa ya Iringa, Ruvuma (Songea), Lindi, Lake Manyara, Tanga na Mara (Musoma); na • Kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi wa kiwanja cha ndege Dodoma; na • Kuanza ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Moshi. 	<p>kuruka ndege kwa kiwango cha changarawe kwa kiwanja cha Nachingwea; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Geita (asilimia 78) na Songea (asilimia 34).
Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria (<i>Terminal III</i>); • Kuunganisha umeme wa gridi ya Taifa kwenye jengo hilo na kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi na ukarabati jengo la pili la abiria (<i>Terminal Building II</i>); na • Kuweka miundombinu katika jengo la Tatu la Abiria (<i>Terminal III</i>). 	Kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria.
Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato	Kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza kulipa fidia kwa mali za wananchi watakaopisha eneo la mradi.	Kuendelea na uhakiki kwa ajili ya ulipaji wa fidia. Aidha, taratibu za awali za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri zinaendelea.
Kiwanja cha Ndege Tabora	Ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, maegesho ya magari, barabara za kuingia na kutoka kiwanjani na jengo la uangalizi wa hali ya hewa.	Kusainiwa kwa mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua jengo jipya la abiria, barabara ya kuingilia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, barabara ya kiungio na jengo la uchunguzi wa hali ya

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		hewa.
Kiwanja cha ndege cha Kimataifa Songwe	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria, usimikaji wa taa za kuongozea ndege; Ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka Ndege, barabara ya kiungio pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege. 	Kusainiwa kwa mikataba kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na ufungaji wa taa za kuongozea ndege. Aidha, taratibu za ununuzi zinaendelea ili kumpata Mkandarasi atakayemaliza ujenzi wa jengo la abiria.
Ufungaji wa rada nne za kuongozea ndege za kiraia	<ul style="list-style-type: none"> Ufungaji wa rada nne za kuongozea ndege za kiraia JNIA, KIA Mwanza na Songwe 	<ul style="list-style-type: none"> Kwa rada za JNIA, KIA na Mwanza ni Kukamilika kwa miundombinu ya rada, kukamilika kwa ufungaji wa mtambo, na kuendelea kwa majaribio ya mitambo. Kwa rada Songwe hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi wa miundombinu ya majengo unaendelea na umefikia asilimia 25.
Ununuzi wa Rada ya tatu (3) ya Hali ya Hewa	Ununuzi wa rada ya tatu (3) ya hali ya hewa zitakayofungwa mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma.	<ul style="list-style-type: none"> kulipa asilimia 90 ya mkataba wa ununuzi wa Rada tatu (3) za hali ya hewa zitakazofungwa Mtwara, Mbeya na Kigoma na kupokelewa kwa vifaa mbalimbali vya hali ya hewa.
NISHATI		
Miradi ya Kuzalisha Umeme		
Ujenzi wa Mradi wa Kinyerezi I Extension – MW 185	<ul style="list-style-type: none"> Ufungaji wa mitambo na kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme 	<ul style="list-style-type: none"> Kukamilika kwa utengenezwaji wa mitambo yote minne (4) na kuanza kufungwa katika eneo la mradi; Kukamilika kwa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi I kV 220; Kuendelea na upanuzi wa njia ya msongo wa kV 132 kutoka Kinyerezi I hadi kituo cha kupoza umeme cha Gongo la Mboto; na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> • Utekelezaji umefikia asilimia 85.
Kufua Umeme wa Rusumo MW 80	<ul style="list-style-type: none"> • Kujenga miundombinu ya kuingiza maji katika handaki; • Ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme; • Ufungaji wa mitambo katika kituo cha kuzalisha umeme; • Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme; na • Kukamilisha miradi ya kijamii kwa wananchi wanaozunguka eneo la mradi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na kazi ya kufunga mitambo ambapo umefikia asilimia 52; • Kukamilika kwa milango ya kuingiza na kuchepusha maji (spillway and intake gates); na • Kukamilika kwa asilimia 56 ya kazi ya uchimbaji wa handaki la kupitishia maji.
Kufua Umeme Mtwara MW 300 kwa kutumia Gesi Asilia	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha uthamini na kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa mradi; • Kumpata Mtaalam Mshauri wa kusimamia ujenzi wa mradi; na • Kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme na miundombinu wezeshi ya maji, barabara na gesi asilia.
Mradi wa Kakono - MW 87	<ul style="list-style-type: none"> • Kutwaa ardhi na kulipa fidia katika eneo la mradi; • Kutafuta Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi na njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 220 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa kazi za usanifu wa mradi.
Mradi wa Umeme wa Jotoardhi - Ngozi (Mbeya)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na utaratibu wa ununuzi wa mtambo wa kuchoronga visima vya utafiti 	<ul style="list-style-type: none"> • Kupatikana na kuajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kuandaa mpango kazi wa uchorongaji (<i>Drilling program</i>) na kusimamia uchorongaji; • Kuendelea na uhakiki wa uwepo wa rasilimali ya jotoardhi;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza tathmini ya ardhi hitajika kwaajili ya uchorongaji; • Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Mazingira (<i>Environmental Management Strategy</i>); na • Kuanza kwa ununuzi ya mitambo kwa ajili ya uchorongaji (<i>walk over rig</i>)
Mradi wa Ruhudji - MW 358 (Njombe)	<ul style="list-style-type: none"> • Kumpata Mtaalam Mshauri wa kusimamia ujenzi wa mradi na kumpata Mkandarasi wa kujenga mradi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na taratibu za uhuishaji wa gharama za mradi; na • Kupata mtaalam mshauri kwa ajili ya kukamilisha uhuishaji wa upembuzi yakinifu.
Malagarasi – MW 45 (Kigoma)	<ul style="list-style-type: none"> • Kutwaa ardhi na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; • Kumpata Mtaalam Mshauri na Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi na njia ya umeme ya msongo wa kV 132 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa usanifu wa mradi; na • Kuendelea na upimaji na uthamini wa eneo la mradi na njia ya kusafirisha umeme na mpango wa kuhamisha wananchi watakaopisha mradi.
Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme		
Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 220 Makambako – Songea	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea kuunganisha wateja ikiwemo vijiji vya Lutikila, Ifinga na Mbangamawe mkoani Ruvuma vilivyoongezeka; • Kukamilisha kazi ya kufunga <i>Reactor</i> na <i>Distribution Panels</i> katika vituo vya kupoza umeme vya Makambako, Madaba na Songea 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuunganishwa kwa umeme vijiji 122 vinavyopitiwa na mradi ambapo wateja 16,281 kati ya 22,700 wameunganishiwa umeme katika Wilaya za Makambako, Njombe na Ludewa na wilaya za Songea Vijijini, Songea Mjini, Namtumbo na Mbinga; na • Kukamilika kwa ufungaji wa <i>Reactor</i> katika kituo cha kupoza umeme Madaba.
Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 400 North West Grid Line (Iringa – Mbeya –	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha uthamini na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi; 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanyika kwa mapitio ya taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu kati ya Mbeya na Sumbawanga; • Kukamilisha uthamini wa mali zitakazopitiwa na mradi na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Nyakanazi)	<ul style="list-style-type: none"> • Kumpata Mtaalam Mshauri wa kusimamia ujenzi wa mradi katika sehemu ya Iringa - Mbeya - Tunduma - Sumbawanga (km 624); • Kuhakiki na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi • Kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi katika sehemu ya Nyakanazi - Kigoma (km 280); • Kufanya tathmini ya mali za wananchi zitakazoathiriwa na mradi; na • Kuandaa nyaraka za zabuni za kumpata Mtaalam Mshauri wa kusimamia mradi katika sehemu ya Sumbawanga - Mpanda - Kigoma (km 480) 	<p>uainishaji wa mipaka ya mkuza wa mradi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kwa upande Kigoma - Nyakanazi kazi zilizofanyika ni pamoja na kupatikana kwa Mtaalam Mshauri ambapo anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na uandaaji wa nyaraka za kimkataba kwa ajili ya kumpata mkandarasi; • Kupata wazabuni watakaonunua vifaa vya kuunganishia umeme wateja 5000 (<i>Last mile connection</i>) katika wilaya za mkoa wa Kigoma; na • Upatikanaji wa eneo la kujenga kituo cha kupoza umeme Kidahwe
Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 220 North West Grid (Geita - Nyakanazi)	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi; • Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi; • Upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita kitakachojengwa kupitia mradi wa Bulyanhulu - Geita; na • Usambazaji wa umeme katika vijiji 32 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na utafiti wa kina, uchunguzi wa udongo na usanifu wa mradi; • Ulipaji wa fidia kwa kipande cha Lot A (Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kv 220, Geita - Nyakanazi); • Kukamilika kwa utafitina upimaji udongo na kuendelea kwa kazi za kukata na kujaza udongo na usanifu katika kipande cha Lot B (ujenzi wa vituo vya kupoza umeme Geita na Nyakanazi); • Kuendelea na utafiti wa kina katika kipande cha Lot C (kusambaza umeme kwenye vijiji vya Geita hadi Bwanga na Nyakanazi hadi Kakonko)

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 220 Bulyahulu - Geita	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 220; • Kukamilisha ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha kV 220 Geita; • Upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha kV 220 Bulyanhulu; • Kukamilisha ujenzi wa njia za kusambaza umeme za msongo wa kV 33 na kV 0.4; na • Kuunganisha umeme kwa wateja wapya 1,500 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa asilimia 82 ya ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme pamoja na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme; • Kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi; na • Kazi ya kuvuta nyaya kwa ajili ya usambazaji wa umeme vijijini imefikia asilimia 92.
Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji - Chalinze - Dodoma	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha upembuzi yakinifu; • Kufanya uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi na kulipa fidia; • Kumpata Mtaalam Mshauri wa kusimamia mradi; na • Kumpata Mkandarasi wa kujenga njia ya kusafirisha umeme 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu; na • Kuendelea na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi
Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida - Arusha - Namanga	<ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa asilimia 67 ya utekelezaji wa mradi huu ambapo nguzo (Tower) 621 kati ya 1,072 zimefungwa.
Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Kinyerezi - Chalinze	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha upembuzi yakinifu; • Kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na • Kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa njia 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	ya kusafirisha umeme na kituo cha kupoza umeme	
Miradi ya Nishati Vijijini kupitia REA	<ul style="list-style-type: none"> • Utekelezaji wa mradi 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuunganishwa kwa umeme jumla ya vijiji 7094 na hivyo kufanya vijiji vilivyopatiwa umeme nchini kote kufikia 9,112.
Miradi ya Kusambaza Gesi Asilia Viwandani	<ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha viwanda vya Shreeji Silicates Tanzania Limited, LN Future na Kings Aluminium; na • Kujenga <i>trunk-line</i> kutoka Mwenge hadi Tegeta na kuunganisha wateja mbalimbali wakiwemo Estim Construction, Chem & Cortex, Polypet, Interchik, Giraffe Hotel, Jangwani Sea Breeze, Ramada Resort Hotel, Landmark Hotel, Seascape Hotel na White Sands Hotel 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia (<i>trunk-lines</i>) yenye urefu wa kilometa 17 na uwezo wa kuhudumia zaidi ya wateja 3,000 wa majumbani Mtwara, kilometa 18 yenye uwezo wa kuhudumia zaidi ya wateja 10,000 wa majumbani Dar es Salaam, na kilometa sita (6) yenye uwezo wa kuhudumia viwanda zaidi ya 20 Mkuranga - Pwani; na • Kuendelea kwa majadiliano ya kimkataba ya mauziano ya gesi kwa viwanda mbalimbali
Utafiti katika Vitaluvya Songo SongoMagharibi, 4/1B na MnaziBayKaskazini	<ul style="list-style-type: none"> • Kumpata Mshauri Mwelekezi wa kukusanya, kuchakata na kutathmini taarifa za mitetemo ya 3D zenye ukubwa wa kilomita za mraba 693.1 kwa kitalu cha 4/1B na Mnazi Bay Kaskazini kwa maeneo ambayo hayajafanyiwa utafiti; • Kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kutathmini athari za mazingira kwa kitalu cha 4/1B na Mnazi Bay Kaskazini; na 	<ul style="list-style-type: none"> • Kupatikana kwa Mshauri Elekezi wa Kuhakiki ubora wa data za mitetemo za mfumo wa 3D wakati wa uchukwaji na uchakataji katika kitalu cha 4/1B; • Tafsiri ya data za mitetemo za mfumo wa 3D katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini imekamilika; na • Uchambuzi wa kitaalam wa zabuni ya kumpata mshauri mwelekezi wa uchorongaji wa visima vya utafiti umekamilika.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kufanya tafiti za kijiolojia na kijiofizikia, kumpata mbia wa kimkakati wa kutekeleza mradi na kufanya maandalizi ya awali ya uchorongaji wa kisima cha utafiti kwa upande wa Kitalu cha Songo Songo Magharibi 	
ARDHI NA MAENEO YA UWEKEZAJI NA BIASHARA		
<p>Progamu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa Hatimiliki za Kumiliki Ardhi 600,000 na Haki za Hatimiliki za Kimila 450,000; • Kuhuisha Ramani 250 za ujazo mdogo (Sheets of small scale base maps (1:50,000); • Kuidhinisha michoro ya upimaji ya viwanja 600,000; na, • Kurasimisha makazi holela 600,000. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upimaji wa viwanja 37,351 katika Halmashauri ya Mbeya Jiji 521, Kahama 3526, Shinyanga 308, Msalala 302, Bariadi 1446, Ilemelea 1200, Sengerema 1800, Misungwi 71, Magu 1535, Ukerewe 1434, Geita 2100, Chato 2528, Bukombe 2767, Iringa 375, Sumbawanga 254, Njombe 4048, Simanjiro 978, Halmashauri ya Mji wa Nzega 2463, Wilaya ya Nzega 4000, Songea 138, Namtumbo 4659, Kondo 172, na Gairo 799; • Kuzinduliwa rasmi kwa Mipango Kabambe ya Jiji la Dodoma na Mji wa Tunduma na kuidhinishwa kwa Mipango Kabambe ya Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Geita na Babati; • Kuandaliwa na kuidhinishwa kwa michoro ya mipangomiji 334 ya urasimishaji yenye jumla ya viwanja 148,000 na kutoa hati miliki 3,469 kupitia mfumo wa kielektroniki katika Jiji la Dar es Salaam; • Kuanzishwa kwa ofisi za ardhi katika mikoa 26; • Kuhalalisha ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa vijiji 920 kati ya 975 vilivyokuwa na migogoro ya matumizi ya ardhi na maeneo ya hifadhi na mapori; • Kutatuliwa kwa migogoro ya ardhi 1,544; na

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<ul style="list-style-type: none"> Kuandaliwa kwa mipangokina ya vitovu vya vijiji katika vijiji vitano (5) katika Wilaya ya Morogoro na kutoa hati za Hakimiliki za Kimila 5,845.
Programu ya Umilikishaji wa Ardhi	<ul style="list-style-type: none"> Kuandaa Haki za Hatimiliki za Kimila 40,000 na Hatimiliki za Kumiliki Ardhi 5,000 kwa Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi; na, Kuimarisha Mifumo ya Kiseru, Kisheria na Kitaasisi. 	<ul style="list-style-type: none"> Kuandaliwa kwa taarifa 59 za Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kijiji na taarifa za Mipango Kina ya Makazi ya Vijiji 86; Kuchapishwa kwa Hati za Hakimiliki ya Kimila (CCRO) 20,841 katika Wilaya za Kilombero (7,191), Ulanga (7,523) na Malinyi (6,127); kusajiliwa kwa CCRO 35,497 katika Wilaya za Kilombero (9,154), Ulanga (14,418) na Malinyi (11,925); Kuchukuliwa kwa CCRO 43,897 na wamiliki katika Wilaya za Kilombero (15,707), Ulanga (11,736) na Malinyi (16,454); Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Ardhi za Halmashauri za Wilaya za Kilombero (asilimia 90), Ulanga (asilimia 70) na Malinyi (asilimia 60); na Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Baraza la Ardhi na Nyumba ya Wilaya ya Kilombero.
Mipaka ya Kimataifa	<ul style="list-style-type: none"> Kuimarisha mipaka ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Democratic Republic of Congo na Zambia yenye urefu wa kilomita 1,278; na, Kuongeza Ukanda wa Bahari na Upimaji katika Maji 	<ul style="list-style-type: none"> Kufanyika kwa kikao cha majadiliano cha namna ya kuimarisha mpaka kati ya Tanzania na Kenya wenye urefu wa km. 128 kutoka Ziwa Natron hadi Namanga; na Kufanyika kwa kikao kati ya Tanzania na Burundi cha majadiliano ya uimarishaji wa mpaka wenye urefu wa km. 100 kutoka Kagunga hadi Manyovu.
HUDUMA ZA FEDHA		
Benki ya Maendeleo TIB (TIB – DFI na TIB Corporate Bank – TIB)	<ul style="list-style-type: none"> Kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 144.5 katika sekta za viwanda, maji, nishati, utalii, kilimo na miundombinu ya Serikali za mitaa; 	<p>Benki ya TIB</p> <ul style="list-style-type: none"> Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 554.68 ambapo mapato ya benki kwa mwaka 2019 yalikuwa shilingi 79,916,960,171.51;

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Kukuza mizania ya Benki kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 872.9; • Kupunguza kiwango cha mikopo chechefu kutoka asilimia 32 ya mwaka 2018 hadi asilimia 22.5 kwa mwaka 2019; na • Kuongeza faida kutoka Shilingi bilioni 8 mwaka 2018 hadi Shilingi bilioni 9 mwaka 2019. 	<p>TIB Corporate Bank</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 165.6 kwa mwaka 2019 kwa ajili ya shughuli mbalimbali zilizohusiana na kilimo, viwanda, madini, biashara na watu binafsi.
Masoko ya Mitaji na Dhamana	<ul style="list-style-type: none"> • Kubuni, kuboresha na kutekeleza mikakati mbalimbali ya utoaji wa elimu kwa umma ili kuongeza uelewa juu ya masoko ya mitaji na dhamana. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchambua na kuidhinisha hatifungani ya Benki ya Biashara ya NMB na hivyo kufanikisha kuuzwa kwa hatifungani za shilingi bilioni 83.30. • Kuidhinishwa kwa uuzwaji wa hisa 588,000,070 za kampuni ya Vodacom Tanzania kwa Shilingi bilioni 499.80 ambapo, Serikali iliweza kupata kodi kiasi cha Shilingi bilioni 146; • Kutoa jumla ya leseni 76 kwa waombaji waliokidhi matakwa ya sheria; • Kuendesha mashindano kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu kuhusu masoko ya mitaji na uwekezaji; • Kutoa mada mbalimbali kuhusu fursa zinazopatikana kwenye masoko ya mitaji; • Kutengeneza na kusambaza shajara na vipeperushi vyenye elimu ya masoko ya mitaji na dhamana; na • Kutoa mada na semina zinazohusu masoko ya mitaji kwa Waheshimiwa Wabunge, vyombo vya ulinzi na wsalama pamoja na wanafunzi wa vyuo na shule za sekondari.
Benki ya Maendeleo ya Kilimo	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa mikopo kwa ajili ya miradi ya 	<ul style="list-style-type: none"> • Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 59.59

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>uchakataji mazao, kilimo cha umwagiliaji, ujenzi wa maghala ya kisasa, miradi ya kilimo kwa kutumia zana bora za kilimo (mechanized agriculture);</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha vituo vya huduma za zana za kilimo; na • Kutoa dhamana za mikopo ili kuchagiza mabanki na taasisi za fedha kuongeza ukopeshaji kwa miradi ya kilimo kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (Smallholder Farmers Credit Guarantee Scheme - SCGS). 	<p>katika kipindi cha mwaka 2019 ambapo imewanufaisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa wa mazao na wafugaji katika mnyororo wa thamani;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 36.374 kupitia benki za biashara nane (8) na kuwanufaisha wakulima wadogo wapatao 5,808 kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo; • Kutolewa mafunzo kwa wakulima wadogo wapatao 20,399 toka benki ilipoanza huduma zake mwaka 2016; na • Kufunguliwa kwa ofisi moja ya kanda za nyanda za juu kusini katika mkoa wa Mbeya.
BIASHARA NA MASOKO		
<p>(i) Mradi wa Kukuza Shughuli za Kibiashara katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika - SADC</p> <p>(ii) Mradi wa EU - EAC wa kuboresha upatikanaji wa masoko:</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa kupitia na kupunguza vikwazo visivyo vya kikodi; • Utekelezaji wa Sera ya Viwanda na Mpango Mkakati; • Uendelezaji wa mnyororo wa thamani na kuboresha uzalishaji wa mazao ya chai, kahawa, alizeti, viungo, embe, parachichi pamoja na kuwawezesha wakulima na wafanya biashara kuyafikia masoko ya Jumuiya ya Ulaya; • Kuendelea kushirikiana na 	<p>Biashara</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuendelea na majadiliano ya biashara ya kikanda (EAC, SADC, AfCFTA) na kimataifa (WTO) kuingia mikataba ya ufunguaji wa masoko katika maeneo ya kipaumbele na majadiliano ya biashara; • Kuimarisha Mfumo wa usajili wa Makampuni kupitia mtandao; • Kuratibu Mikutano ya majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania; • Kuimarisha Sekta Ndogo ya Biashara (SMEs) ili kuongeza Ushindani; • Kuboresha na Kuimarisha Chuo cha Biashara (CBE) kwa kufanya upembuzi yakinifu wa kuboresha makazi ya watumishi katika

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<p>kuhamasisha jumuiya ya wafanyabiashara juu ya fursa za masoko ya upendeleo ambayo Tanzania inanufaika; na</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kufanya majadiliano ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi nyingine, Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kupanua fursa za masoko na uwekezaji. 	<p>eneo la Oysterbay Dar es Salaam, ukarabati wa mifumo ya TEHAMA na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Kampasi ya Dar es Salaam na Dodoma, pamoja na kuanza ujenzi wa Kampasi ya Mbeya.</p> <p>Masoko</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuwaunganisha Wazalishaji, Wasindikaji na Wafanyabiashara na Masoko ya Ndani na Nje ya Nchi; • Kupanua wigo wa Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala; • Kuimarisha masoko ya mipakani kwa ajili ya wajasiriamali wadogo waweze kuuza nje ya nchi; • Kufanya utafiti wa masoko ya ndani na nje ya nchi kwa bidhaa na mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini yanayozalishwa nchini; • Kuimarisha utoaji wa taarifa za Biashara na Intelijensia ya Masoko; na • Kuendeleza Miundombinu ya Biashara na Maonesho.
KUIMARISHA USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO		
Utawala Bora na Huduma kwa Wananchi		
Azma ya Serikali Kuu Kuhamia Dodoma	<ul style="list-style-type: none"> • Kuharakisha Azma ya Serikali Kuu Kuhamia Dodoma kuendelea na ujenzi wa mji wa Serikali na Jiji la Dodoma kwa kuimarisha miundombinu ya masoko, huduma za jamii, barabara, mfumo wa maji safi na maji taka 	<ul style="list-style-type: none"> • Jumla ya watumishi 15,361 wa Wizara, Ofisi ya Rais Ikulu na taasisi zake, muhimili wa bunge, vyombo vya ulinzi na usalama na baadhi ya taasisi za serikali wamehamishiwa Makao Makuu ya Serikali, Dodoma; • kukamilika kwa ujenzi wa awali wa Ofisi za Serikali katika mji wa Serikali, Mtumba na maandalizi ya ujenzi awamu ya pili unaendelea; • kutolewa hati 67 za umiliki wa viwanja kwa mabalozi

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<p>wanaowakilisha nchi zao hapa nchini na mashirika ya kimataifa zitakazoweza kuanza ujenzi;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Hati 190,000 zimetolewa ili kuhakikisha uendelezaji unazingatia sheria ya mipango miji; • kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara za lami na changarawe katika maeneo ya Dodoma ikiwemo Mji wa Serikali, umeme, usafiri na usafirishaji, masoko; na • kukamilika kwa Mpango Kabambe wa jiji la Dodoma ambao utakidhi na kuendana na uendelezaji wa Makao Makuu ya nchi.
Mfuko wa Bunge	<ul style="list-style-type: none"> • kuanzisha Bunge mtandao na kituo cha kurusha matangazo ya redio na televisheni ya Bunge, ukarabati wa majengo ya Bunge na ukarabati wa ukumbi wa Bunge; • ujenzi wa nyumba za makazi ya viongozi wa Bunge na Ununuzi na ufungaji wa mitambo ya usalama; • kujengea uwezo Idara ya Bajeti; na • Kuwezesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Wabunge na Watumishi. 	<ul style="list-style-type: none"> • kukamilika kwa ukarabati wa ghorofa ya tano katika jengo la Utawala; • kukamilika kwa ukarabati wa ofisi na kumbi za vikao vya Kamati za Bunge; • kununuliwa na kusimikwa kwa vifaa vya kituo cha matangazo ya redio na runinga; na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA (<i>Tablets 460 na Servers 2</i>) kwa ajili ya Bunge Mtandao (e-Parliament). • kukamilika kwa mfumo wa kuchakata taarifa za kiuchumi (<i>Macro Economic Model Forecasting</i>); • kutolewa mafunzo kwa watumishi 45 na wabunge 26 wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu uchambuzi wa taarifa za Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na • kukamilika kwa mfumo pamoja na ununuzi ya vifaa vya kuhifadha takwimu za kibajeti na kiuchumi. • Kutolewa kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Wabunge na Watumishi kwenye maeneo ya uandaaji wa Miswada, Sheria, na Bajeti; • kutolewa kwa mafunzo ya utafiti wa Kibunge na ujumuishwaji

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<p>wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge;</p> <ul style="list-style-type: none"> • kukamilika kwa mfumo wa kieletroniki wa kutunza kumbukumbu za ofisi na mfumo wa kieletroniki wa Maktaba; • kuandaliwa kwa Mipango Mikakati ya Vyama vya hiari vya Kibunge (APNAC, TAPAFE, TYPF). • Kununuliwa na Kufungwa kwa mitambo ya usalama na • ujenzi wa nyumba za makazi yaViongozi wa Bunge ambapo nyumba ya Katibu wa Bunge imekamilika kwa asilimia 80 na ya Naibu spika ipo katika maandalizi ya awali ya ujenzi.
Utoaji Haki na Huduma za Kisheria	<ul style="list-style-type: none"> • kuimarisha utoaji Haki kwa njia ya Mtandao (e-Justice); • kuunganisha taasisi za haki jinai katika mfumo mmoja wa kielektroniki; • Kuanza ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania jijini Dodoma; • Kuendelea na ujenzi wa mahakama nchini kote zikiwemo Mahakama Kuu mbili (2) zinazoendelea kujengwa mkoani Kigoma na Mara na kuanza kujenga nyingine katika mikoa ya Morogoro, Mwanza, Dodoma na Singida. Pamoja na kujenga Mahakama za Wilaya 32 na Mahakama za Mwanzo 20; • Kuimarisha matumizi ya TEHAMA; 	<ul style="list-style-type: none"> • kukamilika kwa Mfumo wa Kielekroniki wa Ukusanyaji Taarifa za Usajili wa Mashauri Mahakamani na kuhifadhi takwimu za Mahakama; • kuimarishwa kwa matumizi ya TEHAMA katika mifumo ya utoaji haki; • kuanzishwa kwa kanzidata ya Wanasheria walio katika utumishi wa umma ili kuharakisha upatikanaji wa huduma za utoaji haki nchini. • kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu Kigoma na Mara; • kuendelea na ukarabati mkubwa wa Mahakama Kuu Sumbawanga; • kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi Manyara, Simiyu na Geita; • kukamilika kwa Mahakama za Wilaya za Longido, Chato, Geita, Bukombe, Bariadi, Njombe, Ruangwa, Kilwa, Chunya, Kondo • kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Kasulu,

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> • Usimamizi wa kamati za maadili ya mawakili wa kujitegemea, udhibiti na kuwaondoa kwenye orodha mawakili wanaokiuka maadili pamoja na kujihusisha na vitendo vya kushawishi na kutoa rushwa; na • Kuimarisha usalama wa Raia na mali zake. 	<p>Wanging'ombe, Bunda, Makete, Sikonge, Kilindi na Rungwe ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji;</p> <ul style="list-style-type: none"> • kukamilisha ukarabati wa nyumba tatu (3) za kufikia Majaji mkoani Mtwara; • kukamilika kwa ujenzi wa nyumba mbili (2) za Majaji Kigoma na nyumba mbili (2) za Majaji Musoma; • kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba mbili (2) za Mahakimu Loliondo; • kuanza kwa ujenzi wa vituo sita (6) Jumuishi vya Haki katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Dar es salaam, Arusha na Dodoma; • kuendelea na ujenzi wa majengo ya mabweni katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama na kukamilika kwa Mfumo Mpya wa Usajili wa Mashauri (<i>Judiciary Statistics Dashboard System</i>). • kukamilika kwa ujenzi wa majengo sita ya ghorofa (yenye floor 3 kila moja) kwa ajili ya kuishi familia 24 za Askari Musoma – Mara katika kitalu namba mbili; • kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za makazi ya askari Mabatini Mwanza; • kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa bweni la kuishi wanafunzi 180, madarasa ya wanafunzi 140 na ofisi za walimu na stoo katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 362 za makazi ya askari polisi nchi nzima kati ya nyumba 400 zilizopangwa kujengwa ambapo nyumba 38 zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji; • Kuendelea na ukamilishaji wa kituo cha Zimamoto na Uokoaji

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<p>Wilayani Chato (Geita);</p> <ul style="list-style-type: none"> • ununuzi wa magari matano (5) na boti mbili (2) pamoja na vifaa vya kuzimia moto; na • kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Uhamiaji Jijini Dodoma ambao umefikia asilimia 21.
<p>Usajili wa Vizazi na Vifo kwa ufadhili wa <i>Unicef Support to Multisectoral</i></p>	<ul style="list-style-type: none"> • kusajili matukio muhimu ya binadamu, hususan vizazi na vifo Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa Usajili wa Watoto chini ya Miaka mitano. 	<ul style="list-style-type: none"> • kusajiliwa kwa vizazi 4,257,705 vya watoto wenye umri chini ya miaka 5 katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Shinyanga, Geita, Lindi, Mtwara, Mara, Simiyu, Dodoma, Singida, Morogoro, na Pwani ambapo kiwango cha usajili kimeongezeka kutoka asilimia 38 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 45 mwaka 2019; • Kusajiliwa kwa Vizazi 325,583 vya watoto walio shuleni katika wilaya 19 za Kigamboni, Temeke, Kinondoni, Ilala, Iringa, Kilindi, Ludewa, Makete, Wang'ing'ombe, Njombe, Songea, Singida, Musoma, Tarime, Bunda, Bariadi, Maswa, Kahama na Manyoni; • kusajili na kutoa vyeti vya vifo 52,753; na • kuboreshwa kwa usajili wa Vizazi na Vifo kwa kutumia Mfuko wa TEHAMA kwa kufunga mfumo wa kielekroniki wa Usajili wa vizazi na Vifo katika vituo 166.
<p>Mradi wa upatikanaji haki za kisheria na haki za binadamu (<i>Access to Justice & Human Rights</i>)</p>	<ul style="list-style-type: none"> • kuimarisha mfumo wa upatikanaji haki za kisheria na ulinzi wa haki za binadamu kwa wanawake na watu walio kwenye makundi maalum 	<ul style="list-style-type: none"> • kuimarika kwa Mifumo ya Utoaji Haki na kulinda Haki za Binadamu; • kupungua kwa mianya ya rushwa kwenye Mifumo ya Haki-Jinai ambayo ni kikwazo katika kupiga vita umaskini; • kuanza kwa huduma ya mahakama inayotembea kwa mikoa ya Dar es salaam na Mwanza; • kutolewa kwa mafunzo ya kujenga uwezo wa Kamati za Ulinzi

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
		<p>wa wanawake na watoto katika wilaya za Kasulu na Sengerema;</p> <ul style="list-style-type: none"> • kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya msaada wa kisheria ili kutoa fursa na mazingira mazuri ya kupata Haki; na • kutolewa kwa mafunzo kuhusu sheria ya huduma ya msaada wa sheria kwa watendaji wa Serikali zaidi ya 1080 ili kuwajengea uwezo watendaji wa Vijiji, Vitongoji na mitaa.
Vitambulisho vya Taifa	<ul style="list-style-type: none"> • usajili na utambuzi wa wananchi, wageni wakazi na wakimbizi waliofikia umri wa miaka 18; • kuendelea na utoaji wa vitambulisho vya Taifa katika mikoa yote nchini; • kukamilisha mfumo wa mawasiliano katika wilaya 34 na makao makuu ya wilaya; • kuunganisha mfumo wa vitambulisho vya Taifa pamoja na mifumo ya taasisi nyingine (40); • kukamilisha sheria ya usajili na utambuzi wa watu; kununua vifaa vya usajili na vitendea kazi kwa kila wilaya; na • ujenzi wa ofisi za makao makuu - Dodoma na ofisi za usajili katika wilaya 42. 	<ul style="list-style-type: none"> • kutoa namba za utambulisho na Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wenye umri wa miaka 18 na kuendelea ambapo jumla ya watu 21,511,321 wametambuliwa na kusajiliwa, • namba za utambulisho 16,211,654 ambapo vitambulisho 5,787,869 vimezalishwa; • kuendelea na usajili na utambuzi wa wakimbizi katika kambi (Nyarugusu, Mtendeli, Nduta) na makazi (Mishamo, Ulyankulu, Katumba) na Dar es Salaam ambapo jumla ya wakimbizi 200,074 wamesajiliwa; • kuunganishwa kwa ofisi 10 za usajili na utambuzi za Wilaya na Makao Makuu kupitia Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa; • kununuliwa kwa vifaa mbalimbali kwa ajili ya usajili ikijumuisha vifaa vya TEHAMA, gari moja (1) na mashine mbili mpya za uchapaji wa Vitambulisho vya Taifa zenye uwezo wa kuzalisha vitambulisho 9,000 kwa saa; na • kuendelea na uunganishaji wa mifumo ya mawasiliano kati ya taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi ili kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali ambapo jumla ya Taasisi 10 zimeunganishwa.

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji Nchini	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanza Ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji Jijini Dodoma na Kuendelea na mradi ya ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika mikoa mbalimbali nchini 	<ul style="list-style-type: none"> • kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji Jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 21, • kuendelea ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi umefikia asilimia 53, • kuendelea ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Geita umefikia asilimia 60, • kuendelea ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara umefikia asilimia 21, • kuendelea ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara umefikia asilimia 65, • kuendelea ujenzi wa nyumba ya makazi ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza umefikia asilimia 98, • kuendelea ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Masaki - Dar es Salaam umefikia asilimia 75, na • kuendelea na ukarabati wa Nyumba za Makazi ya Watumishi zilizopo Ibinzamata - Shinyanga umefikia asilimia 85.
MAENEO MENGINE MUHIMU KWA UKUAJI WA UCHUMI NA USTAWI NA TAIFA		
Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi		
Mchango wa Serikali katika Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha Sera na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta Binafsi ya mwaka 2019; • Kuboresha sera za masuala ya uchumi katika usimamizi wa fedha, riba na kodi; • Kuendelea na utekelezaji wa Mwongozo wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara; 	<ul style="list-style-type: none"> • Kufutwa na kupunguzwa kwa ada na tozo 54 zilizokuwa zikitozwa na Wizara, Wakala, Idara na taasisi zinazojitegemea; • Kuandaliwa kwa <i>Information Memorandum</i> kwa viwanda vilivyo rudishwa Serikalini baada ya kubinafsishwa; • Kutambua na kuiwezesha sekta isiyo rasmi kwa kutoa vitambulisho maalum; • Kuongeza uzalishaji wa umeme na kuunganisha mikoa iliyokuwa inatumia umeme wa genereta katika gridi ya taifa; • Kuendelea kujenga miundombinu wezeshi ya barabara, maji,

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
	<ul style="list-style-type: none"> Kuandaa kanuni na miongozo ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; na Kuendelea kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya uwezesaji yenye miundombinu ili kuvutia wawekezaji zaidi. 	<p>umeme katika maeneo yaliyotengwa na halmashauri zote nchini kwa ajili ya wafanyabiashara;</p> <ul style="list-style-type: none"> Kufanyika kwa mikutano mbalimbali na wadau wa sekta binafsi ili kujadili na kutatua changamoto zinazowakabili; Kuboresha sekta ya usafiri na usafirishaji kwa kufufua baadhi ya njia za Garimoshi ya Tanga - Moshi - Arusha, kuongeza safari za ndani na nje ya nchi kwa shirika la ndege ATCL na hivyo kuwawezesha wafanyabiashara na wawekezaji kusafiri na kusafirisha kwa urahisi na kwa gharama nafuu; na Upanuzi na uboreshaji wa bandari ikiwemo ya Dar es Salaam kumewezesha muda wa kupakia na kupakua mizigo kuwa rahisi.
Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi		
Miradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Dawa Muhimu na Vifaa Tiba itakayotekelezwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika Mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya	Kuwapata wabia wa ujenzi wa viwanda vitatu (3) vya uzalishaji wa dawa muhimu na vifaa tiba na kuanza ujenzi	<ul style="list-style-type: none"> Kuendelea na taratibu za kutafuta wabia wa mradi
Mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza	<ul style="list-style-type: none"> Kutafuta mbia wa kutoa huduma <i>Service Providers</i> kuendesha huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka. 	<ul style="list-style-type: none"> Kukamilika kwa upembuzi yakinifu; na Kuandaliwa kwa nyaraka za zabuni kwa ajili ya watoa huduma
Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya	<ul style="list-style-type: none"> Kukamilisha upembuzi yakinifu wa 	<ul style="list-style-type: none"> Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa miradi

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Nyota Nne na Kituo cha Kibiashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere	miradi	
Mradi wa ujenzi wa reli ya Mtwara - Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa <i>Standard Gauge</i>	Kukamilisha kwa upembuzi yakinifu	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha hatua za kumpata Mshauri Elekezi (Transaction advisor) kwa ajili ya kuandaa nyaraka na kututafutia Mwekezaji kwa mfumo wa Ubia baina ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP)
Mradi wa Ujenzi wa Hosteli wa Chuo cha Maendeleo Vijijini (IRDP)	Kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa mradi
Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo	Kukamilisha kwa upembuzi yakinifu	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu.
Ujenzi wa Reli ya Tanga - Arusha - Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu ya <i>standard gauge</i>	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha upembuzi yakinifu na kutangaza zabuni ya kumpata Mbia 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa hatua za kumpata Mshauri Elekezi (<i>Transaction advisor</i>) kwa ajili ya kuandaa nyaraka na kututafutia Mwekezaji kwa mfumo wa Ubia baina ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP).
Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara:	<ul style="list-style-type: none"> • Kumpata Mtaalam Elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu na kuutangaza mradi kwa ajili ya kumpata Mbia 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa awali na kuendelea na hatua za kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kuandaa upembuzi yanikifu
Mradi wa Ujenzi wa Hosteli za Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi za Dodoma na Dar es Salaam	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha kwa upembuzi yakinifu. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa mradi.
Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano, Kituo cha Kibiashara na Jengo la Watu	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha upembuzi yakinifu. 	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha hatua za kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kuandaa taarifa ya upembuzi yakinifu.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21

Jina la Mradi	Malengo /Shughuli 2019/20	Shughuli Zilizotekelezwa 2019/20
Mashuhuri katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro		